

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Hamsini na Sita – Tarehe 26 Agosti, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Taarifa ya Majibu ya Serikali kuhusu Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Hati za Uhamishaji Fedha Na. 1 na Na. 2 za Mwaka 2011/2012 (*Statements of Reallocation Warrants No. 1 and 2 of 2011/2012*).

Majibu ya Serikali kuhusu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2009.

Majibu ya Serikali kuhusu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2009.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Chuo Kikuu cha Dodoma kwa miaka ya 2008/2009 na 2009/2010 (*The Annual Report and Accounts of the University of Dodoma for the years 2008/2009 and 2009/2010*).

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaanza na maswali ya Ofisi ya Waziri Mkuu na atakayeuliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida.

Na. 490

Kuwawezesha Wajasiriamali

MHE. ZARINA S. MADABIDA aliuliza:-

Vijana wengi wanaomaliza Vuyo na kuwa na ujuzi mbalimbali lakini hawana ajira wala hawawezi kujiajiri baada ya kukosa mitaji na ili waweze kupata mikopo Benki lazima wawe na dhamana ya mali isiyohamishika ambayo hawana, wakiwemo na wajasiriamali wengi wadogo wadogo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha kwa mitaji vijana hao ili waweze kujiajiri na kutumia taaluma walijonayo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wajasiriamali kukuza mitaji ya biashara zao ili waweze kuinua kipato chao na kuchangia pato la Taifa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli vijana wengi wanaomiliza vyuo na kuwa na ujuzi mbalimbali wanakabiliwa na tatizo la mitaji. Kwa kutambua tatizo hili, mwaka 1996 Serikali ilitunga Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana. Pamoja na mambo mengine, Sera hii imetoa mwongozo kwa vijana, wazazi, wadau wa elimu na hasa waelimishaji wanaotayarisha Mipango ya Maendeleo katika sekta mbalimbali za maendeleo ya namna ya kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za kujipatia ajira na mapato. Kwa mfano, aya ya 5.7, aya ndogo ya 5.7.1 na 5.7.2 zinatoa maelekezo kwa Wizara ya Fedha ya namna ya kuwasaidia vijana kupata mitaji.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuwasaidia wananchi wakiwemo vijana kupata mitaji Serikali iliandaa Sera ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi mwaka 2004 na baadaye Sheria ya Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi namba 16 ya mwaka 2004. Baraza la Uwezeshaji limeelekezwa kuweka mikakati mahsusii ikishirkiana na Wizara ya Maendeleo ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kutambua mahitaji ya mitaji kwa vijana kwa nia ya kuwawezesha kuititia vikundi vyao rasmi.

Mheshimiwa Spika, kuna nguzo tisa za uwezeshaji na kati ya nguzo hizo zilizoainishwa kwenye sera, nguzo nne zinaweka mkakati wa namna ya kuwawezesha wajasiriamali wakiwemo vijana wa rika mbalimbali kupata mitaji kwa ajili ya kuendeshea shughuli za kiuchumi na hizo nguzo zimeorodheshwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sera na sheria ya kuwawezesha wananchi kiuchumi tumepata mafanikio mengi, ikiwemo kuongeza idadi ya wanaokopeshwa, kuongeza ajira, kutoa huduma za ushauri wa ugani kwa wajasiriamali kuititia *SIDO* na kuimarisha *SACCOS* mbalimbali na kwa kushirkiana na sekta binafsi kubuni mradi wa kukuza ushindani wa biashara na kadhalika. Napenda kuwashauri vijana kuijunga katika vikundi au ushirika kwa wale walio kazini na kuhakikisha wamesajiliwa.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swalii la nyongeza. Nashukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako. Lakini vijana ninaowaongelea ni wale ambaa wanamaliza vyuo ambaa hawana kazi, hawawezi kuijunga na *SACCOS* kwa sababu hawana fedha. Je, Wizara yako inasemaje kuhusu vijana hao kwa sababu mpaka sasa hivi halii ilivyo hawana jinsi yoyote ya kuweza kujikwamua kimaisha. Naomba jibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Madabida kwa kuijielekeza kwenye matatizo na mahitaji ya mitaji ya vijana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, vijana wanaomiliza vyuo huwa hawana kazi hawaajaajiriwa na kwa hivyo pengine ni vigumu sana kuijunga na *SACCOS*. Lakini inawezekana vile vile wakiwa vyuoni kwa mfano, Madaktari, Wahandisi, Wahasibu wanawenza wakaunda vikundi vyao ambavyo si vya *SACCOS*, lakini kuititia vikundi hivyo wakawenza kuliona Baraza la Uwezeshaji ili liweze kuwapa namna ya kupata mitaji na mimi binafsi kwa sababu Baraza liko chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tutawaelekeza kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba wajielekeze kwa vijana hao kwa sababu ndio nguvu kazi au rasilimali muhimu ya Taifa letu na ndio tunaowategemea kujenga uchumi wetu hasa katika soko hili huria.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Ningependa kuuliza kwamba kwa kuwa mtaji pekee wa vijana hawa ni elimu yao. Je, kwa nini Serikali isivihamasithe vyombo vya fedha vikatumia yeti vyao halisi kama dhamana kwa ajili ya kupewa mikopo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kumshukuru sana Mheshimiwa Selasini, Mbunge wa Rombo kwa kuibua jambo

ambalo ni muhimu na ambalo kwa kweli linaweza likasaidia sana kwa vijana kupata mitaji. Suala la vyeti vyao ambavyo kwa kweli vina thamani. Leo Waziri wa Fedha anaendelea na mjadala wa Wizara yake na Mheshimiwa Gavana wa Benki Kuu yuko hapa na Wakuu wote wa Taasisi za Fedha wako hapa. Napenda niungane nae kwamba kwa kweli vyeti vinaweza vikatumika kama dhamana kwa vijana wanaomaliza vyuo vyetu kuweza kupata mitaji. Lakini ningependa vile vile kuwakumbusha na kuwaasa vijana kwamba wasitegemee tu ajira za kuajiriwa wapende na wao kujajiri kwa sababu ndio namna ambavyo kwa kweli wanaweza kujihakikishia ajira badala ya kubaki wanarandaranda kutafuta ajira.

Na. 491

Ombi la Kuligawa Jimbo la Rungwe Magharibi

MHE. CYNTHIA H. NGOYE (K.n.y. MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA) aliliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe iliomba Tume ya Uchaguzi kuligawa Jimbo la Rungwe Magharibi kwa kuwa jioagrafia yake ni ngumu kwa kuwa na milima na mabonde, ukosefu wa madaraja, barabara kuwa mbovu, Kata 26, Vijiji 120 na wakazi karibu laki tatu :-

Je, Serikali itakuwa tayari kuititia upya maombi hayo na kuligawa Jimbo hilo ili kurahisisha zoezi zima la kuchochea, kuhamasisha na kusimamia maendeleo Jimboni humo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali namba 213 la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela tarehe 12 Julai, 2011, Jimbo la Uchaguzi hugawanywa kwa kuzingatia vigezo 13. Vigezo hivyo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Idadi ya watu;
- (ii) Upatikanaji wa mawasiliano;
- (iii) Hali ya Kijiografia;
- (iv) Mgawanyo wa wastani wa idadi ya watu;
- (v) Hali ya kiuchumi ya Jimbo;
- (vi) Ukubwa wa eneo la Jimbo husika;
- (vii) Mipaka ya kiutawala;
- (viii) Jimbo moja lisiwe ndani ya Wilaya au Halmashauri mbili;
- (ix) Kata moja isiwe ndani ya Majimbo mawili;
- (x) Mpangilio wa maeneo ya makazi ya watu;
- (xi) Mazingira ya Muungano;
- (xii) Uwezo wa Ukumbi wa Bunge; na
- (xiii) Idadi ya Viti Maalum vya Wanawake.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea jumla ya maombi 47 ya kugawa Majimbo kutoka Halmashauri mbalimbali, likiwemo Jimbo la Rungwe. Baada ya kupokea maombi hayo, Tume iligawa Majimbo kwa kutumia vigezo nilivytota ambapo Jimbo la Rungwe halikuwa miongoni mwa Majimbo yaliyopata alama nyingi kuweza kuwa na sifa za kugawanywa. Majimbo yaliyogawanywa ni Tunduru, Nkasi, Maswa, Kasulu, Bukombe, Singida Kusini na Ukonga.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zoezi la kuititia upya mipaka ya Majimbo ni endelevu, endapo Jimbo la Rungwe Magharibi litakidhi vigezo na kupata alama zinazohitajika, litagawanywa.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwa majibu yake mazuri. Pamoja na hayo naomba nimwulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, ifikapo mwaka 2015 Jimbo la Rungwe Magharibi

linakisiwa litakuwa na watu laki tatu, je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuahidi wananchi wa Rungwe Magharibi kwamba wakati huo basi vigezo hivi kwa kuwa bado vitaendelea kuwa ni vigezo muhimu, Jimbo hili linaweza likapata sifa ya kuweza kugawanywa?

Swali la pili, kuna vijiji ambavyo viko mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya ya Rungwe yaani Tukuyu, Vijiji vya Mkumburu, Isabula, Kipande katika Tarafa ya Ukuwe viko mbali sana na hali ya miundombinu ya barabara katika maeneo hayo ni ngumu sana hivyo hawawezi kufikia kumwona Mheshimiwa Mbunge huko Tukuyu. Je, Serikali inaweza kuwafikiria watu hao basi angalau kuwatengenezea barabara ambazo ni za kudumu ili waweze kusafiri kwa urahisi kufika katika Makao Makuu ya Jimbo?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza linasema kwamba ifikapo mwaka 2015 idadi ya watu Jimbo la Rungwe Magharibi litafikia laki tatu na anapenda kujua kwamba kama naweza kuahidi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kwamba kuna vigezo 13 ikiwemo kigezo cha idadi ya watu na nikaahidi kama vigezo vitakuwa vimetimia na kwamba vinatosheleza, Serikali haitasita kuligawa Jimbo la Rungwe, lakini ni hapo ambapo vigezo vinavyotakiwa viwe vimefikiwa ikiwa ni pamoja na idadi ya watu.

Pili, kwamba kuna vijiji ambapo viko mbali sana na ambapo yupo Mheshimiwa Mbunge na kwamba barabara ni mbovu. Kwa kweli nawapa pole wananchi hawa ambao wako mbali ambao wanapata adha ya kufika kwa Mbunge wao. Ninachowea kusema hapa ni kuishauri na kuielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na kwa kushirikiana na wananchi wa vijiji hivyo, waone umuhimu wa kutengeneza barabara ambazo zinaweza kuwafikisha Makao Makuu ya Jimbo na vile vile kufikia huduma mbalimbali ambazo ni muhimu sana kwa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Kirigini swalii la nyongeza.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika,

SPIKA: Aha! Samahani Mheshimiwa Kirigini, Waziri wa Nchi TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, napenda kuwapa taarifa watu wa Rungwe kwamba kwa kutambua ukubwa wa Wilaya ya Rungwe, kwa kutambua wingi wa watu katika Wilaya ya Rungwe Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa yaani Waziri Mkuu ameridhia kuanzishwa kwa Halmashauri ya Wilaya Busekelo katika Wilaya ya Rungwe. Kwa hiyo, tutaanza na Halmashauri hizo mbili huko mbele ya safari kama kila Halmashauri zitafuzu kuwa Jimbo basi itatazamwa kulingana na itakavyokuwa. Lakini taarifa njema kwa Rungwe ni hiyo kwamba, tunaanza na Halmashauri mpya ya Wilaya ya Busekelo.

SPIKA: Lakini na ukumbi wetu tumeshapanua hatuwezi kupanua zaidi ya hapo. Hilo nalo mlifahamu. Mheshimiwa Kirigini nilikwita.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii muhimu. Kwa kuwa kilio cha wananchi wa Musoma Vijiji kwa takriban miaka 10 sasa ni kuhusu kukata Jimbo hilo ambalo lina watu zaidi ya laki tano na Kata 34. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kulikata Jimbo hili ili yaweze kuwa Majimbo mawili au hata matatu ili kuharakisha shughuli za maendeleo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba Wilaya ya Musoma Vijiji ni kubwa ndio maana Mheshimiwa Rais ameamua kuanzisha Wilaya mpya ya Butiama inayozaliwa kutokana na Musoma Vijiji.

Lakini pia tumetafakari eneo linalobaki la Musoma Vijiji ni tukasema basi tutakuwa na Manispaa ya Musoma lakini pia tutaendelea kuwa na Halmashauri ya Wilaya ya Musoma Vijiji ni. Maana yake ndio kusema kwamba Wilaya ya sasa ya Musoma itakuwa na Halmashauri tatu badala ya moja iliyopo sasa. Tunadhani kwamba huo ni mwanzo mzuri na tutakuwa tumezogezza huduma kwa wananchi wa Wilaya ya Musoma.

Na. 492

Ahadi ya Ujenzi wa Hospitali ya Kitomanga

MHE. SAID M. MTANDA aliuliza :-

Katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu 2010, Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga Hospitali ya Wilaya ya Lindi Kitomanga:-

- (a) Je, ni hatua zipi zimeanza katika mchakato wa ujenzi wa hospitali hiyo?
- (b) Je, ni fedha kiasi gani zinatarajiwa kutumika katika ujenzi huo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Said Mtanda, Mbunge wa Mchinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi inao mpango wa kupanua Kituo cha Afya cha Kitomanga kuwa na hadhi ya Hospitali ya Wilaya. Kwa kuzingatia hilo Halmashauri katika mwaka 2004/2005 – 2005/2006 iliidhinishiwa kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa Wodi mbili za wagonjwa pamoja na nyumba nne za watumishi na ukarabati wa jengo la Utawala ambalo limeshakamilika. Mwaka 2008/2009 Halmashauri ilipata shilingi milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la maabara ambalo limeshakamilika. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2010/2011, Halmashauri iliidhinishiwa shilingi milioni 250 kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara, kujenga chumba cha upasuaji, ujenzi wa Wodi mpya mbili ambapo Mkandarasi amekamilisha ujenzi wa msingi wa Wodi hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi imetenga katika Mpango wa Maendeleo kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya kujenga jengo la X-Ray.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika swalii langu la msingi sehemu (b) nilitaka kujua ni fedha kiasi gani kwa ujumla zitatumika katika ujenzi wa Hospitali hiyo. Kwa hiyo, majibu hayo hayako wazi. Lakini maswali mawili madogo ya nyongeza kwanza nilitaka kufahamu kwamba katika kipindi hiki 2010/2011, ambapo zilitengwa shilingi milioni 250/- hadi sasa vifaa vya maabara havijanunuliwa. Je, ni lini vifaa vya maabara vitanunuliwa?

Pili, kwa kuwa sasa hali ya Hospitali hiyo imeshaanza kuwa ya kuridhisha kuelekea hadhi ya kuwa Hospitali ya Wilaya, je, ni lini Madaktari wanaostahiki kuwa pale watapelekwa ili huduma zianze kupatikana eneo hilo hasa kwa wakazi wa Jimbo la Mchinga na Wilaya ya Lindi Vijiji?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimpongeze Mheshimiwa Mtanda anavyofuatilia kwa ukaribu sana maendeleo ya Jimbo lake la Mchinga. Katika maswali yake suala la kwamba mpaka inapokamilika tutakuwa tumetumia kiasi gani cha fedha si jambo unaloweza kujua leo kwa sababu kila siku kuna kuperomoka kwa shilingi, kuna kubadilika bei ya vifaa vya ujenzi na kadhalika. Kwa hiyo, inakuwa vigumu kusema kwamba mpaka tutakapomaliza tutatumia kiasi kadhaa. Suala la kununuliwa vifaa, hapa nataka niseme kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Lindi katika kikao chake cha tarehe 30/11/2007 ilipitisha azimio la kuomba Hospitali ya Misheni ya Nyangao kuwa Hospitali ya Wilaya na Serikali imetiliana mkataba na Wamisionari wanaoendesha

Hospitali ya Nyangao kuwa ndiyo Hospitali ya Wilaya ya Lindi. Sasa tunafanya nini pale Kitomanga?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Lindi ni kubwa ndiyo maana ina Majimbo matatu na hakuna Hospitali kubwa kwenye barabara ya kuelekea Dar es Salaam. Kwa hiyo, Serikali inafanya jitihada hizi ili tuwe na Hospitali inayoweza kuhudumia watu kwenye barabara kubwa kwenda Dar es Salaam kutokana na ajali na kadhalika. Kwa hiyo, kinachofanyika pale ni kuifanya Hospitali ifanane na Hospitali ya Wilaya lakini haitakuwa Hospitali ya Wilaya kwa sababu Sera ya Serikali ni kuwa na Hospitali moja tu katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa nya maabara, suala hili tutalifuatilia pamoja na Madaktari kama nilivyosema tunakaribia sasa kukamilisha, Madaktari watatafutwa na vifaa nya maabara vitanunuliwa kwa muda muafaka.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongenza. Kwa kuwa hali ya Hospitali ambayo Mheshimiwa Waziri ametoa majibu ya kupata Madaktari Bingwa, inafanana na swali langu. Je, Serikali sasa iko tayari kutupatia Madaktari Bingwa kwa Hospitali ya Wilaya ya Mafia kwani Wilaya ya Mafia ni Kisiwa na inakuwa vigumu wanawake na watoto wanapopatwa na matatizo kupata huduma ya haraka kwa sababu usafiri wa kutoka Mafia hadi kwenda Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ni zaidi ya wiki kwa kuwa wanatumia usafiri wa majini. Je, ni lini Serikali itatupatia Madaktari Bingwa kama walivoyutahidi kutupatia Daktari Bingwa wa *X-Ray*.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, tumelipokea ombi hilo na kwa sababu Sera zetu ni kwamba Madaktari Bingwa hawa tunawapeleka katika Hospitali za Mkoa ambazo nazo zinatoa huduma za rufaa lakini kwa sababu za kijiografia za Mafia ombi hilo tumeliangalia na namhakikishia Mheshimiwa Mbunge katika mgao wa Madaktari ambao tunategemea kuupanga mwezi wa Tisa au wa Kumi Wilaya ya Mafia tunategemea kupeleka Madaktari hao Bingwa.

Na. 493

Ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya Mpya

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Serikali ilitangaza Wilaya mpya kuititia Bunge la Tisa wakati wa Mkutano wa Bajeti zikiwemo Wilaya ya Ikungi na Mkalama kwa lengo la kusogea huduma kwenye jamii:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaanza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya hizi?
- (b) Je, ni lini uteuzi wa viongozi na watumishi katika Wilaya hizi utafanyika?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa wakati linajibowi swali namba 66 la Mheshimiwa Vicky Kamata, Mbunge wa Viti Maalum na swali namba 131 la Mheshimiwa Christina Mughwai Lissu kwamba uanzishaji wa Mkoa na Wilaya ya Utawala unatawaliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 2(2) na Sheria ya Taratibu ya Uanzishaji Mamlaka za Mikoa na Wilaya Sura 397. Kwa kuzingatia Sheria hizo mchakato wa kuanzisha maeneo hayo unazingatia hatua mbalimbali hadi kukamilika kwake ikiwemo Mheshimiwa Rais mwenyewe kuonesha nia ya kuanzisha maeneo hayo ambapo dhamira hiyo hutangazwa katika Gazeti la Serikali, uhakiki wa mipaka na kuwashirikisha wananchi wa maeneo

hayo kutoa maoni ya mwisho ambapo hupewa siku sitini kukamilisha kazi hiyo na kutoa tangazo la kuanzisha Wilaya hizo katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, fedha kwa ajili ya kujenga Makao Makuu ya Wilaya mpya za Ikungi na Mkalama zitatengwa baada ya kukamilika kwa taratibu za uanzishwaji wa maeneo hayo kisheria.

(b) Mheshimiwa Spika, uteuzi wa viongozi na watumishi wa Wilaya hizi utafanyika baada ya kukamilika kwa taratibu za kisheria za kuanzisha Wilaya hizi kama nilivyoeleza katika sehemu (a) ya jibu langu la msingi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuvute subira kwa kuwa nia ya Mheshimiwa Rais bado ipo na mara taratibu hizo zikikamilika Wilaya hizi zitaanza.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Dokta Parseko Kone ameandaa majengo ya kuanzia na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema mchakato bado unaendelea. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kuna kila sababu ya kuharakisha mchakato huu ili fedha ziweze kutolewa ukarabati wa majengo haya ya kuanzia uanze kufanyika?

Swali la pili, kwa kuwa maeneo yaliyotengwa na Mkoa ya kujenga Wilaya zote hizi mbili Wilaya ya Ikungi na Wilaya ya Mkalama yana mashamba ya wakazi wa vijiji hivyo. Je, Serikali itakuwa tayari kuwafidia wamiliki wa mashamba hayo ili kuepusha migogoro ambayo inaweza kujitekeza wakati wa kuanza ujenzi wa Wilaya zote mbili?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza maelezo kwamba majengo ya kuanzia yapo tayari tuharakishe niseme huu ndiyo utaratibu utakavyokuwa katika Mikoa na Wilaya zote. Hatutakuwa na uwezo wa kusema tukamilishe kujenga jengo halafu ndiyo Wilaya ianze. Dhahiri tutaanza katika maeneo ya muda, nakumbuka Mkoa wa Mfano wa Rukwa ulipoanza Makao Makuu ya Mkoa yalianzia Kantaramba Sekondari. Kwa hiyo, niseme hoja ya msingi ni kupata Wilaya, tutajenga, tayari tumeshapata Wilaya. Lile la kuharakisha lipo ndani ya uwezo wetu pale TAMISEMI. Mkuu wa nchi atakapotamka kwamba Wilaya fulani ianze siku fulani zitaanza.

Mheshimiwa Spika, suala la mashamba ya wakazi. Nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni. Huwezi ukakuta shamba la mtu ukasema hapa najenga Makao Makuu ya Wilaya kwa sababu mimi ni Serikali hutapewa kitu, hapana. Ikitokea tumechukua shamba la mtu kwa nia ya kuweka Makao Makuu ya Wilaya, Sheria za nchi zinataka tumfidie.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa ni mwaka mmoja sasa unapita tangu Serikali itangaze nia yake ya kuanzisha Mikoa mipyä minne, Halmashauri za Wilaya pamoja na miji na kwa kuwa Waziri Mkuu alishawahidi kulitolea tamko suala hilo hapa Bungeni. Je, mpaka sasa Mheshimiwa Waziri awaeleze Watanzania hatua hiyo imefikia wapi kuelekea Makao Makuu kupata Wilaya mpya?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, nataka nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwamba kule Mbozi na wao wamo katika kupata Wilaya mpya na ameuliza hili kwa sababu yeye ni mdau kule kwake, anategemea kupata Wilaya, nimpongeze katika hilo. Niseme tu kwamba maelezo yangu kama nilivyoeleza katika jibu la msingi. Ukitaka kuanzisha Wilaya na Mikoa yapo mambo mengi yanahuksika ndani yake. Lakini moja linachukua muda sana ni kuchora mipaka ya Wilaya au Mkoa. Lazima ueleze Mkoa huu mpaka utakuwa jiwe fulani, digrii fulani kushoto, inachukua muda kidogo. Nasema kazi hiyo imetuchukua muda tumeikamilisha na niwaahidi kwamba, tupo katika hatua za mwisho shughuli hii tutaikamilisha.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameleeza hapa Bungeni hivi punde kwamba ili kuanzisha Wilaya ni lazima kutambua mipaka yote ya Kata kujua mipaka inapita wapi na kwa kuwa Wilaya ya Songea ilipoanzishwa mipaka inatambua sasa hivi mchakato wa

kuanzisha Mji mdogo wa Madaba. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri je, ni hatua gani sasa imefikiwa katika kuanzishwa huo Mji Mdogo wa Madaba?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama Mbunge wa Peramiho, kwa jinsi anavyofuatilia kwa ukaribu sana kupatikana kwa Mji wa Madaba. Nadhani kila fursa anayoipata hapa ndani anazungumzia Mji Mdogo wa Madaba. Niseme kwamba baada ya kusikia kilio cha Mheshimiwa Mbunge wakati tunajadili Bajeti ya Waziri Mkuu, Ofisi yangu inatuma wataalam kwenda Itigi kule Manyoni ambako umeombwa Mji Mdogo pamoja na Madaba ili kazi hiyo ya mipaka na nini lazima ifanyike ili muda muafaka ukifika tutaifanya Madaba kupata hadhi ya Mamlaka ya Mji Mdogo.

Na. 494

**Fedha Zinazopatikana kwa Kuweka Mlio wa Wimbo
Kwenye Simu ya Mkononi**

MHE. VITA R. KAWAWA aliuliza:-

Simu za mkononi zinatumia baadhi ya milio ya nyimbo za wasanii wetu na pindi mtu anapopiga simu anaambibiwa abonyeze alama ya nyota kwenye simu yake ili achague wimbo anaoutaka uingizwe kwenye simu yake lakini anakatwa kiasi fulani cha pesa:-

(a) Je, Serikali katika makato hayo inafahamu ni kiasi gani wasanii wanafaidika na makato hayo?

(b) Je, Serikali inapata kiasi gani cha kodi kwenye makato hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Makampuni ya Simu nchini hununua nyimbo za wasanii kutoka makampuni yanayosambaza kazi za wasanii hao. Hivyo, Makampuni ya Simu hulipa gharama zinazotokana na tozo hizo kwa makampuni yaliyopewa haki ya kununua na kuuza kazi za wasanii. Hata hivyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa Wizara yangu inawasiliana na Wizara ya Habari, Vijana na Utamaduni na Michezo ambayo inaratibu shughuli za haki miliki za wasanii nchini ili kuweza kufahamu kwa kiasi gani wasanii wanafaidika kutokana na nyimbo zao kutumika katika simu za mkononi.

(b) Mheshimiwa Spika, mapato yanayokusanywa na Makampuni ya Simu kutokana na watumiaji wa simu za mkononi kuingiza nyimbo katika simu zao ni sehemu ya mapato yanayotokana na huduma zingine kama vile za kupiga simu, kutuma ujumbe mfupi wa maneno na huduma za intaneti ambayo yote kwa pamoja hutengeneza mapato ya jumla ya Makampuni hayo ya Simu ambapo Serikali kuititia Mamlaka ya Mapato (TRA) hukusanya mapato hayo kulingana na viwango vya kodi ya mapato kwa wakati husika.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kwa sasa kila huduma katika simu za mkononi hukatwa fedha ni zaidi ya hizi alizozitaja Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, Serikali ina *mechanism* ya kutosha ya kutambua makato yote yanayokatwa na Makampuni haya ya Simu ili kuweza kukatwa kodi na kujazia katika Mfuko Mkuu wa Serikali?

Pili, kwa kuwa biashara hii ya simu za mkononi ina wateja wasiopungua milioni 16 na kama Serikali inao uwezo huo wa kutambua hizo *transactions* zote na je, inaweza kuja kila baada ya miezi mitatu kutwambia imekusanya kiasi gani cha fedha?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, Serikali inakusanya mapato kutoka Makampuni ya Simu kwa kutumia *TRA*. *TRA* ina uwezo wa kuweza kukagua vitabu yva Makampuni yote ya Simu ili kujua makampuni haya yanaingiza mapato kiasi gani na kuyatoza kodi. Pamoja na hayo Serikali ina mpango wa kuweka mitambo mingine ambayo itaweza kuangalia kwa namna gani makampuni haya *transactions* zote zinapita katika makampuni haya. Kwa hiyo, tuipe muda Serikali ijpange na ifanye utafiti wa kutosha kuweza kuweka mitambo hiyo ambayo itaweza kuangalia namna ambavyo makampuni haya yanapata mapato yake.

Sehemu ya pili, kwa kuangalia taratibu zilizopo Serikali hutoa taarifa ya mapato na matumizi kila mwaka kulingana na taratibu zilizopo. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali siku zote inatoa taarifa ya mapato na matumizi yake kulingana na taratibu zilizopo.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa simu za mikononi sasa hivi zinatumika kama *mobile bank* kwa mfano *M-Pesa*. Je Serikali inakata tozo yoyote kutohana na huduma hiyo ya kibenki?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la nyongeza huduma za kutuma fedha kama *M-Pesa* ni moja kati ya huduma ambazo zinaingizia mapato Kampuni za Simu, kwa hiyo, zinajumuishwa katika mapato yake ya jumla na kodi hutozwa kulingana na mapato yote yanayopatikana kwa kampuni hizo.

Na. 495

Kiwanda cha Kubangua Korosho –Kibaha

MHE. SILVESTRY F. KOKA aliuliza:-

Kiwanda cha kubangua korosho cha *TANITA* kilichopo Kibaha hakifanyi kazi na kimeota magugu kinyume cha njia bora ya Serikali kuleta ubinafsishaji kufufua viwanda:-

- (a) Je, ni nani mwekezaji au mmiliki wa kiwanda hicho kwa sasa?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kiwanda hicho kinachochaea kilimo cha korosho na kuinua ajira na uchumi wa Kibaha na wananchi wake?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Kubangua Korosho cha *TANITA* kilichopo Kibaha kilibinafsishwa kwa Kampuni ya *Safa Petroleum and Mineral Company Limited* kwa mkataba uliosainiwa tarehe 16 Machi, 2005.
- (b) Mheshimiwa Spika, kabla ya ubinafsishaji, Bodi ya Korosho ilikuwa imekodisha Kiwanda cha *TANITA* kwa Kampuni ya *M/S Harom International Limited* ambaye alifungua kesi Mahakamani ikidai ipewe kipaumbele kuuziwa kiwanda kwa kuwa kampuni ilikuwa mkodishaji jambo ambalo halikuwa la msingi. Taarifa niliyonayo ni kwamba, kesi hiyo sasa imekwisha. Wizara yangu sasa itamfutilia mwekezaji *Safa Petroleum and Mineral Company Limited* ili afanye ubanguaji wa korosho kulingana na mkataba wa ubinafsishaji vinginevyo akikaidi atachukuliwa hatua za kisheria.

MHE. SYLVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa sasa kiwanda hiki kilishapata mwekezaji; na kwa kuwa wafanyakazi wao wapatao 567 waliahidiwa kwamba punde kiwanda kitakapopata wawekezaji, watapata kipaumbele cha kuendelea na ajira. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba mwekezaji huyu anaendelea kuwarudisha wafanyakazi hawa katika ajira yao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa wafanyakazi hao 567 bado wana madai yao mbalimbali toka mwaka 1997 na hadi leo hii hawajakamilishiwa madai yao. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wafanyakazi hawa wanalipwa mafao yao sawasawa kabla mwekezaji hajaanza kazi yake ipasavyo katika kiwanda hiki?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa tumemala mgogoro ule na kiwanda kinatakiwa kifanye kazi, habari ya wafanyakazi, matatizo walijokuwa nayo yatashughulikiwa kwa mujibu wa sheria za ajira. Tutashirikiana na kampuni ile, tutashirikiana na Wizara ya Kazi inayohusika kuangalia haki za wafanyakazi hao ambazo zimelindwa au zilivyo na kwa hakika kwa vyovoyote vile hatutawadhulumu.

Mheshimiwa Spika, tutakachokifanya ni kufuata tu sheria za ajira na haki za wafanyakazi zinalindwa namna gani. Naomba awe na subira, Serikali itazishughulikia.

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba wafanyakazi wa Mbarali *NAFCO* na Kampunga *NAFCO*, wanadai madai yao ya kulipwa fidia baada ya mashamba hayo kubinafsishwa bila mafanikio. Wamefika mpaka Mahakamani, Mahakama imeamuru walipwe, lakini mpaka sasa bado hawajalipwa. Je, Mheshimiwa Waziri atanihakikisha kwamba atasaidia kuhakikisha wananchi hawa wanapata haki zao?

SPIKA: Haya, swali lingine kabisa! Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, nilikuwa Mbarali takriban wiki tatu zilizopita, sikuongea na wafanyakazi, lakini niliweza kupata malalamiko ya wafanyakazi walioko pale. Ninachowea kusema tu ni kwamba, suala la wafanyakazi pale, kama bado wana matatizo ambayo hayajakamilika, nalo tutalishughulikia. Najua wana matatizo mengi zaidi ya hilo, ikiwa ni pamoja na mashamba ambayo walitaka yashughulikiwe. Kwa bahati nilimwambia hata Mheshimiwa Kilifi kwamba nilipokuwa kule nimetoa ahadi ya Serikali kwamba wananchi wote waliokuwa katika shamba lile, tumetoa ahadi, Serikali imetoa shilingi milioni 500, tuwatengenezee mashamba ya umwagilaji pemberi, wakati matatizo mengine yanashughulikiwa na Serikali. Kwa hiyo, naomba pia Mheshimiwa Kilifi naye awe na subira. Lakini wakati wanasubiri hili tatizo lao la wafanyakazi, wafanyakazi wale *followback position*, kupata maeneo mengine tumelishughulikia tayari.

Na. 496

Mfumo wa Stakabadhi kwa Zao la Pamba

MHE. AUGUSTINO M. MASELE aliuliza:-

Bei ya zao la pamba nchini imekuwa haitabiriki ambapo Serikali ikitoa bei elekezi ambayo ni ya chini sana na kutoa mwanya kwa wafanyakabiashara wa zao hilo kununua kwa bei ndogo kisha wao kuuza kwa bei kubwa na kupata faida zaidi ya wakulima ambao hubaki maskini na hivyo kutishia uzalishaji wa zao hilo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mfumo wa stakabadhi ghalani ambao utawalinda wakulima wa zao la pamba wasiendelee kupunjwa na wachuuzi wanaolangua pamba?

(b) Je, kuna ukweli wowote kuwa Benki ya *NMB* ina mpango wa kudhamini mfumo wa stakabadhi ghalani?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mbunge wa Mbogwe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, bei ya pamba hapa nchini inatawaliwa na mwenendo wa bei katika Soko la Dunia. Kwa lengo la kulinda maslahi ya wakulima wa pamba, Serikali imeweka utaratibu wa wadau kukutana kabla ya msimu kuanza na mara bei zinapobadilika ili kuweka bei dira. Bei dira maana yake ni nini, ni bei ambayo mnunuzi haruhusiwi kununua chini ya bei hiyo. Mfumo wa stakabadhi ghalani ulianza kwenye mazao ya pamba na kahawa, lakini haukuonesha mafanikio kwa upande wa zao la pamba kutokana na kudorora kwa ushirika wa pamba, kwa sababu ufanisi wa mfumo huo hutegemea kwa kiwango kikubwa, uimara wa Vyama vya Ushirika. Ili mfumo huo umnufaishe moja kwa moja mkulima, ni muhimu wakulima kuijunga katika Vyama vya Ushirika imara ambavyo vina uwezo wa kukopesheka.

Mheshimiwa Spika, mkakati uliopo ni wa kuhamasisha wakulima kuunda vikundi vya wakulima ambavyo kwa kuanzia vitasajiliwa kama *pre-cooperatives* kwa lengo la kuimarisha ushirika katika ngazi ya chini. Baada ya vikundi kuimarika na kuingia kwenye Vyama vya Msingi, dhamira ya Serikali ni kuanzisha mfumo wa stakabadhi ghalani katika zao la pamba. Pamoja na kuwa na Vyama vya Ushirika, ili mkulima apate faida ni muhimu kuwepo na viwanda vitakavyomwezesha mkulima kuchambua pamba yake ili aweze kuza nyuzi na mbegu badala ya kuza pamba ambayo haijachambuliwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani, wakulima wameweza kujipatia mikopo kutoka Benki za *NMB*, *CRDB* na *KCB*. Kwa mfano, katika msimu wa 2009/2010, *NMB* ilitoa shilingi bilioni 20.66 na kuongeza hadi shilingi bilioni 42.9 katika msimu wa 2010/2011 hasa katika zao la korosho. Kwa hiyo, ni kweli kwamba *NMB* inadhamini mfumo wa stakabadhi ghalani.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kumuuliza Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa zao la pamba linasimamiwa na Bodi ya Pamba hapa nchini Tanzania; lakini kwa bhati mbaya sana inaonekana kwamba Bodi ya Pamba imeshindwa wajibu wake, badala yake inaonekana kwamba inafanya kazi ya uwakala wa wanunuzi wa zao la pamba. Nasema hili kwa sababu...

SPIKA: Naomba upunguze, usitupigie hotuba maana unasema peke yako! Malizia swalı ni nini sasa!

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Nataka kuiuliza Serikali, ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima kuondokana na Bodi ya Pamba kuwa inawapangia bei kwa sababu, bei iliyopangwa sasa hivi ilikuwa ni 1500/= na 1100=/. Baada ya wafanyabiashara kuona....

SPIKA: Mheshimiwa, uliza swalı ndipo tutakuelewa, maana ukizunguka sisi wenzio hatukuelewi pia. Uliza, swalı lako nini?

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Nataka kuuliza kwamba Bodi ya Pamba sasa imefikia wapi kuhusu suala la bei ya pamba ambayo sasa hivi hajilikanı ni shilingi ngapi? (*Makofı*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Pamba haikupanga bei ya pamba. Bei lengwa ya pamba ilipangwa na wadau wa pamba na bei hiyo ilipangwa kutegemeana na bei ya pamba duniani. Bei ya mwanzo ya pamba ilipokuwa inapangwa tarehe 9 Juni, bei ya dunia ya pamba ilikuwa Dola 1.54 za Kimarekani. Baadaye bei hiyo ilishuka mpaka hata ilifikia Dola 1.08. Kwa hiyo, hakuna kitu ambacho Bodi ya Pamba ingefanya kuzuia pamba hapa kwenye soko letu ibakie katika lengo lile lililokuwa limewekwa awali. Hata hivyo, bei ya pamba sasa imeanza kupanda na katika Wilaya nydingi ikiwemo Wilaya

ya Bariadi, Bunda, Musoma, Maswa, wanunuzi sasa wananunua kwa bei kati ya shilingi 1,000 kwa kilo mpaka 1,100/= kwa kilo.

SPIKA: Swalii la nyongeza lingine! Mheshimiwa Suleiman Nchambi! Nampongeza kwa kupata watoto mapacha, wa kiume na wa kike. (*Makofii/Kicheko*)

MHE. SELEIMAN M.N. SULEIMAN: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa awali, wakulima wa pamba waliuza pamba yao kwa kati ya bei ya shilingi 1,100 iliyopangwa na Bodi ya Pamba na baadaye wengine wakauza kwa 800 na sasa 1,100; Je, Serikali iko tayari kufidia wakulima waliouza pamba ile kwa shilingi 800 ili wao wanufaikie kama waliouza kwa shilingi 1,100?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, swalii hili lina maeneo mawili, wapo wakulima ambao wadau walipopanga bei ya shilingi 1,100 kwa kilo, walikopesha pamba yao kwa wanunuzi kwa makubaliano kwamba watalipwa shilingi 1,100. Serikali itasimamia walipwe haki yao ya makubaliano ya shilingi 1,100 kwa kilo. Aidha, baada ya bei ya soko kushuka, wako wakulima ambao waliuza pamba yao katika bei ambayo ilikuwa sokoni ambayo ni chini ya shilingi 1,100 na hiyo ni bei ya soko ambayo Serikali haiwezi kuwafidia wakulima hao.

Na. 497

Barabara za Jimbo la Manyovu

MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

Barabara ya Lami ya kilomita nne inatoka Mnanila kuelekea Burundi na kuacha eneo lingine kutouunganishwa:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha barabara ya kiwango cha lami kutoka Mnanila kuititia Buhigwe mpaka Kasulu Mjini?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuipandisha hadhi barabara ya Heru Juu – Muyama (Tarafa) ili ihudumiwe na Serikali Kuu?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Albert O. Ntibaliba, Mbunge wa Manyovu lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara ya Mnanila (Manyovu) kuititia Buhigwe hadi Kasulu Mjini, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti, haiwezi kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali kuititia Wakala wa Barabara itaendelea kuifanya matengenezo kwa kiwango cha changarawe ili iweze kuitika wakati wote.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Barabara Na.13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009 imeweka utaratibu wa kuziweka kwenye madaraja stahili barabara zote nchini. Namshauri Mheshimiwa Mbunge afuate utaratibu uliopo kwenye sheria ikiwa ni pamoja na kuitisha maombi kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa (*Regional Roads Board*).

MHE. ALBERT O. NTIBALIBA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri kabisa. Lakini, kwanza nitumie nafasi hii kuipongeza Wizara ya Ujenzi na Serikali nzima kwa kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Manyovu kwenda Mwandiga. Lakini, vile vile nimpongeze kwa kutambua umuhimu wa barabara hii ya kutoka Mnanila kuititia Wilaya mpya ya Buhigwe mpaka Kasulu ambayo sasa barabara hii umuhimu wake unaunganisha barabara inayotokea Burundi kuititia Kasulu, Nyakanazi kwenda mpaka Rwanda, Kenya kwenda Mwanza. Kwa hiyo, sasa hivi biashara pale imekwishakuwa kubwa na kwa kuwa Wizara imetambua huo umuhimu na imesema kwamba fedha ni kidogo, naiomba Serikali kwa umuhimu huo, itafanyaje na kwa uharaka upi ili fedha ziweze kupatikana ili barabara hiyo iweze kujengwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza, tunapokea pongezi alizotupa Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya barabara ya Manyovu-Mwandiga. Lakini, vile vile kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, Serikali inaungana naye kabisa kutambua umuhimu wa barabara ya Mnaniila kwenda Buhigwe-Kasulu. Siyo tu kwamba inaunganisha na barabara ya kwenda nchi jirani, lakini vile vile ujenzi wa barabara hii utafungua fursa za kiuchumi za Wilaya mpya ya Buhigwe na vile vile ni barabara ambayo ni fupi hata kwa wananchi wanaotaka kuelekea Mwanza na sehemu zingine.

Mheshimiwa Spika, tatizo letu kama nilivyosema ni ufinyu wa bajeti na Serikali haitaacha kuangalia *possibilities* hapo baadaye, maana hii ni bajeti ya kwanza tu, lakini bajeti ijayo tunaweza tukaanza kuangalia *possibility* ya kutenga pesa, lakini siyo sasa.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Rais alipokuwa na ziara Mkoani Kigoma alikubali ombi la wakazi wa Jimbo la Kigoma Kusini la kuanganisha barabara ya kilomita 48 ambayo ilikuwa inaanzia Malagarasi kwenda Nguruka na ile ya Kidago kwenda Uvinza, ambapo katikati ilibaki kama kilomita 50. Mheshimiwa Rais kwenye mkutano wa hadhara alikubali ombi ile mbele ya Balozi wa Abudhabi na Balozi alipitisha ombi ile mbele ya mkutano wa hadhara. Naomba kujua *status* ya jambo hili imefikia wapi kutoka Serikalini?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa swalii la msingi ilikuwa la barabara ya kutoka Manyovu kwenda Kasulu yenye jumla ya kilomita 42. Swalii alilolichomekeea Mheshimiwa Kafulila ni la kutoka Kigoma kuelekea Uvinza hadi Malagarasi. Lakini, napenda tu nitoe taarifa kwa Mheshimiwa Kafulila na wananchi wa eneo la Kavilamimba ambapo Mheshimiwa Rais alipokuwa kule alitoa ahadi. Ni kweli Mheshimiwa Rais alitoa ahadi na hatua za kuhakikisha kwamba barabara hiyo na hasa zile kilomita 50 zinatengenezwa kuanganisha kwenye eneo ile la Uvinza hadi Malagarasi ziko kwenye *process* na tumekwishaandika barua na huu ni utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi ambapo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. (*Makofii*)

Na. 498

Hali ya Zahanati Nchini

MHE. MHONGA S. RUHWANYA aliuliza:-

Ingawa Serikali imeahidi ujenzi wa Zahanati katika kila Kijiji nchini, lakini Zahanati zilizopo hazina huduma zinazostahili kwa sababu zina uhaba wa watumishi, vifaa vyta maabara, dawa na kadhalika

Je, Serikali haioni kuwa ni vema kuimarisha na kuboresha kwanza Zahanati zilizopo kabla ya kujenga nyingine mpya?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi hususan akinamama wajawazito hapa nchini wanapoteza maisha kutohana na kukaa mbali na huduma za afya zikiwemo Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali imeweka mkakati wa kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Katika mpango huu, Serikali imeanza ujenzi wa Zahanati katika kila Kijiji, Kituo cha Afya, kila Kata na Hospitali ya Wilaya katika kila Wilaya hapa nchini ili kuhakikisha kila mwananchi anapatiwa huduma za afya karibu na mahali anapoishi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mpango huo, Serikali inaendelea kuboresha Zahanati zilizokuwepo ili ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na kuongeza watumishi, vifaa na dawa. Serikali imefanya juhudhi za makusudi katika kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojunga na fani mbalimbali za afya kwa kupanua na kukarabati vyuo kwa lengo la kuongeza udahili wa wanafunzi katika mafunzo ya ngazi ya Cheti, Stashahada, Shahada na

Uzamili. Kutokana na jitihada hizi, kumekuwa na ongezeko la wadahiliwa kutoka 1,013 mwaka 2005/2006 hadi 6,713 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, napenda pia ielewewe kuwa Vijiji ambavyo vina Zahanati za Mashirika ya Dini, binafsi, Serikali haitajenga Zahanati nyingine bali itahakikisha Zahanati hizo zinatoa huduma kwa wananchi kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Serikali.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na mpango huo wa ujenzi wa zahanati na kuboresha zile ambazo zipo, lakini pia Hospitali za Mikoa na zile za Rufaa zinakabiliwa na matatizo kama hayo ikiwemo Hospitali ya Mkoa wa Kigoma haina Madaktari Bingwa na vifaa vya kupimia hakuna. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuweka mkakati maalum wa kuboresha hospitali hizo za Rufaa na za Mikoa?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli hospitali zetu za mikoa zinakabiliwa na matatizo na changamoto mbalimbali ikiwemo Madaktari Bingwa pamoja na vifaa. Hili tumeliona na katika bajeti yetu iliyopitishwa na Bunge hili, tumeonesha ni namna gani tunaweza tukakabiliana na tatizo hili, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mhonga na wakazi wa Mkoa wa Kigoma hasa Hospitali ya Kigoma tumeliona tatizo hilo, ni moja ya hospitali ambayo nimeelekeza kupeleka Madaktari Bingwa kwa sababu kuna uhaba mkubwa sana wa Madaktari hao katika hospitali hiyo.

Na. 499

Serikali Kupunguza Bei ya Uzalishaji wa Gesi

MHE. JOHN J. MNYIKA (K.n.y MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY) aliuliza:-

Umeme wa gesi asilia kuwa nishati mbadala ya umeme unaofuliwa kwa mitambo inayotumia mafuta ya diseli na ule unaotokana na nguvu ya maji (*Hydroelectric power*) ili kupunguza matumizi ya mkaa unaotengenezwa kwa kukata miti mingi:-

Je, kwa nini Serikali isitoe ruzuku kwa wazalishaji wa gesi ili bidhaa hiyo ipatikane kwa bei nafuu ili kushawishi watu kutumia umeme wa gesi asilia zaidi majumbani badala ya mkaa na kunusuru misitu yetu?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, lakini kabla ya hapo kwa ridhaa yako naomba nitoe maelezo kidogo kwa swali liliolulizwa jana la Mheshimiwa Lekule Laizer.

Mheshimiwa Spika, jana wakati najibu swali kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Lekule aliulizia upatikanaji wa umeme katika maeneo ya Longido, katika majibu yangu nillelekeza majibu yangu ambayo yalikuwa yanaelekea kujibu matatizo au hoja zilizopo za kupeleka umeme Loliondo kwa Mheshimiwa Ole Telele, naomba nimwombe msamaha Mheshimiwa Lekule kwa mchanganyiko ule.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Longido hakuna umeme wa jenereta, umeme ule unatoka Kenya, lakini mkakati bado upo wa kusambaza umeme pale na kazi zinaendelea pamoja na maeneo yale mengine ya Longido, Oldonyo Sambo na kwingineko. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Lekule kwamba kazi inaendelea lakini siyo umeme wa jenereta, ni umeme wa gridi ule ambaa tuna *inter connector* kutoka Kenya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda, kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay Mbunge wa Mbulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi sasa ufuaji wa umeme unaoingia katika gridi ya Taifa kwa kutumia gesi asili unafikia kati ya asilimia 35 na 45 kwa siku. Serikali sasa imeamua kutekeleza miradi mipyä ya ujenzi wa Bomba la gesi kutoka Mnazi Bay hadi Dar es Salaam kuititia Songo Songo kwa madhumuni ya kuunganisha rasilimali hii na hivyo kutumia kufua umeme, Mtwara *Megawatt* 300, Somanga Fungu *Megawatt* 230, Dar es Salaam pamoja na mitambo iliyopo sasa ya dharura ambayo baadaye itabadiishiwa kutumia gesi. Hii ni kwa ajili ya kukabiliana na matatizo ya upatikanaji wa umeme na gesi kwa ajili ya magari, majumbani, viwandani, mahotelini na kwenye taasisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mantiki ya kupunguza mzigo wa bei za gesi kwa mtumiaji wa umeme, ilioita tamko Na. 246 kusamehe kodi, ushuru au malipo ya aina yoyote kwenye gesi asili na miundombinu inayotumika kuitisha gesi katika Wilaya za Kilwa, Rufiji, Mkuranga, Temeke, Ilala na Kinondoni. Serikali pia itaanizisha Mfuko wa kuendeleza nishati ya umeme ambao utatumika kama mtaji (*equity*) wa kuendeleza uwekezaji katika sekta ya umeme na hivyo kuwa ni kivutio kwa wadau wanaotaka kuwekeza kwenye sekta hiyo kutoka kwenye sekta binafsi. Aidha, kuwepo kwa Nishati utasidia kuwekeza zaidi katika miradi ya umeme na nishati mbadala, *electricity and renewable energy* ili kuboresha upatikanaji wa nishati zinazowenza kutumika majumbani badala ya mkaa unaotokana na miti na mwanga unaopatikana kwa matumizi ya koroboi na mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia kwa kushirikiana na *REA* na taasisi zingine inahamasisha matumizi ya gesi kwenye mitungi kama chanzo cha nishati majumbani kitokanacho na gesi (*LPG*) kwa ajili ya matumizi ya jikoni na taa. Mikakati iliyopo, ni kupunguza gharama za upatikanaji vifaa husika ili kuhamasisha matumizi ya vifaa hivi badala ya mkaa na taa za koroboi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa matumizi ya gesi asili ndio suluhisho la dharura la kupunguza gharama za maisha kwa wananchi ambayo inachangiwa na kupanda kwa mafuta kwenye soko la dunia na kwa kuwa sasa hivi tunavyozungumza kwa Dar es Salaam ni kituo kimoja tu Ubungo ndicho kinachouza gesi kwa matumizi ya magari na sehemu kubwa ya wananchi majumbani wanatumia gesi ya mitungi kutoka nje ya nchi, je, Serikali ipo tayari kuongeza pesa kwa shirika la *TPDC* kwa dharura ili kuongeza kasi ya kuhakikisha gesi inatumika kwenye magari pamoja na gesi ya ndani itumike majumbani kwa kujenga kiwanda cha (*LPG*)?

Mheshimiwa Spika, swalí la pili, kwa kuwa, sasa hivi tunavyozungumza mgawo wa umeme unaendelea kwa kiwango kikubwa Dar es Salaam na maeneo mengine tofauti na kauli ya Serikali ilioitoa hivi karibuni. Je, Serikali inatoa kauli gani hivi sasa ya kushughulikia jambo hili?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza tukubaliane, tulichosema kwenye matumizi ya gesi asilia hapa, swalí la Mustapha Akunaay lilikuwa linarejea kwenye kutafuta namna ambayo matumizi ya gesi yanaweza kuelekea nyumbani. Katika hili kwa ajili ya lengo la kupunguza gharama za matumizi ya gesi, Serikali imelizungumzia hili mara kwa mara na tumesema hatuwezi kuingia kwenye uwekezaji kila kitu sisi wenyewe. Kwa sasa hivi mradi ambao nadhani unaweza ukatupelekea kwenye kufikisha gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani ni mradi wa *LPG Extraction*, tumeshausema hapa, hii gesi badala ya kuileta kutoka nchi za nje tutaizalisha wenyewe kwa gesi ile inayokwenda kwenye umeme na mabaki yake kwa maana inayotumika kwenye *LPG extraction* itumike kwenda kwenye mitungi.

Mheshimiwa Spika, ni mradi ambao una thamani ya kama dola milioni 40, *TPDC* wameshautolea matangazo na wawekezaji mbalimbali wamejitekeza nadhani kwa sasa hivi huo ndio mgogoro, lakini huo ndio ufumbuzi wa tatizo hilo. Tukiweza kuzalisha *LPG* kwa gesi yetu wenyewe halifu upande wa pili Serikali ikaiondolea kodi ile mitungi, kitu ambacho ndicho tunachokusudia kufanya, tutahamasisha watu kununua mitungi lakini na gesi yenywewe itapatikana kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni jambo ambalo linafanyiwa kazi, lakini kwa sasa hivi mbali ya kupunguza bei ya mitungi tunaona tunguze

gharama ya *LPG* yenyewe kwa sababu gesi sisi tunayo. Lakini ni lazima tuwe na uzalishaji wa hiyo *LPG*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuanzisha kituo cha kuzalisha kuweka kwenye magari nakubaliana na wewe. Tumesema humu ndani kwamba, ni lazima kuwe na vituo zaidi, huwezi mtu ukawa uko Mbagala kituo ni kimoja tu, mpaka uje Ubungo, ujaze urudi tena Mbagala, tukiwa na vituo kama sita au saba Dar es Salaam inaweza ikasaidia tunalfanyia kazi lakini pia na wingi wa magari uwepo. Sasa hivi kuna magari machache mno kwa kuwa na vituo kama nane au tisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mgawo wa umeme...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri pamoja na Muhimbili Hospitali, Dar es Salaam kutokuwa na umeme hivi sasa. Muhimbili hakuna umeme hakuna maji, jibu kwa pamoja.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, wakati tulipokuja hapa wiki iliyopita tatizo lilikuwa kwenye upatikanaji wa gesi Dar es Salaam na upatikanaji wa mafuta. Sasa hivi tumejiwekea utaratibu ambapo tunapata taarifa za mara kwa mara kila asubuhi kuhusu nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, kulingana na yale yaliyopatikana leo asubuhi, tunajua kwamba jana tulikuwa na matatizo grid ilitoka kidogo usiku na kwa maana hiyo maeneo mengi yalingia kwenye giza na baada ya mafundi wa *TANESCO* waliporudisha grid ndani ya dakika 45, maeneo mengine bado yakabaki chini. Kuhusu suala la Muhimbili naomba nikalifuatilie kwa sababu kwa upande wa Dar es Salaam mgawo uliokuwepo jana ulikuwa ni wa megawati 150 na ukiwa na mgawo wa megawati 150 kwa utaratibu wa kugawa kwenye maeneo maalum ya Dar es Salaam Muhimbili haiwezi kukosa umeme. Kwa maana hiyo, kwa umeme kidogo utakaokuwepo ni lazima Muhimbili na maeneo mengine kama hospitali za Temeke ni lazima zipate umeme ndiyo utaratibu tuliojiwekea. Kama umeme hakuna Muhimbili ina maana kuna tatizo lingine lakini siyo la uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee na tutajua tatizo hilo na tutalitolea taarifa.

SPIKA: Ahsante, Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha. Muda hautoshi kabisa na Wizara inayokuja ina wachangiaji wachache na inabidi tumalize leo kwa hiyo naendelea.

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni waliopo hapa.

MBUNGE FULANI: Taarifa

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge naomba ukae, wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 50 kutoka shule ya Sekondari ya Viwandani, wapo wapi wasimame walipo, ahsanteni, karibuni sana na msome kwa bidii. Tuna wanafunzi 25 wa Kidato cha Nne kutoka shule ya *Star Evening Class programme* Dodoma wengine walikuja jana na wengine wamekuja leo, wasimame mahali walipo, ahsanteni sana, msome kwa bidii hata kama ni *evening programme*.

Waheshimiwa Wabunge tunao viongozi 20 wa Wanawake wa Kanisa la Biblia, eneo la Dodoma wapo wapi wasimame, ahsanteni sana na tunawashukuru sana. Tunao wanafunzi 50 na Walimu wao kutoka shule ya sekondari ya Ng'ong'ona, Dodoma, karibuni sana. Tuna wanafunzi sita kutoka shule ya msingi Ubembeni, Kondo wakifuatana na Walimu wao naomba wasimame, ahsanteni, karibuni sana na msome kwa bidii. Wageni wengine walitambulishwa jana.

Mheshimiwa John Mnyika, Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anawatangazia Wabunge wa CHADEMA kwamba, saa saba na robo mchana leo kutakuwa na kikao chao katika ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge ofisi inatangaza kwamba kuna nyaraka muhimu zifuatazo zitagawiwa kwa Wabunge wote. Hizi ni Taarifa za utekelezaji wa ahadi za Serikali Bungeni kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, halafu kuna taarifa ya Haki za Binadamu kwa mwaka 2010, *The*

Tanzania Human Rights Report 2010, nyaraka hizi zitagawiwa. Kwa hiyo, mhakikishe mnazo kama mnapenda kuwa nazo.

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema leo hii tuna kazi nyingi kuliko muda tulionao na yote haya yametokea kutokana na matatizo tuliyokuwa nayo kwa hiyo kila kitu tumekibana mahali pamoja. Ndiyo maana taarifa zingine tunazikataa na kama ni ya muhimu, naomba uniandikie hapa nitajua kwamba nifanye nini.

Ilikuwa nimpe nafasi Mheshimiwa Machali kuhusu suala la Muhimbili, kwa hiyo naomba Waziri akatafute taarifa na aturudishie habari sasa hivi, kwa sababu Muhimbili nasikia wanaanza kutumia kibatari, maji hayaendi hospitali kwa sababu ya ukosefu wa umeme.

Waheshimiwa Wabunge tuendelee. Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Wizara ya Fedha

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Ahsante, sasa nitamwita Mheshimiwa Abdulkarim Shah na Mheshimiwa Anastazia Wambura ajandae.

MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kwanza kuweza kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Fedha. Kwanza kabisa, naomba nitoe pongezi za dhati kwa Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote walipo chini ya Wizara hii kwa umahiri wao, ubinadamu wao na uzalendo wao walionao, katika kuhakikisha kwamba yale wanayoyafanikisha na kuyatafuta kupitia *TRA* chini ya Kamishna Jenerali Kitilya, Mwenyezi Mungu atawajalia waweze kufanya mambo yote vizuri na haya tuliyokuwa tumeyasema kwa kipindi cha miezi mitatu yote, basi *Inshallah* yaweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kuzipongeza tena taasisi zote zilipo chini ya Wizara hii, nawapongeza na kuwatachia kila la kheri. Lakini sitoacha kuwashukuru na kuwapongeza tena ndugu zetu wa *PPF*, nawapongeza kwa sababu wapo chini ya Wizara hii na inasimamiwa na Wizara lakini pia kuna mambo ambayo wameyafanya, hakika naamini kila binadamu yatakuwa yamemgusa.

Mheshimiwa Spika, hakuna kitu kilichonigusa kama kuanzisha mpango wa kuwasaidia watoto yatima ambao wazazi wao wamefariki waliokuwa wanachama wao na wao wakawenza kuwasaidia. Hakika hili jambo ni kubwa ambalo hata Mwenyezi Mungu ametuagiza sisi binadamu. Mkurugenzi Ndugu William tunakutakia kila la kheri na mpango huu uweze kuendelea kuwasaidia watoto hawa ambao sasa hivi mnaishia kidato cha nne na Mungu atawapa nguvu muweze kuwasomesha watoto hawa wafike kidato cha sita na naamini kupitia mpango huu mashirika mengine ya Mifuko hii ya jamii wataweza kuangalia na wao waweze kufanya hivyo. naamini kwa uzalendo wao Wakurugenzi wa Mifuko hii Mungu atawazidishia naamini watayatekeleza.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza *PPF* kwanza kwa kuweza kupata tuzo ya utawala bora katika mashirika haya ya jamii katika Afrika Mashariki. Nampongeza sana *Director General*, Ndugu William na kumtakia kila la kheri kwa ufanisi aliouonesha wa utawala bora katika Jumuiya hii ya Afrika Mashariki, basi naamini kwamba mpango huu ataendelea nao na aweze kusifiwa na naamini Tanzania nzima wanatusikia mimi binafsi nasema, nakutakia kila la kheri tena. Lakini pia nawapongeza *PPF* kwa mpango wao wa kujenga nyumba za kuweza kuwasaidia wananchi ambao wana vipato vya chini, mmeanzia Mwanza, hongereni sana.

Lakini nawaomba sana muweze kuendelea na sehemu nyingine mje Dar es Salaam, mje Dodoma, lakini msiache kuja Mafia na maeneo mengine. Mafia ardhi tunayo, watu wapo wa

kuweza kuhimili hali halisi na kuweza kumudu kulipia nyumba hizi. Mheshimiwa Waziri chini ya taasisi yako ya PPF tunawaomba sana mje Mafia na ardhi tutawapa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba tena nipongeze mifuko mingine ya pensheni. Serikali yetu tumeona katika mjadala mzima wa miezi miwili na zaidi, kila siku Waheshimiwa Wabunge, walikuwa wakisema kuhusu mapungufu ya miradi mbalimbali. Lakini tunashukuru kwa Serikali kuona kwamba kupitia mifuko hii yetu ya jamii naamini mambo yaliyoelezwa na hasa hili la mwisho la umeme tukiweza kuitumia *NSSF* mimi naamini mambo yetu yatakuwa mazuri.

NSSF wana uwezo, *PPF* wana uwezo pamoja na mifuko mingine ya jamii. Hakika, hawa watu laiti kama na haya Mashirika mengine yanekuwa wanafanyakazi kama walivyokuwa wanafanya viongozi hawa wa taasisi hizi *NSSF*, *PPF* na wengine nasema nchi hii tusingekuwa na shida. Wapeni kazi hii *NSSF* na *PPF* na mifuko mingine ya jamii na naamini ndio itakayoweza kulinda maslahi ya taifa hili kuliko kuangalia kuuza Mashirika yetu na kuacha miradi hii inakwenda holela na matokeo yake sasa tunakuja kusemeana mbovu hapa ndani na watu wanaanza kulaumiana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa kuweza kufanya mipango hii na wameweza kwa mfano michango ya *NSSF*, *PPF* na Mashirika mengine wametujengea Chuo Kikuu cha Dodoma. Hakika nawapongeza sana. Vitengo mbalimbali kama vya *Computer PPF* na wengine mabweni wameweza kuyajenga. Nasema tuitumie mifuko hii. Mimi kupitia Ramadhani hii nawaombea Dua wale Ma-DG na watendaji wao wote wa mifuko hii Mwenyezi Mungu awazidishie hekima, awape busara awazidishie uzalando awalinde na Mahasidi na *Inshallah* mambo yao yatakuwa mazuri kwa sababu wameweka nia ya kutusaidia nchi hii. Naamini kwamba Mwenyezi Mungu anaisikia Dua hii na Mungu atawalinda na atawaongoza wao na familia zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tumelalamika kipindi kilichopita kwa mambo mengi sana hapa tumeongea na siyo kulalamika tunaongea. Lakini yako mambo wakati mwingine Serikali tukiwaambia labda wanakuwa ama wanafanya shughuli zao kwa siri. Binafsi nilizungumza suala la *UDA* mimi suala hili linaniuma. Tumelizungumza na tumefuatilia na tumeona kwamba mpango wa uuzaaji wa Shirika la *UDA* haukuwa sahihi umefanyika uhuni na ninasema kwa sababu vithibitisho tunavyo wao katika kuuza hisa zao kama Jiji limeshindwa tunasema mali zile zirudishwe kwa Serikali. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kupitia Msajili wa Hazina chukua asilimia hizi, bila hivyo mpango wa kuliiza shirika hili, leo tuna mradi wa mabasi ya kasi, mabasi yale yatasimama wapi, yatawekwa wapi na wao halafu bahati mbaya badala ya kuzungumza mambo mazuri matokeo yake yale tunayosema hapa tunaambiwa wengine wale wanaochangia, sijui wanachangia kutoka Makalioni, wengine sijui wanachanga kwa sababu wana Wahindi sijui wanataka kuwapata.

Hakuna cha Wahindi, hakuna cha nani. Tunachosema Shirika la *UDA* ni mali ya Watanzania ni mali ya wananchi ambao hawana magari ya kuwapeleka watoto wao shulen. (*Makofî*)

Angalieni tuijulize sisi, mimi, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na wao wenye Bodi wao watoto wao wanapanda mabasi wanatumia *UDA* wanapanda daladala? Watoto wao wanawapeleka kwa magari na hawajui uchungu wa mtoto kumwamsha saa 11.00 alfajiri aende akagombee pale basi daladala inachukua watoto wawili, wengine wanabaki pale na kuweza kudhalilika wakati mwingine na shule hawafiki wanachelewa wakifika shule wanateswa.

Tunaomba kama Jiji limeshindwa naomba mradi huu waangalieni uchukueni Serikali lakini mpango wa kuliiza hatukubaliani nao. Nasema naomba wana Dar es Salaam nawaomba Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam wote wanafunzi wote wa Dar es Salaam wanaotumia mabasi haya *UDA* ndio shirika pekee litakaloweza kuwasaidia. Madaladala kila siku tunashuhudia tukidhalilishwa.

Naomba wanafunzi msikubali shirika letu hili kuuzwa shirika hili ndio mkombozi wenu na tunasema hapa Mheshimiwa Waziri, tuna ushahidi kwamba hata siku ya kufanya kikao chao Msajili wa Hazina hakwenda, na kwa nini hakwenda? Kwa nini hakwenda kwa sababu aliyeitisha Kikao siyo mwana hisa. Kama angekwenda basi tungenesema na ninyi Serikali mmehusika katika kuwadhlumu watu wa Dar es Salaam na kulidhulu shirika hili ambalo ndio tegemeo letu sisi walalahoi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana kupitia Kikao hiki niwapongeze na kuwashukuru watendaji wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Waziri wa Fedha, leo akiondoka kesho kubwa anaanza kugawa fedha, fedha zetu za barabara zinakuja, tukae imara katika ujenzi wetu lakini naishukuru Wizara ya Fedha kwa kuiongezea Fedha na kukubali kuwapa Wizara ya Nishati na Madini. Naomba kupitia kikao hiki bahati nzuri Mheshimiwa Waziri yupo na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, nasema katika fedha mlizoongeza tafadhalii tunataka mashine zile mbili mpya zije Mafia mnunue kupitia mpango wa usambazaji umeme Tanzania na Mafia ni eneo la Tanzania tumetengeka tunapata adhabu.

Juzi tumesafirisha baada ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri wa Afya pamoja na Uchukuzi kusafirisha alitokea mgonjwa mwingine hatuna umeme, hatuna *x-ray* tunapata gharama ya kusafirisha wagonjwa. Ukiwepo umeme zile *tools* za pale Hospitali zinafanya kazi. Tunaomba ule mpango wa kutuletea machine zilizotumika kutoka Njombe hatuzitaki na nitashangaa wana Njombe mkikubali mashine zile zitolewe kule zinazoweza kukaa *standby* kwenu ninyi kwa mgao huu halafu mziruhusu ziende sehemu nyingine. Msikubali na sisi hatutaki zile mashine zilizokua zimetumika, tunataka mashine mpya, fedha mmepata na uwezo mnao wa kuzinunua. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi kwa leo sina mchango mwingine chonde chonde mti na macho tunasema shirika letu la *UDA* ndio lillo nisimamisha hapa niweze kusimama. Nalitetea na ninakuomba Mheshimiwa Waziri hili usilifanyie masihara, roho za watu zinawatoka watu wana machungu ya kuuza nyumba za Serikali bado wanazo, sasa msimalize maeneo haya ya Mashirika ya Umma.

Nakuomba sana uchungu wananchi bado wanao hawajasahau, lakini tunasema sisi sasa hivi tunataka shirika hili na ukitembea nchi nyingi kabisa duniani mpango wa usafiri wa miji mikuu ni masuala ya miji yenye ni Serikali. Msikubali kuchukuliwa na watu hawa baada ya muda wataanza kugoma, watapandisha nauli matokeo yake sasa watu watachelewa kazini. Shirika letu nasema liendelee wakishindwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha chukua hii nafasi muweze kuliokoa shirika hili. Pia Mifuko ya *NSSF*, *PPF* watanunua hizo hisa. Mali za bilioni 20 hatukubali ziuzwe kwa bilioni 1.5 na matokeo yake fedha hizo hizo watiliane mifukoni. Tunaendelea, tunajua leo ndio siku ya mwisho tunasema kwa mwaka huu hatutapata muda ya Serikali tutaona. (*Makof!*)

Tukirudi Bunge Iijalo tutawashawishi Wabunge, tuandae hoja binafsi ya kuweza kuunda tume itakayoweza kushughulikia mpango huu wa shirika hili. Hatutaki shirika la *UDA* liuzwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nakutakia na wewe kila la kheri, nakushukuru kwa uongozi wako mahiri na naamini kwamba Mwenyezi Mungu na wewe atakulinda na atakuongeza katika kuhakikisha kwamba Bunge letu linakwenda vizuri. (*Makof!*)

Naomba kuunga mkono hoja na kuwatachia Wabunge wote turudi nyumbani salama salimini. Ahsante. (*Makof!*)

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niwe mmojawapo wa wachangiaji kwa siku ya leo na ni siku ambayo ni ya mwisho katika Bunge letu hili la Bajeti. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena siku ya leo kuchangia kwa mara nyingine katika Bunge la Bajeti.

Lakini kwa sababu tunakaribia kuondoka wengine wanaweza kuondoka leo, wengine kesho na siku zijazo, ninachukua nafasi hii kumwombwa Mwenyezi Mungu aitakase safari ya kila mmoja wetu ili kusudi tuweze kwenda nyumbani salama na hata tutakaporejea tena Bunge Iijalo

turejee salama. Vile vile pia na kwa wasafiri wote ambao wanasaferi kwa vyombo mbalimbali Mwenyezi Mungu aweze kuwajalia safari njema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina kero moja kubwa sana inayohusiana na kodi. Nina mambo mengi ya kuzungumza lakini ninaomba nianzie kwanza na hili. Tunalotaka kulizungumza hasa ni kuhusiana na ukwepaji wa kodi. Kama kuna maeneo tunaibiwa kodi za ndani ni katika hili eneo la utoaji wa risiti pungufu au kutokutoa risiti kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunaibiwa sana na wafanyabiashara wadogo na wakubwa. Hili ni eneo ambalo inabidi Serikali liangalle kwa umakini sana sana. Lakini kibaya zaidi ni kwamba utakuta Dar es Salaam ndio eneo kubwa sana ambalo tunalitegemea, lakini Dar es Salaam ndipo mahali ambapo pamekuwa kichochoro kikubwa sana kwa kutokutoa risiti.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wengi Mkoani takribani asilimia 80 hivi wanapata bidhaa zao kutoka Dar es Salaam. Lakini cha kushangaza ukijaribu kwenda Kibaha pale kwenye mizani utakuta kwamba takribani asilimia 70 ya risiti zile zinazotolewa za kusindikiza mzigo ziko under valued. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, huu ni wizi mkubwa sana lakini tatizo siyo kwa hawa wanaonunua zile bidhaa tatizo ni kwa wale wauzaji kule Dar es Salaam. Kwa sababu wengi wanapokuwa wakinunua zile bidhaa wanataka wapewe risiti kulingana na risiti na kulingana thamani ya bidhaa zao lakini wale wauzaji (wafanyabiashara) kule Dar es Salaam wanakataa na wanawatishia wanasema kwamba mkikataa wengine watakuja na watanunua bidhaa hizi. Kwa hiyo, inabidi wanunue tu hivyo.

Lakini tatizo linakuja pale mfanyabiashara yule anapofika kule Mkoani anapotaka sasa kuthaminisha bidhaa yake inakuwa ni ngumu haiwezekani kuiweka katika mahesabu thamani halisi ya biashara ile haipatikani. Huu ndio mwanzo sasa wa ukwepaji wa kodi kwa sababu itabidi na hata yeje kule Mkoani atumie njia hii hii ya ukwepaji wa kutoa risiti au kutoa risiti yenye thamani pungufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli dhamana ambayo tumeipa *TRA* ni kubwa na wanajitahidi sana. Lakini kama wananchi hatutashiriki katika kudhibiti huu ukwepaji wa kodi kwa kweli kazi itawawia ngumu kwa sababu wao ni wachache, wafanyabiashara hapa nchini ni wengi na watumiaji wa bidhaa nchini ni wengi kwa hiyo, ni vema Watanzania wote tukashiriki katika hili suala.

Mheshimiwa Spika, *TRA*, wamekuwa na mikakati mbalimbali ya kusaidia kuboresha makusanyo, kuboresha ukusanyaji wa kodi. Mfano mmojawapo tunaona kwa sasa hivi wameanzisha kutumia *electronic physical devise* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba risiti zinatolewa. Lakini hata hivyo wafanyabiashara waweze kuweka kumbukumbu zao vizuri na hii *device* imeunganishwa na mtandao wa *TRA*.

Lakini cha kushangaza ni kwamba pamoja na hizi *device* utakuta wafanyabiashara wengi wanadai kwamba ni mbovu mara nydingine, lakini hata wateja wenyewe mara nydingi huwa hawana tabia ya kuomba risiti. Kwa hiyo, unakuta hazifanyi kazi iliyokusudiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa nitoe mifano michache ambayo ni ushuhuda wangu mimi mwenyewe niliokutana nao kwa kuzingatia hili suala la ukwepaji wa kodi ni maeneo mengi sana ambayo nimekuwa nikikutana nayo. Lakini hii ni michache tu ambayo nitaitolea mifano.

Eneo la kwanza ni katika Vituo vya Mafuta. Mara nydingi ninapokuwa nikijaza mafuta katika vituo vya mafuta ni lazima niombe risiti ndio nipewe, ni vituo vichache sana vya mafuta ambavyo huwa vinatoa risiti. Ninapokuwa nikiomba risiti huwa natumia lugha moja ni kwa nini huwa hamtoi risiti? Sasa majibu mara nydingi huwa ni matatu si Dar es Salaam, si Dodoma si wapi majibu yake la kwanza wanasema wengi huwa hawapendi kuchukua risiti.

Kwa hiyo, kosa liko kwa wanunuzi wenyewe. Lakini jibu la pili, wanasema ukitaka risiti tutakupatia. Kwa hiyo, ina-indicate kwamba ni hiari ya mtu kuchukua risiti au kutokuchukua risiti. Jibu la tatu wanakuuliza kwani wewe unataka risiti. Kwa hiyo, hii inaonyesha ni jinsi gani tusivyokuwa na utamaduni wa kudai risiti au kuona umuhimu wa risiti. Wafanyabiashara wa vituo vya mafuta hawana utamaduni wa kutoa zile risiti.

Ninapokuwa nikisubiri kupata ile risiti inashangaza sana kuona kwamba wenzangu wenyе magari yanajaza mafuta na yanapita sioni hata mmoja akiwa anapewa risiti. Kwa kweli ni kiasi kikubwa sana cha fedha ambacho kinapotea katika eneo hili la mafuta ya petroli na dizeli. (Makof)

Lakini mara nyingine nimekuwa nikiwalaumu *TRA* kwamba hivi wao wanafanya nini, kwa nini hawapiti kukagua? Lakini kuna siku ambayo tena niligundua kwamba *TRA* wameelemewa na wakati mwingine huwa wanadanganywa.

Tarehe 29 Aprili, 2011 tulikuwa na harambee pale Ukumbi wa *Istana Dar es Salaam* ambapo ilibidi mimi nikalipie siku hiyo fedha kwa ajili ya ukumbi. Cha kushangaza ni kwamba wakati nataka kulipia nilitolewa kwenye lile eneo ambapo ni ofisi maalum ya kulipia nikaingizwa kwenye kichochoro wakafunga mlango na ufunguo.

Sasa nilipotaka kuuliza kwa nini mmenileta huku kichochoroni wakaninyamazisha usiongee kwa nguvu. Nikauliza ni kwa nini nisiongee kwa nguvu? Wakasema *TRA* wako huku wanakagua. Kwa hiyo, pale nilishtuka na nilitamani hata kupiga yowe za mwizi lakini kwa sababu tu nilitaka kulinda heshima ya Mheshimiwa Mkapa, ambaye alikuwa mgeni rasmi nilliona Harambee ile ingevurugika. Kwa hiyo, niliamua kuvumilia na hivyo kwa sasa hivi naomba nitoe wito kwa nafasi hii kwamba, *TRA Dar es Salaam* waangalie na warudie kufanya ukaguzi katika ile hoteli ya Istana iliyoko Dar es Salaam. Wanadanganywa sana na inawezekana ni wafanyabiashara wengi ambaao wanatumia mtindo huu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kuna *Dodoma Hotel* ambapo pia tarehe 8 nilikwenda pale nilikuwa na wageni nikapata huduma lakini cha kushangaza huduma niliyoipata mara ya kwanza ilikuwa na gharama kubwa tu. Lakini kupata risiti ilikuwa ni kazi kubwa sana. Nilisubiri dakika 45 kiasi kwamba ilinilazimisha kuomba tena huduma ya pili. Nilipopata hiyo huduma ya pili nikaomba tena risiti ya tatu risiti haikuja.

Lakini ajabu ni kwamba zikaja risiti za hizi huduma mbili ambazo zimeingizwa kwenye kompyuta ninazo hapa. Ile huduma ya kwanza ambayo ina gharama kubwa iliandikwa kwa mkono. Iko hapa, unaona imeandikwa kwa mkono na ninaomba baadaye nikupatie. Sasa utakuja kuona kwamba kweli tunaibiwa kwa mfumo huu wa risiti. (Makof)

Mheshimiwa Spika, wataalam wa uchumi wanasema hivi (*value has a value only if its value is valued*) kwamba thamani inathamani endapo thamani yake itathamanishwa. Ni vigumu sana kujua kwamba ni jinsi gani, ni thamani gani, tunayopoteza kutoptana na ukwepaji huu wa kodi? (Makof)

Mheshimiwa Spika, lakini sisi wenyewe Wabunge pamoja na wananchi tumekuwa ni mashahidi kwa jinsi ambavyo tumekuwa tukihangaika katika kuitisha Bajeti za Wizara mbalimbali. Tunasingizia Kasungura kadogo.

Lakini kusema kweli Kasungura siyo kadogo kiasi hicho ambacho tunadhani. Mimi nadhani wananchi wote tuichukulie kwamba ukwepaji huu wa kodi thamani yake tuichukulie kwa jinsi gani tunavyopata upungufu wa Bajeti tunavyokosa huduma kutoptana na mahitaji yetu katika Wizara mbalimbali na sisi wenyewe ni mashuhuda hata sasa umeme hatuna.

Lakini ni kutoptana tu na ukwepaji wa kodi. Tujiulize nchi nyingine wanaweza wezaje kujimudu katika Bajeti zao, wanajitosheleza kwa vipi? (Makof)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie tu kidogo kuhusu unafuu wa kodi ya VAT. Ukiangalia sheria ya kodi ya VAT jedwali Namba 3 utaona kwamba tunakuwa tukipunguza sana wigo wa kodi badala ya kuongeza uwigo wa kodi.

Hii inajionyesha tangu mwaka 1998 sheria hiyo ilipoanza kutumika ni makundi matano tu yalikuwa yamepata msamaha wa kodi. Lakini hadi sasa tuna makundi zaidi ya 32 ambayo yanapata msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani tulitazame upya hili pengine tuirudishe Sheria hii ya VAT, tuangalie lengo lile ambalo lilitupelekea kuanzisha Sheria ya VAT, tuangalie je lengo hili linatekelezwa na huko tunakokwenda ni wapi? (Makof)

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi utakuta kwamba hata wale watumishi wa Taasisi za Serikali amba pengine wameingia katika mfumo wa VAT, wanakuwa hawaelewii maana ya VAT.

Juzi tu mimi nimemaliza kulipia kiwanja kule Itega, pale CDA baadaye Afisa mmoja ananipigia simu kwamba natakiwa nilipe VAT, lakini kumbe VAT ile nilikuwa nimeshalipia kwenye gharama za awali za kiwanja ndio baadaye nilipochukua hatua ya kumwelewesha vizuri na yeye mwenyewe akakubali. Kwa hiyo utakuja kuona kwamba ni wengi tu amba hawalelewii hili na pengine Serikali irudi sasa tena iangalie kama kweli hakuna wananchi walolipishwa VAT mara mbili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mengi ambayo niliyonayo, lakini kuna jambo lingine moja ambalo linanikera sana na hili ni kuhusiana na huu kuchafuli wachafuliwa kwa Wabunge. Sasa kumetokea tena mingongono mingine ambayo imekuwa ikisambaa sambaa sambaa kuhusiana na hii CHC. Kuna baadhi ya Wabunge amba wamepewa pesa nyngi ili kusudi waweze kuisemea CHC, lakini ninachoshangaa ni kwa kwamba kwa nini Serikali imekaa kimya kwa nini haikanushi? Kwa nini, haitoi ufanuzi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nichukue nafasi hii kumwombwa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akitimisha hoja yake atupe ufanuzi kuhusiana na hii minong'ono ambayo inatembea, nadhani si mimi pekee yangu ambayo nimeisikia, ni wengi amba wameisikia na huku ni kulidhalilisha Bunge, ninaomba sana sana tupate ufanuzi ili kusudi wananchi waweze kujua ukweli ni upi.(Makof)

Mheshimiwa Spika, kabla sijamalizia nilikuwa naomba nichukue nafasi hii na mimi kujunga na wenzangu kuzipongeza Taasisi za fedha ambazo ziko chini ya Wizara ya Fedha kwa kazi ambayo wanayofanya kwa kuanzia na PPF amba wanawasaidia watoto yatima, lakini pia waliweza kutulete madawati kwa baadhi ya shule za Kata kule Mtwara. Nawapongeza sana naomba muendelee na moyo huo, NMB nao walishawahi kutoa misaada kwa watoto walio katika mazingira hatarishi, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mtawanya, CRDB nao pia wamejitalidi sana kusaidia vikundi mbalimbali vya ujasiliamali.

Naomba wasiichie hapo tu, wa akina mama wa Mkoa wa Mtwara wanajitalidi sana kufanya shughuli za kujajiri, shughuli nyngi tu ikiwa ni pamoja na kilimo cha uyoga, utengenezaji sabuni na batiki na mambo mengine mengi kama usindikaji wa vyakula na wanataka sana waboreshe hizi bidhaa zao, waboreshe waweze kupata cheti cha TBS ili kusudi wakuze biashara hizi na kujipatia kipato zaidi. Pengine waweze kuingiza katika mfumo wa kodi. Sasa naomba vyombo hivi vya fedha viwakumbuke akina mama hawa kuwapa mikopo ili waboreshe biashara zao ziende katika viwango.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niwatakie kila la heri, kila mmoja wetu alie humu ndani ikiwa ni pamoja na wewe mwenyewe, Wenyeviti na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika shughuli zenu kuanzia sasa, ahsante sana, naunga mkono hoja. (Makof)

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Fedha. Kwanza kabisa naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru tena wananchi wa Jimbo la Buchosa kwa kuendelea kunipa ushirikiano

nikiwa hapa Bungeni nawashukuruni sana. Nipende pia kuwapa pole familia yote ya Ndugu yangu Nzwenge aliefariki usiku wa kuamkia jana na Mungu akinijalia nitawahi mazishi yake, Ndugu zangu wa Buchosa, tuko pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi hii, nadhani hili halina mashaka, kwa sababu ndipo hapo kanakoitwa kasungura kanakopatikana. (*Makof*)

Kwa hivyo, nianze kwa kusema kwamba suala la ukusanyaji wa mapato linapaswa kuwekewa umuhimu mkubwa sana. Leo kama alivyokuwa anasema hapa Mjumbe aliemaliza kuongea sasa hivi, mifano iko mingi mno ya ukwepaji wa kodi, watu bado wanakwepa kodi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani jana alisema ule utaratibu wa wafanyabiashara wakubwa kutokaguliwa mizigo yao, mimi naomba nimshauri sana Mheshimiwa Waziri kwamba sikubaliani nao kwa sababu huko ndiko kodi kubwa inakokwepwa. (*Makof*)

Lakini liko pia la usalama wa nchi hii, Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka katika Seminari ya wenzetu ya kupambana na madawa ya kulevyta, sasa tutawakamataje, kwa sababu naamini kwamba wafanyabiashara wa dawa za kulevyta sio kina Tizeba ni watu wenye mitaji mikubwa wenye kuweza kuwa na mitandao na kama mizigo wanayoingiza hapa nchini haikaguliwi kwenye *entry points*, kwa nini hizi dawa zisiendelee kuingizwa nchini? Zitaendelea kuingizwa na tutaendelea kuwaona wanakuwa matajiri kumbe wenyewe tumewapisha kabisa, kanja tumefunga milango piteni. Niombe sana hii *practice ikome*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba Mheshimiwa Kitilia yuko hapa ndani, eneo hilo naomba uliangalie upya wataingiza humu madude, silaha zinazotumika ovyo kuharibu usalama na amani ya nchi hii. Kwa nini zisipite huko kama mizigo haikaguliwi wakati inaingia nchini. Kwa hivyo, hilo ni eneo ambalo niliona nianze kulizungumzia.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili ni hili ambalo ningeomba Waziri wakati anahitimisha atuweke vizuri. Nakumbuka wakati wa hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Nahodha alizungumzia kama vile vitambulisho vya wakazi vitaanza kupatikana mwishoni mwa mwaka huu.

Ukisoma mpango wa Maendeleo, inaonekana Serikali inajipanga kuanza kufanya jambo hili kutoa vitambulisho hivi mwaka 2013, hizi ni *statement* mbili za Serikali zinazopingana. Kwa hivyo, niombe tuwekwe vizuri ni kwa nini nazungumzia vitambulisho? Kwa sababu ni kuititia vitambulisho ndiyo wigo wa walipa kodi utapanuka. (*Makof*)

Leo ukichukua takwimu za Idara ya ukusanyaji wa mapato ni asilimia kidogo sana ya Watanzania wanalipa kodi ukiacha watumishi wanaokatwa kwenye mishahara yao moja kwa moja. Wengine wote wanaofanya biashara mpaka apate *TIN*, ukiuliza leo Watanzania wangapi wanayo *TIN*, hawafiki hata asilimia 20. Kwa hivyo, wako asilimia 80 wanaendelea kupeta hapa Tanzania wanapata kipato lakini hawalipi kodi na Sheria ya mapato iko wazi kwamba kila anae *earn* aliye kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, tujitahidi Serikali iliweke katika umuhimu wa hali ya juu sana suala la vitambulisho vya wakazi. Na nilikuwa nawazo, linaweza kuwa sio zuri sana kwenye masikio ya wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini kwa sababu vitambulisho hivi sio hati za kutuhakikishia usalama na lina umuhimu zaidi wa kiuchumi kuliko kiusalamu, labda lihamishwe kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani kwa sababu hadithi ya huko imekuwa ndefu sana, liende Wizara ya Fedha ambako litatuweka vizuri kupata mapato ili sasa tuwe na tembo, tuwe tunakuja humu kugawana tembo na tembo akionekana mdogo, tuwe tunakuja humu kugawana nyangumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanaofanikiwa ambao Bajeti zao sio tegemezi ukiangalia kwa makini ukifuatilia nchi mbalimbali utakuta kwamba ni kwa sababu raia wao wana vitambulisho ambavyo ndani yake kuna takwimu za kila mmoja kwa hivyo mapato yake yanajulikana, biashara zake zinajulikana, hakuna ukwepaji wa kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuzungumzia leo, ni kuhusu ushuru wa Forodha. Ushuru wa Forodha, tuseme ukweli hapa ni kero kwa wafanyabiashara wadogowadogo sana, namshukuru sana Mheshimiwa Mkullo katika hotuba yake alisema eneo hili sasa kitaangaliwa upya, hasa la magari.

Naomba liangaliwe upya haraka. Watu wanatelekeza mali zao pale, mtu anaingiza gari kanunua gari kokote huko kwa dola 2000 anafika hapa kuna ka-process kanaitwa ku-up lift, inakuwa up *lifted* mpaka dola 8000, kwa hivyo anachokifanya ni kutelekeza gari.(*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa kinachosikitisha, anadaiwa an TRA dola labda shilingi milioni 12 baada ya ku-up lift, ikifika ameshindwa kuliwa lile gari, linazwa kwa milioni 3, tungetegemea kwamba katika kulipiga mnada basi liuzwe kwa milioni 12 kwenda juu ili Serikali ipate mapato yale iliyoyatarajia. Kwa hivyo, inaonekana na kama tu mchezo gari likionekana zuri Afisa yule ana-assess kalipenda basi litapigwa kodi hilo mpaka ulitelekeze huko. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia hii *discretion* ya *assessors*, nafahamu kwa sababu nimeongea na Kamishana Mkuu wa TRA kuhusu hili jambo akanieleza upo mfumo sasa ambao kodi kwa ajili ya bidhaa mbalimbali unafahamika.

Lakini Mheshimiwa Kitilya naomba nikushauri kama upo unasiliza, mfumo huo umetoa *range* ya chini, bei za chini kabisa zinazopatikana kwenye soko na bei za juu, kwa hivyo inabaki bado ni *discretion* ya huyo Afisa wako kuamua amoze kiasi gani mlipaji au kwa bei ya chini ya soko au bei ya juu ya soko, bado mwanya wa watu kunyongwa mikono upo na ndiyo maana wala hatusemi uongo hapa, ukiwa na *connection* ushuru bwelele, hujulikani au una mdomo mrefu kama akina nani hapa basi bei ni zile za *maximum* kila siku. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niombe sana *discretion* ipungue kwa sababu *discretion* ndiyo mwanya wenyewe, huo ndiyo uchochoro wenyewe wa jamaa zetu kutufanyizia. Ijulikane tu kwamba utaratibu ni huu.

Mheshimiwa Spika, gari inayouzwa na Serikali ilikuwa inatumwa na Afisa wa Serikali, sasa inatakiwa iuzwe kwa sababu imechoka, inapigwa *depreciation 20% per year*, ikifika miaka mitano iko kwenye *zero value* kwa hivyo ikuizwa, inauzwa kwa shilingi labda elfu 20, laki mbili, laki tatu. Gari inayoletwa kutoka nje, ina miaka kumina tano, imenunuliwa kwa dola 2000 inakuwa *up-lifted* hii *contradiction* ya nini? Kwa magari ya ndani yana *depreciate*, magari ya nje yana- *appreciate*. Naomba sana Serikali iliazame upya hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia Wizara iwe makini zaidi katika kuishauri Serikali namna ya kugawanya fedha kwa Wizara mbalimbali. Tumeona hapa Wizara zinakuja, kila moja inanungunika haina pesa, haina pesa, lakini yapo mafungu nimeyatafiti Wizara kwa Wizara yanatia woga, wakati tulikuwa tunahangaika Mheshimiwa Ngeleja hana pesa ya kuleta umeme wa dharura, yako maeneo yalikuwa yamepewa pesa nyigi *very unnecessarily*, kwa mfano; mafunzo nje ya nchi na safari nje ya nchi, nimepiga hesabu nimekokotoa bilioni 53, *this is just a lot of money*. Naomba sana *next time* tusifanye hivi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hoja kwamba hata utaratibu mzima wa kupitisha Bajeti tuuangalie upya. Bunge halipati nafasi ya kutosha kwa niaba ya wananchi. Mwenyewe unaona sasa hivi hata tunavyoenda kwa hii Wizara, zimeunganishwa mbilimbili, lakini kikubwa zaidi tupate nafasi ya kutosha kuiangalia ile *framework* nzima kabla haijaja kusomwa na Waziri wa Fedha kama Bunge. (*Makofî*)

Pale ndiyo tutayaona mapungufu mapemba na tusije tukaingia kwenye *Appropriation Bill* kabla hatujatoa mawazo yetu. kinachotokea sasa hivi anasoma Waziri, Bill inapita ndiyo tunaanza kuchambua, kwa hivyo ni kama jambo ambalo linakuwa kidogo halitupi nafasi nzuri ya kuweka inputs kama wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, wako watu wanafanya vizuri, lakini nina mashaka kwanza na hili kambo linaloendelea kila. Wabunge wengi, wananchi wanalamika juu ya ubadhilifu na nini

katika Halmashauri zetu nchini hapa. Pesa nyingi inayotolewa na Serikali kule ingetumika vizuri, maendeleo tungeyaona makubwa sana nchi hii. (Makof)

Mimi nasikitika kwamba ripoti ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Serikali eneo hili linalonungunikiwa sana na wananchi wote, *clean certificates* zinazidi kuongezeka, *it doesn't make sense*. Kwa nini mahala ambako pananungunikiwa na kila mtu *literally*, huko huko ndiyo hesabu ziko sahihi na nimwombe sana Mzee Uto jitazame kutokea nyuma, kwamba haya mambo ya *certificate*, kweli inawezekana wapo wanaofanya vizuri, wanafanya kazi *diligently*, lakini sio katika *scale* hii, inatia mashaka *no wonder* hata akina Jairo wamepata *clean certificate* juzi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwapongeze watu wa *NSSF* wamefanya kazi nzuri. Amesema Mheshimiwa Shah, lakini na mimi naomba niwapongeze, nyumba mlizotujengea kule Mwanza, niomba niwape ushauri, harakisheni bado wapo watu wanununguniha hawana Hati, lakini naamini wakipata Hati, zitawasaidia wanaotaka kupata mitaji kutoka kwenye Taasisi za fedha wapate mitaji.(Makof)

Mfumo wenu ule mliouanzisha wa kusomesha watoto ni mzuri, sawa, lakini ndugu yangu Elio embu peleka huo mfumo mpaka Chuo Kikuu kwa sababu kumsomesha mtoto... (*Kengele*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (Makof)

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nilishakata tamaa, lakini kwa huruma yako nakushukuru sana kwa kunijalia na mimi nafasi niseme machache sana juu ya Wizara hii.

Kwanza ni-declare *interest* mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Kwa hiyo, yale ambayo yaliwasilishwa na Mwenyekiti wetu kwa niaba yetu sisi nayaafiki yote na ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Waziri na timu yake na Serikali kwa ujumla watayazingtaia katika kuboresha Bajeti zijazo.

Moja ya eneo ambalo niombe sana Serikali iliangularie ni hili ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge waliopita, Mheshimiwa Umbulla na Dokta pale, lakini katika taarifa yetu ya Kamati kwenye ukurasa wa nne na wa tano, Kamati imejihuisha sana na kwamba tufike mahala sasa tulizamie suala la kuongeza mapato na kuongeza wigo wa kupata mapato kwa ajili ya Serikali yetu. Kwa kweli hilo ni suala muhimu sana. (Makof)

Mara nyingi tumekuwa hapa tukigombana kuhusu namna ya kutumia ziel fedha. Wizara hii inataka hiki, Wizara inataka hivi, ooh, mimi nataka hiki, lakini mimi nina wasiwasi kwamba tumezama sana katika kuona kwamba Serikali yetu inapata mapato ya kutosha. Kwa hiyo, michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo imetolewa na ile ambayo iko kwenye ukurasa wa nne na wa tano kwa Taarifa ya Kamati ya Fedha namna ya kuimarisha vyanzo vya mapato nadhani ni muhimu sana tuviangarie hivyo. Kuna haja kubwa sana kama Bunge tuzame katika kuangalia kwamba haka kasungura kanakoitwa haka tufanyefanyeje mpaka sasa awe sijui tembo. Au tunaambiwa awe kama mimi mwenywewe. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nadhani kama Serikali waliangularie nitashukuru sana. Kwa sababu hii tabia ya kodi kila siku kutegemea bia, kuongeza bia, ingawa mimi siipendi sana. Siyo siipendi, siyo kwamba siipendi. Ningombwa watu waache. Lakini waKO watu wanaipenda.

Sasa hii kuongeza kodi ya bia kila siku, kodi ya soda kila siku, kodi ya sigara kila siku, nadhani ni utamaduni ambao umefika mahali lazima tuuangularie hivi hakuna vyanzo vingine vya mapato ambavyo tunaweza tukavizingatia badala ya kuendelea kwenye bia, kwenye soda na kwenye nini. Yako maeneo ambayo yanatajwa siku zote hapa, mambo ya madini. Hivi Serikali ni kiasi gani ambavyo wanafanya kuona kwamba katika maeneo haya ambayo yanazungumzwa na Waheshimiwa tunaweza tukapata fedha. Mambo ya misamaha haya ameelleza mwenzangu, tulikuwa tano mpaka sasa sijui misamaha ipo karibu zaidi ya thelathini na kitu.

Mheshimiwa Spika, nadhani suala la vyanzo nya mapato ni muhimu sana kuliangalia. La pili, ni kwamba napata tatizo sana na shilingi yetu ya Tanzania inavyomomoyoka. Thamani yake inavyoshuka siku hadi siku. Ni jambo mojawapo la kusikitisha sana. Mimi hua nasikitika kwa sababu taarifa tunazopata ni kwamba dhahabu yetu inapanda bei katika soko la ulimwengu. Inapanda vizuri tu siku hadi siku. Sasa mimi siyo mchumi. Lakini wako wachumi hapa. Hivi ni kwa kiasi gani dhahabu hii inaweza ikasaidia shilingi yetu ya Tanzania isiendelee kushuka thamani. Hakuna mchango wowote wa dhahabu hii ambayo inapanda siku hadi siku thamani yake ikasaidia kupunguza tatizo hili la kushuka thamani kwa shilingi yetu ya Tanzania? (Makof)

Mheshimiwa Spika ugomvi mwengine ambao tunaupata ni kwa sababu ya kushuka kwa thamani yetu ya shilingi. Kwa sababu juzi Serikali ilifanya kazi nzuri ikapunguza bei ya mafuta. Lakini hata siku tatu nne hazijafika tukarudi kule kule kwenye bei zile za zamani za mafuta. Na sababu iliyoelezwa ni kwamba shilingi yetu imeendelea kuoungua na kwa sababu wenzetu hawa wanununa mafuta kwa dola na kadhalika.

Sasa tuna jitihada gani basi sasa ya kuilinda hii shilingi yetu. Mimi nadhani Mheshimiwa Waziri pamoja na Gavana wa Benki Kuu ipo haja kubwa sana ya kuangalia nana ya kuisitiri hii shilingi yetu ya Tanzania ili kusudi maisha bora kwa kila Mtanzania yanaweza yakapatikana. Kama shilingi yetu itaendelea kupanda siku hadi siku kama inavyofanya sasa kwa kweli hata hayo maisha bora kwa kila Mtanzania ni vigumu sana kupatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ombi langu au ningenda Mheshimiwa Waziri anisaidie baadaye ni kwa kiasi kupata kwa bei ya dhahabu na madini mengine yana mchango katika kusaidia mmomonyoko huu au kudongoka hii thamani yetu ya shilingi ya Tanzania. Pili, mimi sina uhakika kama usimamizi wetu katika masuala ya *money laundry* na *Bureau de Change* uko perfect, sina hakika. (Makof)

Mheshimiwa Spika, huko ni katika baadhi ya maeneo ambapo fedha za nchi za nje zinapotea sana. Tunahitajni kila dola moja, dola mbili, dola tatu au kila aina ya fedha zetu za kigeni ili tuweze kijikimu katika mambo yetu mbalimbali. Lakini katika mambo haya mawili ni kweli tuna soko huria tumeanzisha haya mambo ya *Bureau de Change* sina uhakika kama usimamizi uko wa kweli kweli wa dhati kabisa kutoka Benki Kuu na Wizara katika kuona kwamba hatudanganywi danganywi na hatuibowi. Hisia za walio wengi ni kwamba tunaibiwa sana katika hizi *Bureau de change* ndio hiosia za watu wengi.

Sasa naomba na Serikali na hili nalo hebu waliangalie na waturidhishe kweli usimamizi uko mzuri, hatudanywi, hatuibowi? Nitashukuru sana kupata maelezo. Lakini katika *money laundry* pia pamoja na Sheria imepita hivi lakini nina wasi wasi kwamba ziko fedha nydingi ambazo henzieleweki, hazitozwi kodi, zinasambaa ndani ya nchi. Kwa ajili hiyo nchi inapata matatizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nzungumzie suala la pensheni. Penseheni ni muhimu kwa wananchi wetu. Huko nyuma nadhani suala la pensheni halikuangaliwa vizuri. Ndiyo maana watu walostaa fu kwa kweli maisha yao ni dhalili sana, duni sana. Kama anakumbuka sawa sawa juzi juzi tulikuwa tunasoma gazeti hapa Katibu Mkuu wetu Mstaafu, Mheshimiwa Philip Mangula, alipokuwa anajibu baadhi ya tuhuma hapa, anasema anaishi kwa pensheni yake ni shilingi laki moja na thelani. Hivi laki moja na thelani kweli kwa mtu kama ye ye atafanye.

Lakini hata kwa siku za nyuma mlimsikia Generali Sarakikiya naye akilalamika hivyo hivyo kwamba kipensheni kile anachopata ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sana tukawa tunaangalia namna ya kuboresha pensheni zetu hizi. Kwa sababu pensheni ikiboreka na watu wakawa na uhakika kama pensheni zao zitakuwa nzuri mtu hatapenda kuingia kwenye vishawishi. Wakati mwengine watu wanalamikia kuingia kwenye vishawishi nya kufanya mambo ya ovyo ovyo kwa sababu anajua kesho na kesho kutwa huko hajui maisha yake yatakuwa namna gani. Hajui, anasema bora nichukue changu mapema ili kusudi huko mbele ya safari na mimi niweze kuishi kama wengine.

Kwa hiyo nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Spika, suala liendelee. Huko nyuma tuliwahi kushauri kwamba wenzetu katika nchi nyingine kima cha chini cha pensheni kinaendana na kima cha chini cha mshahara. Ndiyo wenzetu wanavyofanya. Ukibadilisha kima cha chini cha mishahara *automatically* na ile kima cha pensheni nacho kinakwenda pamoja wala habari ya kuja hapa tena jamani ongezeni pensheni haitakuwepo ni *automatic* kima cha chini cha Serikali kikiongezeka basi na vile vile kima cha chini cha pensheni kimekwenda sambamba na hiyo. Mimi huo ndiyo utaratibu nzuri.

Sasa kwa kuanzia pengine inawezekana ikaonekana kwamba kima cha chini cha mshahara ya Serikali ni laki tatu na ngapi basi angalau nusu yake. Lakini nasema kuwe na *formula* maalum angalau nusu yake basi, inajulikana kama kima cha chini ni shilingi laki nne basi nusu ya hiyo laki mbili hawa wastaa fu hawa wapate walau shilingi laki mbili itasaidia kuwaweka sawasawa na vile vile itasaidia kuondoa vishawishi kwa maisha ya baadaye. Naomba sana hilo liangaliwe. Katika hilo pia tulishauri.

Nakumbuka Mheshimiwa Mkulo, Waziri wa Fedha, alikubali wakati wa Bajeti kwamba kwa wale wanaopata pensheni miezi sita ni mingi sana. Mtu akaye miezi sita hajapata chochote kijijini kule mstaa fu kwa kweli anapata maisha magumu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi niombe sana Mheshimiwa Waziri na kama nakumbuka sawasawa ulikubali kwamba walau ilipwe pensheni kwa wale wanaopata miezi sita sasa ilipwe kwa miezi mitatu ili kuwasaidia wananchi wale na ingawa haijaboreka sana, lakini shilingi elfu hamsini siyo sawa na zile shilingi 10,000 za zamani ndiyo maana ilikuwa miezi sita, hamsini mara tatu laki moja na nusu inaweza ikamsaidia, baada ya miezi mitatu anapata kulikoni kumweka miezi sita mwananchi kule kijijini hapati.

Mheshimiwa Spika, ninayo hapa inaitwa *Government Notice 206 ambayo ilichapishwa tarehe 26 Juni, 2009 inasema The Public Service Retirement Benefits Acts Cap. 371 ambayo inaonyesha Mheshimiwa Rais alishakubali marekebisho ya pensheni. Ninayo document hapa Mheshimiwa kama unataka niiwasilishe katika Meza yako niko tayari. Inasema kabisa na imeweka tabulation jinsi pensheni itakavyoongezwa kwa mfano nikinukuu sehemu ndogo tu. Naomba ninukuu. "And where as I Mustafa Haidi Mkululu, the Minister for Finance and Economic Affairs I am satisfied that the President in terms to increase the minimum pension payable to the persons and enjoying retirement benefits under the provision of the public service retirement benefits Act Cap. 371. And now therefore, in the exercise of the powers conferred about the Minister under Section 3 of the Section 30 of the Public Service Retirement Benefits 371 do hereby order as follows. This order may be desisted as the Public Service Retirement Benefits Minimum Order to 2009. The rights are minimum pension in despite in the schedule to this order shall be payable to persons who retired from the public service and qualify for payment for pension."*"

Mheshimiwa Spika, ipo *schedule* imewekwa hapa kuanzia shilingi 36 sasa nilitaka kujua hii amri ya Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Mkulo, Waziri wa Fedha akakubali imetekelezwa lini mbona haijatekelezwa? Mbona mpaka leo watu wanapata pensheni ndogo sana? Sasa kama kitu kilishaamuliwa na Serikali, Rais alishatoa maelezo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi na yeye kasema na mimi nakubaliana na hiyo, toka mwaka 2009 hivi kuna kigugumizi gani mbona haya marekebisho ya pensheni hayajafanyika mpaka hivi sasa? (*Makofii*)

Ningependa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho nipaye majibu juu ya suala hili kwa sababu kwa kweli moja ya kero ya wananchi wetu waliofanya kazi kwa imani na kwa uadilifu mkubwa wamejilinda, hawakuingia kwenye vishawishi. Hao sasa hivi ndiyo wanaoteseka. Kwa sababu maisha yao hawakuyaangalia wakati huo walikuwa wako *too loyal* kwa Serikali yao na kwa wananchi wao. Hawakutaka kuingia kwenye vishawishi kabisa sasa wamekuwa *victim of circumstances* kwa sababu ya ule uadilifu wao na imani yao na kuipenda nchi yao sasa ndiyo wanateseka maskini ya Mungu wanapata pensheni shilingi 50,000/=. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho yake anipe jawabu ya huu waraka ambao Mheshimiwa Rais aliutoa, alitoa maelekezo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha akakubali na ukatolewa toka Juni, 2009 kwa nini mpaka leo haujatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii ndogo ulionipa lakini ni muhimu sana. Nimesimama kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Mkoa wa Dodoma na wakulima wote wa zabibu Mkoani Dodoma na kwingine kokote ambako wanalima zabibu.

Mheshimiwa Spika, naamini wewe mwenyewe ni mkulima wa zabibu na Mheshimiwa Waziri Mkuu pia mtoto wa mkulima naye anajifunza kulima zabibu. Imani kubwa ni kwamba hili nitakalolisema pia na nyie mna maslahi nalo. Zao la zabibu katika mkoa wetu wa Dodoma na sisi ndiyo almasi yetu na ndiyo dhahabu yetu na ni zao ambalo kwa hakika ukiltinganisha na duniani nyingine wanakolima zabibu, zabibu ya Dodoma inavunwa mara mbili kwa mwaka. Hakuna nchi yoyote duniani ambayo wanaweza kuvuna zabibu mara mbili kwa mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zao hili lilipata mwanguko miaka ya 1990 na likafa kabisa baada ya kiwanda kilichokuwa cha *DOWICO* kufa na hivyo wakulima wakakosa mahala pa soko la kuza zabibu zao. Lakini kuanzia miaka ya hivi karibuni au tuseme mwaka 2004 zao hili limepata uchangamfu mpya baada ya kuanzishwa kwa viwanda, kikiwepo kiwanda cha *SITAWICO* ambapo kwa kushirikiana na *Tanzania Distilleries Limited* wamekuwa wanunuaji wakubwa wa zao hili la zabibu pamoja na viwanda vingine vidogo vidogo vilivyoko hapa Mkoani Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zao hili sasa limepata sura mpya na sasa kuanzia mwaka 2004 walikuwa wanaweza kununua lita 62,520 ya zabibu. Lakini mpaka mwaka 2010/2011 wameweza kununua lita 816,000.

Maendeleo haya ni makubwa na yamekuwa makubwa kwa sababu Serikali ilikuwa imefuta ushuru *Excise Duty* ambayo ilipelekea sasa kuwa zabibu ikitengenezwa kwa maana ya viwanda vyetu hivi inakuwa katika ushindani wa soko na zile *wine* zinazotoka nje ya nchi yetu. Sasa baada ya kuwa ushuru kuwa upo hivyo lakini halisi ikoje.

Mheshimiwa Spika, bei ya zabibu duniani ni shilingi 250 kwa kilo kwenye soko la dunia. Lakini kwa hapa Dodoma hawa hawa *processors* hawa wanao-produce hizi *wine* wananunua kwa mkulima kwa shilingi 800 hadi 1,000 kwa hapa Tanzania.

Ukiangalia tofauti ya bei hii ndiyo inayopelekea huu msamaha uwe na umuhimu mkubwa sana, wakati sasa tunapozungumzia kilimo kwanza na wakati uzalishaji katika mashamba duniani wenzetu wanazalisha kwa heka moja kiasi cha tani 10.5 kwa heka moja.

Lakini sisi Dodoma kwa heka moja tunazalisha tani 2.5. Sasa ili uweze kumvuta huyu mkulima ni lazima uweke msamaha fulani ili huyu mnunuaji aki-process aweze kupata faida. Vinginevyo zabibu yetu ya Dodoma itakuwa na kwamba huyu anayetengeneza *wine* ya Dodoma hataweza kushindana na anaye-import kutoka nje. Tunasema tuko kwenye Kilimo Kwanza. (*Makofi*)

Sasa kwa kutokufanya hivyo na maamuzi haya yamefanyika na Serikali ya kufuta hiyo *wave* iliyokuwepo ya ushuru huu sjui kama walitafakari umuhimu na ulazima wa Sera ya sasa ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi juu ya Kilimo Kwanza. Kwa sababu wangkuwa wanalionia hili wasingetakiwa kusubiri wapewe taarifa na wenye viwanda kwa sababu wanaiona hiyo hali halisi ya soko ilivyo. Mimi nafikiri hapa hapakuwa na *dual diligence* kwamba hawakuweza kufanya utafiti wa kutosha juu ya zao hili.

Sisi Wabunge wa Mkoa wa Dodoma kwa niaba ya wenzangu wote niseme kabisa hatukufurahishwa na jambo hili. Tunaiomba sana Serikali iangalie upya jambo hili na kwa kuwa mwezi Januari kutafanyika *Budget Review* basi wakati wa *Budge Review* hii waangalie namna ya kurudisha ile *waive* ili ule ushuru uondolewe zabibu yetu iweze kushindana, *wine* yetu iweze kushindana na *wine* ya nje ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *wine* inayotengenezwa *Tanzania Presidential Wine*, nyingine ile inaitwa *M Ambassador* na nyinginezo ni *wine the best* hata Wazungu wenyewe wanaotoka huko, Italia, Brazili na *South Africa* wanasema haiwezi kushindana na *wine* nyingine. Hatua hii na fursa hii ni muhimu sana kwa taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana Waziri wa Fedha na Wataalam muliangalie jambo hili kwa jicho hilo ambalo na sisi tunaliona. Wote najua pengine hamkufanya kwa dhamira mbaya, pengine ni kwa bahati mbaya.

Lakini hivi tunavyozungumza kwa hali itakavyokuwa ni kwamba *wine* ya nje itauzwa kwa bei ndogo kuliko *wine* ya Tanzania na kwa maana hiyo *SITAWICO* na *Tanzania Distillaries* na viwanda vingine vidogo vidogo hapa nchini hawataweza tena kutengeneza na wala kununua zao hili kutoka kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa nimetoka Iringa nimeona biashara imechangamka, wananchi wanalima zabibu, magari ya hawa wenye viwanda yanapita kununua hizo zabibu huko. Jambo hili limetusikitisha sana, ningeomba Serikali ilifikirie upya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Mapato *TRA*. Yapo malalamiko kutoka kwa wananchi wanaonunua magari nje na kuyaleta Tanzania. Kwani yafikapo hapa nchini hutozwa kodi kubwa za kukadiriwa ambazo kodi hizo huwa kubwa kushinda hata bei ya gari karibu na bei ya kununulia gari nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, je, ni vigezo gani vinatumika kukadiria kiasi ambacho tozo (kodi) inakuwa kubwa kuliko bei ya gari au karibu na bei ya gari au bidhaa nyingine yoyote?

Mheshimiwa Spika, kuhusu deni la Taifa ni dhahiri kwamba nchi nyingi zinakopa ili kufikia malengo waliyojiwekea. Lakini lazima kama nchi tuwe na ukomo wa mikopo hiyo ikiwa ni ya ndani au ya nje ukizingatia wanaolipa madeni hayo ni Watanzania na madeni hayo hulipwa na riba juu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* deni la Taifa limeongezeka kutoka asilimia 38 kutoka triliioni 7.6 mwaka 2008 mpaka shilingi triliioni 10.5 mwaka 2009/2010 ambapo mpaka Juni, 2011 deni la Taifa lilikuwa dola za Kimarekani milioni 11455.4 sawa na asilimia 17.1 ambapo asilimia 80 ni deni la nje. Na inasikitisha kwani mikopo hiyo ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sio mitaji ya kusaidia kuongezeka kwa uwekezaji katika mashirika yetu ya umma ambayo yanazalisha kuliongezea Pato Taifa.

Mheshimiwa Spika, tujipange upya, tukope lakini mikopo iwe ya faida. Hii ya sasa ni ya hasara na vizazi na vizazi vitaendelea kulipa pesa ambazo hawataona tija yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya wastaafu, tumeshuhudia wazee wetu waliotumikia Taifa letu wakihangaika kudai malipo yao bila mafanikio. Naitaka Serikali iache kuwazungusha wazee kuwalipa mafao yao hasa wale wa *East Africa*. Ni aibu kwa nchi yetu, tunaonekana hatuthamini utumishi wa wazee wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia pensheni inayolipwa kwa wastaafu ni ndogo, iongezwe ili ikidhi haja kwani maisha yanapanda sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho napendekeza wazee wote bila kujali walifanya kazi za ofisini au walikuwa wakulima kwani wazee wote kwa njia moja au nyingine wanalitumikia Taifa angalau 50,000 kwa mwezi kwani maisha ya wazee wa Tanzania ni watu waishio maisha magumu sana. Hii inahu hasa wale ambao hawamo katika mfumo rasmi wa malipo ya pensheni kutokana na

nafasi walizozitumikia katika ofisi mbalimbali nchini. Iwahu su wale ambao hawapo katika mfumo huo rasmi.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, *Tanzania Investment Bank (TIB)* na *Tanzania Agricultural Development Bank (TADB)* wakati tunajadili mpango wa maendeleo ya miaka mitano ilikubalika kuwa kuanzia Bajeti 2011/2012 Serikali itapeleka shilingi bilioni 100 (*TIB*) na shilingi bilioni 100 (*TADB*) kila mwaka wa fedha kwa mfululizo wa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, kwa nini katika hotuba ya Waziri wa Fedha hakuna mahali popote alipoonyesha ahadi hii na hakuna jedwali la mabadiliko linaloonyesha ongezeko la hizo bilioni 200?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Benki ya Posta (*TPB*) ina mtaji wa shilingi bilioni 10.5 na kwamba inapungukiwa shilingi bilioni 4.5 kufikia mtaji wa shilingi bilioni 15 inayotakiwa na sheria ya uanzishwaji wa benki hii itaiwezesha Serikali kuwa na benki imara ya biashara na kwamba itashindana na akina *NMB*, *Barclays*, *Stanbic* na *CRDB*. Faida yake ni kuwa faida inayopatikana inabaki hapa nchini (mfano mwaka jana walipata faida karibia shilingi bilioni moja).

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isiongeze mtaji wa shilingi bilioni 10, ili tuifanye benki kushindana na kuimariika?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna pengo kubwa baina ya riba za kuweka kwenye benki na riba tunazotozwa tunapoenda kukopa, ukiweka unalipiwa riba ya 3% lakini wewe ukikopa ni 18% au zaidi, pia kuna *arrangement fees* ambayo 1.5% au zaidi. Kufanya riba kufikia 20%, riba hii ni kubwa sana, badala ya kumwezesha mwananchi kiuchumi inamfilisi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali kupitia *BOT*, ina mpango gani kuhakikisha kuwa asilimia ya kuweka inafiki 5% na ile ya kukopa inafiki 12%?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni 12.4% ya Watanzania watu wazima wanapata huduma ya benki ambapo ni watu milioni mbili kati ya watu milioni 20. Je, Serikali kupitia *BOT*, itaanzisha lini Benki Jimboni Kisese sambamba na kupanua mtandao wa huduma za fedha nchini?

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali inatekeleza miradi mingapi? Na imepokea fedha kiasi gani toka *NEPAD*?

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutamka kuwa naunga mkono hoja iliyotolewa mbele yetu na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia ongezeko kubwa la kasi la *SACCOS* hapa nchini. Hata hivyo wakati hali ikiwa hivyo inasikitisha kuona sekta hii ikitabiliwa na usimamizi wa *SACCOS*, ndio maana sio ajabu sasa kuona *SACCOS* zikiachwa kuendelea kufanya shughuli za kupokea akiba za wanachama na kutoa mikopo wakati *SACCOS* hizi hazijafanyiwa ukaguzi wa hesabu zake kwa miaka miwili mfululizo kinyume kabisa na taratibu za fedha.

Swali la kujuliza hapa ni je, katika hali hii tunajiridhisha vipi na usalama wa akiba za mwanachama? Upo ushahidi kuwa wakati wa tatizo la *DEC* mionganoni mwa wahanga wakubwa wa janga lile ni *SACCOS* ambazo zilichukua akiba za wanachama na kwenda kupanda mbegu *DEC*. Katika hali hii Serikali haiwezi kukwepa lawama kwa kushindwa kusimamia kikamilifu sekta ya fedha.

Mheshimiwa Spika, udhaifu huu unajidhihirisha vilevile kuwa pamoja na sheria ya kutaka *SACCOS* zenye mtaji wa shilingi milioni 800 na kusimamiwa moja kwa moja na Benki Kuu, bado *SACCOS* nydingi ambazo zimevuka kiwango hicho hazisimamiwi na Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, *VICOBA* ni mfumo ambao unazidi kupata umaarufu mkubwa hapa nchini na wananchi wengi wa vijiji wanautumia mfumo huu kupata huduma za kifedha. Changamoto iliyopo ni kwamba usalama wa fedha za wananchi ambao wanaweka hisa zao

katika vyombo hivi upo mashakani. Hii ni kutokana na ukweli kuwa pamoja na sheria ya ushirika kutambua *VICOBA* kama asasi zilizopo katika hatua za awali za kupewa hadhi ya kuwa *SACCOS*, bado hakuna mwongozo thabiti wa jinsi ya kudhibiti na kukagua asasi hizi na sheria ipo kimya kuhusu nguvu ya kisheria kwa asasi hizi kuweza kuingia mikataba. Kasoro zote hizi zinahatarisha usalama wa fedha za wananchi. Serikali ina wajibu mkubwa wa kurekebisha kasoro hizi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa ajira kwa vijana. Wakati ambapo vijana wanachangia karibu asilimia 60 ya idadi ya watu nchini, 15% ya vijana hao hawana ajira. Hii ni hatari kwa usalama wa nchi yetu. Lazima tuchukue hatua za haraka kupata majibu kuhusu uwezeshaji wa vijana kwa maendeleo endelevu. Sekta ya uvuvi hususan katika ukanda wa bahari ambayo hatujaitumia kikamilifu itumike ili rasilimali za mazao ya bahari zitumike katuondolea tatizo la ajira. Mradi wa *SELF* ujielekeze katika kuibua mifumo ya ukopeshaji katika sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, moja ya masharti mahsus kwa mradi wa *SELF* kupata fedha katika awamu ya pili ni kuhakikisha kuwa mradi huu *una-transform into an independent entity*, ili kutohatarisha upatikanaji wa fedha toka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Naishauri Serikali kuharakisha mchakato wa *transformation* ya *SELF*.

Mheshimiwa Spika, jitihada zetu za uwezeshaji zimekuwa zikikabiliwa na changamoto ya targeting kiasi kwamba matokeo tarajija yamekuwa yakifikiwa taratibu sana na kugusa watu wachache. Nashauri ili kujinasua na tatizo la ajira kwa vijana tunazishe miradi midogo ya kilimo kwa kutumia taaluma ya umwagiliaji wa matone kama iliyooneshwa Wizara ya Kilimo wakati wa Nanenane mfumo ule unaweza kunyweshea eka 50 bila matatizo. Eneo kama hili linaweza kutoa ajira ya uhakika kwa vijana wengi. Tuelekeze mabilioni ya JK katika miradi ya jinsi hii.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, kwa hotuba yake nzuri. Pia nawapongeza Naibu Mawaziri Mheshimiwa Gregory George Teu na Mheshimiwa Pereira Ame Silima bila kumsahau Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naanza sasa kuchangia kwa kuwa kuna wafanyakazi wanapostaafu baadhi yao wanapata taabu sana kupata klinua mgongo, hivi Serikali inaweza kutuambia inakuwaje mpaka wanacheleweshewa kupata mafao yao?

Mheshimiwa Spika, mfanyakazi atapoajiriwa inajulikana tarehe yake ya kuajiriwa na inajulikana tarehe yake ya kustaafu, tunavyoja Serikali yetu imeweka utaratibu wa mfanyakazi anapostaafu ndani ya miezi sita anapewa mafao yake. Sasa Waziri aniambie ni kwa nini wastaafu wengine wanacheleweshewa mafao yao?

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye klinua mgongo, kuna wastaafu wanapewa shilingi 60,000 kwa miezi mitatu hii shilingi 60,000 ukiigawanya kwa mwezi unapata shilingi 20,000 kwa mwezi. Naomba Serikali iwaangalie Watanzania hawa wazalendo wametumikia nchi yao kwa muda mrefu tuwaonee huruma, Serikali iwaongezee angalau shilingi 50,000.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudu kubwa ya kudhibiti mfuko wa fedha nchini. Ni kweli kwa sababu ya mabadiliko hasi ya uchumi duniani ni wazi kuwa shilingi ya Tanzania nayo itaguswa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kusimamia vizuri utendaji kazi wa mifuko ya fedha za wastaafu kama *NSSF*, *PPF*, *LSPF* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iwe na uangalifu katika kutumia mifuko hii kwa uwekezaji. Kama kule inakowekeza fedha za mkopo hazitarudishwa mapema (*payback*) kuna uwezekano mfuko ukakosa fedha ya wastaafu ambao kila mwaka wapo.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wamechoka na taratibu zozote zinazoashiria kuhujumu mali za umma.

Wizara ya Fedha inasimamia uuzaji wa Mashirika ya Umma (Hazina ndio *Registrar*) ambaye ana hisa katika mashirika hayo. Nashauri Serikali Mashirika haya yaendelee kuuzwa kwa uwazi na uadilifu zaidi. Hisia za udanganyifu kama zilizotokea kwa UDA ni vema ziachwe ili kuisafisha Serikali katika tuhuma zisizokuwa za msingi. Serikali ikumbuke inahitaji kurudi madarakani kutawala.

Mheshimiwa Spika, kero ya wastaifu wa Afrika Mashariki inaleta sura mbaya kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Nashauri Serikali ifuatilie kesi yao Mahakamani, ili imalizike na Serikali itoe tamko kila mwananchi aelewewe kuwa wastaifu hao hawana cha kudai. Vinginevyo Serikali iwalipe kifuta machozi ili kuondoa manung' uniko mengi. Hata hivyo wengi wao wazee sana na wana umri mfupi wa kuishi.

Mheshimiwa Spika, ziko fedha zinalipwa kama *OC* katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya. Fedha hizi wakati mwengine zinapangwa kiasi fulani mfano shilingi milioni 12, lakini Hazina inapeleka pungufu ya Bajeti iliyopangwa. Hali inaleta matatizo mengi katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya kiutendaji. Ikumbukwe kuwa Mkuu wa Wilaya kazi yake sio kukaa ofisini bali kwenda vijijini kutatua kero za wananchi. Kama Mkuu wa Wilaya atakuwa hana fedha ya mafuta kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti itakuwa vigumu kutenda kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ipo *capital flight* kubwa inayofanyika kwa *Bureau de Change* kutokutoa risiti kwa wanaobadilisha fedha za kigeni. Upo pia mchezo wa *Bureau* hizi kupandisha bei ya kununua dola ya Marekani kuliko *Bureau* nyininge, kwa nia ya kukusanya dola nyangi mara moja na baada ya muda *Bureau* inafunga au kuuza duka kwa mfanyabiashara mwengine. Nashauri Serikali ifuatilie kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ipeleke fedha za miradi katika Halmashauri za Wilaya kwa wakati. Ucheleweshaji unafanya miradi isikamilike na kuleta usumbufu kwa wananchi. Inawezekana kabisa Serikali ikapeleka fedha kutegemeana na hali ya hewa. Mfano yapo maeneo yana mvua nyangi yatahitaji fedha za kuchimba mabwawa zipelekwe mapema kabla ya kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Spika, naiomba na kuishauri Serikali iweke mkazo na ukali kwa benki zetu ili ziwe na sera ya mikopo ya nyumba mikopo kuititia mishahara ya wafanyakazi ni kidogo sana, wabuni mbinu nyininge za kuweza kurudisha fedha za nyumba ili Watanzania waweze kujenga nyumba nafuu. Katika Wilaya ya Moshi Vijijini Mkoani Kilimanjaro eneo la Njia Panda ni eneo ambalo limekuwa haraka kwa makazi na kiuchumi. Nashauri Serikali iishauri *NMB* iweke tawi ili kunusuru fedha za wananchi na Serikali, kuna mizani ambaeo unafanya kazi saa 24.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali idhibiti *other financial institutions* ambazo zinatoa mikopo kwa riba kubwa sana (*above 22%*), mfano *Blue Financial* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wapo watu ambaeo wanakopesha walimu na wafanyakazi wengine bila kuijandikisha na *payback* ni 50%. Watu hawa wadai *collateral* kadi za *ATM*, vitambulisho vya Benki na kadhalika. Nashauri Serikali ifuatilie mfano ni Nzega Mjini wapo watu wa aina hii na wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZAKIA H. MEGHJI: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake kwa maandalizi ya Bajeti hii na kusimamia Bajeti iliyopita pamoja na matatizo mengi ya kiuchumi Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, suala la kuhakikisha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya nishati ili kuwa na uhakika wa umeme kupatikana kabla ya Januari, 2012 ihakikishwe kuwa fedha hizi zinapatikana. Jambo hili ni muhimu kwa sababu ni ahadi ya Serikali Bungeni na imeathiri sana ukusanyaji wa

fedha na hivyo kuwa chini ya mchango kwa kuwa uzalishaji viwandani umekuwa wa kiwango cha chini. Jambo hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, suala mikopo kupitia *TIB* kwa ajili ya wakulima, fedha zilizoongezewa *TIB* ni kuhakikisha kuwa *TIB* inaweza kutoa mikopo kwa ajili ya wakulima. Ni muhimu kuhakikisha kuwa mikopo hii pia inawafikia wakulima wadogo. Kwa maana hiyo ni vizuri kuweka asilimia maalum ya kuwapa wakulima wadogo na wa katilili uondoaji wa umaskini upanuke zaidi, kwa kuhusisha wakulima zaidi. Mchakato wa kuanzisha Benki ya wakulima nao pia uanzishwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya ujenzi wa nyumba, si rahisi kwa mtu mwenye kipato cha kawaida kuweza kujenga nyumba. Hata ukitaka kufanya hivyo kwa kutumia kipato chake itachukua miaka mingi kwa maana hiyo itakuwa vigumu kwake kwani vifaa vya ujenzi vinapanda bei kila siku. Sheria ya *Mortgage Financing* ilishapitishwa toka mwaka 2008, hivi sasa ni miaka mitatu. Japokuwa baadhi ya benki zinatoa mikopo lakini tatizo ni kuwa taratibu za *Mortgage Financing* zinazotumika na nchi nyengi hazitumiki. Riba ya mikopo hii ni kubwa sana na kwa hivyo si rahisi kwa mtu kuchukua mikopo. Ni vizuri suala hili la *Mortgage Financing* likashughulikiwa kikamilifu. Naamini pia baada ya *National Identity Card* kupatikana pengine kutakuwa hakuna sababu ya kutokufanya hivyo, kwa hiyo, ni muhimu utaratibu huu ukaanza.

Mheshimiwa Spika, suala la Serikali kukopa ndani ya nchi. Suala hili ni budi liangaliwe vizuri. Ilivyokuwa Serikali haikopi kutoka vyombo vya fedha nchini ilitoa nafasi kwa wafanyabiashara kuweza kupata mikopo na hivyo kuweza kuijendeleza kibashara, kuwekeza na kadhalika. Inaonesha kuwa kila asilimia ya mikopo ya Serikali ikiongezeka, mikopo kwa wafanyabiashara nchini inapungua.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni dunia imekumbwa na msukosuko wa kiuchumi. Tanzania kama sehemu ya dunia haikusalimika na mtikisiko huo wa uchumi kwani Tanzania yenye Bajeti tegemezi kwa kiasi kikubwa imeathirika kwa kupungukiwa misaada kutoka nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania kupitia Bunge ilidhinisha kiasi cha shilingi trilioni 1.7 ili kuyanusuru baadhi ya makampuni kutokana na mtikisiko huo wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, naitaka Serikali iwaeeleze Watanzania ni makampuni yapi yaliyonufaika na mpango huo? Ninaitaka pia Serikali itueleze kiasi hicho cha fedha kilichotolewa kilinusuru uchumi kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, katika mukutano huu wa Bunge Serikali iliagizwa ieleze wazi orodha ya makampuni yaliyonufaika na kiasi hicho kikubwa cha fedha za umma katika kunusuru uchumi lakini tunapomaliza mukutano huu wa Bunge Serikali hajawa tayari kutoa orodha ya makampuni hayo. Hii inatia shaka juu ya matumizi sahihi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, katika ripoti ya Mkaguzi wa Fedha za Umma tunaambiwa kuwa CAG hakupata ufanuzi wa zaidi ya shilingi bilioni 48 kutoka baadhi ya makampuni yaliyopewa fedha hizo za kunusuru uchumi na wala haielezwi ni utaratibu gani ultumika kufanya malipo hayo.

Mheshimiwa Spika, utata huu unaweka wingu zito katika mchakato mzima wa shilingi trilioni 1.7 zilizoidhinishwa kama mpango wa kunusuru uchumi.

Mheshimiwa Spika, shilingi yetu imeendelea kushuka thamani kila siku na Benki Kuu ya Tanzania haionekani kuchukua hatua yoyote kuinusuru hali hiyo. Hivi sasa bei ya *USD* moja sawa na shilingi 1650! Aidha, inaanza kuwa ni jambo la kawaida katika nchi yetu kufanya biashara kwa fedha za kigeni hususani dola ya Marekani. Hii ni kwa sababu watu hawana imani tena na shilingi

ya Tanzania ambayo inashuka thamani kwa kasi. Kufanya biashara kwa fedha ya kigeni ni jambo hatari sana kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, zamani Benki Kuu ilikuwa na utaratibu wa kuwa na hifadhi ya dhahabu kama njia mojawapo ya kudhibiti ubora/thamani ya shilingi yetu. Serikali ina mpango gani wa kurejesha utaratibu huo wa kuwa na hifadhi ya dhahabu katika Benki Kuu?

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni ubora hafifu wa noti mpya zilizoingizwa katika soko hivi karibuni. Noti hizi zimelalamikiwa kuwa ubora hafifu kwani zinachakaa upesi na zinachuja rangi. Ubora huu hafifu umesababisha urahisi wa kughushi noti na kupelekea wingi wa noti bandia katika soko jambo ambalo ni hatari sana kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, ninaitaka Benki Kuu kuhakikisha kuwa noti zinazoingizwa katika soko zina ubora unaokidhi viwango ikiwa ni pamoja na kudhibiti uwepo wa noti bandia katika mzunguko wa fedha.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. Napenda kutoa masikitiko yangu kwa Kamati kutoshirikishwa katika baadhi ya mambo muhimu yanayohusu uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili, mkutano huu unaoisha leo, Serikali illifanya mabadiliko ya fedha/Bajeti kwa kuhamisha shilingi bilioni 95 kutoka Wizara ya Ujenzi na kuziongezea katika Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi. Aidha, katika Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini iliyokataliwa na Bunge hili na baadaye Wizara hiyo ikaja na mpango wa dharura wa umeme utakaoiwezesha *TANESCO* kukopa jumla shilingi bilioni 523 kwa udhamini wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mambo haya yote Kamati ya Fedha na Uchumi haikushirikishwa ili itoe maoni yake na badala yake wanakamati waliyashuhudia mambo haya ndani ya Ukumbi wa Bunge sawa na Wabunge wengine.

Mheshimiwa Spika, naitaka Serikali itambue umuhimu wa wajibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi katika masuala muhimu ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru Mheshimiwa Waziri kwa mipango mizuri ya uchumi, hakika ikifanyiwa kazi Taifa letu litabadiilika japo kwa kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *VICOBA* imeonyesha uwezo mkubwa kusaidia wananchi hasa wa hali ya chini hasa vijijini ambayo *SACCOS* haina uwezo kama ilivyoonyesha *VICOBA* kwa namna zote, kwa kurejesha na hata kwa elimu ya ujasiriamali na kuleta umoja wa namna ya pekee. Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka kutoa kipaumbele kwa *VICOBA* na kutoa sera rasmi ili *VICOBA* vikopesheke na Benki kama inavyofanya katika *SACCOS*? Hakika nashauri ifanyike haraka kuingiza *VICOBA* ili tuwafikie wananchi wengi na kujenga Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, hongera nyingi kwa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kazi nzuri wanayoifanya. Uchumi wetu unakuwa vyema na zipo dalili nyingi nzuri na upo mwanga mbele ya safari yetu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu kodi, *tax base* yetu ni ndogo. Wananchi wachache sana wanashiriki kulipa kodi. Wananchi wengi wakiwamo wafanyakishara wanadhani kodi ni adui na si jukumu lao kulipa. La kufanya ni kuangalia njia zote za kupanua wigo wa kodi lakini kutoa elimu ya ulipaji kodi na umuhimu/faida ya kodi. Usimamizi mzuri wa fedha zinazolekezwa Halmashauri ili kujenga

barabara, shule, zahanati na kadhalika. Kazi hiyo ifanyike vyema ili wananchi waelewe kazi ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu MKUKUTA, dhana ya VICOBA ni nzuri sana. Jambo hilo lilielezwa kwa wananchi Mbinga na wamelipokea vizuri. Wizara kupitia Idara ya Kuondoa Umaskini imefanya semina na kuandaa walimu wa kuhamasisha. Vikundi vimeundwa katika Kata 12 bado 12. Walimu hawa bado mpaka leo hawajapata posho zao. Kazi iliyofanyika ni nzuri sana. Vikundi vingi vipo tayari sasa lakini wanaambiwa fedha hamna.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ifikirie kumaliza kazi kama ilivyoahidi kwenye Bunge la Tisa wakati Naibu Waziri kwa niaba ya Serikali akijibu swali langu. Narudia kusema kazi iliyofanywa ni nzuri ni vyema ikaisha na Wizara ikaeneza sehemu nytingine. Ni ukombozi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za Benki, mdhibiti wa mabenki ni Benki Kuu ya Tanzania, lakini inaelekea kama *BOT* hawapo kwa maana benki hizi zinaendesha mambo kama zitakavyo. Riba kwenye mikopo ipo juu bila sababu za kuridhisha na riba za amana ni ndogo sana hivyo zinakatisha tamaa mtu kuweka amana. Uchumi wetu unahitaji watu wawekeze kupitia mikopo lakini pia amana zinatakiwa.

Mheshimiwa Spika, pili, sasa hivi benki zimeanzisha *commission* kwa mtu anayeweke fedha kwenye akaunti ya mtu mwингine hutozwa shillingi 1,000, nadhani hii si halali. Kuna tofauti ipi ya mtu kuweka kwenye akaunti yake na mtu kuweka kwenye akaunti ya mtu mwингine?

Mheshimiwa Spika, benki hizi zinatengeneza faida kubwa sana kama inavyothibitishwa na *meganic* zao ya kila robo mwaka. Hii haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, malipo ya mishahara kupitia Benki, huu ni utaratibu mzuri wa kisasa lakini watumishi wetu wa vijiji ambako huduma za kibenki hazipo. Lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha (2006) aliahidi kuliangalia jambo hili lakini mpaka leo hakuna juhudhi zinazoonyesha kutatua tatizo hilo. Wafanyakazi hao hulazimika kusafiri kwa shillingi 5,000 hadi 10,000 kufuata mshahara na wengine hulazimika kulala na kurudi siku ya pili. Gharama hizi zinatakiwa zifidiwe na Serikali kwani wafanyakazi hawatakiwi kuingia gharama kupata mshahara wake. Naomba kupendekeza Serikali itengeneze utaratibu wa kuondoa adha hii.

Mheshimiwa Spika, Benki za Umma (*Twiga* na *TPB*), ni ukweli uchumi unakua lakini bado tunahitaji kuharakisha safari yetu. Benki hizi zimeweza kuhimili vishindo nya wakubwa na zinastahili pongezi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kuziongezea mtaji benki hizi hasa wakati huu ambao hatuna benki za kilimo na viwanda. Hivyo *Twiga Bancorp* pamoja na kumpongeza Mtendaji Mkuu na wafanyakazi iongezewe mtaji ili nayo ikopeshe katika kilimo hii itaongeza ushindani na *TIB* lakini wao sasa wanakopesha katika eneo la uchimbaji visima ili watu wapate maji ya kunywa na kumwagilia, *it is a good idea*. Wapewe nguvu pia hizi ni benki zinazoweza kuelekezwa kwamba asilimia labda 20 ya mikopo yao ilekezwe kwa wakulima na wanaviwanda vidogo.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Fedha ni chombo muhimu sana katika kusimamia fedha za umma. Pamoja na kusimamia ukusanyaji wa mapato na kubuni vyanzo nya mapato yatakayokidhi matumizi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii ina changamoto nydingi sana katika usimamizi wa mali za umma sasa je, Wizara imejipanga vipi ili kuhakikisha nchi yetu inakuwa na uchumi wa kuridhisha kwa wananchi wa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, upo ucheleweshaji wa kupeleka fedha katika Wilaya zetu kwa ajili ya maendeleo je, Wizara inalionna hilo kuwa ni tatizo sugu? Kama jibu ni ndiyo, Wizara imejipanga vipi ili kuepuka ucheleweshaji wa fedha za maendeleo katika Wilaya zetu?

Mheshimiwa Spika, kuna fedha ambayo huwa inarudishwa kutoka Halmashauri zetu ambazo zinatokana watumishi kuacha kazi, watumishi kustaafu na mtumishi kufa. Je, fedha hii inaingizwa kwenye Bajeti ipi? Na inatumikaje?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watumishi wengi sana waliostaafu bado hawajapata haki zao au kucheleweshewa malipo yao je, Wizara imejipanga vipi kuondokana na tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, fedha za wafadhili huchelewea kufika katika sekta husika ili kukamilisha miradi iliyopangwa na kusababisha miradi kutokamilika kwa muda uliopangwa. Je, Wizara inasemaje kuhusu hilo? Je, upo mkakati wa kuhakikisha fedha ya wafadhili inawasilishwa kwa muda uliopangwa kwa mpango kazi wa mradi husika?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nategemea Wizara itafanya jitihada za kuhakikisha uchumi wa nchi yetu unakua na kuimarishe mikakati ya ukusanyaji wa mapato ambayo yatasababisha kukidhi matumizi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu suala la kushuka kwa fedha ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatumia mikakati gani kufanya utafiti wa kina na hatimaye kubaini tatizo linalosababisha kushuka kwa thamani ya pesa yetu?

Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni sheria gani ya nchi inayoruhusu matumizi ya fedha za nje hasa dola za Kimarekani katika utoaji huduma na vilevile katika malipo ya kodi ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kushindwa kudhibiti matumizi holela ya dola za Kimarekani ndiko kulikopelekea kushusha thamani ya pesa yetu?

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ni lini sasa shilingi ya Tanzania itawekewa kinga na Serikali ili *transaction* zote nchini zifanywe kwa kutumia *legal currency* ambayo ni shilingi?

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza kuona Serikali inaruhusu matumizi ya pesa za nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali isimamie fedha yetu kikamilifu, kwani jambo hili halifanyiki kwa wenzetu wa nchi zilizoendelea ili kulinda nguvu ya pesa zao yaani *official currency* ya nchi husika.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Ushuru cha *TRA* ni sawa na mpiga ramli wa kienyeji cha kushangaza mimi binafsi niliagiza gari langu moja na la pili la Mheshimiwa Mipata.

Mheshimiwa Spika, magari mapya nilinunua toka Oman, Muscat cha ajabu kitengo cha *TRA* hawakuwa tayari kukubali risiti wala maelezo yangu hata baada ya kuwaeleza kuwa kama mimi nimedanganya hata senti moja nipo tayari kusalimisha hayo magari na kuwajulisha kuwa Muscat, Oman kuna Balozi wa Tanzania wamtume aende akselini kwenye hiyo kampuni walikataaa, pia niliaweleza nipo tayari hata kutoa nauli kwa mfanyakazi yeoyote wa *TRA* na kama akikuta nimedanganya nipo tayari hayo magari wataifishe maana ni mapya kabisa *Model 2011* na yapo *Show Room* yanauzwa kwa mtu yeoyote. Cha ajabu makadirio ya kwanza eti walikisia gari langu eti shilingi bilioni moja na la Mheshimiwa Mipata shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Spika, je, hiyo gari gani? Huo si upigaji wa ramli au kutafuta rushwa tu? Mwisho wa yote hata hivyo baada ya kulalamika sana haikusaidia kitu wameniibia kimachomacho labda sikutoa rushwa, gari langu wamezidisha zaidi ya shilingi 12,000,000/= gari la Mheshimiwa Mipata wamezidisha shilingi 8,000,000/= hiyo ni halali wakati nimetoa ushahidi wote

hata kusalimisha magari hayo kama nilichukua risiti feki na kusababisha hayo magari kukaa bandarini muda mrefu sana kwa ajili ya makisio ya ajabu.

Mheshimiwa Spika, wapi gari linauzwa kwa shilingi bilioni moja au milioni mia tano muanze kubishana kama mko kwa mganga wa kienyeji baada ya kutuungezea hiyo bei *TRA* wanatueleza eti wametusaidia sana kupunguza bei toka shilingi bilioni moja mpaka karibu dola zaidi ya 63,000 badala ya dola halali 53,000 yaani *RO 20,300* na la Mheshimiwa Mipata bei halali dola 31,000 *RO 12,300* sasa siku hizi kuna mtandao nchini kama chungwa mimi sikununua magari mwezini.

Mheshimiwa Spika, huo ni uwazi, ni wizi na njia za rushwa tu. Naomba haki itendeke nirudishiwe pesa zangu na Mheshimiwa Mipata. Hatukubali kuibiwa mchana kweupe hao *TRA* Kitengo cha Ushuru wao wanajifanya Miungu wadogo wakisema basi hakuna mjadala. Mjadala uwe na chochote hiyo haki ipo wapi na kukaa Kusini watumishi wa *TRA* maana mimi nimefika kwa Kitillya na hata kwa Waldi lakini hakusaidia kitu chochote kile, nimeonekana muongo mkubwa kabisa ila wao ndio wakweli, hakuna mtu anataka kudhulumu kodi, kodi ni haki, kila mtu alipe lakini kihalali.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri inayoifanya pamoja na shida nydingi zinazolikabili Taifa, ufinyu wa Bajeti na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua mpango wa *MCC* kwa Mkoa wa Singida umefika wapi. Mkoa huu ni wa mwisho kwenye orodha ya Mikoa maskini nchini lakini haukutengewa kabisa miradi ya *MCC* kama mikoa mingine iliyotengewa, na Wizara hii ilitutaka tuwasilishe miradi ya Wilaya ya Manyoni na Wilaya zingine za Mkoa wa Singida, kitu ambacho kilifanyika na kupewa ahadi kwamba miradi hiyo itaingizwa kwenye mpango wa *MCC* ili kuusaidia mkoa huo kupiga hatua ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu na nawasilisha.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wote kwa kuandaa Bajeti nzuri na kuiwasilisha vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza hasa kwa uendeshaji mzuri wa shughuli za Wizara ambayo ni kubwa na ngumu kuendesha.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza *TRA* kwa utendaji na jitihada zao. Bado ni muhimu kuongeza jitihada kwa kuwa bado mahitaji ni makubwa. Nashauri tuangalie *taxation of rental Income* wadogo waendelee kama ilivyo, lakini hawa wakubwa wenye *appartments* tuangalie sheria upya, tuondoke kwenye mahesabu, twende tu kwenye *direct taxation* ili tuboreshe *percentage* kutoka 10% twende juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa ndani, tunashukuru utaratibu mpya wa kuondoa utaratibu wa ajira hizi *say* kwenye Halmashauri na kadhalika inawapa wakaguzi hawa uhuru zaidi. Mategemeo watafaa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni uajiri watumishi wanaofaa na wa kutosha waajiriwe haraka na wapewe mishahara ya kufaa.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Spika, hongera kwa Waziri wa Fedha kwa hotuba yake ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kwa siku za karibuni kumeibuka tatizo la namna ya kulipa karo kwa wanafunzi/wanachuo kupitia mabenki. Aina ya misururu mirefu inayojitokeza katika mabenki wakati wa kufungua vyuo inaturudisha nyuma na kuwa kama kile kipindi cha *RTC* ambapo watu walibidi kupanga mawe kuwashikia nafasi kwenye foleni. Hali ilivyo sasa licha ya foleni hizo kuwa mateso kwa wanafunzi lakini mara nydingi imesababisha wizi au upotevu wa pesa

hasa kwa wanafunzi wapya. Vibaka hupata mavuno katika kipindi hicho kwani vijana wakijipanga tangu asubuhi bila kupata kifungua kinywa, inapofika mchana huwa wana njaa na hata kuanza kusinzia kwa sababu huwa wamechoka, pia kutokana na kuwa huwa wameamka mapema.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ikizingatiwa kuwa mabenki ni machache sana nchini hasa kwenye maeneo ya vijijini, vijana au wazazi wote hulazimika kusafiri mwendo mrefu kwenda Makao ya Wilaya kulipa karo. Mathalani Wilaya ya Magu inazo sekondari za Kata 39, hebu fikiria wanafunzi/wazazi wanaorundikana kwenye tawi moja la *NMB* kulipia karo katika kipindi cha siku chache. Hakuna namna nyininge ya kulipia karo hizo? Gharama ya usafiri na chakula hata malazi kwa mtu anayekwenda kulipa karo inaongeza gharama ya shule kwa wazazi maskini lakini pia ni adha kubwa. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atupatie ufanuzi wa namna ya kuondoa kero hii.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Busega Benki ya *NMB*, ilishatuma wataalam wake kuja kufanya utafiti wa kuanzisha tawi la benki katika Mji wa Lamadi. Sasa ni mwaka mzima tangu watu hao waje na hatuoni hatua zozote zimechukuliwa. Mji wa Lamadi wenye wakazi karibu 40,000 una biashara nydingi zikiwemo za mazao, utalii, maduka, mashine za pamba, mahotelii na kadhalika.

Naomba kufahamu ni lini benki hiyo itaanza kufanya kazi kwani mzunguko wa fedha uliopo ni mkubwa. Kuendesha biashara kwa fedha ya mfukoni ni hatari na inavutia ujambazi. Tunaomba tawi la benki Lamadi haraka.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na wataalam wa Wizara kwa hotuba iliyowasilishwa. Naipongeza Wizara kwa juhudzi za kuimarisha ukaguzi wa ndani, matumizi ya teknolojia za kisasa katika shughuli mbalimbali za Wizara na kadhalika. Hata hivyo, bado Wizara hii inahitajika kufanya maboresho/mabadiliko katika mambo mengi kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Fedha na Uchumi na Kambi Rasmi ya Upinzani. Kwa maoni yangu, mambo ambayo yanahitaji kufanyika haraka ni haya yafuatayo:-

Kwanza tathmini makini ya utekelezaji wa sera ya ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, pili, kuimarisha usimamizi wa Mashirika ya Umma kwa kuanzisha Ofisi ya Mashirika ya Umma (itakayosimamia Mashirika yenye hisa zaidi ya 51% za Serikali), na Kampuni/Shirikia Hodhi la Taifa (baada ya kurekebisha *CHC*) lenye kusimamia Mashirika yenye hisa za Serikali chini ya 51%, tatu, pendekezo la *windfall tax* kwenye dhahabu ili Serikali ipate mrahaba stahiki na nne, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ipunguzwe ili ibaki miwili tu (unaohudumia watumishi katika Serikali/Mashirika ya umma na ule unaohudumia watumishi katika Mashirika binafsi) na iwe chini ya usimamizi wa Wizara ya Kazi na Ajira.

Kadhalika, watumishi waliostaafu zamanii wakati mishahara (na mafao) ilipokuwa midogo waongezewe mafao yao kulingana na upandaji gharama za maisha. Aidha, watumishi wa Vyuo Vikuu vya Serikali (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na kadhalika) waliokuwa kwenye utaratibu wa pensheni wa *Senior Staff Superrannuation Scheme (SSSS)*, waliostaafu kabla ya Machi, 2011 wapangiwe utaratibu wa kulipwa pensheni ya kila mwezi kama watumishi wastaafuli wenza wanavyolipwa. Hawa sio wengi, hivyo Serikali isiwe na kigugumizi kuhusu hili na tano kwa kuwa Wizara hii ni muhimu kwa uchumi na maendeleo ya Taifa, watumishi wa Wizara wawe makini, waadilifu na wazalendo ili usimamizi wa fedha za umma uwe imara.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iziongezee mtaji Benki za Posta na Benki ya Twiga. Benki ya Posta ni Benki ya Serikali 100%. Ina mtandao mzuri nchi nzima na ni benki inayoweza kujitandaza katika Wilaya zote kwa urahisi. Hata hivyo, haiwezi kufanya hivyo sasa hivi kwa kuwa haina mtaji wa kutosha ili iweze kufanya biashara ya kukopesha kwa mapana na kuwekeza katika maeneo mbalimbali. Benki ya Twiga (*Twiga Bancorp Limited*) pia inamillikiwa na Serikali 100%, lakini nayo haiwezi kupanua shughuli zake za kibashara kwa kuwa na mtaji mdogo.

Mheshimiwa Spika, mimi ninashauri kuwa badala ya kuanzisha uititiri wa mabenki ambayo yatagharimu kiasi kingi zaidi cha fedha (mathalani Benki ya Vijana na Benki ya Wakulima

zilizopendekezwa), Serikali iziwezeshe Benki ya Posta na Benki ya Twiga kwa kuziongezea mtaji wa shilingi bilioni 15 kila benki ili zifanye kazi ya kuwakopesha wananchi pamoja na vijana na wakulima. Kiasi cha fedha hii kinaweza kuhamishwa kutoka kwenye Fungu 98, Kasma 4168 ya Wizara ya Ujenzi (ya Miradi maalum ya Ujenzi).

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii ningependa kutoa ushauri kwa Wizara hii ambayo ndiyo Wizara kiongozi na mhimili wa uchumi wa nchi yetu hasa kutohana na ukweli kuwa taasisi zote nyeti za kifedha zinazoshughulika moja kwa moja na mwenendo na uchumi wa Taifa letu kwa mfano Benki Kuu, *TRA* na Benki mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu kwa sasa lipo katika mtihani mkubwa hasa kutohana na kupanda kwa bei ya mafuta ya nishati ambayo ni petroli, dizeli na mafuta ya taa halafu kupelekea kupanda kwa thamani ya dola na shilingi yetu kushuka thamani kila siku.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Wizara ya Fedha kuhakikisha kuwa uchumi unaimarishwa kwa kuvutia uwekezaji wa vitega uchumi ili hatimaye nchi yetu iweze kuwa na bidhaa kuongezwa thamani badala ya hali iliyopo hivi sasa ya kusafirisha ng'ambo bidhaa ghafi.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kwa dhati kabisa kuchukua hatua ya kufufua viwanda nya kuongeza ubora wa zao la pamba ili kuliingizia Taifa fedha za kigeni na hivyo kuboresha pato kwa wakulima wa zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, uwianishaji wa mirahaba katika madini ya dhahabu yanayopanda bei katika soko la dunia ni vizuri Serikali ikaona uwezekano wa kuingiza kipengele kama hiki katika mikataba itakayokuja mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato (*TRA*) iongeze wigo wa ukusanyaji mapato kwa kuingiza pia sekta zisizo rasmi katika mfumo wa utozaji kodi.

Mheshimiwa Spika, aidha, naishauri Serikali kuliangalia kwa makini suala la utoaji wa mikopo kwa wananchi wengi zaidi na kupunguza riba kwenye mikopo inayotolewa na vyombo nya fedha hasa mabenki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja huku nikishauri pia uimashaji wa Soko la Hisa la Dar es Salaam na kushauri kufunguliwa kwa matawi ya masoko ya hisa Mwanza, Arusha na Mbeya ili kutoa nafasi ya kuwepo kwa fursa kwa Watanzania wengi zaidi kushiriki katika uwekezaji ndani ya nchi kwa kununua hisa katika masoko husika ya hisa.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mustapha Mkulo kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Fedha. Siyo kwa sababu yoyote bali uwezo wake, uadilifu wake na uchapakazi wake, ndiyo vimemfikisha hapo. Nimpongeze kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, aidha, niwapongeze Manaibu Waziri, Mheshimiwa Teu na Mheshimiwa Silima kwa jitihada wanazofanya katika Wizara ambayo ndiyo injini ya nchi. Bila kumsahau Katibu Mkuu Khija na Manaibu wake na watendaji wakuu wote. Kipekee na kwa umuhimu mkubwa nimpongeze Bibi Monica Mwamunyange (*CFB*) kwa utendaji wake wa umakini, usikivu, uvumilivu, upole na uwezo mkubwa wa kueleza hali halisi hata kama haiwezekani na unaelewa na kuridhika, pamoja na watendaji wake wote hasa Mr. Cheyo, Mr. Khamisi (maarufu) na Afisa anayehusika na Halmashauri kwa misaada wanayotoa katika maelezo na shida zetu za Kitaifa na hususan Wilaya ya Kilindi. Mrs. M. Mwamnyange ni *asset* kubwa kama *Tanzanite*, muilinde, muitunze.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilindi ilipatiwa Shilingi bilioni moja na milioni 500 kwa ujenzi wa jengo la Halmashauri mwaka 2007 lakini kutohana na mikataba tunaosema mbovu ulikuwa unatekelezwa kutokana na fedha zinavyopatikana. Kutokana na hilo kila baada ya mwaka fedha zikawa zinaongezeka kutokana na gharama kupanda. Hivyo, hadi leo ghorofa ya kwanza

imekamilika na tumelazimisha kuhamia juu na ukumbi unahitaji takriban bilioni mbili na milioni mia tano. Niombe tusaidiwe fedha hizo ili sasa mradi huu amba ni muhimu kwa Wilaya ya pembezoni ya Kilindi tukamilishe.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilindi haina Ofisi ya *TRA*. Wananchi wanalazimika kwenda Handeni kilomita 102 toka Songe, Makao Makuu. Hii inaleta ugumu katika ukusanyaji na ulipaji kodi, ila pia ni mwanya wa rushwa, kwani watumiaji wanahitajika kwenda Handeni, suala ambalo ni gharama na gumu. Kama mtu anakamatwa na *traffic*, pikipiki ime-expire leseni, analipa faini kisha analipia akakatiwe leseni Handeni. Inabidi asitumie pikipiki hata kama ni wiki kusubiri leseni, ilhali unakuta yeye ana bodaboda. Hivyo, akiendesha anakamatwa tena na kutoa faini. Je, anakamatwa mara ngapi mpaka leseni ije? Kwa vile huduma inapanuka kila siku naomba tupatiwe ofisi ya *TRA*, tupo tayari kutoa jengo kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Tume ya Pamoja ya Fedha, kwa kazi nzuri wanayofanya kwa mustakabali wa Muungano wetu, naomba wapewe msukumo na uvezeshaji zaidi ili jukumu lao liwe rahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, *TIB* (Dirisha la Kilimo) siyo la wakulima wadogo wadogo, hii si kweli kabisa. Dirisha hili limekaa kibiashara zaidi. Kama kweli imedhamiriwa kwa wakulima wadogowadogo, basi hatua za makusudi zichukuliwe, iweze kufahamika ni wakulima au vikundi vingapi hadi leo vimepata vikwazo, changamoto na matatizo ili tujue mapungufu na kutoa ushauri tuendaje.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliamua fedha zinazolipwa na wadau wa *EPA* ziende kwenye shughuli za kilimo *TIB*. Napenda kufahamu fedha hizo zinaporejeshwa zinakwenda moja kwa moja *TIB* au zinakwenda kwanza *BOT*.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara kama mdau mkubwa wa wizi wa Fedha za *EPA*, hivi karibuni kuna kesi ambazo zimemalizika na Mahakama ya Kisutu imetoa uamuzi na moja ya hukumu mbali na watuhumiwa kufungwa, ni pamoja na kufilisiwa mali zao, je, Wizara husika kama mdau, imejipanga vipi kimkakati kuhakikisha hakutokuwa na udanganyifu wa mali kwa watuhumiwa ili fedha hizo za umma ziweze kufidiwa kiuhalali.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa ni kiasi gani ambacho kimerudishwa kwa wale wote walioamua kurudisha fedha za *EPA*.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Spika, kuhusu *TRA*. Kwanza niipongeze *TRA* kwa kufanya kazi nzuri ya ukusanyaji wa mapato hapa nchini. Lakini pamoja na ukusanyaji huu mzuri bado *TRA* haijapanua wigo katika ukusanyaji huu wa mapato. Napendekeza kuwa Wizara iangalie uvezekano wa kupanua wigo wa watu kutoa kodi. Misamaha ya kodi pia ipunguzwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kwanza, nawapongeza watendaji wote wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutafuta wanachama na kutoa huduma bora kwa wafanyakazi hapa nchini pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Mifuko hii lakini bado kuna changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, *PSPF* na *PPF* inakabiliwa na changamoto za kutoakutoa mafao kwa wakati. Napendekeza kuwa Serikali ijithabidi kuboresha utoaji wa huduma kwa wastaafu kwa wakati. Vilevile kwa kuwa Mifuko hii ina fedha nzuri na inawekeza kibiashara basi napendekeza kuwa Mifuko hii iwekeze katika kutoa huduma nyingine kama vile umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwa kuwa nchi yetu ni maskini, hivyo, tupunguze kukopa. Hata kama duniani kote wanakopa lakini si lazima wakati wote tukope. Tupunguze utegemezi.

Mheshimiwa Spika, Wizara inapaswa kuwa na kitengo maalum cha maadili ya matumizi ya rasilimali za umma. Uwepo wa sheria hauwezi kufanya watu wasiwe wezi.

Mheshimiwa Spika, Wizara inapaswa kubuni mkakati mpya au mbinu mpya ya namna ya ku-*translate* ukua ji wa uchumi wa nchi ili uendane na maisha ya kawaida ya wananchi walio wengi.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe tamko juu ya malipo ya malimbikizo ya madeni ya Askari Polisi wa Mkoa wa Rukwa waliopunjwa katika malipo yaliyofanywa Aprili, 2011 ambapo kila *cheque* ya malipo ilikatwa Sh. 10,000/= na kusababisha mapunjo makubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe tamko ni lini watumishi wakiwemo Wauguzi, Madaktari, Mafundi Sanifu Maabara na Madawa na Walimu wa Mkoa wa Rukwa watalipwa malimbikizo ya madai mbalimbali kama vile posho za likizo, uhamisho, mafunzo, matibabu, *arrears* za mishahara?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe tamko ni lini wastaifu wa *East Africa Community* watalipwa madai yao (na wengine)?

Mheshimiwa Spika, Taasisi mbalimbali za Serikali kama vile, Mahospitali, Vyuo mbalimbali, Shule za Sekondari, Vyuo Vikuu zimekuwa zikidaiwa madeni mbalimbali kama ya wazabuni, maji, umeme na kadhalika. Je, ni lini Wizara au Serikali italipa madeni hayo ili wananchi waweze kuendelea kupata huduma bora na za kuridhisha kwa wakati?

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Manaibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu pamoja na wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri ambayo Mheshimiwa Mustafa Mkulo Waziri mwenye dhamana amewasilisha vema.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu malipo ya Pensheni kupandishwa sambamba na kupanda kwa mishahara. Ikumbukwe kwamba watumishi wastaifu wengi walifanya kazi miaka mingi iliyopita kipindi ambacho mishahara ilikuwa midogo sana kulingana na hali ya uchumi wa wakati huu. Hivyo, viwango hivyo haviendani kabisa na hali ya maisha ya sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kubadilisha viwango vya pensheni kila mishahara ya watumishi inapopandishwa. Hii itasaidia sana wastaifu kuweza kumudu maisha kwani sasa hivi wanashindwa kabisa kumudu maisha. Nategemea Mheshimiwa Waziri au Manaibu Mawaziri wa fedha wakati wa kujibu hoja za Wabunge watatoa maelezo.

Mheshimiwa Spika, tatu, malipo ya pensheni kutolewa Mikoani kwenye Ofisi za Hazina Ndogo. Napenda kuieleza Serikali kuwa utaratibu wa wastaifu kuendelea kurundikana Dar es Salaam Hazina kusubiri malipo yao ni adhabu kubwa sana kwa wastaifu. Naiomba Serikali kuhamishia huduma hii Mikoani kwenye Ofisi za Hazina Ndogo. Hii itawasaidia kupunguza gharama, kuondokana na adha ya kugongwa na magari Dar es Salaam kwani wengi wao hawajui kutumia taa za barabarani na wataachana na usumbufu wa kufuatilia kumbukumbu zinazokosekana kwa kurudi mikoani.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa taarifa za utaratibu utakaotumika utangazwe kupitia televisheni, redio, magazeti na mabango mbalimbali. Nina hakika tutakuwa tumeonesha upendo na kuwajali wastaifu. Nasubiri majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nne, marekebisho ya mishahara pamoja na Watumishi kulipwa malimbikizo. Kumekuwepo usumbufu wa watumishi wanapopanda madaraja au vyeo kutorekebishiwa na kulipwa mapunjo kwa wakati. Suala hili ukiwaliza waajiri wanasema sio wao bali ni Hazina. Naomba Serikali kuondoa kabisa kero hii ili watumishi wawe wanapata malipo kwa

wakati pamoja na kurekebishiwa mishahara yao. Nitashukuru endapo Serikali itapokea maombi yangu.

Mheshimiwa Spika, tano, malipo ya Mirathi. Vile vile kuna matatizo makubwa sana ya Wasimamizi wa mirathi kupata malipo kwa muda mfupi. Kwani kumekuwa na ucheleweshaji usio na msingi wakati walengwa wa mirathi hiyo wakiwemo watoto wakiendelea kupata shida. Naiomba Serikali ni lini ucheleweshaji huu utakwisha na huduma hii pia kutolewa Mikoani katika Hazina Ndogo kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, sita, gharama ya kununua magari ya Wabunge kuwa kubwa. Napenda kujulisha Serikali kuwa fedha walizopewa Wabunge za mkopo wa kununua magari ya kufanya kazi za Ubunge zimekuwa ndogo kulingana na magari bei kuwa kubwa. Hivyo, magari aina ya Mkonga yananunuliwa kwa Shilingi Milioni tisini, hapo bado gharama ya kulipa ushuru bandarini hujalipa pamoja na Serikali kuchangia gharama hiyo yaani *Exemption*.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuangalia upya namna ya kusaidia tatizo hili kwani wako Wabunge wengi ambao magari yao yapo bandarini wameshindwa kuyagomboa.

Namwomba Mheshimiwa Mkulo Waziri mwenye dhamana atoe majibu ili kuwanusuru Wabunge.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu ambao nategemea Serikali itaungana nami. Hivyo basi, naunga mkono hoja na nawatakia utekelezaji wenye tija kwa Watanzania.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri ye ye binafsi pamoja na Manaibu Waziri wa Fedha kwa kazi yao nzuri. Baada ya utangulizi huo naomba sasa nichangie kama ifuatavyo:-

Kwanza, Mifuko ya Mashirika ya Umma (*Social Security Funds*). Hotuba inaonesha kwamba Mifuko hii imekuwa ikikusanya michango ya wanachama na kulipa wastaifu wanachama wa Mifuko hii vizuri. Hata hivyo, Bunge tunahitaji kupata ufanuzi wa utendaji wa Mifuko hii katika maeneo nyeti yafuatayo:-

- (1) Ukwasi wake (*Liquidity of the Social Security funds*).
- (2) Uwekezaji (*Investments*).
- (3) *Risk Management reports*.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizo (1), (2) na (3) zitaliwezesha Bunge kuelewa kiwango cha usalama wa Mifuko hii na uwezo ziada (*excess financial capacity*) kuendelea kutoa huduma zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anaombwa kutufafanulia mambo haya.

Mheshimiwa Spika, ni changamoto ya kuongeza mapato ya Serikali. Mheshimiwa Waziri amebaini kuwepo kwa changamoto hiyo hapo juu lakini hakuna maeleo ya mikakati ya kukabiliana na changamoto hiyo. Nionavyo mimi ili kuikabili changamoto hiyo, yafuatayo lazima yafuatwe au yazingatiwe:-

Kwanza, uhakika wa umeme. Bila uhakika wa kuwa na umeme au kuendelea kuwa na mgao wa umeme kutasababisha uzalishaji viwandani ushuke sana au usiwepo kabisa na hivyo Serikali kukosa mapato. Serikali inashauriwa kuharakisha kutatua tatizo hili kama Wizara ya Nishati ilivyoahidi.

Pili, kupunguza misamaha ya kodi ya kutozidi asilimia moja ya *GDP*. Mapato mengi ya Serikali yamekuwa yakipotea kwa sababu ya kutoa misamaha ya kodi kwa wadau mbalimbali wanaotakiwa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inashauriwa kuzingatia ushauri wa kutozidi asilimia moja ya pato la Taifa. Naomba kauli ya Mheshimiwa Waziri kuhusu msimamo huu.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Fedha iwe inapeleka fedha za kutosha kwenye kasma husika. Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwenye Idara zote imekuwa ikipewa fedha kidogo mno na hivyo Halmashauri imekuwa ikishindwa kuleta huduma za maendeleo na huduma za jamii kwa wana Ludewa.

Mheshimiwa Spika, siyo sahihi kwa Mkuu wa *PPRA* kuitwa *Director* kwani yeye cheo chake ni zaidi ya hicho. Aldha, kwa kufanya hivyo *Heads of Procurements et cetera* ambao kimsingi ni *Directors* wanakosa stahiki za kuwa *Directors* kwenye idara zao.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji walioshiriki katika kuandaa hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kama miaka miwili au mitatu iliyopita Serikali iliahidi kuwa haitoruhusu tena Serikali kuendelea kuwakopa wananchi, kwa maana ya Serikali kushindwa kulipa madeni. Hivi sasa kuna madeni makubwa ya watumishi wa Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya, Wazabuni ndani ya Wizara hizo. Vile vile wale Mawakala waliosambaza pembejeo bado wanaidai Serikali. Kwa nini Hazina haitoi fedha kwa wakati na za kutosha ili kuondoa uwezekano na mrundikano wa madeni? Je, Serikali ikichelewa kuwalipa hawa, je, inatozwa tozo au riba?

Mheshimiwa Spika, mtikisiko wa uchumi duniani ulisababisha uchumi kuyumba katika nchi nyingi. Mtikisiko huu ulisababisha bei za pamba na kahawa kuporomoka kwenye soko la dunia. Matokeo yake Makampuni ya Watu Binafsi na Vyama vya Ushirika, walipata hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 ili uchumi wa nchi yetu usiyumbe, Rais Mheshimiwa J.M. Kikwete aliridhia mpango wa kunusuru uchumi na Bunge likapitisha kiasi cha fedha trilioni moja nukta saba (1.7 trilioni) ili walioathirika.

- Walipiwe au wafidiwe hasara na
- Walipiwe mikopo ya Benki iliyotokana na uchumi

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya uhakiki wa madai ya kila Taasisi na Hazina iliwajulisha ni kiasi gani watalipiwa (2010).

Mheshimiwa Spika, *KDCU* walilipiwa bilioni mbili ikabaki bilioni moja nukta tisa. *KCU* Hazina iliahidi watalipiwa 734,369,379.49, hadi leo hawajalipiwa kitu. *KNCU* Hazina iliahidi kuwalipia 255,107,570.17, hadi leo hawakulipwa fidia hiyo. Hazina hiyo mwaka huu Aprili 2011 imewaandikia *KCU* na *KNCU* kuwa hailipni tena fidia sababu hawana fedha na muda wa kulipa fidia uliishia 2010.

Mheshimiwa Spika, ni kutowatendea haki wote, hawa waliiza Kahawa kwenye Soko la dunia wakati huo, hivyo walipata hasara. Sasa madeni na riba yameongezeka hivi Vyama vitafilisika. Mfano, *KDCU* wanatakiwa kulipa 295 milioni kila mwaka benki.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika, wakati wa kilele cha Siku ya Ushirika mwaka huu, walikabidhiwa risiti ya Vyama vya Ushirika kumi (10) walikuwa bado wanaombwa kulipiwa deni la Sh.12,106,459,409. Ni lini itawalipa waathirika hawa ili wasije wakafilisika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa kuleta hotuba nzuri hapa Bungeni. Pamoja na pongezi hizi ninayo heshima kubwa kutoa machache na kuishauri Wizara hii. Nami nitafanya hivyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, matatizo ya *Cash Budget*. Utaratibu wa *Cash budget* kwa mtazamo wangu umekwamisha miradi mingi ya maendeleo kutekelezeka kwa wakati.

Napenda kutoa ushauri kuwa Serikali iachane na utaratibu huu wa *Cash budget* badala yake Serikali itoe *Warrant of fund* na iwepo *ceiling* kila robo ya mwaka badala ya kusubiri kukusanya na ndiyo ipeleke fedha za maendeleo. Fedha haziendi kwa wakati muafaka, matokeo yake miradi inapanda (*variation*). Serikali ikope fedha kutoka kwa wananchi kwa njia ya *Treasurer bonds* ili ijazilizie pale penye upungufu na kujenga miradi kwa wakati na pale itakapokusanya basi ilipe hiyo mikopo. Hizi *Treasurer bills* na *Treasurer bonds* kazi yake iwe ni kuziba pengo na kuhakikisha miradi inamalizika au inatekelezeka kwa wakati unaofaa.

Mheshimiwa Spika, pili, kupanua wigo wa kukusanya mapato. Kwa sasa Serikali inajitahidi sana kukusanya kodi katika nyanja mbalimbali ikiwemo bia, sigara, wafanyakazi na kadhalika. Bado kuna wigo mkubwa wa kodi ambazo bado hazijakusanya mfano, wapangishaji nyumba, mafundi ujenzi wa kawaida ambao hawajasajiliwa. Ni vizuri wajenzi wadogo hawa watambuliwe na Bodi ya Wakandarasi *CRB*, wajengewe uwezo ili waweze kulipa.

Mheshimiwa Spika, tatu, noti mpya toleo la mwisho. Noti mpya zilizotolewa hivi karibuni ni nzuri kwa muonekano hata ubora. Tatizo zinaghushiwa kirahisi ni kwa nini? Pia noti hizi inaelekea zilitengenezwa katika *size* ya kuweka kwenye pochi ili zisichakae. Noti hizi zinaonekana kulengwa watumiaji wa nchi zilizoendelea ambapo karibu kila mtu anamiliki pochi. Ndiyo maana noti hizi zinapopelekwa katika mazingira ya vijiji kwa akinamama baada ya kuuza bidhaa zao, pamoja na kuwa nzuri na zenye mvuto na pengine zenye ubora lakini inaelekea zisipotunzwa kwenye pochi zinaharibika haraka sana. Serikali iliangularie suala hili.

Mheshimiwa Spika, nne, hisa za Makampuni ya nchi za nje. Hadi sasa Tanzania au wananchi wa Tanzania hawaruhusiwi kununua hisa za makampuni ya nje ikiwamo na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wakati nchi wanachama wa jumuiya hizi ikiwemo nchi za Uganda na Kenya wanaruhusiwa kununua hisa za makampuni katika soko la mitaji la Dar es Salaam. Tatizo hili la Watanzania kutoruhusiwa kununua hisa nje ni kutokana na sheria za nchi yetu kutoruhusu wananchi wetu kununua hisa za makampuni nje. Je, hii sheria kuzuia watu wakati nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki nchi zao zinawaruhusu na hivyo wao kufaidika na Jumuiya ya Afrika Mashariki wakati Tanzania tunabaki nyuma. Nashauri sheria zote zinazozua Watanzania kununua hisa nje ya nchi ziletwe hapa Bungeni zibadilishwe haraka.

Mheshimiwa Spika, tano, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hapa nchini tunayo Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo *NSSF*, *LAPF*, *PPF*, *GEF* ambayo hupokea michango kutoka kwa wanachama wake kwa ajili ya mafao yao ya izeeni au kwa muda maalum. Mafao yao hutolewa pamoja na riba lakini riba hizi zinatofautiana sana na ziko chini ya *inflation rate*. Mfano, *NSSF* hutoa riba kati ya 2% - 2.5%, *LAPF* 5% - 7%. Utofauti huu unawaumiza hasa wale wanaojunga na hifadhi zinazotoa riba ndogo mfano *NSSF*. Pia hata riba ya 5% - 7% ni ndogo kwani iko chini ya mfumuko wa bei (*inflation*).

Mheshimiwa Spika, sita, ombi la Matawi ya Benki. Naomba Serikali izungumzie na benki mbalimbali ikiwemo *CRDB*, *NMB* na nyinginezo nyngi zipeleke huduma za mabenki (zifungue matawi) yake katika mji wa biashara wa Omurushaka, Wilayani Karagwe. Pia Matawi ya benki yanahitajika haraka katika Miji ya Nyairozi, Nyakaiga na Rwambaizi katika Jimbo la Karagwe, Wilayani Karagwe, Kagera. Kupeleka matawi huko kutapunguza wizi wa kutumia ujambazi na kupeleka huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MESHACK J. OPULKWA: Mheshimiwa Spika, natoa rai kwamba Benki ya Posta ifungue matawi katika Wilaya zote za Tanzania ili kuleta ushindani wa kibenki kati yake na *MMB*, lengo ni kuboresha huduma kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. PUDENCIA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Ofisi ya Taifa ya Taktamu (*NBS*). Ofisi hii imekuwa ikifanya kazi katika mazingira magumu na pia yasiyo na vitendea kazi vibovu. Aidha, Ofisi hii imekuwa ikifanya kazi zake yaani ukusanyaji wa taarifa mbalimbali kwa kipindi kirefu sana kwa mfano, kipindi cha miaka mitano mpaka kumi.

(a)Je, Serikali haioni umuhimu wa ukusanyaji wa taarifa mbalimbali kwa kuwezesha kujua mapungufu katika sera za maendeleo?

(b)Ni kwa nini ofisi hii imekuwa ikuza baadhi ya taarifa (*data*) kwa wanafunzi hasa wanaofanya utafiti?

(c)Je, Serikali inasemaje au ina mipango gani kuhusu kuongeza watumishi na pia kuwa na ofisi za kanda ili iwe rahisi kwa ukusanyaji taarifa mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, pili, je, Chuo cha Mipango, Dodoma (*IRDP*) ni lini ujenzi wa jengo la pili la taaluma utakamilika ili wanafunzi waweze kusoma bila matatizo ya madarasa kama ilivyo sasa?

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali inachukua hatua gani za makusudi ili kukikarabati Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*IFM*)?

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Manaibu wake, Katibu Mkuu, Manaibu wake na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2008/2009, 2009/2010, Mheshimiwa Waziri aliahidi kuwa Wizara itaanza ujenzi wa Majengo ya Chuo au Taasisi ya Uhasibu (*TIA*), Tawi la Mtwara kwa kuwa taasisi hiyo Tawi la Mtwara inaendesha mafunzo yake katika majengo yasiyo rasmi ndani ya Uwanja wa Maonyesho ya Wakulima ambao kwa sasa uwanja huo ni mali ya Chama Tawala, majengo hayo hayana hadhi kabisa ya kuitwa Chuo ukilinganisha na Matawi mengine nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri aliahidi kuwa mara tu ujenzi wa Chuo, Tawi la Singida utakapokamilika, ujenzi wa Tawi la Mtwara utaanza. Napenda kufahamu sasa ujenzi huo utaanza lini ili kutimiza ahadi ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara hii pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nimpongeze sana Mkurugenzi Mkuu wa *PPF* Ndugu William Erio na Wafanyakazi wote wa *PPF* kwa kazi nzuri wanazofanya kwa faida ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, wamejenga nyumba zaidi ya 400 za bei nafuu huko Mwanza na kuziwa kwa wananchi, jambo hili ni zuri sana kwa Watanzania wa kipato cha chini lakini ni faida pia kwa *PPF*.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iwashauri *PPF* waendelee na ujenzi wa nyumba hizi za bei nafuu katika maeneo mbalimbali hapa nchini hususan kwenye Wilaya ya Kinondoni ili wananchi wetu waweze kupata nyumba hizo ambazo ni nzuri sana. Pia niwapongeze *PPF* kwa ujenzi wa Chuo Kikuu, Dodoma hasa ujenzi wa kisasa wa kituo cha *Computer* hapo *UDOM*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo naomba *PPF* waangalie uwezekano wa kuwasomesha watoto wa wanachama wao waliofariki hadi Chuo Kikuu badala ya sasa kuwasomesha hadi Sekondari. Mpango huu ni mzuri na ni faraja sana kwa wanachama wa Mfuko huu pia elimu izidi kutolewa kuhusu mpango huu mzuri wa *PPF* ili wananchi wengi zaidi wajunge na Mfuko huu ili wafaidike na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LOLEIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa hotuba nzuri, pia nawapongeza Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto kubwa sana katika huduma kwa wastaafu na warithi. Nikichukulia tu Jimboni kwangu Busanda Wilayani Geita wastaafu wengi hawajapata mafao yao na wanahangaika sana. Wengine wamefuatilia sasa kwa zaidi ya miaka kumi na hawajafanikiwa kupata mafao yao. Wastaafu wengi hawana nauli maana wengi wanatakiwa kufuatilia Dar es Salaam. Pamoja na juhudzi zilizopo za kuboresha utoaji wa huduma hii lakini huduma hii bado ni kero kubwa sana kwa wastaafu na warithi. Hivyo, naomba Wizara iangalie namna ya kuwasaidia hasa wastaafu wa vijiji wasiokuwa na uwezo hata wa nauli ili wapate mafao yao.

Mheshimiwa Spika, kero ya pili ni madai ya malimbikizo ya bima kwa wanachama wake. Wanachama wengi wanalamika sana kwa sababu wamechangia michango yao vizuri lakini malipo kwa bima zilizoiva inakuwa ni usumbufu mkubwa sana. Kwa kuwa mapato ya bima yameongezeka kama ilivyoelezwa katika Kitabu cha bajeti, ukurasa 57, basi naomba wanachama wote wenye madai yao walipwe. Kama ulivyoahidi ndani ya hotuba kwamba *NIC* itaendelea na kuhakiki malimbikizo na madai yote kulipa ili kurejesha imani kwa wateja, naomba hoja hii itekelezwe kwa haraka ili wanachama wawe na imani tena kwa *NIC*.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

MHE. DAVID KAFULILA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu ubinafsishaji. Naomba Wizara ya Fedha itoe kauli mahsus kuhusu Mwekezaji kwenye Mgodi wa Chumvi, Uvinza. Mwekezaji huyu ni Kampuni ya *Great Lakes Mining* ambaye kwa mujibu wa mkataba aliahidi kuendeleza mgodi huu unaozalisha chumvi katika *Plants* tatu; *Solar plant*, *Thermal plant* na *PVD plant*. Badala ya kuendeleza Mwekezaji huyu ameamua kuuza mali za mgodi huu kama mitambo na nyumba tofauti na sera ya ubinafsishaji. Tulibinafsisha mgodi kwa bei ndogo ili uendelezwe sio uporwe, huu ni wizi. Naomba Wizara itoe tamko kuhusu wizi huu.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu mafao ya waliokuwa wafanyakazi kabla ya ubinafsishaji. Hapa naomba Serikali au Wizara ikutane na wafanyakazi takriban 300 walioachishwa kazi tangu mwaka 1999, lakini wamepunjwa mafao yao. Nimepitia barua za kuachishwa kazi wafanyakazi hawa, ukweli walipunjwa. Kuna wafanyakazi wamefanya kazi miaka 20 mpaka 40 lakini wameambulia mafao ya laki tisa mpaka milioni mbili tu. Naomba Wizara kuititia *CHC* au kadri Waziri anavyodhani inafaa watu hawa wapate kusikilizwa ili tupate ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili. Naomba sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashauri Serikali kuititia Wizara itafute majibu ya haraka ya kukabiliana na tatizo la thamani ya shilingi (*Currency devaluation*). Napenda kushauri Serikali itoe

msukumo mkubwa kwenye sekta ya umeme, reli, bandari, ndege na barabara. Haya ndio maeneo pekee yanayoweza kuongeza uzalishaji wa kasi na hivyo kudhibiti mfumuko wa bei na kujenga uchumi imara.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa machache hayo.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Vile vle naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu na Makatibu Wakuu na Watendaji kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kushuka thamani ya fedha yetu. Suala la kushuka kwa kasi fedha yetu inaathiri sana wafanyabiashara hasa wenyewe viwanda ambavyo wanategemea sana malighafi toka nje.

Mheshimiwa Spika, hili linaleta shida kubwa hasa pale viwanda hivyo vinatengeneza bidhaa ambazo wateja wake ni Serikali na inategemea sheria ya manunuzi. Bei ya malighafi inabadilika kwa kasi sana na hivyo viwanda kushindwa kuweka bei waliyotoa kwa zaidi ya wiki mbili. Hili linahitaji kuangaliwa ili tusije tukaua viwanda yetu vya ndani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo ya thamani ya fedha lakini pia sheria ya manunuzi ina mapungufu mengi sana na haitilii kipaumbele jinsi ya kusaidia na kuboresha viwanda.

Mheshimiwa Spika, nchi zote duniani zina Sheria ya Manunuzi ambayo inalinda viwanda vya ndani kwa kutoa asilimia ya mahitaji hasa ya Serikali kwenye viwanda vya ndani. Lakini kwenye Sheria yetu ya Manunuzi, vipengele vingi sana vinakandamiza viwanda vya nyumbani. Ni matumaini yangu kuwa katika kurekebisha sheria hiyo ya manunuzi hayo yatazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza Serikali kupitia Wizara hii ya fedha kwa kupitisha sheria ya ubia katika Serikali (umma) na Sekta Binafsi. Hili itasaidia sana sekta binafsi kuweza kuziba pengo la mahitaji ya Taifa na sekta binafsi. Hili likisimamiwa vizuri na Serikali linaweza kutatua matatizo mengi sana ambayo Serikali haiwezi kutimiza kwa ajili ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, ili uweze kupata ni lazima utumie. Serikali ilihimiza na wananchi kuitikia kwa vizuri uanzishaji wa vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali na kuanzisha pia vikundi wa *VICOBA* na *SACCOS* ambavyo vikundi hivyo vimekuwa vikijiwekea akiba na kujipatia mitaji.

Mheshimiwa Spika, vikundi hivi vya kuweka na kukopa vingi vimeduwa vikifanya vizuri sana na kuwaondolea wananchi umaskini. Napongeza sana Serikali kwa msaada wa kuimarisha vikundi hivyo. Lakini Mheshimiwa Spika, vikundi hivi bado vinahitaji msaada kukuza mitaji yao ili waweze kuwaflikia watu wengi kwa kipindi kifupi. Naomba Serikali ivisaadie vle vikundi vinavyofanya vizuri kwa kukopesha, kukopa na kulipa mikopo yake waongezewe mitaji kwa mfumo wa mkopo ili viweze kuwahudumia wanahisa wengi.

Mheshimiwa Spika, kuna kundi kubwa sana la vijana ambaa wamemaliza mafunzo ya vyuo vikuu na vyuo vya ufundi. Vijana hawa hali ilivyo sasa hivi hawana ajira wanapomaliza na hawawezi kujiajiri. Lakini hawa ni vijana wanaoweza kuchangia uchumi wa nchi ikiwa watapatiwa mitaji ili waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie ni namna gani inaweza kuwakopesha vijana hawa kwa kuweka mfumo mahsus kwa ajili yao. Vijana hawa hawawezi kujunga na *VICOBA* au *SACCOS* kwa sababu wanakuwa ndio kwanza wametoka shule na hawana kipato chochote. Napendekeza yeti vyao vichukuliwe kama dhamana ya mikopo yao. Serikali ikiridhia hilo itakuwa imesaidia kutoa ajira, kuondoa wazururaji na kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo mengi sana *TRA* kwenye kutoa bidhaa kwenye sehemu zinazoingia hasa bandarini na barabarani. Ukiwa na bahati utachukua siku siyo chini ya wiki mbili bila sababu za msingi, hii siyo tu inaleta usumbufuli kwa wateja lakini pia inapeleke wengi

kukimbilia kwenye bandari za Kenya. Hii inanyima mapato Serikali. Urasimu huu wa kutoa mizigo ni hata pale bidhaa inayoingia haina ushuru.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha mfumo wa malipo ya *TISS* kwa malipo ya zaidi ya Shilingi milioni kumi. Mtindo huo wa malipo unatumwa vibaya na mabenki mengine na kuchelewesha malipo wakati mwingine zaidi ya siku saba bila mtu kupata malipo. Hii siyo tu inaleta usumbufu kwa wateja, lakini pia kuchelewesha mzunguko wa fedha ambaao kwa upande mwingine unadumaza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuja huduma ya kifedha kutumia simu za mkononi *M-PESA*, *TIGO-PESA*. Naomba kujua ni jinsi gani Serikali inafaidika katika huduma hii ya kutumia simu hizi za mkononi.

Mheshimiwa Spika, kumekuja na wizi katika mabenki yetu kuititia hii huduma ya kupeleka pesa kutumia simu za mkononi. Lakini pia kumekuja na ripoti nyngi za wizi wa fedha kutumia *ATM* lakini pia kwenye mabenki na hata *TRA*. Hatua za haraka kudhibiti hali hii zichukuliwe kinyume cha hapo wananchi watapoteza imani na taasisi zao za kibenki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja.

MHE. PHILIP A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha (HAZINA) kuna ucheleweshwaji wa fedha kuingia Wizarani hasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis ambapo mpaka sasa malimbikizo ya madeni ya mishahara ni makubwa mno, jambo ambalo linaibebesha mizigo Serikali.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kule HAZINA kuwepo na dawati la Maafisa wawili kwa kila Wizara hasa Wizara hii yenye changamoto kubwa nchini yaani Wizara ya Elimu na TAMISEMI, Afya, Mambo ya Ndani na Kilimo. Jambo hili litapunguza mrundikano wa madeni ya Walimu, Wakufunzi, Wakaguzi, Madaktari na Maafisa Kilimo na kuleta ufanisi katika utendaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha kuititia Mabenki ya *CRDB* nia ilikuwa Benki hii ihudumie wanachi vijiji hasa wakulima, wenye Vyama vya Ushirika, lakini Benki hii leo haihudumii jamii lengwa bali inahudumia wananchi mijini. Je, wakulima wenye mashamba makubwa na hawana nyumba bora wanafaidikaje na *CRDB* maana hata maana yake ni *Commercial Rural Development Bank*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nashukuru kupata nafasi kuchangia katika bajeti ya Wizara hii. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Wizara kwa utendaji na jitihada kubwa inazofanya katika usimamizi wa fedha na kuinua uchumi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu tumekuwa tukitaarifiwa na Taasisi za Fedha kwamba fedha yetu inazidi kushuka thamani.

Mheshimiwa Spika, kiwango kinachochangiwa kwenye pato la Taifa kutokana na fedha za ndani ni kidogo mno. Wizara ijitahidi kuweka mikakati na mipango ya kuongeza kiwango cha fedha kinachoweza kutuingizia mapato makubwa.

Mheshimiwa Spika, kukopa kwa ajili ya miradi muhimu itakayochochea maendeleo ni jambo jema. Hata hivyo, ni muhimu tukaainisha mahitaji yetu na kuandaa mpango mkakati utakaoainisha vyanzo mbalimbali ambapo tunaweza kupata mikopo na masharti na kuijiwekea sera itakayobainisha namna ya kukopa kutoka nje na katika Benki zetu za ndani.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi na udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii ni chombo muhimu sana kwa Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini. Sekta hii inakabiliwa na changamoto

nyingi kama vile ghamama za uendeshaji na kadhalika. Tuliarifiwa na *SSRA* kuitia sheria za uzinduzi wa Mfuko huu kwamba itafanya tathmini ya Mifuko yetu na kwamba itabaki mifuko miwili. Aidha, wangefanya tathmini ya kuangalia uhai wa Mifuko iliyopo ya Hifadhi ya Jamii. Ningependa Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho yake atoe majibu kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni eneo la Taasisi ndogo za fedha yaani *Microfinances* na Taasisi zingine za kibenki. Kiwango cha mtaji kinachoainishwa kwenye kuanzisha taasisi za fedha upatikanaji wa mikopo yenyeye riba nafuu bado ni tatizo kubwa. Tunapoweka kiwango (*capital*) cha juu tunakwamisha juhudzi za wenyewe nia ya kuwekeza na kutoa huduma ya fedha kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa kuishauri Wizara hii kuweka mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato kwa kuwashauri *TRA*, mfano, hivi sasa sekta siyo rasmi inakua sana mijini na vijijini. Iwapo masharti ya upataji leseni na ulipaji mapato, ili kila Mtanzania aone fahari kulipa kodi Wafanyabiashara wagawanywe kwenye makundi manne:-

- (a) Wafanyabiashara wakubwa;
- (b) Wafanyabiashara wa kati;
- (c) Wafanyabiashara wa wastani; na
- (d) Wafanyabiashara wadogo kabisa.

Mheshimiwa Spika, kila kundi liwe na kiwango kinacholingana na kinachofahamika, tuepukane na mtindo wa sasa wa kila mmoja kujadiliwa kwa matakwa ya mkadiriaji kwa jinsi alivyoambiwa na mwenye biashara. Kibaya zaidi, wazalendo wajasiriamali hukadiriwa mapato na kutozwa mapato mara tu anapokwenda kutoa taarifa ya kusudio la kuanza biashara kwa mtaji alionao kabla hata hajaanza biashara. Tofauti na Mwekezaji kutoka nje hulipa mapato baada ya kupata faida. Hili liangaliwe upya, linasababisha ubaguzi kwa wazawa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ione haja ya kuwa na mpango wa kutoa motisha kwa walipa kodi bila ukwepaji ili kuhamasisha ulipaji kodi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza viwango vya kodi kwa wafanyabiashara ndogo iwe siyo zaidi ya asilimia tano ya mtaji alionao kwa mwaka. Hili likizingatiwa makusanyo ya fedha yataongezeka maradufu.

Mheshimiwa Spika, nimeona nitoe mchango wangu kuhusu ukusanyaji kodi na kuongeza pato la Taifa kwa kiasi kikubwa. Ahsante.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, ni tokea mwaka 2006 wizara hii imekuwa na kawaida kueleza kwenye Bunge lako tukufu juu ya ujenzi wa barabara za Pemba vijijini kutohana na changamoto za Milenia. Mwaka huu Waziri anasema mwezi Oktoba, 2011, ujenzi huo utaanza. Ninachotaka kujua kwa Waziri ni barabara za vijiji gani na mjenzi (*contractor*) ni nani.

Mheshimiwa Spika, kuna usumbufu mkubwa wanaopata wastaafu licha ya kuwa kuna mifuko kwa ajili ya wastaafu hao. Pia warithi wanapata usumbufu juu ya kupata stahili zao. Je, ni lini Serikali itaondoa usumbufu huo?

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa sita tokea 2006 bado imeshindikana kupata utaratibu wa ugavi wa fedha za misaada pamoja na kuchangia ghamama za Muungano, inavyoonekana suala hili limeshindikana. Ushauri wangu ni kwamba, wigo wa mjadala wa suala hilo upanuliwe badala ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar na timu zao. Pia kama itashindikana zile sababu za uwepo changamoto hiyo, kila Serikali iachiwe yenyewe itafute misaada nchi za nje na suala la ushirikiano wa Kimataifa kila nchi iachiwe ifanye kwa upande wake.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Tisa lilipitisha sheria inayohusiana na nchi yetu kwa kupitia mabenki kuwe na mikopo ya muda mrefu katika sekta ya ujenzi wa nyumba *mortgage*. Nchi yetu ujenzi wa nyumba inabidi wananchi wachukue muda refu katika ujenzi wa nyumba zao. Je, Wizara katika kuwafanya Watanzania waweze kujenga nyumba kwa mikopo ya muda mrefu imejipanga vipi? Ninavyoamini na ndivyo ilivyo sekta ya nyumba inaweza ikaleta fedha nyingi katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni utaratibu wa kawaida kila mwaka Serikali kuongeza mshahara wakati wa bajeti kwa wafanyakazi wa Serikali. Ingawa ongezeko hilo la mshahara huwa dogo, ni jambo zuri. Jambo la kusikitisha watumishi waliokwishastaifu, huu ni mwaka wa tatu hawajaongezewa pensheni zao. Nadhani umefika wakati wastaifu hao waongezewa pensheni zao.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) pamoja na majukumu mengine pia ina dirisha la kilimo. Hivi sasa kuna kauli mbiu ya "Kilimo Kwanza". Mikopo ya kilimo inategemewa itolewe na *TIB* wakati uwezekano wa kuendeleza kilimo kwa mikopo *TIB* ni mdogo. Je, Wizara iko tayari kuchukua hatua za dharura kwa kupata mtaji kwa *TIB*.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato na misamaha ya kodi holela, inapunguza mapato ya Serikali. Utafiti unaonesha kuwa, misamaha ya kodi inapoteza wastani wa asilimia sita ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itafute vyanzo vingine vya mapato na pia hii misamaha ya kodi kwa wawekezaji angalau ifikie asilimia mbili ya mapato ya Taifa. Pamoja na hilo, Hal mashauri zetu zinakusanya mapato kidogo sana, washauriwe watafute vyanzo vingine vya kuongeza mapato ili tuweze kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, kuna Makampuni mengi tu ambayo hayalipi kodi, mengine Wafanyakazi wa *TRA* hawayajui na mengine wanayajua lakini wanachukua rushwa na kuyaachia yale Makampuni yaendelee kufanya kazi bila kulipa kodi. Naishauri Serikali ifuatilie na wanaobainika kufanya hivyo, wachukuliwe hatua mara moja.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango katika Ofisi ya Rais imepitia Dira ya Taifa na kutafsiri katika Mpango wa Muda Mrefu wa utekelezaji ikianzia na Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano. Hata hivyo, Serikali haijaaeleza kinagaubaga, mgawanywo wa madaraka na mamlaka kati ya Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha na Uchumi. Tume ya Mipango ina mamlaka gani?

Mheshimiwa Spika, mabilioni ya fedha yanapotea kuwalipa wafanyakazi hewa na uliahidi litafanyika zoezi la kuwatambua wafanyakazi hewa wote na mpaka hii leo zoezi hilo halijafanyika. Sijui Mheshimiwa Waziri anaalewa kuwa kukawia kwa zoezi hili kunasababisha mabilioni ya fedha yazidi kupotea? Namwomba Waziri katika majumuisho aniambie ni lini zoezi hili litafanyika?

Mheshimiwa Spika, napongeza sana kukamilishwa kwa Sera, Sheria na Kanuni za Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (*PPP*). Muhimu tuelewe Miradi *IPTL, Richmond/Dowans* ni sehemu ya *PPP* na Taifa limepata hasara kubwa. Pia ni muhimu tuwe na Watendaji waadilifu na makini ili kunufaika na *PPP*.

Mheshimiwa Spika, huduma za *TRA* zina usumbufu mkubwa sana. Pamoja na kuwa *system* au mtandao, lakini usumbufu umezidi kuliko pale mwanzo walipokuwa wanatumia *manual*. Leo hii kila wakati unaambiwa *system* iko *down*; haieleweki kwa nini kila siku *system* inakuwa *down*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kulipa ushuru, kuna usumbufu mwengine wa kupata *Released Order*. Ukipika kwenye huduma hii, huyo Afisa wa *TRA*, kumtoa ofisini kwenda kukagua mzigo wako inabidi umwombe na huchukua siku mbili ndiyo anakwenda kukagua ule mzigo wako na akirudi kukagua huchukua siku mbili kupata *Released Order* nyingine kwa kisingizio mtandao unasumbua.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inatoza ushuru wa magari mkubwa sana, tofauti na kwenye makontena. Mtu mwenye gari lenye thamani ya USD 3000, hutakiwa alipe Sh. 6,000,000 na yule mwenye *container* la mzigo wa USD 100,000 hutakiwa kulipa Sh. 4,000,000 tu. Nataka nipiatiwe maelezo ya kina kwa nini ushuru wa magari unakuwa mkubwa na wa makontena unakuwa mdogo?

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Gavana Mkuu, Wenyeviti wa Kamati pamoja na Wadau wote wa Sekta hii muhimu na Wafadhili wetu wote ambao wametuwezesha kufanikisha Bajeti yetu leo. Natanguliza kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii mimi nitachangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tazizo la kushuka kwa thamani ya fedha yetu mara kwa mara ni kubwa sana, ambalo linafanya Wananchi wetu washindwe kuielewa Serikali. Hali hii inasababisha kupanda kwa bei za bidhaa, jambo ambalo Mtanzania wa kawaida linampa shida sana katika maisha yake. Fedha yetu imekuwa ikipungua mno kuliko za wenzetu, jambo ambalo linafanya bei ya bidhaa kama za mafuta kupanda. Mafuta yanapopanda bei kila kitu kinakuwa juu.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inasababisha hata bidhaa za hapa nchini nazo zipande bei, kwa sabau malighafi za viwanda vyetu tunapata kutoka nje na usafirishaji wa malighafi hizo unapanda juu.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali yangu siku ya Chama cha Mapinduzi kuwa, iweke mpango mkakati wa kuilinda hii shilingi yetu ya Tanzania isiweze kuyumba. Tukifanikiwa mkakati huu siyo kwamba haitashuka thamani, lakini itashuka thamani kwa nidhamu.

Mheshimiwa Spika, hali hii inasababisha hata uchumi wetu kuyumba; hivyo, Serikali ichukue juhudzi za makusudi kuinurusu shilingi yetu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika Mamlaka ya Kodi Tanzania (*TRA*), nitasimamia sana katika Mkoa wa Dar es Salaam, ambao ndiyo Mkoa wangu na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka hii inatusaidia sana katika ukusanyaji wa kodi na mpaka sasa tumebeba asilimia kubwa ya Bajeti ya Serikali kwa fedha zetu wenyewe, mapato ya ndani. Hili ni jambo jema ambalo linastahi kupongezwa. Nasema hongereni sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, palipo na mazuri pia kuna changamoto zake. Katika Mkoa wangu wa Dar es Salaam, mara nyingine utaratibu unaotumika katika ukusanyaji wa kodi unawakwaza Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka hii inatoa elimu ya kodi japo haipo wazi kwa wateja wadogo wadogo; hali hiyo inasababisha mlipa kodi mdogo kuburuzwa tu.

Mheshimiwa Spika, inafika sehemu Maafisa wa Kodi wanakuwa si wakarimu kwa Wananchi, wanakuwa kama maaskari na Wananchi wanachukuliwa kama siyo Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Afisa wa Kodi anatakiwa kuwa karibu na mlipa kodi kwa maslahi ya Taifa. Maafisa wanawapa shida walipa kodi, wanawafanya wakate tamaa ya kuendelea na biashara. Hali hiyo inasababisha Serikali ikose kabisa mapato na Mwananchi apate maisha magumu. Tujaribu ku-*balance*.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo kuhusu Makampuni ya Simu kutumika kama Benki; maana hata sielewi inakuwaje na nini hatima ya hizi Benki zetu?

Mheshimiwa Spika, fedha zinatumwa kama karanga hasa Mkoani Dar es Salaam kwenye Stendi Kuu za Mabasi ya Ubungo, Mwenge, Kariakoo, Buguruni, Temeke, Gongo la Mboto na Mbagala ndiyo kiboko.

Mheshimiwa Spika, mimi napata mashaka na hali hii; inawezekana Wananchi wanaibiwa na hasa pale wanapotuma fedha na zikawa na utata ambao unapelekeea kwenda Makao Makuu Dar es Salaam. Siyo rahisi Mwananchi wa kawaida atoke Bukoba au Rukwa kufuatilia Sh. 50,000 Dar es Salaam; fedha hizi zinapotea na Wananchi wanabaki na manung'unico tu.

Mheshimiwa Spika, japo imetusaidia sana kurahisisha huduma vijiji, lakini Serikali ijithidi kupeleka benki ndogo ndogo vijiji. Ukosefu wa benki vijiji ndiyo chanzo cha yote hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Hotuba hii katika swala zima la *TRA* na madalali wake.

Mheshimiwa Spika, *TRA* Kitengo cha *Investigation* mara nyingine kinaweza kuuwa watu kwa kupewa taarifa za uongo na chuki za kibashara.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema wazi kuwa, mimi ni mjasiririamali, nayasema haya nikiwa na uhakika maana yamenikuta.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi za kipekee kwa Mkurugenzi Mkuu wa TRA, Mr. Kitilya. Serikali haikufanya makosa kumteua huyu mzee, busara zake zimesaidia kuongeza makusanyo.

Mheshimiwa Spika, katika misukosuko ya *TRA* ukijaliwa kukutana na Mkurugenzi Mkuu ndipo unaweza kupona; vinginevyo, unaweza kufa kwa *BP*.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wananchi wanatumia vibaya Kitengo hiki kuwaangusha wenzao. Hivyo basi, naiomba *TRA* wawe makini na waangalie mazingira, mtatuua ndugu zenu pasipo hatia.

Mheshimiwa Spika, naomba Mkurugezi anipokee ofisini kwake nimpe changamoto za Wananchi wa Dar es Salaam katika swala zima la kodi.

Mheshimiwa Spika, kero nyingine kwa Dar es Salaam ni hawa Madalali wa TRA – Majembe. Jamani kuna malalamiko mengi Dar es Salaam, Wananchi hawafanyiwi uungwana na kujiona wapo katika Taifa lao Huru. Gari linakamatwa hata kama kuna mgonjwa mahututi hapelekwi hospitali kwanza. Je, kweli hii ni haki? Kisa kodi. Je, huyu mlipa kodi hana thamani kwa Taifa?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba *TRA* itupe angalau gawio la makusanyo Mkoa wa Dar es Salaam, japo kwa kutufanya jambo la kijamii katika Wilaya ya Kinondoni, Ilala na Temeke. Naomba Mkurugenzi atusaidie Shule za Watoto wenye Ulemavu wa Akili zifuatazo – Mgulani Walemaru; Mtoni – Maalum; Sinza – Maalum; na Shule ya Uhuru Walemaru.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ushauri wangu uzingatiwe.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kutoa mchango wangu kuhusu Hotuba ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo (Mb), aliyoiwasilisha Bungeni kkuhusu Makaridio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya kodi kwa kiasi kikubwa hayaridhishi. Kuna Makampuni ya nje yameanzishwa na wageni wakishirikiana na wenyeji na baadhi yao hawafuati ule utaratibu uliowekwa na Serikali wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri; je, kuna utaratibu gani uliowekwa na Serikali wa kuweza kubaini mashirika ya nje au wafanyabiashara ambao hawalipi kodi?

Mheshimiwa Spika, wastaafu wengi hapa nchini wanapata matatizo makubwa katika kufuatilia mafao yao. Serikali irekebishe utaratibu uliopo wa ucheleweshwaji wa mafao ya wastaafu. Utaratibu uliopo wa kufuata mafao yao Hazina Makao Makuu Dar es Salaam ni usumbufu kwa wengi ambapo huhitajika fedha za kusafiri kwenda Dar es Salaam, kulipia malazi na chakula, kwa muda wote watakaokuwa Dar es Salaam; ni vyema kuangalia njia nzuri ya kuweza kulipa wastaafu mafao yao mapema na kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, Makampuni mengi ya binafsi hayapeleki kwa wakati mchango wa makato ya mafao ya izeeni *NSSF, PPF* au kwenye mashirika mengine ya akiba. Ningependa kumwuliza Waziri; Serikali huchukua hatua gani kwa makapuni yale yote ambayo hayapeleki mchango ya makato ya mafao ya izeeni ya wafanyakazi wao? Endapo hawachukui hatua zozote, sasa inatoa kauli gani kwa Makampuni ya wazawa na ya wawekezaji ambayo hayapeleki mchango ya Wafanyakazi *NSSF, PPF* au kwa mashirika mengine ya akiba ya wafanyakazi? Wakati mwininge huchelewesha kupeleka mchango yao.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wengi wanapostaafu au kuacha kazi, hugundua kwamba, mchango yao ilikuwa haipelekwi kwenye shirika la akiba ya izeeni ya wafanyakazi; ni vyema Serikali ikatoa kauli yake ili kuondoa usumbufu uliopo kwa wafanyakazi ambao hawawekewi mchango yao ya akiba ya izeeni kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameeleza mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2010/11. Mojawapo ya azma ya Wizara ilikuwa kukuza Pato la Taifa kwa asilimia saba, kudhibiti *inflation* isizidi asilimia tano na kadhalika. Hata hivyo, inaonesha hali halisi haikuwa hivyo. Namwomba Mheshimiwa Waziri, alieleze Bunge lako Tukufu sababu mahususi zilizofanya wasifikie malengo ili iwekwe mikakati itakayosaidia kufikia malengo kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imesema ilikusudia kukusanya bilioni 53.49, lakini ilikusanya pungufu ya lengo hilo, yaani bilioni 30.98, sawa na asilimia 57.92, hii ni asilimia ndogo mno. Hofu yangu pengine malengo hayapangwi ipasayo (*too ambitions*). Pia Wizara imeshindwa kuelezea sababu halisi zilizopelekea kutofikia lengo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Deni la Taifa, kukopa ni jambo baya, lakini kwa sababu ya hali halisi tunawajibika kukopa. Hata hivyo, nchi yetu haipo makini hasa katika matumizi ya mikopo na hata misaada tunayoipokea. Kutokana na amani tuliyonayo hapa nchini, ningetarajia kuona mikopo ambayo inapelekea tuwe na madeni kila wakati inasaidia kututua kero zinazosumbua nchi yetu. Wananchi wa Tanzania ni waungwana sana, kwani si walalamikaji kutokana na madeni makubwa ambayo nchi yetu imekopa. Ushauri wangu; mikopo yote iwe yenye tija, ichangie kukuza uchumi wetu na nchi iweze kulipa madeni tunayokopa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi na udhibiti wa fedha za umma; katika eneo hili Serikali yetu haipo makini hata kidogo. Fedha nyingi za umma zimekuwa zikikwapuliwa mara kwa mara; aidha, kupitia Mikataba mibovu iliyotawaliwa na rushwa kubwa hata kuifanya Serikali ishindwe kutoa huduma muhimu za kijamii na kiuchumi hapa nchini. Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, zote kwa pamoja haziwezi kukwepa lawama za upotevu wa fedha nyingi za umma. Nashauri Serikali iongoze usimamizi wa udhibiti wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *TRA*, Maafisa wake wamejilimbizia utajiri wa kutisha. Serikali lazima iunde *Task Force* ya kuwachunguza Watendaji katika taasisi hii muhimu. Mishahara ya Watendaji wa *TRA* haiendi sambamba na utajiri walionao. Wavuliwe magamba.

Mheshimiwa Spika, nashauri *Paymaster General*, yaani Katibu Mkuu Hazina, awe makini na awe mkali sana. Kwa kuwa ni Alhaji, ahakikishe fedha na mali zote za umma zinatumika kwa manufaa ya Watanzania wote. Nashauri pawepo na *balanced development across Tanzania*.

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee kuhusu utekelezaji wa MKUKUTA. Malengo yote yaliyopangwa ni mahususi na yanalenga kuifikia Dira ya 2025. Hofu yangu; hatuko makini katika utekelezaji wa malengo hayo. Vipaumbele vyetu havijaainishwa vizuri. Lazima kama Taifa, tuelewe vipaumbele ambavyo vinaweza kuharakisha ukuaji wa uchumi. Tatizo sugu la umeme ni moja ya upungufu wa wazi ambaao Serikali yetu itafanya CCM ipoteze kuungwa mkono na Watanzania. Pia Mikataba mibovu ya uchimbaji madini ni eneo lingine ambalo litakwaza utekelezaji wa MKUKUTA, kwani bila ya fedha za kutosha kutoka ndani ya nchi, siyo rahisi kutekeleza MKUKUTA kwa fedha za wahisani. Vilevile Sekta ya Utalii ingeendeshwa vizuri ingechangia utekelezaji wa MKUKUTA na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, eneo la ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, naomba liendelee kupewa kipaumbele ili kusaidia juhudzi za Serikali kukuza uchumi wetu. Nashauri Serikali iweke mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi kuweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuititia Wizara ya Fedha, ihakikishe inaondoa kero zote za malipo kwa wastaafu na pia warithi walipwe haki zao za urithi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MKIWA A. KIMWAGA: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, kwani katika Matawi ya Wizara, upande wa *TRA*, baadhi ya mambo imekuwa kero, pamoja na kukusanya kodi ambayo ndiyo tegemeo la usukani wa uendeshaji wa nchi.

Mheshimiwa Spika, lazima *TRA* watambue wazi kuwa, kuna haja ya kuzalisha walipa kodi wengine na siyo kung'ang'ania walipa kodi wale wale ambaao wanakamuliwa hadi damu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna baadhi ya Makampuni kama *COTECNA*, wanatoza pesa kwa US\$ na si kwa Shilingi ya Tanzania. Hivi uthamani wa pesa yetu utakua lini kwa mambo hayo? Sasa ni wakati mwafaka *COTECNA* wameanza kutoza pesa kwa Shilingi ya Tanzania, huo ndiyo uungwana na uzalendo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri pia tukawa na uzalendo, kwani kuwaruhusu wafanyabiashara wakubwa kutozaguliwa bandarini na kukaguliwa nje ya bandari ni ukosefu mkubwa, kwani wao wafanyabiashara wakubwa ndiyo wakwepa kodi wakubwa na pia ndiyo waingizao bidhaa zilizo na kiwango na zisizo na kiwango. Tuwe makini sana tena sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuchangia Hotuba ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ushuru *TRA*, wafanyabiashara wa Zanzibar wamekuwa wakilalamika sana kuhusu suala hili. Wamekuwa wakitoza ushuru mara mbilimbi na hili linapelekea kuwaumiza wafanyabiashara hawa. Maafisa hawa waliopo Tanzania Bara ndiyo hawa hawa waliopo Zanzibar. Je, Serikali ina mkakati gani kuhusu kutatua tatizo hili la Wazanzibari kutoza ushuru mara mbilimbi na ikiwa Zanzibar ni Jamhuri ya Muungano? Hizi ndizo kero zenyewe za Muungano.

Serikali na Wizara inabidi waangalie kwa makini kuhusu suala hili la (*TRA*), wanawatoza wafanyabiashara ushuru mkubwa na hata wengine kufikia kusamehe bidhaa zao na kukata tamaa kuendelea na biashara zao. Je, Serikali haioni sasa hii ni kumkandamiza mfanyakibashara huyu na siyo kumwinua? Serikali na Wizara iangalie kwa makini katika Kitengo hiki cha Ukusanyaji wa Mapato *TRA*, kuna baadhi ya maafisa wamekuwa wakikusanya mapato haya kwa maslahi

yao wenyewe binafsi na kusababisha hasara kwa Taifa. Endapo itabainika kuwa wafanyakazi hawa siyo waadilifu katika kazi zao, basi wafukuzwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la Benki Kuu (*BoT*), kumekuwa na ubadhifuru mkubwa kwa Watanzania wasiokuwa waadilifu.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu ilitoa noti mpya lakini kuna baadhi ya Watanzania wasiokuwa waadilifu, wamezichukua noti hizi mpya na kuzichapisha na kutoa noti za bandia na kutumika kwa kununulia bidhaa mbalimbali. Hii imepelekeea hasara kwa wafanyakishara wengi. Watanzania wengi ambao hawana elimu hususan vijijini, hawawezi kuzitambua noti hizi mpya za halali na noti mpya bandia. Hizi noti mpya halali zimekuwa hazina ubora na zimekuwa zikichakaa haraka sana kuliko noti za zamani. Nilikuwa napenda kumwuliza Waziri; kwa nini noti hizi mpya hazina ubora na zinachakaa haraka kuliko noti za zamani? Serikali na Wizara wana mikakati gani kwa wahalifu hawa wanaotoa noti bandia ili wasiendelee kutoa na Watanzania waweze kutumia pesa halali?

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya wawekezaji wageni na baadhi ya Watanzania wenyewe hawaithamini pesa yetu ya Tanzania. Kuna baadhi ya hoteli zimekuwa hazitaki pesa zetu, ukila chakula wanataka ulipe kwa dola. Ulipaji huu wa dola umepelekeea kushuka kwa thamani ya pesa yetu. Je, Serikali na Wizara inasemaje kuhusu suala hili? Je, Serikali haioni kuwa hawa wanaofanya jambo hili wanaidhalilisha nchi yetu; mbona nchi za wenzetu kama Korea, Japan, China na nyinginezo ukifika kwao wanaithamini pesa yao hata ukienda kwenye maduka yao unalipa kwa pesa zao? Je, kwa nini sisi Watanzania tunashindwa kuithamini pesa yetu?

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi kufungua benki nyingi lakini benki hizi bado haziwanufaishi Wananchi wengi walipo vijijini. Mikopo mingi ya benki bado ina riba kubwa na masharti magumu, ambayo inapelekeea kwa Mwananchi; wakulima na wajasiriamali wadogo wadogo, kushindwa kukopa mikopo hii inayotolewa na benki. Baadhi ya Benki nyingine hawajaweza hata kufungua Matawi vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Benki ya Wanawake; Mheshimiwa Rais aliona umuhimu wa Benki ya Wanawake na akaifungua, lakini mpaka leo hii haina Matawi Zanzibar na hata baadhi ya Mikoa ya Tanzania Bara haina Matawi. Benki hii inanufaisha wachache na hainufaishi walio wengi kama Mheshimiwa Rais alivyowaahidi akina mama. Je, ni lini Benki hii itafunguliwa Zanzibar na Pemba ili Wanawake wa Kisiwa cha Unguja na Pemba nao waweze kunufaika na Benki hii? Tumekuwa mara kwa mara tunauliza suala hili tunapata majibu ya nadharia bila vitendo. Je, Waziri wa Fedha haoni sasa kuna umuhimu wa kuchukua jambo hili na kuliweka katika Mpango Kazi wa 2011/12 kwa kuwa Waziri ndiye mwenye dhamana husika?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wananchi wengi hasa matajiri walio wachache, wanakuwa wakikwepa kulipa kodi na kupelekeea mapato mengi ya Serikali kupotea. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha vyanzo vyote vya mapato ya Serikali vinadhibitiwa ili kuipatia Serikali mapato ya Taifa?

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja endapo nitapatiwa majibu kwa yote niliyoyachangia kwa maandishi hapo juu.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii katika vipengele visiviyopungua vitatu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naangalia ukusanyaji wa kodi unaofanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Nilipokuwa nachangia Bajeti Kuu, niligusia hili na leo narudia tena kuwa, kuna mianya mingi inayoachwa kwa wafanyakishara wakubwa ambao hawalipi kodi na kulipa chini ya halali.

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu nyingine ambayo ina upungufu mkubwa na ambayo inapoteza mapato mengi kwa watu au wafanyakishara wa kati na wadogo wadogo. Makusanyo madogo madogo hayatiliwi maanani au kupewa uzito wowote. Hii inabidi iangaliwe

kwa umakini mkubwa. Vilevile tuangalie jinsi gani tunapoteza kodi kwenye rasilimali muhimu kama madini, mathalani dhahabu, kuna taarifa zilizopo bei ya dhahabu duniani imepanda kwa kiasi kikubwa, tozo limekuwa likitozwa kwenye dhahabu kwa bei ya zamani. Inabidi *TRA* wawe na *system* ya kutoza kodi kwenye rasilimali muhimu kama dhahabu, iwe *dynamic*, kwa maana inabadilika kulingana na bei iliyopo sokoni, mathalani kwa wabia. Kwa sasa kilo moja ni Dola za Kimarekani 1760. Hii itasaidia sana kuongeza kipato cha nchi yetu. Ikizingatiwa dhahabu inayozalishwa nchini ni tani 60 kwa mwaka kwa mfumo wa *dynamic* wa kukusanya kodi nilioupendekeza, tungepata zaidi ya bilioni 400. Natoa rai Serikali kupitia Mamlaka ya Kukusanya Kodi (*TRA*), wawe makini kwenye vyanzo vingine vingi tu ambavyo vitaleta pato kubwa.

Mheshimiwa Spika, mikibaki hapa hapa kwenye Mamlaka hii, bado kuna upungufu kwenye ukadiriaji wa bei kwa bidhaa ambazo wafanyabiashara wetu huingiza toka nje; mfano, magari au *container*. Inasikitisha sana mtu analeta gari mathalani kutoka UK na imenunuliwa kwenye *reputable company*; mfano, mimi nilinunua gari kwenye BCA – Mnada wa Magari wa Uingereza na lilikuwa na *original invoice* na *details zote*, lakini ukija kulipa kodi gharama halisi ya *CIF* inapandishwa mara asilimia 300 zaidi; je, hii ni haki? Vivyo hivyo kwa vifaa vingine; mara nyangi tumeshuhudia Watanzania wanashindwa kulipa hizo gharama za kodi na kupelekea vitu vyao kuuzwa kwa mnada na Mamlaka ili wao wapate kodi yao na mwingizaji kukosa. Hii siyo *fair* kabisa na inakatisha tamaa kuona Wananchi wanaporwa mali zao kwa njia hii ya *ku-inflate* bei za vifaa na kutofanya *tracing* ya *invoice* ili kujua kama bei zile ni halali au la.

TRA waweke chombo kwenye nchi ambazo Watanzania huingiza (*import*), vitu kuleta nchini ili wawe wanahakiki bei kabla ya kuja Tanzania ili kuepusha unyonyaji huu ambapo tukishindwa kulipia kodi, basi vinauzwa na *TRA* na sisi tunakosa mwingizaji wa mzigo ule hapewi kitu. Hii ni sawa kweli? Naomba majibu kwa hili.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu hizi Benki zetu za Posta na Twiga; kwa kweli jinsi zinavyojiendesha inakuwa vigumu sana kuweza kushindana na Benki zingine zinazoendesha shughuli zao za kibiashara nchini Tanzania. Benki hizi hazina mtaji (*working capital*) wa kutosha kuweza hata kutoa mikopo yenye tija kwa wateja wake kama zifanyavyo Benki zingine zilizoko kwenye biashara hiyo. Hivyo; ni wakati mwafaka sasa Serikali izipe mtaji mkubwa Benki hizi ili ziweze kupata mtaji wa kukopesha kwa kiasi kikubwa, kwani ni dhahiri kabisa kwamba, biashara ya kukopesha ndiyo ambayo inatoa mapato makubwa kwenye Mabenki kutokana na riba zinazotozwa kwa wakopeshwaji.

Mheshimiwa Spika, Benki hizi zikiendelea kuachwa na mtaji wa sasa; ni dhahiri *zita-collapse*.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba Wizara iwe inatoa kipaumbele kwenye Wizara zinazohusika na utoaji wa ajira kwa vijana ili hawa wote waji-*engage* kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi na hii itaondoa kwa kiwango kikubwa, uhalifu nchini. Vilevile vipaumbele viende katika shughuli za maendeleo zenye kuwapa viwezeshi wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo waishio maeneo ya vijijini, kwani huko ndiko kuna wakazi wengi (*population*) ni kubwa sana tena sana, kuliko maeneo yoyote yale na ndyo maskini sana; mfano, kuweza kuwa na miundombinu imara ya barabara, umeme, maji na mingine mengi, ambayo ndiyo vichocheo vya ukuaji wa uchumi wa nchi, kwani viwanda vitaanzishwa na ajira itapatikana.

Mheshimiwa Spika, mwisho na kwa upekee kabisa ni kutoa uharaka wa dhati kuhakikisha *pension* kwa wazee zinatolewa kwa wazee wote. Kada hii ndiyo wanateseka sana, kwani wanalea watoto yatima, wanajihudumia kwa shida baada ya watoto wao kufa na kuachiwa mzigo mkubwa. Mwaka wa fedha ujao iwe tayari.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam, kwa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara iendelee na utaratibu wa kuanzisha *Budget Endowment Fund*. Fedha za kuweka kwenye *Endowment Fund* zitafutwe kwa nchi rafiki na kiasi kilingane na

bajeti nzima ya mwaka mmoja. Bajeti kama ilivyopangwa, itasimamiwa na Hazina kwa kutoa kiasi chote kwa kila *quarter* na kwa *quarter zone* nne kutoka kwenye *Budget Endowment Fund*.

Pesa inayokusanywa kutoka vyazo vyetu itarudishwa kwenye *Endowment Fund*. Kwa njia hii, *budget* itasimamiwa na kutekelezwa kama ilivyopitishwa na Bunge.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja. Pili, nawapongeza wote; Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Manaibu Waziri; Mheshimiwa Pereira Silima na Mheshimiwa Gregory Teu, kwa kuwasilisha vyema Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na kwa kuchapa kazi kwa bidii na kujitahidi kutimiza majukumu ya Serikali kwa uhakika na ufanisi. Nina hoja moja tu katika mchango wangu katika Wizara hii nayo ni malipo ya pensheni kwa wastaafu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali yafuatayo:-

(i) Je, Serikali ipo tayari kubadili mfumo wa kulipa pensheni kwa wastaafu kutoka kila baada ya miezi sita na kuanza kulipa kila baada ya miezi mitatu ili kuwasaidia kukabiliana na makali ya maisha?

(ii) Je, Serikali ipo tayari kuongeza pensheni toka 50,144 mpaka angalau 100,000 kwa mwezi?

(iii) Je, watumishi wa lilitokuwa Shirikisho la Afrika Mashariki katika Idara ya Shirika la Posta Tawi la Shinyanga watalipwa lini madai yao? Orodha yao nimeshaiwasilisha Wizarani.

(iv) Je, Hazina itawalipa lini Watumishi wa Chama cha Ushirika cha Shinyanga (SHIREKU) mapunjo na malimbikizo ya mishahara kama ilivyoahidi kulipa madeni yote ya Vyama vya Ushirika? Nitashukuru kupata majibu ya maswali haya.

Mheshimiwa Spika, ahsante kila la kheri.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, kuititia njia ya maandishi, nichangie Bajeti ya Wizara ya Fedha, ambayo pamoja na kuwa ni hazina ya faifa ni chombo muhimu cha kukusanya rasilimali zinazohitajika katika uendeshaji wa Serikali na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kuchangia juu ya jukumu la kukusanya kodi. Kodi ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa; ni jukumu na wajibu wa kila Mwananchi na asasi yoyote inayopaswa kulipa kodi kuyafanya hivyo. Serikali na *TRA* bado hajatumia kikamilifu fursa ya kuvuna rasilimali hii. Elimu lengwa inapaswa kutolewa, mfumo maalumu unapasha kubuniwa ili kila anayepaswa kulipa kodi afanye hivyo na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, bado kuna upungufu katika ukusanyaji wa kodi, hata kwa hao ambao wamejitokeza au kubainishwa kuwa ni walipa kodi, zinahitajika jitihada za ziada ili kumwezesha mlipa kodi ye ye mwenyewe ajitokeze kulipa kodi. Hii inaendana na mkakati wa kujenga utamaduni wa kulipa kodi. Sambamba na kujenga utamaduni, mikakati ifanyike kuhakikisha walengwa wanalipa kodi ikiwemo kutumia hata nguvu.

Mheshimiwa Spika, moja ya mbinu za kuenga utamaduni wa kulipa kodi ni uboreshaji wa mahusiano ya wadau watatu muhimu katika ukusanyaji kodi. Mlipa kodi atashawishika zaidi na kupenda kulipa kodi iwapo ataona kuwa mtumia kodi (Serikali), anaitumia kodi hiyo kwa malengo yaliyokusudiwa na mlipa kodi huwa na imani pale anapoamini kuwa mkusanya kodi anamtendea ipasavyo katika mchakato wa kutathmini na kukusanya. Zaidi ya mchakato ni kuona au kuaminishwa kuwa huyo mkusanyaji anafanya hivyo kwa maslahi ya Taifa si kwa maslahi binafsi. Sekta nzima ya ukusanyaji kodi ina upungufu katika vigezo nilivyoviainisha hapo juu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Idara au Vitengo vingine ninavyokusanya kodi kwa maslahi ya Taifa, nzungumzie *TRA*. *TRA* bado inayo nafasi kubwa ya kuongeza mapato yatokanayo na ushuru/kodi. Sehemu yenye mwanya mkubwa ni eneo la Bandari na Viwanja vya Ndege. Wapo

wadau wanaowezesha kuondoa mizigo katika vituo tajwa hapo juu, *Port Community*, pendekezo langu ni kuwa, *TRA* ichukue jukumu la uongozi kwa kuhakikisha katika jukumu la kukusanya kodi, isiwepo Idara yoyote inayachelewesha au kuzembea katika mchakato mzima wa kukusanya kodi. Lengo hapa ni kuhakikisha *Port Community* inamwona mtoa kodi kama mteja na wanapompatia huduma katika hali itakayomfanya ashawishike kutumia huduma na hatimaye ushuru/kodi kukusanya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nizungumzie mashine muhimu katika ukusanyaji wa kodi na ushuru. Mashine hii ni Sekta ya Mafuta ya Jamii ya Petroli na gesi aina zote. Mapendekezo yangu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali kupitia Idara zake na *TRA* ihakikishe jinamizi la mafuta ya taa halirudi kutupotezea mapato. Nguvu zielekezwe kwenye kudhibiti mafuta ya ndege na mafuta yapitayo. Nimewahi kushauri inapobidi nguvu au taratibu za kale zitumike.

Pili, tunapoelekea kwenye umeme utokanao na mafuta, mipango mikakati maalum iandaliwe ili mafuta haya yasiingie sokoni na kutukosesha mapato.

Tatu, kwa kuwa majirani zetu wanapenda/wanalazimika kupitisha mizigo yao kutumia bandari zetu. Shuhguli hizi zihamasishwe ili kuongeza matumizi ya mafuta ambayo yatatupatia ushuru wa kodi hasa *diesel*.

Nne, Serikali kupitia Wizara hii isimamie na kusukuma uboreshaji wa miundombinu ya upakuaji na utunzaji wa mafuta ili kuongeza ufanisi katika shughuli.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo wa mizani katika Barabara Kuu unasababisha Serikali kupoteza mapato. Kwanza, kumekuwepo na mlolongo mrefu katika mizani, magari yanapiga foleni hata mita 1,000 au zaidi. Kunakuwepo na ucheleweshaji wa safari kwa sababu hii. Pili, mizani ya aina hii ipo mingi. Tatoo, kunakuwepo na askari polisi ambao hunyanyasa madereva na wasafiri hapo katika mizani.

Mheshimiwa Spika, yote haya yanawafanya wenye magari kukwepa kutumia barabara zetu kama wanaweza. Gari linatoka Bandari ya Mombasa kwenda Burundi, linakwepa kuja Tanzania badala yake linakwenda Uganda hadi Burundi. Jitihada zifanyike turekebishe hali hii ili tusiendelee kupoteza mapato.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Mheshimiwa Spika, mpaka hivi sasa jumla ya Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa ni 331. Mengi ya ubinafsishwaji uliofanyika umegubikwa na wingu la tuhuma za rushwa. Zoezi zima limefanywa bila ya uwazi. Inashangaza mashirika haya yaliuzwa kwa jumla ya shingili 480 bilioni. Hizi ni fedha kidogo sana hasa ukitambua ya kuwa, baadhi ya mashirika haya ni makubwa sana na bei ya wastani ya shilingi 1.5 bilioni ni kidogo mno.

Mheshimiwa Spika, lazima hatua za dharura na za haraka zichukuliwe kuepusha Mashirika mengi ya Umma yasiuzwe kwa bei ya kutupa.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo (Mb), ambaye ni Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri wake wawili; Mheshimiwa Gregory Teu (Mb) na Mheshimiwa Pereira Ame Silima (Mb), pamoja na Watendaji wote wa Wizara husika, kwa kuwasilisha Bajeti ya Wizara husika kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hoja hii, namwomba Waziri na Watendaji wake wanijibu maswali yafuatayo:-

- Wizara imejipanga vipi kuhakikisha kuwa inapunguza Deni la Taifa badala ya kuliongeza?

- Kwa nini Benki Kuu ya Tanzania iliamua kubadilisha noti za zamani na kuleta noti mpya? Noti za zamani zilikuwa na dosari gani? Je, ina maana Wizara imeshindwa kudhibiti noti bandia zilizozagaa mitaani?

- Mfumo upi unaotumika kupata dola au fedha nyingine za kigeni toka Benki Kuu? Kwa nini mtu binafsi hawesi ku-request US \$, Pounds or Euro toka Benki Kuu? Je, Wizara haioni kuwa haiwatendei haki Watanzania wanaotaka fedha hizo toka Benki Kuu? Kwa nini Benki Kuu isianzishe Kitengo Maalum cha kuwahudumia wafanyabiashara maarufu au wanadiplomasia ili waweze kupata huduma hii kwa urahisi badala ya kulanguliwa na *Bureau Exchanges*?

- Je, Wizara imejipangaje kudhibiti uvujaji au matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmasauri zetu; katika Mashirika ya umma kama vile TPA na katika Idara mbalimbali za Serikali?

- Hazina inasema nini juu ya mishahara hewa inayolipwa kwa watumishi hewa wa umma?

- Je, Mradi wa *Self unawanufaishaje Wananchi walio pembezoni mwa nchi kama wale Wakurya wa Tarime?*

- Manunuzi ya umma hutawaliwa na rushwa na hasa hasa *ten percent*. Je, Serikali inasema nini juu ya hii kansa?

- Pamoja na kwamba *TRA* inafanya juhudzi za mara kwa mara kukusanya mapato lakini inasemekana wazi kuwa kuna mianya mingi ya ukwepajji wa kodi toka kwa wafanyabiashara wakora wanjanja. Je, Wizara imejipangaje ili kukabiliana na hali hii?

- Kwa nini Wizara ya Fedha isisimamie maeneo nyeti ya ukusanyaji fedha kama vile bandarini na badala yake wanapewa Wahindi kuhifadhi mizigo ya wateja katika magodown (*warehouses*) ambapo wafanyabiashara hutozwa fedha nyingi sana? Kwa nini *TRA* isianzishe Bandari ya Nchi Kavu Mjini Dar es Salaam ili ihifadhi makontena yote ya wateja badala ya kuyahifadhi kwa Wahindi?

Mheshimiwa Spika, mwisho wa yote, naunga mkono hoja.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, tuna noti mpya za fedha ambazo zina sifa moja tu ya udogo katika kuzibeba, lakini kwa sehemu kubwa noti hizo hazina ubora unaofaa, ikiwemo uchakavu kirahisi pamoja na urahisi katika *kuzi-forge*; hivyo, katika mzunguko wa fedha kunakuwa na fedha nyingi feki. Je, Serikali kupitia Wizara yake ya Fedha na Uchumi itueleze ni namna gani imeweza kukabiliana na hali hiyo tangu imeingia katika mzunguko? Pia Serikali itueleze ni kwa nini hali hiyo imetokea katika mwaka huu na katika noti hizi za fedha?

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi sasa Serikali imekuwa ikitegemea vyanzo vilevile vya mapato ilhali Tanzania ni nchi yenye rasilimali nyingi, zinazoweza kuwa ndiyo mhimili wa vyanzo vya mapato. Hivyo basi; ni kwa nini kila mwaka kodi katika vile vinywaji baridi pamoja na sigara ndiyo vimekuwa mhimili ya mapato katika Taifa letu? Tunaomba maelezo katika hili.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni Sera ya Taifa letu kwa wawekezaji kusamehewa kodi tena kwa kipindi kirefu, kwa miaka kumi, tofauti na wazawa ambaa mara tu siku ya kwanza anapoanza biashara yake, anatakiwa kulipa kodi. Je; ni kwa nini tunawarudisha nyuma wafanyabiashara wazawa tofauti na wageni? Sasa je; ni kwa nini wazawa nao wasipatiwe *grace period* pale wanapoanza biashara yao. Kwa nini tusianzishe sheria itakayowalinda wafanyabiashara wa ndani wenye mitaji midogo kutokulipa kodi kama *grace period* mpaka pale biashara zao zitakapotengemaa?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, hoja yangu kwa Wizara ni moja, ambayo nilishaifafanua kwa kina sana kimaandishi katika Hotoba ya Bajeti na Hotuba ya Waziri Mkuu. Sitalizungumizia kwa kina hapa, kwa sababu ninaamini mlipitia mchango husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sikupata majibu, naomba nijibwi kero hii kubwa ya *TRA*, inapokadiria kodi kwa kutozingatia vigezo wanavyoamua wao. Vigezo ambavyo havizingatii Sheria ya Forodha ya Mwaka 2004 ya *EA*, halikadhalika vinapingana na Mikataba ya *WTO*.

Mheshimiwa Spika, sheria husika zimeeleza kwa kina sana, hatua kwa hatua, namna ambavyo kodi inatakiwa kutozwa na kila hatua ina kigezo chake na ili kuweza kuruka kigezo kimoja kwenda kingine ni lazima kuwe na sababu za msingi, maeleo kutolewa na mteja kujulishwa. Cha ajabu, *TRA* wamekuwa wakifanya uhuni na kuruka vigezo/masharti/vifungu vyote vya mbele na kurukia hatua ya ukadiriaji wao.

Mheshimiwa Spika, hii ni kero kubwa; kuagiza bidhaa nje imekuwa ni kero na mzigo kwa kila mtu! Kama nilivyosema, michango yangu iliyopita nililieleza hili suala kiufasaha sana na kuainisha jinsi ambavyo sheria inakiukwa kwa makusudi. Naomba Serikali itoe kauli kuhusiana na hili! Ubabe huu ndiyo kichocheo cha watu kudanganya na kuiibia Serikali. Sitegemei kuandika hoja hiyo mara tatu na isipate majibu.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba Serikali itoe tamko kuhusiana na mustakabali wa Shirika la UDA hasa ikizingatiwa kwamba, yenye ni sehemu ya mmiliki ikiwa na hisa asilimia 49.

MHE. MUNDE A. TAMBWE: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa umma, kumekuwepo malalamiko kwa Wananchi kuhusu utekelezaji mbovu wa Kanuni za Manunuzi *assets* za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nchi imeingia kwenye giza kwa kukosekana umeme wa uhakika, jambo ambalo Serikali imeshindwa kununua mitambo mipya ya majenereta kutohana na uhitaji wa Kanuni za Manunuzi ambazo zinaitaka Serikali kununua mashine na mitambo mipya ambapo ni gharama sana.

Mheshimiwa Spika, huko vijiji Vituo vya Afya na Zahanati hazina magari ya kubebea wagonjwa na kusababisha vifo vingi hasa pale wagonjwa wanapopewa rufaa kwenda hospitali nyiningine.

Mheshimiwa Spika, sheria hii haina tija katika nchi yetu ukilinganisha matatizo na mahitaji ya Wananchi kupata huduma mbalimbali kwani uwezo wa fedha ya nchi yetu ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mahitaji ya nchi yetu kuwa na ndege, meli, vichwa vya treni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tukiendelea na Kanuni hizi za Manunuzi, hatutaweza kununua ndege, meli na vichwa vipya vya treni. Nashauri Kanuni hii ifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ndiyo injini ya uchumi wa nchi na ina nafasi ya pekee katika kuweka mazingira bora ya kuboresha maisha ya Wananchi. Hivyo, Bajeti ya Wizara hii pamoa na muda wa kuijadili unapaswa kuongezwa. Aidha, Wizara inapaswa kuweka kipaumbele cha kwanza kuongeza kiwango cha mapato ya Serikali.

Wizara irejee vyanzo mbadala ambavyo nilivieleza kwenye Bajeti Mbadala ya Nishati na Madini, tarehe 15 Julai, 2011. Baada ya kuchambua vyanzo hivyo, Wizara ilete bajeti ya nyongeza (*Supplementary Budget*) na kuleta Marekebisho ya Sheria ya Fedha ili Taifa liweze kusonga mbele kwa kasi zaidi katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Aidha, katika kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha, Serikali ikubaliane na mapendekezo niliyoyatoa tarehe 22 Juni, 2011, yenye

kupunguza kodi ya mafuta ya taa, dizeli na petrol ili kuondoa mzigo wa gharama za maisha kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha iongeze kasi ya kuharakisha fedha za Miradi ya Maendeleo zinazopangwa. Kiwango cha chini ya asilimia 30 ni kidogo sana. Wizara iweke kipaumbele maalum kwa Miradi ya Maji na irejee viwango vya fedha vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano. Mfano, wakati mpango ulielekeza katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 zitengwe bilioni 26.8 kwenye Mradi wa Kidunda, Bajeti ya Wizara ya Maji inatenga shilingi bilioni 6.5 pekee. Hivyo, Wizara ihakikishe kwamba, fedha za mkopo toka India kwa ajili ya Miradi ya Maji pamoja na za vyanzo vingine, zinafika zote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi yetu utakua iwapo viwanda ikiwemo vilivyobinafsishwa, vitafanya kazi ipasavyo. Wizara ya Fedha ina nafasi ya pekee ya kuchangia katika azma hiyo hususan kwa vile viwanda ambavyo Serikali ina hisa na umiliki. Hivyo, nakubaliana na maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu marekebisho kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina na Shirika Hodhi la Mali ya Serikali (*CHC*). Kwa udhaifu mkubwa wa kiutendaji na kimuundo kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina na *CHC*, hali ambayo imelifikiwa Taifa letu katika hali ya Viwanda kudidimia. Wizara ya Fedha itoe kauli ni hatua gani za msingi zimechukuliwa toka tathmini ya Viwanda vilivyobinafsishwa kufanyika 2007/2008. Aidha, ieletez hatua mahususi kuhusu Viwanda vya Urafiki, *Ubungo Garments*, Ubungo Maziwa, Zana za Kilimo Ubungo (*UFI*), Usafiri Dar es Salaam (UDA) na *Tembo Chip Boards* (Mkumbara – Tanga). Naomba timu iliyoundwa na *CHC* Juni, 2011, ichukue hatua na nipo tayari kuipa nyaraka na ushirikiano unaostahili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa kesi ya *DEC* inaendelea Mahakamani; na kwa kuwa Serikali toka 2009 ilieleza kuwa imekusanya asilimia 40 ya fedha zilizopandwa; Wananchi hao warejeshewe asilimia 40 hiyo, bila kueleza hatua ya kesi na namna ya kupata fedha zilizozama baada ya kupandwa. Iwapo Serikali itaendelea kushikilia fedha hizo, basi itoe kauli kuwa fedha hizo zitarejeshwa pamoja na riba.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala mahususi ambayo ningependa kushauri katika Fungu 50, Fungu 21, Fungu 22, Fungu 23 na Fungu 45; hata hivyo, kutoptana na ufinyu wa muda, nitawasilisha rasmi kwa Wizara kimaandishi. Aidha, ili Wabunge waweze kutoa mchango vizuri zaidi, Wizara ya Fedha ihakikishe katika Mkutano wa Bunge wa mwanzo wa mwaka wa kujadili mpango; majadiliano ya kina yanaanza kwenye Kamati zote za Kisekta badala ya Fedha na Uchumi pekee.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba yake na naiunga mkono na hata hivyo nachangia hoja hiyo kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, *TRA* kwa kiasi kikubwa sana wanajitajidi kukusanya mapato, naipongeza. Hata hivyo, pamekuwapo na wachache wababaishaji ambao wamepitwa na wakati katika kasi ya mabadiliko yanayofanywa na watumishi na *TRA* kwani wanaendekeza kuomba Milungula, inashangaza kuendelea kulea tabia hiyo huku mishahara yao imeboreshwa. Ni aibu.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wa vijiji na kwenye miji midogo wengi wanalipa kodi kubwa huku biashara zao zikiwa ni ndogo. Hoja wanayotumia *TRA* kukadiria ni kuwa wafanyabiashara hawa watunze hesabu zao ili ziwe suluhisho la ukadiriaji huku wakijua kuwa siyo rahisi kwa huduma hiyo kupatikana vijiji na utaona mtu mwenye biashara ndogo wa kijiji anatozwa kodi kubwa kuliko hata wafanyabiashara wakubwa wa mijini.

Mheshimiwa Spika, *TRA* na kodi za magari. *TRA* ni kandamizi katika kukadiria kodi za magari, hawako tayari kuzingatia bei halisi ya manunuzi ili iwe ndio msingi wa kukadiria kodi inayotakiwa. Katika hili na-*declare interest* kuwa tatizo hili limenipata mimi mwenyewe nilipopata fedha ya gari kwa mkopo wa Bunge niliamua kutafuta bei katika masoko mbalimbali nikiwa pamoja na Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed na kugundua kuwa aina ya gari iliyokuwa inauzwa zaidi ya shilingi 108,000,000/= hapa Tanzania ni sawa na Shilingi 4000 x 12300 = 49,200,000/= , lakini wamegoma kutambua bei halisi niliyonunulia gari hiyo. Ili kutenda haki ni lazima wazingatie bei halisi na hii inaonyesha zaidi ya shilingi 8,000,000/= nimelazimika kulipa bila

haki pamoja na maelezo na uthibitisho wote uliotolewa hawasikii wanakandamiza tu. Wawe wanasikia na kufuatilia kwani kwa sasa dunini iko kiganjani tatizo ni nini kama si ukandamizaji ambao kwa namna nydingine unashawishi milungula?

Mheshimiwa Spika, mwisho, Wizara ya Fedha itoe fedha kwa wakati kwenye miradi inayotekelozwa. Wizara itoe fedha kwenye Halmashauri kulingana na bajeti zao ili watekeleze wajibu wao. Pia, Wizara ifuatilie kwa makini fedha inayotumika kwenye miradi ili kuona thamani ya fedha kama inalingana na kazi iliyotekelozwa.

MHE. IGNAS ALOYCE MALOCHA: Mheshimiwa Spika, naunga nkono hoja lakini nina mchango ufuataao.

Mheshimiwa Spika, *TRA* inajitahidi sana kukusanya mapato, lakini nashauri wawepo washindani wengine ili kuleta ufanisi katika makusanyo.

Mheshimiwa Spika, *TRA* inawasikia wawakilishi wa wananchi hasa pale ambapo waliweka kodi kwene malipo ya mazao ya wakulima ambapo baada ya kulalamikiwa wamekuwa wasikivu na kuondoa makato kwenye mazao yaliyokuwa yananunuliwa na *NFRA*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ijitahidi kuhakikisha Hazina wanaka watumishi waaminifu. Pamekuwepo fununu kuwa kuna watumishi wasio waaminifu wanaoshirikiana na watumishi wenzao wasio waaminifu kuiba fedha kama vile kuongeza fedha za miradi, au *OC* kwene Halmashauri na baadaye huwadai watumishi kujenga hoja ya kuzichukua na wanagawana hili linalofanyika kwani pamekuwepo manenomaneno.

Mheshimiwa Spika, hii mishahara hewa ni ushirikiano kati ya maeneo yenyе ajira na Hazina, pia tafadhali Wizara idhibiti maeneo yote yanayotuaibisha kama nchi/Serikali kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, jitihada za kukusanya mapato lazima ziungwe mkono na kila mzalendo na katika suala la kuimarishe fedha ya Tanzania Wizara idhibiti fedha haramu na feki. Fedha haramu zinatokana na mauzo ya madawa na zinapatika kwa mafisadi, zinatuharibia *stability* ya uchumi wa nchi. Tuungane ili kuhakikisha uchumi wa nchi unabaki imara.

Mheshimiwa Spika, ahsante naunga nkono hoja.

MHE. DKT. SEIF S. RASHIDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Pamoja na juhudzi nzuri za Serikali katika mipango mbalimbali ya Wizara hii ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kwanza nzungumzie tozo zinazowekwa katika biashara za watu wa chini hasa wilayani na hasa nyumba za kulala wageni ambazo taratibu zake katika baadhi ya maeneo ikiwemo Wilaya ya Rufiji ni za kuudhi na ukandamizaji.

Mheshimiwa Spika, tunashuhudia watendaji wa mamlaka ya kodi na wakusanyaji ushuru wa Halmashauri kuingia kwene nyumba hizo usiku na kuwaamsha wapangaji kwa madai ya kukagua idadi yao. Sio tu ni udhallishaji kwa wapangaji na usumbufu kwa wenye nyumba hizo za wageni (*guest house*) bali ni ufuatilaji wa uonevu kwa wafanyabishara hii. Kwa vile hakuna biashara nydingine yoyote ambayo afisa wa Serikali anakuwepo akishuhudia uuzaji wa biashara na kurekodi kila mtu anayenunua bidhaa kwa nia ya kutoza kodi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kutoa kauli ya kusimamisha zoezi hili linalofanywa kwa nia ya kujua idadi ya wapangaji ndani ya nyumba hizo za wageni usiku ili utaratibu mwingine utumike kwa wafanyabiashara hii kutozwa kodi yenyе kulinda heshima na kujua kwamba ni wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iongeze kasi ya upatikanaji wa vitambulisho vyenye uwezo wa kuwatambua Watanzania na kuwezesha sio tu kuwatambua walipakodi bali ni pamoa

na wale wote wenye uwezo wa kulipa kodi na ni matumaini yangu kuwa tukifika hapo basi kiwango cha kodi kitatambulika.

Mheshimiwa Spika, naomba mchakato wa taasisi za hifadhi ya jamii ziongeze mtandao wa kuwafikia watu wengi zaidi na hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, napongeza utaratibu mzima wa uongozi, lakini naishauri Serikali kuondokana na kuacha kuongeza maeneo ya utawala kama Mikoa Wilaya na Kata. Leo tupo katika kuboresha miundombinu ya barabara, mawasiliano yamekuwa ni ya kuwezesha kufanya mikutano kwa kutumia mitando ya simu, kusafirisha taarifa mbalimbali kwa kutumia utandawazi wa *internet*, yote haya na mengine mengi yanaongeza uwezo wa watu wachache kusimamia na kuongeza maeneo makubwa zaidi kuliko yalivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuweka maeneo ambayo baada ya hapo hakutakuwa na mgao zaidi wa nchi. Maeneo ya utawala yanapokuwa mengi siyo kigezo cha mafanikio.

Mheshimiwa Spika, mwisho nakushukuru na naunga mkono hoja.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Spika, moja ya sababu zinazoifanya Bandari ya Dar es Salaam ionekane kutokufanya kazi kama ipasavyo ni uchelewaji wa mizigo kutoka ukiambatana na *storage charges* ambazo zinaonekana hazikwepeki. Ninaomba suala hili lichunguzwe na utatuzi upatikane kwa TRA kupunguza ukiritimba unaoishilia mizigo kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, sula la *Tax Holiday* liangaliwe tena ili tusikose kodi ambazo tunastahili kuzipata. Hii ni pamoja na unafuu unaopewa Makampuni ya huduma za utalii kuhusu magari wanayoingiza ambayo yanapouzwa ili yahudumie wananchi kama daladala ndipo ushuru ambaao ultakiwa ukusanywe mwanzoni unapokusanywa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri na ninawaomba waendeleze juhudii zao hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hotuba kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, makampuni ya simu yanatuibia sana, wanakata pesa hata kama hujatumia muda wa hewani. Je, Serikali ina mkakati gani wa kulidhibiti hilo?

Mheshimiwa Spika, wimbi la fedha bandia limekithiri. Je, fedha hizi zinatengenezwa wapi na Serikali haiwajui wamiliki?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na usumbufu mkubwa Hazina wa kuchelewesha cheki zinazotoa kiwango ili wenye magari wakalipie TRA. Kwa nini wanachelewa au ni lengo la Serikali kuchelewesha ili lingize *storage charges*? Hii ni hatari jamani watananzania wana hali ngumu.

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Spika, kwanini Serikali mnalionia swala la *UDA* ni dogo? Kwanini wahusika waliotia saini ya *transfer* ya *share* za *UDA* kama Meya wa Jiji la Dar es Salaam asisimame kazi na kudharau barua ya Waziri Mkuu ya Februari, 2011 kuzuia *transfer* lakini wamefanya.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maeneo yafuatayo;

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa malipo ya mishahara ya watumishi wa umma. Kumekuwa na malalamiko mengi ya kuwepo kwa malipo ya mishahara hewa kwenye taasisi za Serikali na Mawizara hasa Wizara ya Elimu ambapo kumekuwapo na mishahara hewa zaidi ya

milioni mia sita. Hivyo, Serikali ifanye ukaguzi ambao utabaini wizi wa fedha za umma ambazo ni pesa za walipakodi ambao ni wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, nashauri watumishi wote walohusika na ubadhirifu wa fedha hizo wakamatwe ili wafikishwe mahakamani na wafilisiwe mali zao kwa manufaa ya umma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema katika mkutano huu wa nne, iliyoniwezesha kuchangia na kushiriki mijadala mbalimbali katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2010/11 iliyopelekea uandaaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza katika maeneo yafuatayo:

Moja, Mamlaka ya Mapato (*TRA*) na ukusanyaji wa mapato. Pamoja na kazi nzuri inayofanya na mamlaka hii ya mapato, bado changamoto ya wigo wa walipa kodi kuwa mdogo inatakiwa kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo. Pia kuna shughuli nyngi zisizo rasmi hazikusanywi kodi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ihakakishe zoezi la vitambulisho kwa raia wa Tanzania, ili kupanua wigo wa walipa kodi na kuboresha kiwango cha makusanyo ya mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara itekeleze maoni ya Waheshimiwa Wabunge wakiongozwa na Kamati ya Fedha na Uchumi juu ya kupunguza misamaha ya kodi hadi kufikia asilimia moja ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kiasi cha shilingi bilioni 680 kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 ni mingi sana kiasi kwamba misamaha hii ni kupitia Sekta ya Madini na kituo cha uwekezaji. Naiomba Wizara ifanye tathmini ya matumizi ya misamaha hiyo ili kujiridhisha kama inakidhi matarajio ya kutolewa kwa msamaha hiyo.

Mbili, ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Naipongeza Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu kwa kazi nzuri iliyofanya kwa mwaka 2009/10. Lakini kwa mujibu wa kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 20, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilielezwa kutekeleza yafuatayo; kukagua mafungu yote 49 ya Wizara na Idara za Serikali, hesabu za Mikoa yote 21, hesabu za Halmashauri zote 133, Manispaa na Majiji, Balozi 31 pamoja na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii sio sahihi kwa kuwa mwaka wa fedha 2010/11 Wizara na Halmashauri baada ya mwaka wa fedha 2010/11 kuishia 30 Juni, 2011 hupewa kipindi cha miezi mitatu hadi tarehe 30 Septemba, 2011 ili kuandaa hesabu zao tayari kwa kukaguliwa na CAG. Leo tarehe 26 Agosti, 2011, inakuwaje taarifa kuwa hesabu hizo zimekaguliwa wakati hata hazijakamilika kuandaliwa. Taarifa hii sio sahihi!

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya CAG ya mwaka 2009/2010 Kambi ya Upinzani Bungeni kuititia mse maji wa Wizara ya Fedha na Uchumi na kuititia pia hotuba ya Klongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kuwa kuititia ripoti hiyo ya CAG zaidi ya shilingi trilioni 2.5 zilipotea. Mshangao wangu ni kuwa Serikali haikuweza kujibu chochote, jambo ambalo linafanya wananchi na watanzania kuamini kuwa Serikalini kuna ubadhirifu wa kiwango hicho. Ukweli ni kwamba taarifa ya CAG inatafsiriwa visivyo na Kambi ya Upinzani na wadau wengine pengine kwa kukosa uelewa wa taarifa hizi na namna ambavyo ripoti hii ya CAG baada ya kuwasilishwa, Maafisa Masuuli wanapewa siku 21 kujibu hoja na CAG anafanya uhakiki na hoja nyngi huwa zinafutwa na taarifa hiyo inawasilishwa kwenye Kamati za Kudumu za Bunge za kusimamia fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, naoimba Wizara kwa kushirikiana na ofisi ya CAG itoe elimu kwa umma juu ya tafsiri ya ripoti ya CAG ili kuondoa dhana potofu inayojengwa na wadau hasa Kambi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa ukusanyaji wa kodi na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza Serikali naomba kutoa ushauri kama ifuatavyo; kuendelelea kuongeza ukusanyaji wa mapato viwanja vyta ndege mipakani pamoja na bandari.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la kutokuwepo sarafu ya shilingi hasa vijiji ni ukizingatia wao hutumia hela ndogondogo. Je, tatizo nini kimetokea? Je, ni Serikali imeacha kutengeneza sarafu hizi au ni uzembe wa mabenki kuacha kuzibeba na kuzipeleka vijiji au wilayani?

Mheshimiwa Spika, wakati wa majumuisho naomba Serikali inieleze mkakati uliopo wa kunusuru sarafu hii na hata kusaidia wananchi wa vijiji ili waweze kutumia fedha zao kwa utaratibu wao bila kulazimishwa kununua kitu wasichokusudia.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA: Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema ili nami niweze kuchangia kwa maandishi hotuba ilio mbele yetu. Aidha naomba nimpongeze sana Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake wote.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia kama ifuatavyo; mchango wangu unakwenda moja kwa moja kwenye mabenki ya watu binafsi kama *Blue Bank, FAIDIKA*, na mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wamekuwa wakipata taabu sana na benki hizi kwani benki hizi zinatoa riba kubwa sana ukilinganisha na pato la mshahara wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wamekuwa wakiingia mikataba na mabenki haya bila kujuwa wanafanya nini. Haiwezekani mfanyakazi akope shilingi 1,000,000/= halafu akatwe Shilingi 3,000,000/= au akope shilingi 2,000,000/= akatwe 6,000,000/. Nashindwa kuelewa hizi ni *interest* gani ambazo benki wanazotoza au ni wizi na utapeli mkubwa. Wafanyakazi hawa na hasa Walimu wa Shule za Msingi na Askari Polisi wameumia sana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachojua mtu anakopa ili apate unafuli fulani wa maisha lakini sasa imekuwa mtu huyu anapokopa anaumia zaidi na anashindwa kabisa kuendesha maisha yake.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuangalia upya mikataba ya watu wanaoendesha hizi benki, pia iwepo sheria ambayo haitawaruhusu hao wamiliki kuingia moja kwa moja mikataba na wafanyakazi hao. Wawe wanaingia na waaajiri na kuwepo na sheria ya kumlinda huyu mfanyakazi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwasemee wafanyakazi wetu wastaafu. Kumekuwa na malalammiko makubwa na mengi ya wastaafu. Mimi naomba Serikali iwajali wastaafu hawa tuwaenzi kwa kazi nzuri walizozifanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, Zabibu ni zao ambalo limeweza kushamiri tena baada ya kudorora na baada ya kufa kwa kiwanda cha *Dodoma Wine*. Aidha, uanzishwaji wa kiwanda cha *CETAWICO* kwa ushirikiano na *Tanzania Distilleries Ltd* na viwanda vingi vidogovidogo vimeamsha zao hilo na mashamba yaliyokuwa yamekuwa yamefufuliwa na

mapya yanaanzishwa kwa kasi kubwa sana kwa sababu ya kupatikana kwa soko hilo. Aidha, pia ni sera ya CCM kulinda viwanda vya ndani na kilimo kwa ujumla wake. Lakini ushuru (*excise duty*) kwa *Wine* zinazotengenezwa hapa ndani ya nchi utasababisha *Wine* zinazotengezwa ndani ya nchi kushindwa kushindana na zile zinazotoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu hizo naishauri Serikali ikubali kuondoa ushuru huo ili kusaidia kilimo cha Zabibu ambacho ndilo zao pekee la kudumu katika Mkao wetu wa Dodoma, maana *CETAWICO* ndio wanunuaji wakubwa wa Zabibu ya Dodoma. Kwa maelezo haya ombi langu ni kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aone haja ya kuondoa ushuru huo ili kusaidia zao la Zabibu na viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wangu naambatanisha barua ya *Tanzania Distilleris* kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa nia ya ombi hilo hilo. Wana-Dodoma tutafurahi sana endapo Serikali itakubaliana na ombi hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninatanguliza shukrani.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na wananchi wa Jimbo la Babati Vijiji. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Kayanza Pinda kwa kazi nzuri ya kuongoza nchi yetu na kulinda uchumi pamoja na matatizo ya kiuchumi duniani.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake ya Wizara ya Fedha kwa jitihada kubwa wanayofanya ya kukusanya mapato na kubuni njia mbalimbali kuiongezea Serikali njia ya kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri Serikali na Wizara ya Fedha ijitajidi kuwa na watalaam mbalimbali wa sekta zote ya kiuchumi na huduma za jamii, wawe wote katika Wizara ya Fedha wajue maswali mbalimbali na wawe tayari kupokea ushauri. Wizara ya Fedha haina wataalam wa kilimo, maji, mifugo, na ya sekta nydingine, wakati wa kupanga bajeti ya Wizara mbalimbali huleta matatizo. Hata wakishauriwa ni vigumu kuelewa na kupanga kwa ushauri unatolewa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo moyo wa nchi, wakiwa wabunifu na wakijipanga vizuri kukusanya mapato na kutanua wigo wa mapato basi nchi yetu ingepata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwapatie mafunzo ya muda mfupi wataalam wa Wizara kwa sekta mbalimbali na ninaamini uchumi wetu utakua na Serikali itaweza kukusanya mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara iendele kutoa elimu kwa wananchi ili walipe kodi kuchangia maendeleo ya nchi yetu na wigo wa makusanyo ukiwa mpana kodi zaidi itokusanya na itachangia maendeleo ya mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho Wizara ya Fedha irekebishe suala la kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwenye vipuri vya matrekta. Bunge hili tukufu lilipitisha kuondolewa kwa kodi hiyo ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwenye vipuri vya matrekta yote, lakini TRA imetangaza tofauti na inaendelea kukusanya kodi (*VAT*) kwenye vipuri vya maktekta na kukwamisha kuboresha Kilimo Kwanza na gharama ya vipuri kubaki kuwa ya juu na pia kutangaza tofauti na maamuzi ya Bunge.

Pia, tungependa kujua kama hiyo kodi (*VAT*) ya Ongezeko la Thamani iliokusanya itarudishwa kwa waliolipa baada ya tarehe Mosi Julai, ile gharama ya kilimo ipungue na matrekta mengi yakarabatiwe na wenye kuza vipuri hivyo wawewe kushindana na wenzao wa Kenya na Uganda, la sivyo watafunga biashara zao kwa kukosa biashara itakayokwenda Kenya na Uganda.

Pia, Wizara iwe na mpango wa kudumu kukutana na sekta mbalimbali ili kupata maoni ya namna ya kuboresha sekta hiyo na isiwe wakati wa kuandaa bajeti tu, iwe ni mpango wa kudumu

na wa muda wote. Kianzishwe kitengo cha elimu ili kupokea maoni na ushauri lakini pia wataweza kutumia kitengo hicho kuzishauri Halmashauri mbalimbali na taasisi zingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ahsante na ninaunga mkono hoja.

MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni juu ya, moja, shukrani kwa Gavana kwa uamuzi wake wa kufanya *study* juu ya mfumo wa *VICOBA* kwa Mikoa ya Ruvuma, Njombe Iringa na Morogoro. Naomba matokeo ya *study* hiyo yatoke mapema ili kusaidia Serikali kuweka mfumo rasmi wa kutekeleza na kuimarisha utendaji wa *VICOBA*.

Pili, naomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi katika kuongeza fungu la mtaji kwa Benki ya Twiga kwani benki hii inahitaji angalau shilingi bilioni 10 ili kukidhi hali ya benki hii.

Tatu, naomba *TRA* ijkite katika kupanua vyanzo vya mapato ili kuongeza kodi, sasa hivi kuna wafanyabishara wengi ambaa si rasmi na hivyo hawalipi kodi. Naomba jitihada za kurasimisha biashara hizo ili zitozwe kodi.

Nne, Serikali imejitahidi kuinua uchumi lakini tatizo lipo katika kupunguza umaskini. Nashauri kitengo cha kuondoa umaskini kuandaa mikutano na wadau mbalimbali wanaotekeleza programu za kuondoa umaskini ili kupanua uwezo na uzoefu katika utekelezaji wa programu za kuondoa umaskini.

Tano, programu ya *Self ipewe* mtazamo na msisitizo zaidi ili iweze kuendea katika mikoa yote kwa haraka na wananchi wapate mitaji na waendeshe shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Waziri wa Fedha na Naibu Mawaziri Mheshimiwa Pereira Ame Silima na Mheshimiwa Gregory G. Teu kwa hotuba nzuri. Napenda kipekee niwapongeze Katibu Mkuu Kijjah na Naibu Katibu Mkuu na Kamishna wa Bajeti kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, katika kupidisha mizigo bandarini iliyotoka nje ya nchi utaratibu unachukua muda mrefu sana. Moja ya sababu za ucheleweshaji ni kuzuka kada moja ya matapeli wakubwa kati ya *Clearing Agents*.

Mheshimiwa Spika, kijana mmoja ambaye ni mpiga kura wangu aliletu mtambo mdogo (mashine) ya kuchuja maji kutoka China wenye thamani ya US dola 4000. Akatafuta *Clearing Agent*. *Clearing Agent* akamjazia fomu na kueleza kuwa mtambo ni wa kutengeneza maji ya kuniwa ya chupa. *Clearing Agent* akarudi baada ya siku mbili akamwambia mpiga kura wangu kuwa *TRA* imekadiria kuwa alipe shilingi milioni 15 za *Customs, Excise* na *VAT*. Kijana akaja kuniomba mkopo nimsadie alipe. Ndio nikapata wasiwasi, mbona huu mtambo mdogo ni wa uzalishaji, kwa nini kodi karibu mara mbili ya *CIF Price*? Nikaona nimulize *Commissioner General* wa *TRA*, naye mtu wa Mungu huyu akashangaa akaniahidi atanipa majibu. Baada ya saa moja tu ndugu Kitilya akanipigia simu na kuniarifu kuwa mtambo huo hauna kodi na kijana amuone Afisa wa *TRA* anayehusika akalipa gharama ndogondogo za *handling* jumla shilingi 800,000/= akachukua mzigo. Hivi sasa amezalisha *mineral water* na analipa kodi.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Wizara hii ichukue hatua za haraka kuondoa matapeli hawa katika kufanya biashara ya *Clearing and Forwarding*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kati eneo la mafuta. Kikukweli mimi nashangazwa sana na bei ya mafuta kwani mafuta mpaka yanafika *Port*

Dar es Salaam ni 650 \$(650 x 1600) = 1,040,000 kwa maana ya shilingi 1,040/= /itre, ukiongeza kodi na tozo bei hiyo haiwezi kuzidi shilingi 1,600/= kwa lita. Je jambo hili la wizi pia Wizara inashindwa kushughulikia ili

- (i) Kuongeza kipato cha kodi
- (ii) Kuleta maisha bora

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwani mafuta ndio chanzo cha kuonekana kwa gharama zote.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Mifuko ya Pensheni na Hifadhi ya Jamii katika miradi mbalimbali. Pamoja na kazi mbalimbali zinazofanywa na mfuko ya pensheni ya Hifadhi ya Jamii, ningeshauri sasa Serikali ione umuhimu wa kuitumia mifuko hii hususan *NSSF* katika kuwekeza kwenye miradi ya umeme hasa wa Makaa ya Mawe na Chuma cha Liganga. *NSSF* imeonyesha *interest* ya kuwekeza katika mradi mkubwa wa umeme kwa kutumia Makaa ya Mawe ya Kiwira, ni busara sasa Serikali kutumia uzalendo na kuwapa wazawa kazi hii maana itasaidika mara mbili. *NSSF* watalipa kodi, watatoa ajira, watapunguza na hata kumaliza tatizo kubwa la umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la *UDA* limeongelewa kwa mapana sana na Waheshimiwa Wabunge wengi. *UDA* ni Shirika la Umma ambalo linatakiwa litoe huduma ya usafiri kwa umma na Watanzania hususani wanafunzi. Mchakato wa kuliiza shirika hili pamoja na kutofuata taratibu, unaonesha kuna harufu ya rushwa kwa wote walohusika na mchakati mzima wa kuuza shirika hilo. Kwa kuwa, shirika hili ni muhimu hasa kwa watu wa kipato cha chini ni busara sasa Serikali ikasitisha uuzwaji wa Shirika hilo na kuliacha liendelee kuwa chini ya Serikali na badala yake uongozi mzima utazamwe upya ili kulinusuru shirika kuliwa na wajanja wachache.

Mheshimiwa Spika, Hazina ni Idara muhimu sana katika Wizara hii kwani ndiyo inayoratibu masuala yote ya fedha za umma. Kwa kuwa, Hazina inahusika na utoaji wa fedha za mikopo kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Lakini imeonekana kwamba ama imekuwa ikitoa fedha nusunu au kuchelewa kutoa pesa hizo kwa Bodi ya Mkopo. Matokeo yake ni kusababisha migomo na maandamano yasiyokoma kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kama tulivyoshuhudia *U-DOM, U-DAR ES SALAAM*, Muhimbili na kadhalika. Kwa kuwa, ripoti ya *CAG* ya mwaka 2009/2010 imeainisha matatizo haya yanayosababishwa na Hazina, ni vizuri sasa ikafanya kazi yake ipasavyo na kwa uadilifu mkubwa kwani pesa zinazotolewa ni mkopo na zinatakiwa kulipwa baada ya muda fulani na si zawadi hivyo, Hazina ifanye kazi yake isikwepe jukumu kwa kutoa visingizio visivyo na maana.

Mheshimiwa Spika, pia Hazina inahusika na uandaaji wa Pensheni za wastaafu. Lakini utaratibu wake ni wa usumbufu mkubwa kwa wastaafu na mara nyingi zinakuwa haziwekwi kwa wakati na hivyo kusababisha kero kubwa. Hazina pia ingeona umuhimi wa kupunguza muda wa kutoa pensheni kutoka miezi 6 hadi 3 hasa kwa wale wastaafu ambao kiwango chao ni zaidi ya laki moja ili waweze kutatua matatizo madogomadogo kama kulipa ada za watoto na matibabu.

Mheshimiwa Spika, *TRA* inatakiwa ifanya kazi yake ya kukusanya kodi hasa zile zenye mwaya kukwepwa. Mfano sijui ni utaratibu gani ambao *TRA* inautumia katika kukusanya mapato kwenye michezo ya Bahati Nasibu inayoendeshwa na Makampuni ya simu nchini. Makampuni ya simu yamekuwa yakiendesha Bahati Nasibu na kujipatia pesa nyingi sana, lakini nina wasiwasi endapo *TRA* ina vifaa vya kung'amu ni pesa kiasi gani zinapatikana kwa michezo hiyo na ni kiasi gani *TRA* inapata kodi yake stahiki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali imeanzisha maduka ya *duty free* Majeshini, kwa maana kwamba yanauza bidhaa zake kwa bei nafuu. Lakini *TRA* inatakiwa izungukie maduka hayo yote ijionee jinsi bei zake zilivyo kubwa sawasawa na maduka haya wameshindwa kutoa huduma kwa bei inayotakiwa na badala yake kujipatia faida mara mbili ni vizuri wakanyang'anywa leseni zao na kupewa wengine wenye sifa na huruma kwa Wanajeshi wetu

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mustafa H. Mkullo na timu yake kwa kazi nzuri. Ninaunga mkono hoja na ninaomba nipiatiwe majibu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wamejitatidi kujajiri kwa kuanza biashara katika sekta ya fedha hususan kuanzisha kampuni au Wakala wa Bima (*brokers*) *Community Banks, Credit Finance* na kadhalika. Je, Wizara ya Fedha ina mkakati gani wa kutoa kichocheo kwa vijana hawa ili biashara zao zikue kama ilivyo katika nchi nydingi yaani *Affirmative action?*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Tanzania ni nchi maskini duniani na biashara zake za fedha (*Financial Services Sector*) inalindwa na *WTO provisions under special and differential treatment for the Least Developed Countries*. Wizara ina mpango gani kuwasaidia wazawa katika sekta hii ya *Finacial Services* kukua? Je, Wizara ina habari juu ya uwepo wa mwanya huu au hapana? Kama ndiyo, kwa nini haujatumika?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali imeuza hisa zake katika benki nydingi, hivi sasa ni Benki gani ambayo Serikali imebaki na hisa nydingi? Kama sikosei Benki ya Posta ni mojawapo ya Benki ambazo haijabinafsishwa na Serikali ina hisa kubwa. Je, Wizara ya Fedha ina mkakati gani wa kuongeza rasilimali katika benki hii ili iweze kuibuka upya na kutoa huduma bora zaidi hasa vijijini ambapo zamani ilikuwa inategemewa sana? Nchi nydingi zimeimarisha Benki za Posta kwa kutumia *TEKNOHAMA* kwa mafanikio makubwa badala ya kuachia makapuni ya simu kufanya biashara ya benki bila usimamizi stahili. Niko tayari kufafanua zaidi masuala haya kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha atayahitaji

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa linaongezeka kama ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinavyosema kwamba limeongezeka kwa 38%, hivyo, napenda kuishauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 na 62 ya Katiba kwamba Deni la Taifa liendane na ukuaji wa uchumi. Mfano, deni la Taifa ni zaidi ya dola za Kimarekani milioni 11 lakini uchumi wa mtu mmoja haukui. Napenda kupata majibu kutoka kwa Serikali kwa nini deni la Taifa linakua huku maisha yakiendelea kuwa magumu na Tanzania kuwa ndani ya nchi 10 maskini duniani?

Mheshimiwa Spika, *TRA* inavyokandamiza watu na kukiuka utaratibu. Napenda kupata majibu kutoka Serikalini, kwa nini wananchi wa Mukalazi katika Tarafa ya Mabamba wanakaguliwa ili watoe risiti wakati wanaponunua vitu na kwenda majumbani kwao badala ya kugaua wenye Maduka? Kwani sheria za kodi ikiwemo *the Income Tax Act 2006* inaeleza kuwa kujua na *ku-calculate* kodi atakaguliwa muuzaji na si wanunuzi mitaani.

Mheshimiwa Spika, mifuko ya Hifadhi ya Jamii yaani *NSSF, LAPF, PSPF* na kadhalika, naipongeza mifuko hii kwa kujihusisha na masuala ya kiuchumi. Lakini napenda kujua Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha wastaafu wanaongezewa posho zao na pia kuja hatua gani zinachukuliwa kwa wananchi waliokuwa wanachama wa Mashirika haya wanapozungushwa kudai mafao yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu kutoka Serikalini je, Benki Kuu inawezaje kuzikagua na kuzisimamia benki hizi za ndani kwa kuzingati kwamba inakopa kwenye benki hizi na kutokana na uingizwaji holela wa dawa za kulevyo. Je, Serikali ina uhakika na mitaji yao?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mungu kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kawaida ya nchi kukopa nje fedha nyngi ambazo zimekuwa zikutumika kwa matumizi ya kawaida kuliko hata matumizi ya maendeleo. Pia, ni vizuri sasa nchi ikope na kuwekeza katika mitaji zaidi na maendeleo kuliko kukopa kwa ajili ya matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kukopa huku kunaifanya nchi iwe na rundo la madeni, kwa nchi isiyoweza kuwasaidia watanzania wa hali ya chini na kujikuta mikopo ya nchi kwa namna fulani inawanufaisha wajanja wachache walio Serikalini na kutoonekana kwa mabadiliko kwa maisha ya watanzania wenyе hali ya chini hasa walioko vijijini.

Mheshimiwa Spika, hii imepelekea wananchi kuipigia Serikali kelele hasa pale inapotamkwa kuwa uchumi wa nchi unakuwa huku watanzania wanazidi kuwa maskini kila siku.

Mheshimiwa Spika, bado kuna mianya mingi sana ya ukwepaji wa kodi katika ulipaji forodhani. Ukubwa wa kodi ambaо hupewa mzigo walipaji wachache umepalekeea watanzania wakimbiе na kupanga kukwepa kodi na kufanya makusanyo ya kodi kuwa kidogo sana. Bado tatizo la ukusanyaji kodi ni kubwa kwa kuwa wakusanya kodi (*TRA*) bado hawajajenga urafiki na wafanyabiashara. Kumekuwa na uadui kati ya mlipa kodi na mtoza kodi, bado kodi kwa mtanzania inaonekana kama nyanyaso na sio wajibu.

Mheshimiwa Spika, bado elimu ya walipa kodi ni ndogo na imekuwa ndogo kwa kuwa watoza kodi wana elimu ya kutoza kodi wakati walipa kodi hawana elimu na siyo wote wanaojua faida ya kutozwa kodi bali kasi ya kuwatambua walipa kodi ni ndogo na hii hupelekeea kodi kuwa inalipwa na watu wachache.

Mheshimiwa Spika, misahama ya kodi kwa wawekezaji imepita uwezo wa nchi kusamehe. Misamaha yetu sasa ingaliwe upya na kama ikiwezekana sasa misamaha isitishwe na itolewe tu pale inapobidi.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya fedha za kigeni ndani ya nchi kumepelekea sana kuifanya thamani ya fedha yetu kuonekana duni na dola kupaa. Inasikitisha sana kuona hata kodi zinazotozwa na *TRA* kwa magari yatokanayo na uagizwaji nje ya nchi hutozwa kwa thamani inayokokotolewa kwa thamani ya dola ambayo imekuwa ikipanda na hasa kutokana na kushuka kwa kasi ya shilingi ya Tanzania kunafanya kodi ya gari itofautiane katika mwaka mmoja tu wa fedha. Kuna haja ya kuangalia upya jinsi ya kukokotoa ushuru wa magari. Imetoka *formular* mpya ya ukokotaji wa magari ambayo imepigwa kelele na watu wengi.

Mheshimiwa Spika, fedha nyngi sana hupotea nje kwa ukaguzi wa ubora wa magari kabla hayajaja (*TBS*). Tuna vijana wengi wenyе uwezo wa kuanglia upya jinsi ya kuruhusu kufanya ukaguzi na fedha ibaki hapa.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara inapopangwa hupangwa kwa nia nzuri ya kutaka kurekebisha au kumaliza matatizo fulani katika Wizara mbalimbali. Lakini kinachosababisha kuanguka kwa uchumi mzuri ni utekelezaji mbovu wa matumizi ya fedha katika Halmashauri nyngi na Wizara wenywewe.

Mheshimiwa Spika, matumizi mabaya ya fedha na mipango isiyotekelzeka ni sababu kubwa ya kuua uchumi wa nchi na maendeleo yake, kwa ujumla uandaaji, usimamisi na ufuatilaji wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, bado tatizo linakuja ni mipango mingi inayopangwa lakini ni ngumu kutekelezeka. Mfano, vijana ni nguzo ya Taifa na Serikali inaelewa hilo. Lakini vijana hawashirikishwi katika sera na mipango ya kitaifa na ya kisekta. Serikali katika Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inasema katika kila Halmashauri zitengwe 5% kwa ajili ya vijana lakini ukifuatilia, ni kwamba vijana wamesahaulika.

Bajeti hiyo haiwafikii kabisa na badala yake zinazopangwa kwa ajili yao zinapelekwa katika mipango mingine kabisa. Hilo ni pengo kubwa. Naomba Wizara ya Fedha ifuatilie sana ugawaji wa fedha katika bajeti zake ili zitumike jinsi ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mfano mwagine ni Wizara ya Nishati na Madini. Hii vilevile haitoi nafasi kwa vijana, vijana hawajanufaika nayo. Serikali iwape kipaumbele vijana amba ni nguvukazi ya Taifa. Serikali imeshindwa hata kuwapa mikopo nafuu ili wapate vitendea kazi vya kisasa kwa uchimbaji wa madini. Huko ni kuua nguvukazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kundi lingine ni wanawake, wanawake wakumbukwe sana kwani ukimuelimisha mwanamke mmoja umeelimisha umma wote na uchumi wetu utakua sababu akinamama wakiwezeshwa wanabidii sana ya uzalishaji mali. Wakianzisha shughuli na kuunda vikundi Serikali iwasapotili wachangie pato la taifa kuliko kuacha fedha zipotee bure kwa ulipaji mishahara hewa. Hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho naishauri Serikali kwa Wizara ya Ujenzi irudishe mfumo wa utengenezaji wa magari katika yadi ya Idara ya Ujenzi, tofauti na sasa pesa nyingi za Serikali zinapotea kwa ujanja kwa ajili ya kutengenezaea magari ya Serikali mbali ya Halmashauri husika. Mfano, gari linatoka Rukwa linapelekwa Tabora kutengenezwa tu. Huo ni wizi na ujanjaujanja wa kuiangusha Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Tizeba, tutaangalia utaratibu mpya, lakini mpaka sasa tutatumia muda tulio nao. Kwa hiyo, naomba nianze kuwaita watoa hoja Naibu Waziri mmoja mmoja atapewa dakika na Waziri atapewa dakika 40. Nafikiri nianze na Mheshimiwa Teu dakika 10. Mkianza kupongeza wake zenu muda hautoshi. (*Makofiki/Cheko*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kidogo kuchangia hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo. Napenda kuunga mkono hoja kwa kuzingatia masuala muhimu ya kitaifa na ambayo ni nyenzo muhimu katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2020-2025, malengo ya *Millenium* ya 2015. Ukuta wa awamu ya pili na llani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuchangia baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa 2011 kama ifuatavyo:-

Kwa ujumla Mheshimiwa Spika, ningependa niseme kwamba nina moja la ujumla ambalo niseme kwamba kuna lugha ambayo ilikuwa inatumika hapa ya kasungura kadogo. Tukikumbuka tulikotoka miaka 1961 tangu Uhuru wa Nchi yetu, miaka 50 iliyopita ukilinganisha na hali yetu ya sasa hivi, ni kweli tumetoka mbali. (*Makofiki*)

Mwanzo ilikuwa kwamba programu ziliikuwa chache na fedha ilikuwa ni kidogo na watumiaji walikuwa ni wadogo na sasa hivi tumefikia baada ya miaka 50 hapa tulipo kwa kweli Bajeti iliyopo sasa hivi mbele yetu ya trilioni 13.5 si haba. Ni kitu kikubwa wala siyo sungura kadogo. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tunapotoka hapa tukirudi majumbani kwetu na kazi ambazo tulikuwa tunazismamia sasa ni utekelezaji. Tusipate kisingizio kwamba kasungura, tumegawana ni kadogo. Lakini ni kitu kikubwa sana hiki ambacho tunategemea utekelezaji wake utakuwa ni wa hali ya juu sana. (*Makofiki*)

Mheshimiwa Spika, nikianza kujibu hoja. Hoja ya kwanza ilikuwa inahusu kwamba Serikali iboreshe mazingira yatakayowawezesha wananchi wetu wa kawaida hapa nchini kupata mikopo ya kibenki na kuweza kujenga au kujenga nyumba.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha rasmi mradi maalum ambao unaitwa *Housing Financing Project*, Januari, 2011 na mradi huu ulipata masaada wa dola 40 kutoka Benki ya Dunia. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tunapotoka hapa tukawahamasishe wananchi wetu waweze kutumia fursa hii ya kwamba, kuna utaratibu ambao Serikali imeuanzisha kupitia *Housing Financing Project* wa kuweza kupata nyumba au kununua nyumba bora. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali vile vile imeunda au immeanzisha rasmi mradi maalum wa mikopo ya nyumba ambao, si mikopo ya nyumba bali Serikali imeunda Kampuni ya utoaji wa mikopo ya nyumba, ambayo inaitwa *Tanzania Mortgage refinance Company*, tangu 2011 na kutimiza masharti yote ya upatikanaji wa mikopo hiyo. Kwa hiyo, wananchi nawaomba kupitia Wabunge, tuwahamasishe ili waweze kutumia fursa hii ambayo iko mbele yao.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ni kwamba, ulipaji wa malimbikizo ya madai ya wateja wa *NIC*. Ulipaji wa malimbikizo ya madai ya wateja wa bima wa *NIC*, uliana mnamo mwezi Aprili, 2011. Shirika limejiwekea utaratibu wa malipo ambao unafanyika kwa wakati mmoja kwa nchi nzima ya Tanzania. Hadi kufikia mwezi Julai, Shirika limeweza kulipa shilingi bilioni 10.1 kwa wateja wa bima za maisha na shilingi bilioni 1.8 kwa wateja wa bima zisizo za maisha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni Wizara itoe Taarifa ya Serikali kuhusu madai kuwa, kuna wafanyakazi wa mfuko *PPF* wamesimamishwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili Serikali inayo taarifa kwamba, kulikuwa na wafanyakazi sita wa *PPF* walismamishwa kazi na walifunguliwa mashtaka kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa mfuko. Watumishi hao walikuwa wameleta matatizo pale kwenye Mfuko. Walikuwa wanawashawishi wenzao wasitoe michango na hivyo kuleta hali mbaya ya Mfuko. Kwa hiyo, hatua za Kisheria zilichukuliwa, wakaweza kuchukuliwa hatua na kufukuzwa kazi hao sita. Lakini baada ya uchunguzi ambao ulifanya watatu waliweza kurejeshwa na watatu walishindwa kurejeshwa baada ya kuthibitishwa kwamba, walikuwa wana hatia na mmojawapo inaelekeaa anachukua hatua za kukata trufaa. Kwa ujumla wao walikuwa sita, watatu wamerejeshwa, watatu wana hatia na mmoja anaelekeaa kukata rufaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilio mbele yangu ni sio sahihi kwa Mkoo wa *PPRA* kuitwa *Director*, kwani cheo chake ni zaidi ya hicho. Hii inasababisha *Heads of Procurement* ambao kimsingi ni *Directors*, wanakosa stahiki za kuwa *Directors* kwenye Idara zao.

Mheshimiwa Spika, hapa kuna mawili, kuna *PPRA* na kuna *PPU*, ile Sera ya ununuzi. Serikali imeliona hilo kwa hiyo, Mkoo wa Sera ya Ununuzi ambaye yuko chini ya Wizara ya Fedha yeze sasa hivi amepandishwa hadhi na atakuwa ni Kamishna wa manunuzi na wale ambao watakuwa chini yao watakuwa Wakurugenzi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni Mifuko mingine iige mfano wa *PPF* katika kutoa fao la elimu kwa watoto wasiozidi wanne.

Mheshimiwa Spika, hapa naomba niungane na Wabunge, kutoa pongezi kwa Mfuko huu wa *PPF* kwa kazi nzuri ambayo umeifanya mpaka sasa ya kuweza kusaidia hawa watoto ambao wana ulemavu na wakaweza kusomeshwa kwa mfuko huu. Mifuko imepokea ushauri huu na itaufanyia kazi baada ya kuangalia uwezo wa mifuko, tuongeze mafao mengine yakiwemo haya ya elimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ieleteze kuna mipango gani ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, yaani *PSPF* na *PPF*, kuwekeza katika maeneo mapya kama reli, bandari na umeme.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba mifuko hii inafanya kazi nzuri na tuna ushahidi wa kutosha kwamba, *NSSF* sasa hivi wamejikita katika kuzalisha umeme. Sasa hivi mifuko mingine hii nayo vile vile itabidi iangalie uwezo wa kuweza kuisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kwamba uwekezaji unaofanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika uwekezaji wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu, ufanyike nchi nzima badala ya

Mwanza na Dar-es-Salaam pekee. Ushauri huu umepokelewa na mifuko itafanya hivyo kueneza nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuwepo kwa mfumo mzuri wa mawasiliano kati ya Wanachama, Mwajiri na Mifuko ili kurekebisha mapungufu yanayokuwepo kabla ya wanachama kustaaifu.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu ni mzuri. Tunaiagiza mifuko iuzingatie.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba, *GEPF* iwfakie wavuvi ili waweze kuchangia na kufaidika na mafao ya aina mbalimbali yanayotolewa kama inavyofanywa kwa maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, *GEPF* imeweza kuwafikia wavuvi kutoka sehemu mbalimbali.

Tayari mfuko una jumla ya wanachama 171 ambaio ni Wavuvi kama ifuatavyo; soko la *Ferry* Dar-es-Salaam wavuvi 58 wameshafikiwa, soko la Kasedha Tanga wavuvi 73 wameshafikiwa, soko la Mwaloni Mwanza wavuvi 40 wameshafikiwa na *GEPF*.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni Wizara, iishauri *PPF* waendelee na ujenzi wa nyumba za bei nafuu katika maeneo mbalimbali hasa Wilaya ya Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu umepokelewa na Mfuko wa *PPF* uko kwenye mchakati wa kununua eneo katika mji wa Dar-es-Salaam, ili kufanikisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, *PPF* iwasomeshe watoto wa wanachama wao waliofariki, hadi Chuo Kikuu, badala ya sasa kuwasomesha hadi Sekondari.

Mheshimiwa Spika, Mfuko umechukua wazo hili na mpaka sasa hivi mfuko unafanya mkakati wa kuwasomesha wanafunzi hadi kidato cha sita na hapo baadaye wataendeleza hii waweze kuwasomesha watoto hadi Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, malipo ya pensheni kupandishwa, sambamba na kupanda kwa mishahara.

Mheshimiwa Spika, hili bila kupoteza muda naomba kwamba hili nalo Hazina tutaliangalia sana japokuwa kwamba, uwezo wa mapato yanayokusanywa ndio unaowezesha Serikali kufikia uamuzi huu. Lakini hata hivyo Serikali kuititia Wizara ya Fedha, itaanza kuangalia hii ili kuangalia hivi vima, kwa sababu Wabunge wengi wamellilalmikia hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihamishie huduma za malipo ya pensheni katika Ofisi za Hazina Ndogo Mikoani, ili kuwaondolea adha kubwa hawa ambao wanapata mafao.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu umepokelewa na kama tulivyosema kwenye hotuba yetu kwamba Hazina ndogo sasa hivi, kuanzia mwaka huu wa Fedha, zitaandalialiwa ili ziweze kupokea huu mzigo wa kulipa malipo ya mafao katika mikoa. Na yale malipo ambayo huwa yanapelekwa Benki, yataendelea kupelekwa Benki moja kwa moja kwenye akaunti za wale ambao wanastahiki hayo mafao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustapha Mkullo; awali ya yote naomba niilunge mkono. Pamoja na ufinyu wa muda, napenda niwashukuru wapiga kura wa jimbo la Chumbuni na ushirikiano ndio utakaotusaidia.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuchangia baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili hoja hii iliyopo mbele yetu. Hoja ya kwanza ilikuwa ni kupanua wigo wa kodi.

Mheshimiwa Spika, ni lengo la Serikali kupitia kwenye Mamlaka ya Mapato kuhakikisha kwamba, kodi zinakusanywa zaidi ili zitusaidie kuongeza ukubwa wa kisungura. Hili linataka kutekelezwa kwa kutumia vitalu na lengo hasa ni kuongeza angalao walipa kodi angalao 20% kwa kila mwaka. Hili litategmea zaidi miradi inayoendelea ukiwemo *MKURABITA* na Vitambulisho Vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba, sekta isiyo rasmi iingizwe katika mfumo wa kodi na vikwazo viondolewe.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia taasisi zake inafanya tafiti kuhakikisha kwamba, walipaji wa kodi wanaongezeka kutoka kwenye sekta isiyo rasmi. Yapo matatizo ya Kisera, ambayo Serikali itayashughulikia nay a Kiutawala, Mamlaka ya Mapato imejipanga kuyatekeleza katika Mpango wake wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na wazo la kushauri kwamba, tutumie *Windfall Gain Tax* kwenye dhahabu.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba, wazo hili *in fact* ni wazo lakini ni wazo la Serikali, kabla hatujashauriwa jana. Na limo katika Mpango wa Miaka Mitano na Serikali tayari inachukua hatua za kufaa kulitekeleza.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na wazo kutoka sehemu moja kwamba, wazo la kugawana mapato limeshindikana baina ya Serikali zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa kwamba, wazo hili bado halijashindikana na hatua za kufaa zinachukuliwa iapasavyo. Maandalizi ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo haya, upo katika hatua ya mwisho na karibuni utawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba, Benki ya Posta na *Twiga Bancop* ziongezewe mtaji.

Mheshimiwa Spika, hili ni lengo hasa la Serikali la kuhakikisha kwamba benki hizi zina-operate kama *banks* kwa kufuata matakwa ya Benki Kuu na kuijendesha kwa tija ili ziweze kusaidia kuinua uchumi. Aidha, Serikali inapanga kuanzisha Mfuko kutoptana na mapato ya gawio ili kuhakikisha kwamba, fedha kwa ajili hii zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba watu wana wasiwasi *TIB* na *TADB*, kama inaweza ikawasaaidia walengwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Kanuni zimeshatayarishwa kwa ajili ya ukopeshaji na zitatumika kwa ajili ya mikopo kwenye sekta ya kilimo na uwekezaji mwingine.

Uchanganuzi yakinifu umeshafanyika na mapendekezo kuhusu utekelezaji tayari uko kwenye ngazi za maamuzi. Taasisi mbalimbali za kifedha zinasaidiwa hasa kuanzia kwa taasisi za wananchi kama *SACCOS* ambazo riba ziko chini.

Mheshimiwa Spika, *TIB* imeshaimeshatoa mikopo Zanzibar kutoptana na hoja kwamba, pengine haivuki bahari, haivuki Chumba. *Infact* imeshaitoa baadhi ya mikopo na iko kwenye meza inashughulikia mikopo ya kiwanda cha sukari hivi sasa. *TIB* pia imepanga kufungua tawi Zanzibar mwakani.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kwamba, Mifuko yote ya Jamii iwekwe kwenye Wizara moja.

Mheshimiwa Spika, hili ni wazo zuri na kuna kazi ambazo zinaendelea kufanywa kupitia Mamlaka ya Udhibiti, *Actual Evaluation* ikikamilika itatupa mwelekeo wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali imekuwa ikiuza *data* kwa wanafunzi na wasomi?

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, huwa inatoa *data* bure; isipokuwa kuna watu ambao huwa wanahitaji *data* kwa utaratibu maalum na *data* ambazo zinahitaji kushughulikwa zaidi. Hao ndio ambao hutakiwa wachangie chochote, vinginevyo *data* ziko wazi zinifikika na hata kwenye mtandao zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu sensa ya watu na makazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, maandalizi kuhusu sensa yanaendelea vizuri, maeneo yanaendelea kutengwa, maandalizi ya madodoso yanaendelea kushughulikwa, majaribio imeshakamilika Mikoa 18 ambayo ni 85% ya lengo na kukamilisha kabisa inatarajiwa kwenye mwezi wa Disemba, mwaka huu. Kazi ya kuweka mifumo kwenye mfumo wa *Digital* inaendelea kutumia wataalam wa Chuo cha Ardhi na itakamilika kwa wakati. Serikali imetenga shilingi billioni 114.4 kwa ajili ya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu Mfumo wa Malipo baina ya Benki, *TIS*, huchelewesha malipo.

Mheshimiwa Spika, *TIS* inaendeshwa na kumilikiwa na Benki Kuu na inahusisha malipo ya ziada ya milioni 10. Inaboresha ufanisi na inakamilisha malipo kwa mujibu wa Kanuni chini ya saa mbili. Na itafanya vizuri zaidi iwapo urekebishaji unoendelea wa kuwataka mabenki ambayo yanatumia njia hii kutimia *Straight Through Processing* ambapo malipo yatakwenda moja kwa moja kwa mteja.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu fedha za *EPA* kwamba, zilikubaliwa ziende kwenye shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuthibitisha kwamba, fedha za *EPA* zilizorudishwa Serikalini zilikuwa billioni 69.3 kupitia Benki Kuu. Na kati ya hizo, billioni 19.3 zilipelekwa *TIB* na billioni 50 zilipelekwa kwenye ununuzi wa pembejeo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba, kwanini kumetengwa billioni 100 kwa ajili ya dharura? Ni vigezo gani viliviyotumika?

Mheshimiwa Spika, hizi ni fedha ambazo zilitengwa kwa majanga na mahitaji ya majanga yanatofautiana. Fedha hizi zinakuwa zinatengwa kwa kutumia usoefu na mahitaji halisi hutegemea na matukio yenyewe. Tunataraja kwamba, hizi zitatusaidia kwa *nature* ya tatizo ambalo totalipata.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu marekebisho na malimbikizo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa kwamba, malimbikizo hulipwa baada ya kuhakikiwa na malimbikizo mengi sasa hivi yameshalipwa, hasa yaliyowasilishwa kwenye mwezi wa saba ambayo sasa hivi yanashughulikwa. Pamoja na hilo, Serikali inapanga kutumia mfumo mpya wa *Loson Version Nine*, ambao utawezesha Taasisi mbalimbali kuweza kufanya mabadiliko kwenye hesabu zao na urahisi wa kuitumia; mafunzo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge, kwa kuendesha kwa umakini majadiliano ya Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2011/2012. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati mbalimbali za Bunge, kwa michango na ushauri walioutoa wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Nafurahi kwamba, nilianza tarehe 10 na leo nahitimisha mjadala wa Bajeti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Kilosa, kwa uvumilivu wao kwa kipindi hiki nilichokuwa nashughulikia masuala ya kitaifa kwa takriban miezi mitatu. Nawaahidi kwamba baada ya shughuli hizi tatu, tutaendelea kushirikiana katika shughuli tulizopanga kuzitekeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kuwa maoni, ushauri na maelezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge yanasaidia sana katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2011/2012. Aidha, zipo baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambazo ni muhimu katika historia ya maelezo kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa umma.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu imechangiwa na Wabunge wengi, kwa kuzungumza, na hasa kwa maandishi. Napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao; Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda - Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Mbunge wa Handeni, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto - Waziri Kivuli wa Fedha na Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Devotha Likokola - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Khatib Said Haji - Mbunge wa Konde, Mheshimiwa Abdulkarim Ismail H. Shah - Mbunge wa Mafia, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura - Mbunge Viti wa Maalum, Mheshimiwa Dkt. Charles J. Tizeba - Mbunge wa Buchosa, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga - Mbunge wa Singida Magharibi, Mheshimiwa George B. Simbachawene - Mbunge wa Kibakwe, Mheshimiwa Gregory G. Teu - Mpwapwa Naibu Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Pereira Ame Silima - Naibu Waziri wa Fedha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wafuatao walichangia kwa maandishi, nao ni Mheshimiwa Jitu V. Soni - Mbunge wa Babati Vijjini, Mheshimiwa George G. Simbachawene alichangia tena kwa maandishi, Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila - Viti Maalum, Mheshimiwa Regia Mtema - Viti Maalum, Mheshimiwa Ester A. Bulaya - Viti Maalum, Mheshimiwa Idd M. Azzan - Mbunge wa Kinondoni, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia - Mbunge Mtwara Vijjini, Mheshimiwa Deo H. Filikunjombe - Mbunge wa Ludewa, Mheshimiwa William A. Mgimwa - Mbunge wa Kalenga, Mheshimiwa Diana M. Chilolo - Viti Maalum, Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa - Mbunge wa Meatu, Mheshimiwa Pudenciana W. Kikwembe - Viti Maalum, Mheshimiwa Benardetha K. Mshashu - Viti Maalum, Mheshimiwa Gosbert N. Blandes - Mbunge wa Karagwe, Mheshimiwa Lolecia J. M. Bukwimba - Mbunge wa Busanda, Mheshimiwa David Z. Kafulila - Mbunge wa Kigoma Kusini, Mheshimiwa Zarina S. Madabida - Viti Maalum, Mheshimiwa Philipo A. Mulugo - Mbunge wa Songwe, Mheshimiwa Anjellah J. Kairuki - Viti Maalum, Mheshimiwa Susan L. Kiwanga - Viti Maalum, Mheshimiwa Ali Khamis Seif - Mbunge wa Mkoani, Mheshimiwa Muhonga S. Ruhwanya - Viti Maalum na Mheshimiwa Luhanga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa. (*Makofî*)

Wengine ni Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula - Mbunge wa Mkinga, Mheshimiwa AnnaMaryStella J. Mallac - Viti Maalum, Mheshimiwa Vincent J. Nyerere - Mbunge Musoma Mjini, Mheshimiwa Felix F. Mkosamali - Mbunge wa Muhamwe, Mheshimiwa Prof. Anna K. Tibaijuka - Mbunge wa Muleba Kusini, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda - Viti Maalum, Mheshimiwa John J. Mnyika - Ubungo, Mheshimiwa Suleiman M. N. Suleiman - Mbunge wa Kishapu, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe - Mbunge wa Mwanga na Mheshimiwa Beatrice M. Shelukindo - Mbunge wa Kilindi. Kama kuna kuna wengine nimepitwa, nitaendelea kuwataja kadri muda unavyokwenda. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ambayo ningependa kuichangia, inahusu uchumi wa nchi yetu ambaa unaendelea kukua wakati maisha ya mwananchi wa kawaida bado hayajanufaika na uchumi huu. Napenda kutoa ufanuzi ufuatao: kuongeza kwa pato la Taifa kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii katika nchi. Aidha, pato hili huzalishwa na Watanzania wenye kipitia shughuli mbalimbali za kiuchumi za kilimo, ujenzi, mawasiliano na shughuli mbalimbali. Kadhalika, ili ukuaji uchumi jumla uweze kupunguza umaskini, ni muhimu sekta zinazokua haraka ziwe zile zinazoajiri watu wengi.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kiuchumi za kilimo zinaajiri zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania na zimendelea kukua kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia nne kipindi cha miaka mitano illyopita. Hata hivyo, shughuli nyingine za kiuchumi, zikiwemo mawasiliano, ujenzi na uchukuzi, japo zinakua kwa kasi kubwa, mchango wake katika kupunguza umaskini wa kipato ni mdogo kwa vile shughuli hizi zinaajiri sehemu ndogo ya Watanzania wote. Serikali inachukua hatua mbalimbali kuendeleza shughuli za kiuchumi za kilimo ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi bora ya zana na pembejeo za kilimo, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi bora ya zana na pembejeo za kilimo. Kilimo cha umwagiliaji, ujenzi wa miundombinu wa barabara viji ni masoko na uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya kilimo kwa lengo la kuongeza ajira na kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuboresha uzalishaji katika shughuli za kiuchumi na kilimo, Serikali imeendelea kuwajengea wananchi mazingira mazuri na kuwahimiza kupanua wigo wa vipato vyao vya kufanya shughuli nyingine za kiuchumi nje ya kilimo. Mikakati inayowekwa ni pamoja na kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kijijini, kuvutia uwekezaji kwa kuboresha mazingira ya biashara kwa lengo la kuongeza fursa za ajira na kuwawezesha wananchi kiuchumi kipitia mifuko mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilihusu kupunguza misamaha ya kodi ili isizidi asilimia moja ya pato la Taifa. Serikali inatoa misamaha ya kodi kipitia Sheria za Kodi na zisizo za kodi kwa nia ya kutoa vivutio vya uwekezaji au unafuu wa wigo wa uwekezaji wa makundi ya watu kwa nia ya kutekeleza sera mbalimbali za Taifa. Ni kweli kuwa misamaha ya kodi inapunguza mapato ya Serikali. Pamoja na kuwa misamaha hiyo iliyotolewa kwa nia njema ya kuisaidia Serikali kipitia malengo yake ya kumhudumia mwananchi, imebainika kuwa misamaha hiyo wakati mwengine imetumika vibaya, hivyo kutoleta matokeo yaliyotarajiwu. Kwa hali hiyo, Serikali inaendelea kipitia baadhi ya misamaha ili kuangalia kama bado inahitajika au la. Hatua mbalimbali zitachukuliwa na Serikali ili kupunguza misamaha hiyo na hatimaye tufikie lengo linalokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kipitia misamaha ya kodi ili kuhakikisha kuwa misamaha isiyo na tija inaondolewa. Aidha, Serikali inajandaa kutumia fursa za mfuko wa dhamana wa ushauri wa sera na usimamizi wa kodi, yaani Tanzania *Trust Fund for Revenue Policy and Administration for Development Country* ulioanzishwa na Shirika la Fedha la Kimataifa ili kuweza kufanya uchambuzi wa misamaha ya kodi na kipitia upya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ilihusu kutathmini mapato ya njia ya mawasiliano na mitandao ya simu ili Serikali itoe kodi zinazohusika. Serikali kipitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, itaendelea na hatua madhubuti za kujenga uwezo wa wafanyakazi wake ili kuongeza uwezo wa kutathmini *transaction* za makampuni ya simu na hivyo kubaini mapato ya Serikali kutokana na shughuli za makampuni hayo.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka huu wa fedha, mamlaka ya mapato Tanzania itaananza kitengo cha kodi za kimataifa katika Idara ya Walipakodi Wakubwa, ili kujenga uwezo wa kushughulikia ulipaji kodi kwa makampuni ya kitaifa ili kupambana na ukwepaji kodi unaofanywa na makampuni ya simu katika kulipa kodi stahiki.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu kusimamishwa kazi kwa kaimu Mkurugenzi Mkuu wa *CHC*, au *Consolidated Holding Cooperation*. Kufuatia Mheshimiwa Waziri Mkuu kupokea nakala ya barua yenye tuhuma zilizotolewa na waliojita wafanyakazi wa *CHC* iliyoandikwa kwa

Mheshimiwa Zitto Kabwe na kunakiliwa kwa Waziri Mkuu pamoja na watu wengine, Mheshimiwa Waziri alinielekeza nimpatie taarifa kuhusu masuala yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kupata ukweli kuhusu tuhuma zilizotolewa, nimeagiza Bodi ya Wakurugenzi *CHC* izifanyie kazi tuhuma hizo na wanilettee taarifa. Bodи baada ya kuzitathmini tuhuma hizo, iliamua Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa *CHC* aende likizo siku 28 ili kupisha uchunguzi wa tuhuma hizo wakati yeze akiwa hayupo.

Mheshimiwa Spika, tuhuma zilizotolewa ni nzito na zinahusu ubadhirifu mkubwa wa mali za *CHC*. Chombo pekee kinachohusika kuchunguza ubadhirifu uliotuhumiwa ni Bodи ya Wakurugenzi ambayo imepewa madaraka na sheria iliyounda *CHC*. Siyo kweli kuwa Waziri wa Fedha alimfukuza kazi au kumsimamisha Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa *CHC*, wala Waziri wa Fedha hakutoa agizo la kufukuzwa kazi kwake. Vilevile Mkurugenzi Mkuu wa *CHC* hajafukuzwa kazi, ila amepelekwa likizo ili kupisha uchunguzi wa *Controller and Auditor General*. Kwa hiyo, kwa masikitiko makubwa madai yaliyotolewa na Waziri Kivuli, Mheshimiwa Zitto Kabwe ni ya uwongo na ya uzushi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali haikuwahi kuleta Bungeni hoja ya kuunganisha *CHC* na Ofisi ya Msajili wa Hazina, Serikali ililetta hoja ya kuongeza uhai wa *CHC* kwa kipindi kingine cha miaka mitatu na kwamba baada ya kipindi hicho kazi zozote zitakazokuwa zimesalia zitahamishiwa katika Ofisi ya Msajili wa Hazina. Nasikitika kusema kwamba huu ndiyo msimamo wa Serikali hadi hivi ninavyozungumza.

Mheshimiwa Spika, nijumuisho hapa hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Wambura kwamba kuna tetesi kwamba wako watu waliorubuniwa kuhusiana na *CHC*, kwa masikitiko makubwa, naomba nikiri kwamba ni kweli tulipokea habari kwamba kuna tuhuma kwamba baadhi yetu walirubuniwa ili waitete *CHC* kwa nguvu zote. Serikali ililetta maombi kwamba iongezewe muda wa miaka mitatu, lakini nguvu zote zilielekezwa kwamba Shirika hili libadilishwe liwe la udugu na lilitetewa kwa nguvu zote. Hilo la rushwa, kwa sababu hapa ni Bungeni, zilitajwa Shilingi milioni 60 na yenye we inachunguzwa. Tumemwomba *Controller and Auditor General* achunguze haya ya wafanyakazi, lakini pia achunguze madai ya kwamba kuna rushwa ilitembea kushawishi Shirika Hodhi la Serikali, lipewe muda wa kudumu, badala ya muda iliyokuwa imepewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyotolewa Bungeni baada ya *Controller and Auditor General* kutoa taarifa yake. Hoja nyininge ilihusu utekelezaji wa agizo la Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma kwa *Controller and Auditor General* kufanya ukaguzi maalum kwa PPF, kuhusiana na mafao kwa kada ya watumishi wa mkataba.

Mheshimiwa Spika, *Controller and Auditor General* ameteua timu ya wataalam saba kutoka Ofisi yake kufanya kazi hiyo kwa mujibu wa hadidu za rejea zilizotolewa na Kamati. Timu hiyo ilianza kazi mwezi Julai na ripoti ya ukaguzi itawasilishwa kwenye Kamati kama ilivyoagizwa mara tu kazi hiyo itakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge ilihusu kupanga bei za bidhaa na huduma zitolewazo nchini kwa kutumia Dola za Kimarekani au kwa lugha ya kitaalam *dollarization*. Kifungu Na. 26 cha Benki Kuu sura 167, kinatoa mamlaka kwa Benki Kuu kutoa sarafu na fedha ya Tanzania ambayo lazima ikubalike kwa malipo yote hapa nchini, yaani *legal tender*. Hii ina maana kwamba ni kinyume cha sheria kwa mtu ye yeyote kukataa kupokea shilingi kama fedha ya malipo ya bidhaa au huduma inayotolewa hapa nchini. Sheria inamaanisha kuwa shilingi ndiyo fedha au sarafu pekee ambayo huwezi kukataa kupokea. Sheria hiyo haitamki kwamba ni kosa kutaja bei au kufanya malipo kwa kutumia sarafu nyininge zaidi ya shilingi ya Tanzania. Kwa hiyo, kama muuzaji na mnunuzi wanakubaliana, siyo kosa kufanya malipo ya dola. Kosa ni kukataa kupokea shilingi ya Tanzania kwa malipo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwataje Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, nilishamtaja, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Esther

Matiko, Mheshimiwa Christina Mughwai, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Betty Machangu Mheshimiwa Dada yangu Zakia Hamdan Meghji na Mheshimiwa Gaudence Kayombo

Mheshimiwa Spika, hoja nyiningine ilihusu tathmini ya sera ya ubinafsishaji. Kati ya majukumu ya *CHC* katika kipindi cha nyongeza cha miaka mitatu *CHC* kushirikiana kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Wizara za kisekta itafanya tathmini kwa utekelezaji wa Sera za Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Sambamba na zoezi hili, kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, itafanya tathmini ya zoezi la ubinafsishaji, yaani *post privatization monitoring and evaluation* kwa lengo la kubainisha utekelezaji wa makubaliano kimkataba na kupendekeza hatua za kuchukuliwa ikiwa pamoja na kuyanyang'anya. Aidha, baadhi ya mashirika nyeti kama vile *TANESCO, Tanzania Railways Limited*, Bandari na mashirika mengine ambayo ni nyeti kwa Taifa yataendelea kurekebishwa au kuboreshwa ili kuleta ufanisi zaidi katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, suala la Mheshimiwa Shah, la *UDA*, tumelipokea na tutalifanyia kazi. Hoja nyiningine ilihusu kuondolewa kwa ushuru wa bidhaa katika mvinyo unaotengenezwa katika soko la ndani ili kuongeza ushindani wa mvinyo utokao nje na kusaidia wakulima wa zabibu wa Mkoa wa Dodoma. Hili llichangiwa na Mbunge George Simbachawene, kwa niaba ya Wabunge wote wa Dodoma kwa maandishi na kwa kuzungumza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ushuru wa bidhaa utozwa kwa nia ya kudhibiti utumiaji wa bidhaa ziletazo madhara katika mwili wa binadamu au kama vile sigara, vinywaji mbalimbali vya kilevi, ikiwemo mvinyo pamoja na bidhaa za aina ya mafuta ya petroli. Aidha, ushuru wa bidhaa utozwa katika bidhaa au huduma maalum kwa nia ya kuongeza mapato ya Serikali. Mvinyo unaotengenezwa hapa nchini ulikuwa hautozwi ushuru wa bidhaa ukilinganishwa na mvinyo unaoagizwa kutoka nje ya nchi. Pamoja na kwamba utaratibu huu ulikuwa na nia ya kutoa unafuu wa kodi ili kuongeza ushindani na mvinyo kutoka nje, uchambuzi wa kitaalam umeonyesha kuwa utaratibu huo ulikuwa ukikiuka ushindani wa biashara kwa bidhaa zinazofanana na hivyo kupunguza mapato ya Serikali. Ili kupanua wigo wa kodi pamoja na kuleta ushindani ulio wa haki. Serikali imeamua kutoza ushuru wa bidhaa katika mvinyo unaotengenezwa hapa nchini, kwa kuwa suala hili ni la kisera, Serikali itaendelea kulifanyia kazi, lakini kwa sababu ya wito wa Wabunge wa Mkoa wa Dodoma, napenda niahidi kwamba tutalifanyia kazi na ikiwezekana kurekebisha kama itabidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyiningine ilihusu Serikali kuimarisha ufuatilaji wa kodi ya majengo. Serikali inakubaliana na ushauri huu na kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania itaendelea kuimarisha ufuatilaji wa kodi za majengo hasa katika Halmashauri za Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, tangu Mamlaka ya Mapato Tanzania ianze kukusanya kodi hii kwa niaba ya Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam, imekabiliwa na changamoto nydingi za kiutendaji, zikiwemo kukosekana kwa takwimu sahihi kutoka katika Halmashauri za Manispaa ya Mkoa wa Dar es Salaam, kuhusu idadi ya nyumba, wamiliki na thamani halisi ya nyumba hizo. Zoezi linaloendelea ni kutathmini nyumba katika Mkoa wa Dar es Salaam, nimebaini kuwa idadi ya nyumba zitakazoongezeka kutoka makadirio ya idadi ya nyumba, ni 83,505 hadi kufikia zaidi ya nyumba 435,000. Nyumba hizo zote zimefanyiwa tathmini upya na thamani yake imepatikana. Hatua hii pamoja na kukamilika kwa mfumo wa kuweka nyumba kwenye ramani, yaani *Geographical Information System* itaboresha ukusanyaji wa kodi za majengo kwa kiwango kikubwa na hivyo kuongeza mapato. Aidha, utaratibu huu utaenezwu kwenye Halmashauri nyiningine zote nchini na hasa Mwanza, Arusha na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, hoja ya uchapishaji wa noti mpya ni kwamba, tarehe 17 Desemba, 2010 Benki Kuu ya Tanzania ilizindua toleo jipya la noti ya Sh. 500/=, Sh. 1,000/= Sh. 5,000/= na Sh. 10,000/= ambazo zilianza kutumia tarehe 6 Januari, 2011.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida, Benki Kuu hutoa muda maalum wenye kikomo wa kubadili noti za zamani ili kuingiza mpya pekee pale tu panapokuwa na sababu maalum zilizosababisha kubadilisha kwa toleo la noti kwa mfano sababu za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei; pili, sababu za kiusalama kama vile kuibwa kiasi kikubwa cha fedha;

tatu, kuigwa noti bandia kwenye mzunguko. Mabadiliko ya noti zetu hayakutokana na sababu nilizotajaji hapo juu.

Mheshimiwa Spika, napenda ifahamike kuwa Benki Kuu inaweza kubadilisha noti zake baada ya miaka kati ya mitano mpaka saba kutokana na sababu kuu zifuatazo:-

Moja, maendeleo ya teknolojia ya kiuchapaji. Maendeleo haya yanawezesha mabenki kuchapisha noti bora zaidi na zeny alama nzuri zaidi ambazo ni ngumu kughushiwa.

Pili, mzunguko mkubwa wa fedha katika uchumi ambao husababisha uchakavu wa noti. Uchumi wetu kama ilivyo kwa nchi nyngi zinazoendelea bado unatumia fedha taslimu katika shughuli za kibashara. Hali hii hufanya mzunguko wa fedha kuwa mkubwa zaidi ikilinganishwa na nchi ambazo hazitumii kwa wingi fedha taslimu. Nchi zilizoendelea kwa mfano hutumia zaidi kadi za kielektroniki na malipo kupitia mabenki kuliko fedha taslimu. Mzunguko mkubwa wa fedha hulazimu Benki Kuu kuingiza noti katika mzunguko mara kwa mara. Katika kuingiza noti mpya kwenye mzunguko, Benki Kuu huweza kutumia fursa hiyo kutoa noti mpya ambazo zimeboreshwa zaidi kutokana na mabadiliko ya kiteknolojia.

Mheshimiwa Spika, hizi ndizo sababu kuu zilizofanya tubadili noti zetu na kuziingize kwenye mzunguko noti hizi mpya. Uamuzi huu hata hivyo hauathiri ugavi wa fedha kwenye mzunguko. Noti za zamani bado ni halali na zitaendelea kutumika sambamba na hizi mpya hadi hapo zitakapomalizika kwenye mzunguko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la noti bandia kuingia katika mzunguko, napenda ielevweke kwamba hili siyo tatizo la Tanzania peke yake, ni tatizo la dunia nzima. Nchi zote duniani hukumbwa na tatizo hili na zinaendelea kupambana nalo. Uhalifu wa kughushi noti na sarafu umekuwepo kwa karne nyngi duniani kote na kila nchi inatumia kiasi kikubwa cha raslimali zake kulidhibiti.

Kwa hapa Tanzania hatua muhimu ambazo zimechukuliwa ni pamoja na hizi zifuatazo: kwanza, tumetoa elimu kwa umma. Benki Kuu imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu alama za kiusalamu zilizopo kwenye noti mpya tangu ilipofanyanya uzinduzi wa noti hizo kupitia vyombo vy ya habari kama vile luninga, magazeti, matangazo, vipeperushi na kutoa elimu kwa Taasisi za Serikali. Lakini elimu hii kuhusu noti mpya na majukumu ya Benki Kuu kwa ujumla inapatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu. Naomba niinukuu: "www.bot-tz.Org" au wasiliana na Ofisi za Benki Kuu zilizopo Makao Makuu Dar es Salaam na matawi yake yote yaliyopo Arusha, Mbeya, Mwanza na Zanzibar. Pili, Benki Kuu imekuwa ikishirikiana na vyombo vy usalama ili kupunguza uhalifu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kadri muda unavyoendelea wananchi wanazidi kuzifahamu noti hizi na hivyo kutambua noti bandia kirahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyngine ilihusu kwamba litolewe tamko kuhusu tatizo la kushuka kwa thamani ya shilingi. Thamani ya shilingi ya Tanzania huamuliwa katika soko huru na hivyo inatarajiwa kupanda na kushuka kulingana na nguvu za kimitaji na ugavi sokoni. Benki Kuu huingilia kati mabadiliko ya thamani ya shilingi yasiyo ya kawaida ambayo huwa ni ya muda mfupi na yanayobainika kuwa hayaendani na hali halisi ya kiuchumi. Endapo mabadiliko ya thamani ya shilingi yanatokana na sababu za kimsingi za uchumi, yaani *Economic Fundamentals*. Benki Kuu haiwezi kuingilia kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na nguvu halisi ya soko na kunawenza kumaliza hazina yote ya fedha za kigeni bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya thamani ya shilingi yametokana pia na tofauti ya mfumuko wa bei kati ya Tanzania na nchi tunazofanyanazo bishara na hali ya soko la fedha duniani. Tathmini iliyofanyika katika kipindi cha Mei, 2011 hadi Agosti, 2011 thamani ya shilingi ilipanda na kushuka kati ya Sh. 1,538/= na Sh. 1,611/=, hii inaonesha kwamba, thamani ya shilingi hupanda na kushuka kulingana na nguvu za soko.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu kwa nini *SACCOS* yenyé mtaji wa zaidi ya shilingi milioni 800 hazisimamiwi na Benki Kuu. *SACCOS* yenyé mtaji wa zaidi ya shilingi milioni 800 zinaweza kusimamiwi na Benki Kuu kama zitaomba leseni ya kuwa Benki. Benki za Maendeleo ya Wananchi, yaani *Community Banks* zinahitaji mtaji wa shilingi milioni 250 tu. Kwa hiyo, *SACCOS* yenyé mtaji wa zaidi ya Shilingi milioni 800 zinashauriwa kuomba leseni na kujandikisha kama Benki. hususan Benki za Wananchi yaani *Community Banks*.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu kwa nini Serikali haijatimiza ahadi yake ya kuwalipa fidia wafanyabiashara waliopata hasara wakati wa m dororo wa uchumi, mfano uliotolewa ni *KCU* kwamba hawakulipwa kabisa. *KNCU* iliahidiwa kufidiwa kiasi cha shilingi 255.1 milioni lakini hadi leo hawakulipwa hata senti moja, ni lini waathirika hao watalipwa.

Mheshimiwa Spika, ni vyema kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba mpango na utaratibu mzima wa kunusuru uchumi uliotokana na m dororo wa uchumi duniani ulikuwa wa mwaka mmoja tu, yaani kuanzia tarehe 1 Julai, 2009 hadi tarehe 30 Juni, 2010 na waathirika wengi waliotuma maombi yao katika kipindi hicho na ambao walikidhi vigezo vilivyowekwa kikiwemo kile cha muda walifikiwa na kunufaika na mpango huo.

Mheshimiwa Spika, yapo makampuni mengi yamewasilisha maombi yao ya fidia ya hasara iliyotokana na m dororo, lakini hayakuweza kukidhi vigezo vilivyowekwa hasa kile cha muda na kuweza kuthibitisha kwamba kampuni husika illipata hasara katika kipindi hicho. Makampuni yaliyoshindwa kufikia vigezo hivyo yalishindwa kunufaika na huduma ya mpango wa kunusuru uchumi.

Mheshimiwa Spika, *KCU* na *KNCU* ni kati ya mashirika yaliyowasilisha maombi yao ya fidia lakini walishindwa kunufaika na huduma hiyo kwa sababu maombi yao yalishindwa kigezo cha muda. Hata hivyo, mpango huo umesitishwa kwa vile muda wake umekwisha na Serikali imeshindwa kupata fedha za ziada kwa ajili ya kuendeleza mpango huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kulipa madeni mbalimbali ya watumishi na wazabuni baada ya kuhakikiwa na kulingana na upatikanaji wa fedha. Hivi karibuni Serikali imeendelea kulipa madeni kwa ajili ya Walimu, Askari na Wazabuni katika vyombo vya ulinzi, madeni ya pango la nyumba kwa ajili ya Waheshimiwa Majaji, madeni ya posho za wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Umma, pamoja na madeni kwa ajili ya kugharamia kuwarejesha na kuwapeleka Mabalozi katika vituo vya kazi. Serikali itaendelea kuyalipa madeni mbalimbali ya watumishi na wazabuni katika Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Taasisi, Mikoa na Halmashauri za Wilaya baada ya kuhakiki madeni hayo na kulingana na upatikanaji wa fedha.

Maafisa Masuuli wameendelea kuelekezwa umuhimu wa kufuata taratibu za ununuzi pamoja na kulipia huduma kwa wakati. Aidha, matumizi ya ulipaji kwa kutumia mtandao wa *IFMs* yameendelea kuhimizwa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine inahusu Serikali kutoa tamko ni lini wastaa fu wa *East African Community* watalipwa madeni yao? Serikali tayari imeshawalipa wastaa fu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki madai yao kwa kufuata utaratibu uliokubalika, yaani hati ya maridhiano kati ya wastaa fu na Serikali. Malipo hayo yalilipwa kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2010 na yalihusu kiasi cha jumla ya Shilingi bilioni 117. Hata hivyo, kwa wale ambao walikuwa kwenye orodha kwa mujibu wa maridhiano na hawakulipwa, wakijitokeza wanalipwa.

Kwa hiyo, napenda kutoa wito kwamba wale wote ambao wanahisi wanastahili kulipwa lakini hawajalipwa, waende kwenye Ofisi yoyote ya Hazina nchini na ikithibitika kwamba kweli wana madai, watalipwa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu Serikali iangalie kwa umakini ukubwa wa deni la Taifa na ufutaji wa madeni yasiyolipika. Serikali inakubaliana na ushauri kuhusu udhibiti wa deni la Taifa. Mkakati wa madeni ya Taifa umeendelea kuwa nguzo ya kusimamia deni la Taifa ambapo kila baada ya miaka miwili tunafanya tathmini ya madeni kuangalia uhimilifu wa madeni na mikopo. Katika mwaka wa fedha uliopita 2010/2011 Serikali iliandaa mkakati wa kusimamia deni la

Taifa kwa muda wa kati ambao ni dira ya kuiongoza Serikali katika ukopaji. Mkakati huu umeainisha na kukokotoa gharama za athari za aina ya mikopo ambayo Serikali inatarajia kukopa na hivyo kuishauri aina bora ya mikopo ambayo Serikali inatakiwa kukopa ili deni la Taifa liendelee kuhimilika. Serikali imeendelea kusimamia kwa umakini deni la Taifa kwa kukopa zaidi.

Hoja nyingine ilihusu taarifa mbalimbali za takwimu zitolewe kwa uwazi ili kuwahusisha wana habari na wana taaluma wa kada mbalimbali. Ofisi ya Taifa ya Takwimu kupitia Sheria ya Takwimu ya mwaka 2002 imepewa Mamlaka ya kutoa takwimu zilizo rasmi nchini. Takwimu hizi zinatayarishwa kwa kufuata mwongozo unaotolewa na Ofisi ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa, yaani *UN Statistics Division*. Kazi ya kutoa takwimu imegawanyika katika sehemu kuu nne: Kukusanya taarifa, kuchambua, kutoa ripoti na kusambaza zilizopatikana kutokana na kazi hizi.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inatumia mfumo wa Shirika la Fedha Duniani, yaani *IMF* kwa kusambaza takwimu kwa wadu wote kwa wakati mmoja. Kwa mfano, matokeo ya tafiti zinazofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu yanazinduliwa kwa wadau wote kwa wakati mmoja. Takwimu zinazotolewa mara kwa mara kwanza Ofisi ya Taifa ya Takwimu inakubaliana na wadau wa takwimu hizo kuhusiana na tarehe ya kutangaza matokeo ya takwimu hizo.

Kwa mfano, mfumuko wa bei, ilikubalika kuwa matokeo ya kila mwezi yatangazwe tarehe 15 ya mwezi unaofuata. Hii inajulikana kwa wadau wote pamoja na waandishi wa habari. Takwimu hizi pia zinapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, kama mtumiaji anatafuta maelezo ya ziada Wataalamu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu wenye weledi stahidi watatoa maelezo hayo ya ziada pale yanapohitajika.

Mheshimiwa Spika, hoja ya uhusiano wa moja kwa moja kati ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mikoa, Halmashauri, Kata na Viji. Mpango wa kuboresha na kuimrisha takwimu nchini, yaani *Tanzania Statistical Master Plan* ulioridhiwa na Serikali mwezi Juni, 2010 utaimarisha uhusiano wa kitakwimu uliopo kati ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mikoa, Halmashauri, Kata na Viji. Ofisi hii itaratibu utekelezaji wa mpango huu ikihusisha mfumo mzima wa takwimu nchini, yaani *National Statistical System*. Mpango huu utahusisha kuwajengea uwezo wa takwimu, wote walio kwenye Mikoa na Halmashauri na hatimaye kufikia ngazi ya Kata na Viji. Hii ni pamoja na kuboresha vitendea kazi katika ngazi hizi ili kuimrisha ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu mbalimbali. Kukamilika kwa mpango huu kutawezesha kuongeza watumishi katika ngazi za Mikoa, Halmashauri, Kata na Viji.

Hoja nyingine ni juu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, inafanya kazi katika mazingira magumu, inatumia vitendea kazi duni na inakusanya takwimu baada ya kipindi kirefu sana kupita, mfano baada ya miaka mitano hadi kumi. Ni kweli kuwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ina changamoto kubwa katika kutoa takwimu nchini. Hali hii kwa kiasi kikubwa kuanzia mwaka 2008 Serikali imeongeza uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika kukabiliana na changamoto kwa kuongeza bajeti yake. Taarifa zinazokusanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu zimegawanyika katika sehemu kuu mbili. Kwanza ni taarifa za kila mwaka na mwezi. Hizi ni takwimu zinazotumika katika kutathmini ukuaji wa sekta husika. Pili, taarifa za muda mrefu kwa kipindi cha miaka mitano au kumi, hizi ni taarifa zinazotoa takwimu za msingi na sura halisi ya sekta husika. Takwimu hizi zinapatikana kwa kufanya utafiti mkubwa kwa njia ya sampuli au sensa. Huu ni utaratibu wa kawaida wa kukusanya takwimu katika Ofisi za Takwimu Duniani.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine, ilishauriwa kwamba Serikali iangalie kwa umakini ukubwa wa deni la Taifa la uftaji wa madeni yasiyolipika. Serikali inakubaliana na ushauri huu wa kudhibiti deni la Taifa, wakati madeni ya Taifa yanaendelea kuwa nguzo ya kusimamia..., hii nimeshaisoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwataje wengine waliochangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Subira K. Mgalu, Mheshimiwa Amina N. Makilagi, Mheshimiwa Esther L. M. Midimu na Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani - Mbunge wa Tunduru.

SPIKA: Siyo kweli. Mwanza huyo, ni Busega, siyo Tunduru. (*Makof*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, samahani ni Busega. Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengaya Kamani - Mbunge wa Busega.

Mheshimiwa Spika, michango ilikuwa mingi na karibu michango kama sita au saba hivi nimeipokea wakati nainuka kuja hapa, hiyo kwa vyovvye vili hatukweza hata kuisoma lakini naahidi kwamba michango yote tutaiweka kwa maandishi. Kama kawaida, taarifa ya michango hiyo itawasilishwa Bungeni ili kila mmoja ambaye amechangia aone tumejibu vipi. Kwa hiyo, wale wote ambaa mlizungumza, lakini michango yenu sikuweza kuizungumza, lakini mjue tu kwamba itashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 21 – Hazina

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona, muda wetu hautoshi tutajaribu tujipe dakika tano tumalizie na *Appropriation Bill*, kwa hiyo, tunaweza kufanya kazi kwa haraka.

Waheshimiwa Wabunge, Fungu la Mshahara ni fungu la 50 msije mkaanza kudai mishahara kwenye fungu la Hazina.

Kif. 2001 - *Gov't Budget Division*.....Sh. 843,912,416,200/=
Kif. 2002 - *Policy Analysis Division*... Sh. 150,284,132,700/=
Kif. 4001 - *External Finance Division*...Sh. 6,362,538,000/=
Kif. 7001 - *Poverty Eradication and Empowerment*..... Sh. 2,514,057,100/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 22 – Deni la Taifa

Kif. 1001 - *Administration and General Services*.....Sh. 1,901,850,995,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 23 – Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali

Kif. 3001 - *Public Debt Management*Sh. 530,800,000/=
Kif. 3002 - *Expenditure Management*Sh. 25,993,758,000/=
Kif. 3003 - *Financial Management*.....Sh. 45,721,928,341/=
Kif. 3004 - *Systems and Internal Audit*Sh. 5,451,449,200/=
Kif. 3005 - *Sub Treasury Arusha*Sh. 248,815,119/=
Kif. 3006 - *Sub Treasury Coast*Sh. 207,166,493/=
Kif. 3007 - *Sub Treasury Dodoma*Sh. 405,194,475/=
Kif. 3008 - *Sub Treasury Iringa*Sh. 227,881,153/=
Kif. 3009 - *Sub Treasury Kagera*Sh. 226,660,000/=
Kif. 3010 - *Sub Treasury Kigoma*Sh. 240,428,429/=
Kif. 3011 - *Sub Treasury Kilimanjaro*Sh. 253,220,518/=
Kif. 3012 - *Sub Treasury Lindi*Sh. 235,308,196/=

Kif. 3013 - *Sub Treasury Mara* Sh. 227,882,500/=
 Kif. 3014 - *Sub Treasury Mbeya* Sh. 230,899,800/=
 Kif. 3015 - *Sub Treasury Morogoro* Sh. 271,634,740/=
 Kif. 3016 - *Sub Treasury Mtwara* Sh. 223,289,224/=
 Kif. 3017 - *Sub Treasury Mwanza* Sh. 238,916,090/=
 Kif. 3018 - *Sub Treasury Rukwa* Sh. 240,514,300/=
 Kif. 3019 - *Sub Treasury Ruvuma* Sh. 225,600,220/=
 Kif. 3020 - *Sub Treasury Shinyanga* Sh. 222,995,539/=
 Kif. 3021 - *Sub Treasury Singida* Sh. 224,616,343/=
 Kif. 3022 - *Sub Treasury Tabora* Sh. 238,814,000/=
 Kif. 3023 - *Sub Treasury Tanga* Sh. 225,433,520/=
 Kif. 3024 - *Sub Treasury Manyara* Sh. 226,373,800=/

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7001 - *Pension and Gratuity* Sh. 556,925,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Kif. 1001 - *Administration and General* Sh. 14,943,506,000/=
 Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit* Sh. 2,219,359,000/=
 Kif. 1003 - *Internal Audit Unit* Sh. 181,263,000/=
 Kif. 1004 - *Ministerial Audit Division* Sh. 3,391,915,000/=
 Kif. 1005 - *Regional and Local Gov't Audit
Division* Sh. 5,104,342,000/=
 Kif. 1006 - *Value For Money Audit Division* Sh. 1,355,280,000/=
 Kif. 1007 - *Treasury Audit Division* Sh. 1,958,641,000/=
 Kif. 1008 - *Techn Support, Research
and Consultancy* Sh. 3,556,597,000=/

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA

Kif. 1001 - *Administration and General* Sh. 5,563,134,500/=

MWENYEKITI: Mjue mko wengi na muda hautoshi. Tunaanza na Mheshimiwa Leticia Nyerere, mkiwa *brief* tunaweza kutoa nafasi kwa wengi.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anatoa majumuisho kuhusu *stimulus package*, swali ambalo nilikuwa nimeliuliza na likakosa majibu cha kushangaza, ametueleza makampuni ambayo yalishindwa kufanikiwa kwa mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa hapa tulitaka kujua ni akina nani amba walinufaika na hizi fedha za walipa kodi? Naomba maelezo ya kina, tunataka majibu ya hawa amba walinufaika na fedha hizi za *stimulus package*. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Hilo ni kweli na Wizara imeniangusha kwa sababu kazi hiyo mlipewa wakati swali linajibowi. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni ambayo yalinufaika na *stimulus package* ni mengi, lakini mengi sana ambayo yalinufaika kwa *cash* ya shilingi bilioni 19.2 ni makampuni 97.

MWENYEKITI: Sisi tulichotegemea pale mngesambaza karatasi inayoonyesha makampuni hayo ni yapi. Kwani ni toka zamani, tuna miezi karibu miwili hapa. Hapo hamkujibu. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaagiza karatasi isambazwe.

MWENYEKITI: Yaani tukiishawaambia kwamba jamani kazi ikafanywe, mnatakiwa kwenda kuifanya. Hii ina miezi miwili hapa!

MHE. CHIRISTINA L. MUGWHAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Zamani Benki Kuu (*BoT*) ilikuwa ina utaratibu wa kuweka hifadhi ya dhahabu ili kunusuru uchumi na hasa thamani ya shilingi. Je, Mheshimiwa Waziri atatueleza utaratibu wa kuweka hifadhi ya dhahabu sasa utarejeshwa lini? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christina Lissu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu ilikuwa inafanya utaratibu huu, lakini matokeo yake ikawa inapoteza fedha kuliko *ku-gain*. Kwa hiyo, ikawa inajaribu kutafakari upya *logic* ya kuendelea na utaratibu huo.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha anatoa majibu kuhusiana na suala la *Consolidated Holdings Corporation (CHC)* ametoa maelezo hapa kuhusiana na tuhuma ambazo amezisikia kama tetesi na ameliambia Bunge lako Tukufu kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) pamoja na mambo mengine anafanya kazi tuhuma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina *email* hapa kutoka kwa *CAG*, suala la uchunguzi wa hizo tuhuma za Shilingi 60 zinazosemwa hazimo katika hadidu rejea ambazo zimetoka kwenye Bodi ya *Consolidated Holdings* kwenda kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba Waziri wa Fedha sasa aagize rasmi kwamba ziwekwe ili zichunguzwe. Lakini pili, naomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora) aiagize Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (*TAKUKURU*) pia ifanye uchunguzi huu, na uchunguzi huu uwerekwe wazi, utangazwe wazi na Waziri wa Fedha aahidi kwamba, ikigundulika maneno aliyoyasema ni uongo na uzushi ndani ya Bunge, atajuzulu mara moja nafasi hiyo. Mimi kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma (*POAC*) ikigundulika kwamba siyo mimi tu, bali Mjumbe mwingine ye yote wa Kamati kwa njia moja au nyininge alirubuniwa kwa kupewa fedha kwa ajili ya kuitetea *CHC*, siyo tu nitajiuzulu Uenyekiti, bali nitajiuzulu Ubunge kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba taarifa, kwanza *TAKUKURU* wachunguze, Waziri wa Fedha ahakikishe hadidu rejea zinafanyiwa *amendments* ili suala hilo *CAG* alichunguze na taarifa hiyo itangazwe wazi na mimi na yeye tuweke ahadi hapa mbele ya Bunge ya kuwajibika kuto kana na matokeo ya uchunguzi utakaofanywa.

MWENYEKITI: Haya. Hizo ahadi mimi nilifundishwa kwamba usiape kwa jina la mtu aliye juu sana. (*Kicheko*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nafurahi sana jinsi Mheshimiwa Kabwe Zitto anavyofuatilia suala hili. Mimi mwenyewe kama Waziri wa Fedha sijazona hizo hadidu za rejea ambazo zimepelekwa kwa *CAG*, lakini nitaletewa. Nataka nimuhidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuhuma hizi ni nzito na ndiyo maana nikazisemea kwamba nitazifanyia kazi. Katika Serikali, tuna utaratibu wa mambo yanapokuwa nyeti kiasi hicho, jinsi ya kuvia giza vyombo vya Serikali, vifanye uchunguzi wa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili la wafanyakazi, ni kama hivyo uliviyoliona. Hili la rushwa na Wabunge kurubuniwa litafanyiwa kazi kwa namna na utaratibu wa kiserikali. Naahidi na Waziri

Mkuu wangu ananisikia hapa kwamba, baada tu ya taarifa kukamilika kwa utaratibu wa kiserikali, itawasilishwa ndani ya Bunge lako.

MWENYEKITI: Sasa hili la kujiuzulu, sisi tuhuma hatujazona hapa kwamba liko namna hiyo. Tunasikia, nyie mnabadilishana tuhuma za rushwa, sisi hatujazipata. Mimi nimepata malalamiko ya wafanyakazi, lakini hawakumtuhumu mtu kupokea rushwa. Sasa hili wengine hatulijui. Mnapoapiana muache kazi na mwingine aache na Ubunge kabisa, eeh! (*Kicheko*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kujiuzulu nadhani unatokea nje siku hizi. Kwa sababu kwanza tungesubiri uchunguzi ufanyike, tuhuma zidhihiri, taarifa ipatikane, halafu ndio lije suala la mtu kujiuzulu au kutojhuzulu. (*Makofi*)

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nami kwa kunipatia nafasi. Napenda tu nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba kwa kuwa sasa hivi tuko kwenye soko huria na mafuta yamepanda bei kwa kiasi kikubwa, na katika biashara ya usafirishaji hasa kwa hawa bodaboda na *taxi* imekuwa ni mtafaruku na kila mara ni kugombana, na kwa kuwa watu hawa *Taxi* wamekuwa wakilipa kodi zao kubwa kwa mwezi kwa kiasi cha Sh. 250,000/=.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuliangalia suala hili upya? Je, inasema nini kuhusiana na suala hilo?

MWENYEKITI: Hapa mnaulizwa Mawaziri wote, naomba maelezo ya haraka.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda angerudia, sikumwelewa vizuri.

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Kikwembe na wewe urudie *direct*, usizunguke.

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu ni kwamba, Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia upya kodi wanazotozwa wafanyakabiashara wa bodaboda na *taxi* kwa kuwa sasa hivi mafuta yamepanda bei na abiria wengi wamekuwa wakipenda kupanda bodaboda na siyo *taxi*, hivyo kusababisha mtafaruku katika biashara hiyo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wake kuhusiana na kuwafikiria hao watu wa bodaboda tutauzingatia.

MWENYEKITI: Mtashughulikiae? Maana yake hizo ni ahadi, msidhani mnafanya kazi...!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu yeye anasema kwamba labda kiwango cha mafuta yanayotumiwa na bodaboda ni kikubwa, tutaangalia au tutajaribu kufanya *review* hapo baadaye.

MWENYEKITI: Wanasema Mawaziri wa Fedha hamsikiki. Ndiyo malalamiko yaliyoko huko!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kuhusu suala la bodaboda ambao wanatumia pikipiki tutalichunguza na kuangalia uwerekano wa kuwasaidia.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa hivi sasa huduma ya benki nchini ni asilimia ndogo sana (12.4%) tu ya Watanzania ndio wanapata huduma za kibenki pamoja na taasisi nyingine za fedha na ni kama watu milioni mbili tu kati ya watu wazima zaidi ya milioni 20 wanaoweza kuweka fedha benki. Kwa kuwa riba za benki hivi sasa ukikopa fedha ni asilimia kubwa sana, asilimia 18 mpaka ishirini asilimia 20 na kwamba wewe fedha zako kama umeweka mle riba unayopewa ni asilimia tatu tu.

Je, Waziri atatoa tamko gani leo kwa ajili ya ujenzi wa Benki, kupanua mtandao wa upatikanaji wa huduma za Kibenki na sehemu nyingine nchini? Lakini sambamba na kuhakikisha kuwa asilimia inayotozwa kwa wakopaji inakuwa ni ndogo ili kuwawezesha Watanzania kunufaika

na fedha wanazokopa kwenye Benki kuliko ilivyo sasa badala ya wao kuwezeshwa kiuchumi, sasa wanafilisiwa!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi ufuatao kuhusu mtandao wa Kibenki. Hili ni suala ambalo linafanya na *Private Sector*, lakini kazi ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunawarahisishia na wanajitahidi kushughulikia.

Kuhusu suala la riba tunalifanya kazi, lakini tukumbuke kwamba Serikali imejitoa kwenye biashara moja kwa moja, kwa hiyo, tunachofanya ni kutimiza uzuri wa mazingira ya kushuka kwa riba.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa niaba ya wazee wa Mkoo wa Mara hususan Wilaya ya Musoma ningependa kupata ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa kwa takriban miaka miwili sasa wazee wanaotakiwa kulipwa pensheni na Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (*LAPF*) hawaajaanza kulipa pensheni mpya kama ilivyoamuliwa na Bunge kwa kima cha chini cha Sh. 50,000/= . Sasa ningependa kujua ni kwa nini wazee hawa hawajalipwa kiwango hicho cha kima cha chini kwa Sh. 50,000/= kwa miaka miwili sasa?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Kirigini. Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa uko chini ya Waziri wa Serikali za Mitaa. Ninachowenza kukifanya ni kwamba nalichukua suala hilo, nitazungumza na mwenzangu kuona tatizo ni nini ili tuweze kurekebisha na wazee hawa waweze kulipwa pensheni zao.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Siku za karibuni shule

MWENYEKITI: Naomba muwe *brief* kusudi watu wengi wapate nafasi.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zinapofunguliwa na vyuo, kunakuwa na msongamano mkubwa sana wa wanafunzi kwenda kulipa karo kwenye Mabenki. Kwenye Wilaya nyingine unakuta Benki ni moja, wanafunzi inabidi walale pale kwenye Benki ili waweze kuwahi kulipia. Hivi Serikali haioni kuna haja ya kufanya njia maalum nyingine ili kuondoa hili tatizo kwa sababu tunarudi enzi za zamani za kujipanga kama *RTC*?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kutoa ufanuzi kwamba hili linahusiana na mtandao wa Benki kuhakikisha kwamba zinatika sehemu nyingi zaidi. Lakini kwa kushauriana na wenzetu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis tutaangalia kama kuna namna nyingine ya kulirahisisha.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, mara kadhaa kuanzia kile kipindi cha bajeti mpaka leo Wizara ya Fedha tulizungumzia, naweza nikasema sijui ni wizi wa makusudi unaofanya na *TRA* kwenye mizigo inayoingizwa bandarini na hususan magari! *TRA* kuna utaratibu ambaa umewekwa na makubaliano ya *WTO* lakini vile vile Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004. Lakini kibaya ni kwamba licha ya kwamba mikataba yote miwili pamoja na sheria imeweka vigezo vya kuweza kutoza ushuru. *TRA* imekuwa inaruka vigezo vitatu vya mwanzo na kwenda kigezo cha nne ambacho kinakuwa ni maumivu makubwa sana kwa mlaji.

Sasa nilikuwa naiomba Serikali *iji-commit* kwa sababu nilishaeleza *in detail* kwenye maandishi kwamba itafuatilia kero hii inayowapa madhara wafanyakishara wetu wakubwa na wadogo, inayowapa hasara kubwa Watanzania wa kawaida ambaa wanaagiza bidhaa zao. Naomba *commitment* ya Serikali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi kuhusu swali hili. Utaratibu wa *ku-value* bidhaa kwa ajili ya kutoza ushuru haujakiukwa na *TRA* katika suala hili la magari au vinginevyo au kutathmini vifaa. Hata hivyo, sisi

tuko tayari kama tulivyoahidi katika kitabu chetu ukurasa wa 43 kwamba ukadiriaji wa kodi za magari yanayotumika unaozingatia uchakavu tutaboresha, tutaaingalia nini ambacho kinafanyika. Lakini hata hivyo, kuna taratibu za kutosha za kumlinda mlipaji kodi kama anahisi ametendewa siyo haki. Kwa hiyo, kama pale ambapo itakuwa bado hatujalimaliza, basi kuna *avenues* ambazo haki inaweza ikafuatiliwa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilihoji masuala kadhaa kuhusiana na malipo ya fedha za wananchi wa *DECI* na kuhusiana vile vile na *CHC* kuchukua hatua kuhusu viwanda. Lakini hapa niombe ufanuzi kuhusu suala moja la kisera, hayo mengine tutajulishana kwa maandishi. Kwa mujibu wa Sheria za Fedha wa Ukagazi wa Umma (*Public Audit Act*). *CAG* anapofanya ukagazi wa fedha haangalii wizi tu peke yake, anaangalia vile vile ufanisi wa matumizi ya fedha. Wizara hii ndiyo ambayo inahusika na Ofisi ya *CAG* na inahusika vile vile na *Paymaster General* kwa maana ya Mlipaji Mkuu.

Kwa kuwa imeelezwa hadharani na Katibu Mkuu Kiongozi kuhusiana na namna ambavyo fedha za Wizara ya Nishati na Madini zimetumika kiubadhirifu pamoja na kumtupia Jairo, ningependa kupata kauli ya Waziri wa Fedha kama mtu ambaye *Paymaster General* yuko chini yake, *CAG* yuko kwenye Wizara yake, ni hatua zipo anachukua yeze kama Waziri wa Fedha kutokana na matumizi mabaya ya kibadhirifu ya fedha za umma kwenye suala la nishati na madini?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfumo ambao *Paymaster General* anautumia na kuna mfumo ambao *Controller and Auditor General* anautumia. Lakini kwa sababu swali lilitoloulizwa ni *specific* na bado lipo humu Bungeni kwamba baadaye leo tutaambiwa Kamati itakayoundwa kulichunguza. Ningefikiri hili lingeingia kule kwenye Kamati.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, sasa hivi tunavyozungumza, nchi bado iko katika mgao wa umeme na miezi miwili imeshapita na hii tayari imesha-*impact* kwenye *revenue collection*. Je, katika miezi hii 10 iliyobaki na *projection* ya *revenue* ya Serikali tumeiweka katika *6.7 trillion*. Kwa mawazo yake na katika hali hii bado tuna *shortfall* ya *energy* ya megawati 500 ili i-*contribute* kwa ajili ya *generate production* kwenye viwanda na uchumi kiujuimla. Je, anatarajia kwamba mapato haya kama tumeya-*approve*, leo tunahitimisha, Serikali itapata mapato haya pamoja na hali halisi hii ya umeme ambao haupo?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikiri kwamba ni kweli tatizo la umeme linaathiri uzalishaji. Lakini kwa bahati nzuri Makampuni mengi hasa yale makubwa ambayo yanachangia karibu asilimia 70 ya kodi yametafuta njia zao wenyeza za kutafuta umeme wa ziada. Kwa hiyo, Makampuni mengi kwa kweli japokuwa wanatengeneza bidhaa zao kwa bei kubwa, lakini wanazalisha vizuri. Tutapata *shortfall*, lakini siwezi kukwambia sasa hivi hapa *shortfall* hiyo itakuwa kiasi gani. Kwa sababu mwezi Julai makusanyo ya *TRA* yalifikia asilimia 96 pamoja na kwamba tuna tatizo la umeme. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Mgimwa atuachie tumalize Bunge, turudi Dar es Salaam tukafanye tathmini sawasawa ili tuweze kuona hali halisi sasa itakuwaje. Lakini kwa leo siwezi kuona hali halisi ya kwamba tutaathirika kiasi gani, lakini tutaathirika kwa namna fulani ikiwa mgao wa umeme utaendelea kuwepo kwa muda.

MWENYEKITI: Ni kuuzuia tu.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Kwanza na-*declare interest*, mimi mwenyewe ni mwathirika wa *TRA*. Hiyo ndiyo ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale bandarini *TRA* magari wanatoza bei wanayotaka kama waganga wa kienyeji, wapiga ramli. Nimeagiza magari mawili kwa ushahidi nimemwendea Mheshimiwa Mkulo, Manaibu Waziri, Ndugu Kitilya, Bwana Juma bila msaada wowote, wanakisia gari moja mpaka shilingi bilioni moja, kama waganga wa kienyeji. Huku na huku kwa sababu gari itakaa bandarini imebidi nilipe ushuru kwa bei wanayotaka wao. Anihakikishie Mheshimiwa Mkulo na nimemwambia Bwana Kitilya niko tayari kumpa na dola 1,000 aende *Muscat* aaulizie bei

niliyonunulia magari kwenye Kampuni na Ubalozi wa Oman aulizie, lakini wamekataa. Ni kama majambazi wanatuibia bei ya ajabu ajabu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba warudishe tofauti ya fedha za gari langu na la Mheshimiwa Mipata. Wametuobia mchana kweupe. Kwa hiyo, naomba ajibu, na nimeandika, lakini hata jina langu hakulisoma hapo katika waliochangia. Bwana Kitilya yuko hapa, Bwana Juma aliniona kama mimi ni zezeta. Naomba nifuatilie na niliwaambia gari langu kama limezidi hata riale moja ya Oman niko tayari magari yangu haya Serikali iyachukue, lakini hawakusikiliza. (*Makofii/Kicheko*)

MWENYEKITI: Basi Mheshimiwa tumekusikia. Sasa anacho sema mtawarudishia fedha zao zilizotozwa zaidi kwa magari yao? Kwa sababu swali la mwanzo alishauliza Halima, sasa huyu anasema mtawarudishia tofauti ya fedha hizo za magari yao yeye na Mheshimiwa Mipata?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Keissy nalifahamu vizuri kwa sababu ni kweli alikuja ofisini, lakini pia ni kweli kwamba nimezungumza na Kitilya, kuna matatizo ya aina fulani kwamba gari hili limetengeneza Japan lakini limeuzwa Oman. Kuna gari lingine limetengeneza Japan lakini limeuzwa Uchina. Sasa kuna vi-complications vingi vingi ambavyo vinahitaji vitatuliwe. Nataka nimuhidi Mheshimiwa Keissy kwamba Bwana Kitilya yuko hapa. Nimezungumza naye hata jana wanashughulikia ili waweze kupata ufumbuzi. Sio yeye peke yake, wamenijia Wabunge karibuni hata 20 kwenye suala hili hili. Nataka niahidi kwamba linashughulikiwa na tutalifanya kazi. Sasa kama atarudishiwa fedha au hatarudishiwa, hilo sasa litategemea na sheria za *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kama sikumtaja jina, kama inaruhusiwa, basi naomba niweke jina lake.

MWENYEKITI: Ndio umeshampata Mheshimiwa Keissy. Kwa hiyo, kitu hicho nadhani mwangalie kimfumo. Sio hao wawili, hizi ni *indicators* tu. Mwangalie kimfumo. (*Makofii*)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nadhani Wabunge wenzangu na Watanzania wanashuhudia siku hadi siku shilingi yetu inavyoshuka thamani na moja ya sababu kubwa inayochangia shilingi yetu kushuka thamani ni kuruhusu matumizi ya dola kiholela hapa nchini. Wakati tunashuhudia sisi tunaruhusu matumizi ya dola nchini kiholela, vile vile tunaona nchi za wenzetu zilivyo kuwa *strict* na matumizi ya dola nchini kwa kuhofia tu shilingi yao kushuka, ukienda Afrika ya Kusini, China. Lakini mpaka sasa hivi sijaona mikakati madhubuti ya kunusuru shilingi yetu. Je, Mheshimiwa Waziri ana mikakati gani ya kuhakikisha shilingi yetu haishuki na pia anawaambiaje Watanzania kupiga marufuku matumizi ya dola kwa wageni wanapoingia nchini? (*Makofii*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyo jibu kwenye jibu la msingi ni kwamba wakati fulani sisi wenye we tuliamua kuingia kwenye uchumi huria. Hasa uchumi huria ni kwamba unaichia shilingi itafute nguvu yake kwenye soko, *floating exchange rate*. Sasa nimeeleza kwamba sasa hivi siyo shilingi ya Tanzania peke yake. Kwa mfano, sisi hapa imeshuka kwa asilimia nane. Kenya imeshuka kwa asilimia 14, Uganda imeshuka kwa asilimia 21. Katika kipindi hiki, kuonyesha kwamba matatizo yetu hapa Afrika Mashariki ni ya namna moja, ni kwamba zile nchi ambazo tuna-deal nazo kibiashara, fedha zao zimeongezeka nguvu zaidi kulikoni ya kwetu. Lakini Benki Kuu inajitahidi kila inapotokea wanafanya kitu fulani ili kuhakikisha kwamba tuna-stabilize ile bei. Lakini suala ni kubwa, ni suala nyeti niseme tu kwamba tunalichukua tutazungumza na Gavana tuone jinsi gani tunaweza tukafanya, lakini uwezekano wa kwamba tunaweza tukaamua leo, kwamba kuanzia leo tunarudi kwenye kuhodhi maamuzi. Inawezekana isiwe rahisi kwa wakati huu, lakini tutalifanya kazi.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nimeuliza katika Wizara ya Fedha kutokana na ongezeko kubwa la wastaafu nchini na kwa kuzingatia ugumu wa maisha hivi sasa: Je, Serikali iko tayari kuongeza pensheni ambayo wanalipwa wastaafu kutoka Sh. 50,000/= na ni lini itatekeleza mpango huo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la wastaafu kama nilivyokuwa nimehitimisha hapa kwamba ni nyeti kwamba tayari Serikali ilishaongeza hicho kima cha chini miaka kama sita hivi. Kiwango cha chini kabisa miaka ya zamani ilikuwa ni Sh. 2,000/= na mpaka sasa hivi kufikia Sh. 50,114/= ni hatua na tunasema kwamba kadri Serikali inavyopata uwezo wake huwa ina-consider kima chini. Kwa sasa hivi utaratibu unafanywa ili tuweze kukiongeza kadri inavyopata mapato yetu.

MHE. ANNA K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kwanza ku-declare interest, mimi ni member wa Executive Committee wa ALAT Taifa na ni member wa Executive Committee wa East African Local Government Association.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba *commitment* ya Serikali kwenye fedha za miradi ya Halmashauri zetu zote Tanzania. Kwa sababu ni kweli Serikali inatupelekea fedha nydingi sana za miradi kwenye Halmashauri zetu, lakini fedha zile hazifiki kwa wakati. Kwa hiyo, sisi, hasa sisi Wabunge wa Majimbo, hili linatupa taabu. Ningeomba Mheshimiwa Waziri atoe *commitment* kwamba kipindi hiki, narudia kipindi hiki atatuletea fedha kwa wakati?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli hilo ilikuwa ni tatizo la muda mrefu na nataka nimhakikishie Mbunge kwamba kuna kipindi hiki au mwaka huu wa fedha unaokuja na sisi tumejipanga vizuri na tutahakikisha kwamba fedha ambazo zinapelekwa zitakuwa zinakwenda na wakati.

MWENYEKITI: Ahadi ni deni, ahadi ni deni!

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Serikali yetu inafanya mambo mazuri sana. Pale Mbanga wameanzisha programu ya VICOBA na Wizara ilikuwa imeji-commit kuendeleza ile programu na walianza na Kata 12 na walifundisha walimu na wale walimu waliteuliwa kwenda kufundisha katika vijiji. Wamefanya hiyo kazi, waliahidiwa kupata posho, mpaka leo hawajapata miezi karibu mitatu au minne. Ningefurahi kama Waziri angeweka *commitment* ya kuendeleza project hii ili pia iweze kuendelezwa katika miradi mingine hii ikiwa ni pamoa na kumpongeza Mheshimiwa Devotha Likokola ambaye ni champion mzuri sana wa VICOBA.

MWENYEKITI: Ni VICOBA. Okay!! Ninyi mnajua hiyo habari, hebu jibuni hapo. Nadhani hakuna anayejua habari hiyo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA: Hatujaipata.

MWENYEKITI: Anasema mlipeleka watu kwenda kufundisha habari za VICOBA na wale waliokuwa wanafundisha hawakuwahi kulipwa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tutawasiliana na Mbunge ili tuweze kufuatilia hao ambao hawajalipwa tuangalie kama kuna uwezekano wa kulipwa.

MWENYEKITI: Hawakuwepo wakati wanafanya hivyo. Hawa wote hawakuwepo. Mheshimiwa Missanga.

MHE. MOHAMMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu kama unavyokumbuka nilitoa *specific issue* ya pensheni kwamba Rais na Mheshimiwa Waziri kuititia *Government Notice* Na. 206 ya tarehe 29 Juni, 2009 ilikubalika na kuidhinishwa kwamba pensheni zilekebishwe na *schedule* iko pale na mimi nimekuletea mezani kwako. Sijamsikia Mheshimiwa Waziri alijibu juu ya hilo. Kwa nini haikutekelezwa wakati Mheshimiwa Rais ameshatoa kibali chake?

MWENYEKITI: Bahati mbaya *schedule* yenye sijampa. Unaweza ukijibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishapata hiyo *schedule* kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge tutaishughulikia.

MWENYEKITI: *Schedule* tunayo sisi hapa, alii-*table* hapa mezani, lakini mpate muda kwa sababu majibu yaliyokamili ni bora zaidi kuliko majibu yaliyo nusu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba uvute subira, wataleta majibu kwa maandishi.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Taasisi ya Uhasibu Tanzania, Tawi la Mtware kwa muda mrefu ina kiwanja kinachotarajiwa kujengwa kwa ajili ya kuendeleza taasisi hiyo kwenye Tawi la Mtware na kama ulivytangulia kusema kwamba ahadi ni deni. Kwenye Bunge la Bajeti liliopita la mwaka jana Mheshimiwa Mkulo aliahidi kuwa angetenga pesa kwenye bajeti hii kwa ajili ya kuanza kujengwa kwa kiwanja kile. Lakini nimeangalia mpaka kwenye kitabu cha maendeleo hapa sioni kitu chochote hapa. Anatuambia nini tena?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi yetu iko palepale, lakini kwa mwaka huu utakubaliana na mimi kwamba kila aliyesimama hapa kuna ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, kupanga ni kuchagua, ikabidi tuelekeze pesa mahali fulani, lakini naahidi kwamba tutajenga tutakapokuwa na uwezo.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Moja lilikuwa ni hili alilosema Mheshimiwa Keissy lakini la pili kwanza ni-*declare interest* ni mjumbe wa *ALART* Mkoa wa Rukwa. Ninataka kuzungumzia juu ya fedha nydingi zinazopelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya ambazo utekelezaji wake haulingani na thamani halisi ya pesa zenyewe. Je, Wizara ina mpango gani kuangalia kwamba miradi ile inayotekelawa kwa hela nydingi hizo inalingana na pesa zinazotumika? (*Makof*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanzania katika nchi 14 za Afrika Mashariki tunaongeza kwa Serikali Kuu kuziwezesha *Local Government* kimapato. Katika triliuni 13 zilizopitishwa kwenye bajeti, triliuni tatu zinakwenda kwenye Serikali za Mitaa. Tumevuka malengo yale ambayo nchi za Afrika inataka asilimia 25.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, punguza maneno, tuna matatizo ya muda.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, jukumu la kuhakikisha kwamba fedha zinazokwenda Halmashauri zimetumika vizuri ni jukumu la Baraza la Madiwani ambalo sisi Waheshimiwa Wabunge ni sehemu yake, tukitegemea kwamba Wizara ya Fedha isimamie fedha zinazoletwa katika Majimbo yetu kwa uhakika, tutakuwa hatufanikiwi. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Madiwani kuititia Kamati ya Fedha kuititia Baraza la Madiwani tuhakikishe kwamba fedha zetu zinatumika kama ilivyokusudiwa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kujua baada ya kukadiria, labda wananchi wakashindwa au mwingizaji akashindwa kulipa kodi ile, *TRA* huwa wanauza?.

MWENYEKITI: Kodi gani?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Kodi ya bidhaa kama gari ama kontena ambalo ina kitu kingine, baada ya kukadiria na kodi ikawa kubwa, wanashindwa kulipa na kwa mwananchi wa kawaida hawezi kumfuata Mheshimiwa Waziri au mtu mwingine, zile bidhaa huwa zinauzwa kwa mnada. Nilitaka kujua: Je, wakiuza zile bidhaa huwa wanamrudishia huyo mwingizaji thamani yake halisi alioingizia? Kama hawampi, haoni kama ni kuwaibia wananchi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba uuza ji wa biadhaa unatokana na mwingizaji kushindwa kukomboa na baada ya kuuzwa, kuna mawasiliano baina ya *TRA* na mwingiza ili kutafuta *balance* ya mambo.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, *balance* kama iko chini ndiyo imekula kwako.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunatambua uwepo wa noti bandia kwenye mzunguko wa fedha nchini na uwepo huo wa noti bandia unathiri uchumi wa Taifa na wa mtu mmoja mmoja. Lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha hajaeleza mkakati wa namna gani wa *ku-control* uwepo wa noti hizi bandia. Napenda kujua mkakati wa *ku-control* uwepo wa noti bandia nchini.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tumejibu. Juzi kwenye swal la asubuhi na hata leo wakati Waziri ana *wind-up* amelizingumzia suala hilo. Noti bandia zinasababishwa na utaalami wa kufanya *photocopying* na kila utaalami wa *electronics* unapanda ndiyo tunapata haya matatizo na ni suala ambalo ni taabu sana kulizua. Jambo ambalo linafanyika ni kuhakikisha kwamba noti ambazo tunazitoa zinakuwa na alama za usalama ambazo nafikiri ni jambo muhimu kuliko yote ni elimu kwa watumiaji. Lakini pia vyombo vyetu vya usalama kuhakikisha kwamba vinafuatia kuwepo kwa noti bandia kwa sababu ni suala la kijinai.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hapa mimi nataka kuulizia, kuna hivi vyuo viwili; Taasisi ya Uhasibu Arusha pamoja na Taasisi ya Uhasibu Tanzania. Nilikuwa nikifuatilia mitaala ya vyuo hivi, mingi inafanana na kwa kuwa sasa bahati nzuri vyuo hivi vyote viko chini ya Wizara ya Fedha: Je, Wizara haioni umuhimu sasa wa kuunganisha vyuo hivi ili kiwe chuo kimoja kikubwa chenye nguvu?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mitaala ya vyuo vya uhasibu kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba inafanana, kwa hiyo, viunganishwe na kuwe na chuo kimoja kikubwa. Nafikiri kwa sasa hivi ni suala la ushauri na baadaye tuenze kuangalia. Lakini itakuwa siyo rahisi sana kwa sababu kila sehemu chuo kilipo kama vile Mtwara, sidhani kama wataweza kukubali kwamba chuo kitoke na kiende sehemu fulani. Lakini ushauri tutauzingatia halafu tuangalie uwezekano.

MWENYEKITI: Kwanza huyu Mheshimiwa Opulukwa ni bwana harusi *next month*. Kwa hiyo, Wabunge wote mjue kwamba anafunga ndoa mwezi wa Kumi, na mchangie. Mheshimiwa Mbilinyi. (*Makofii*)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nataka kujua kuhusu sheria na utaratibu wa *TRA* sehemu za mipakani kwa sababu kule Mbeya wafanyabiashara wa usafirishaji abiria kati ya Tunduma na Mbeya, yaani wenye mabasi wamekuwa na tatizo sana na watu wa *TRA* ambapo watu wa *TRA* wanakamata vipodozi haramu. Ni kitu kizuri kutoptana na taratibu za nchi, lakini tatizo linakuja pale ambapo abiria akikamatwa na vipodozi haramu wanachukua *bus*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bus* linakamatwa kiasi kwamba inhabidi watoe faini mpaka shilingi milioni sita hata kama pale abiria mwana mama amekamatwa na *tube* mbili tu za *cream* na wafanyakazi wa *bus* hawawezi kuwasachi wale abiria wanapoingia kwenye ma-*bus*. Sasa sijui Serikali inasemaje kuhusu hilo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tukumbuke kwamba Serikali ina wajibu ya kuwalinda wananchi wake na *tube* mbili anazozizingumzia Mheshimiwa Mbunge zinaweza kuleta madhara makubwa kwa wananchi wa Tanzania. Kinachofanyika *TRA* ni kuhakikisha kwamba inatoza *penalty* kubwa inavyowezekana ilimradi iwe kisheria.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge muda umekwisha, tutapitisha kwa *guillotine*.

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i> Sh. 775,122,000/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>Sh. 26,741,425,500/=
Kif. 1004 - <i>Legal Services</i>Sh. 642,519,300/=
Kif. 1005 - <i>Inform. Education and Communication</i>Sh. 1,160,386,900/=
Kif. 1006 - <i>Internal Audit Unit</i> Sh. 295,578,000/=

Kif. 1007 - *MCC Tanzania*Sh. 553,000,000/=
 Kif. 1008 - *Procurement*
 Mgt UnitSh. 553,993,800/=
 Kif. 1009 - *Public Procurement*
 Policy UnitSh. 798,446,800/=
 Kif. 2003 - *Treasury Registrar* Sh. 38,724,192,100/=
 Kif. 5001 - *Government Asset*
 Management Division Sh. 5,429,430,100/=
 Kif. 6001 - *Financial Mgt, Inform,*
 Systems DivisionSh. 1,777,011,800/=
 Kif. 6002 - *Tax Revenue Appeals*
 BoardSh. 1,227,080,000/=
 Kif. 6003 - *Technical Audit Unit* Sh. 659,131,200/=
 Kif. 6004 - *Tax Revenue Appeals*
 TribunalSh. 894,164,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 21 – Hazina

Kif. 2001 - *Government Budget Division* Sh. 4,743,084,000/=
 Kif. 2002 - *Policy Analysis Division*Sh. 42,541,155,000/=
 Kif. 4001 - *External Finance Division*Sh. 3,124,363,000/=
 Kif. 7001 - *Poverty Eradication and Empowerment*.....Sh. 3,929,392,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 23 – Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali

Kif.3003 - *Financial Management*Sh. 6,858,846,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 45 – Ofisi ya Ukaguzi ya Taifa

Kif.1001 - *Admin. and General*.....Sh. 4,812,494,000/=
 Kif.1002 - *Finance and Accounts Unit*Sh. 5,854,903,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 50 – Wizara ya Fedha.

Kif. 1001 - *Admin. and General*.....Sh. 1,000,000,000/=
 Kif. 1002 - *Finance and Accounts* Sh. 390,000,000/=
 Kif. 1003 - *Policy and Planning*Sh. 4,604,824,000/=
 Kif. 1005 - *Inform. Education and ommunication*.....Sh. 0/=
 Kif. 1007 - *MCC Tanzania*..... Sh. 587,953,176,000/=
 Kif. 2003 - *Treasury Registrar*..... Sh. 350,000,000/=
 Kif. 6001 - *Financial Mgt. Inform.Systems Division*Sh. 1,745,385,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

(Bunge lilitrudia)

TAARIFA

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2011/2012 Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 yalipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii kumpungeza Waziri wa Fedha na Manaibu wake na Watendaji katika Wizara yake kwa kazi nzuri, na kama alivyosema Sungura ni mdogo, lakini akiwa mdogo mkintumia vizuri atakuwa na manufaa zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu muda umepita na inabidi turudi saa kumi kumalizia kazi ambayo imebaki kidogo, kwa hiyo naomba muwahi kwa sababu leo ndiyo siku yetu ya mwisho. Mkifika kama mlivyofika jana, watatu, wanne itakuwa balaa kabisa. Naomba saa kumi *promptly* leo muwahi kusudi tumalize haraka. Tuna kazi kubwa ya *Appropriation Bill*. Kwa hiyo, *Appropriation Bill* sio tumwachie mtu mmoja, inatakiwa sisi wote tuikubali. Kwa hiyo, nategemea mtawahi mapema.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

(*Saa 7.15 Mchana Bunge lilitishwa Mpaka Saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia*)

HOJA ZA SERIKALI

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hiki ni kitu ambacho kinafanyika baada ya sisi kuwa tumemaliza kuititia Bajeti za Wizara zote, tunaanza na Bajeti ya Waziri Mkuu mpaka Bajeti hii tuliyomaliza asubuhi. (*Makofi*)

Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 105(1) ambayo inasema hivi; "Baada ya Bunge kukamilisha kazi ya kujadili na kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara zote kwa mwaka unaohusika, Muswada wa Fedha za Matumizi utawasilishwa Bungeni na kuitishwa mfululizo katika hatua zake zote."

Ya pili yake inasema; "Kwa madhumuni ya Kanuni hii, "Muswada wa Fedha za Matumizi maana yake ni Muswada wa Sheria wenye Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali kwa mwaka wa Fedha unaofuatia."

Ya tatu yake inasema; "Muswada wa Fedha za Matumizi hautapelekwa kwenye Kamati yoyote ya Kudumu wala Kamati ya Bunge Zima, na masharti kuhusu Miswada Kusomwa Mara ya Kwanza hayatumika."

Kanuni ya 105(4) inasema; "Muswada wa Fedha za Matumizi hautatangazwa kwenye Gazeti kabla haujawasilishwa Bungeni."

Waheshimiwa Wabunge, wale wenye nakala ya Muswada mkiangalia mtaona Muswada mzima unazungumzia tu zile *votes* na jumla yake na jumla yake na jumla yake. Tunachokifanya hapa sasa ni kusema, yale yote tuliyokuwa tunasema, sasa yanajumlishwa kwa hilo fungu la mwisho. Kwa hiyo, ni *process* tu ndogo, inachukua dakika chache. Nimewaelezeni kwa maudhui.

Zamani tulikuwa tunafanya hivi, baada ya majumuisho haya yote, tungeingia kwenye *Finance Bill*. Sasa tulipoondoaa hii kusudi tuiwezeshe Serikali kuendelea kufanya shughuli zake wakati sisi tunaendelea kuzungumza hapa, kwa hiyo sasa ile hatua tulimaliza, ndiyo tunaingia kwenye hii Kanuni ya 105. (*Makofi*)

MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya shilingi 13,525,895,350,000/= kwa Matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012. Kutumia Fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, Kuruhusu Kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo (An Act to apply a sum of 13,525,895,350,000/= out of the Consolidated Fund to the serving of the year ending on the 30th day of June, 2012, to appropriate the supply granted for that year, to authorize reallocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purposes)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ullisomwa kwa Mara ya Kwanza*)

Muswada wa Sheria kuidhinisha matumizi ya Serikali ya mwaka 2011 (The Appropriation Bill, 2011)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ullisomwa kwa Mara ya Pili*)

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya shilingi 13,525,895,350,000/= kwa matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012. Kutumia Fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, Kuruhusu Kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo (An Act to apply a sum of 13,525,895,350,000/= out of the Consolidated Fund to the serving of the year ending on the 30th day of June, 2012, to appropriate the supply granted for that year, to authorize reallocation of certain appropriation and to provide for matters connected with those purposes)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ullisomwa kwa Mara ya Tatu*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa tumekamilisha safari yote tuliyokuwa tunaifanya kwa ajili ya *budget session*. Kwa hiyo, kipindi cha *budget session* tumekamilisha sasa. Mbona hamjipongezi wenyewe? (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, nishukuru Serikali kwa mawasilisho yake, viongozi mbalimbali, wafanyakazi katika Serikali yote kuweza kukamilisha mchakato mzima wa Bajeti ya mwaka 2011/2012. Sasa kama tulivyoomba, matumizi yaende kufuatana na vile tulivyoibaliana hapa, na wenyewe kama mlivyoona, Wabunge wenyewe ndiyo hawa. Msitufanyie vinginevyo, mambo mtakayopata mtayajua wenyewe. Kwa hiyo, ni vizuri mkasimamia mali za Serikali. (*Makofi*)

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, leo tumefikisha Kikao cha 56 tangu tuanze Mkutano wa Nne wa Bunge lako Tukufu tarehe 7 Juni, 2011. Mkutano huu ulikuwa mahsus kwa ajili ya kujadili Mpango na Bajeti ya Serikali pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara, Mikoa na Taasisi mbalimbali kwa mwaka 2011/2012. Tumejadili masuala mbalimbali na hasa ya kuiletea nchi yetu maendeleo kwa takriban siku 84. Huu ni muda mrefu ambao kwa

vyovyyote vile inatubidi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuhitimisha shughuli zote zilizopangwa siku hizo kwa amani na utulivu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika muda wa takribani miezi mitatu tumemkosa mwenzetu Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na Waziri wa Maji, ambaye amekuwa katika matibabu nchini India. Napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwanza kumpa pole kwa maradhi na pili kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ili apone haraka na hatimaye kurejea nyumbani kuijunga na Waheshimiwa Wabunge wenzake na wananchi wa Jimbo la Rungwe Mashariki katika ujenzi wa Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa masikitiko makubwa, napenda niwape pole Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili pamoja na Wawakilishi wa Baraza la Mapinduzi kwa msiba mkubwa wa kumpoteza mwenzetu Mheshimiwa Mussa Khamis Silima kutoka Baraza la Wawakilishi pamoja na mke wake mpendwa, Bibi Mwanaheri Twalib waliopoteza maisha katika ajali mbaya iliyotokea Nzuguni, Dodoma. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, jumla ya maswali 499 ya msingi na mengine 1,183 ya nyongeza yaliulizwa na kupata majibu kutoka Serikalini. Vilevile jumla ya Maswali 62 ya msingi na 34 ya nyongeza ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu kila siku ya Alhamisi yaliulizwa na kupata majibu. Ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge vizuri. Maswali yalikuwa mengi, lakini mmeabajibu yote pamoja na yale ya nyongeza kwa umahiri mkubwa. Nawapongea sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunahitimisha mkutano huu tukiwa tumepata fursa ya kujadili Miswada, Maazimio na Kauli mbalimbali za Mawaziri. Miswada iliyowasilishwa na Serikali ni ifuatayo:-

- (i) Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2011 (*The Finance Bill, 2011*);
- (ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Biashara wa Mwaka 2011 (*The Business Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2011*); na
- (iii) Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2011 (*Appropriation Bill, 2011*). (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge pia walikubali Azimio la Bunge la Kuridhia Kuongeza Muda wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya *Umma* (*The Consolidated Holding Corporation*).

- Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu, Mawaziri walitoa Kauli za Serikali zifuatizo:-
- (i) Kauli ya Waziri wa Viwanda na Biashara kuhusu kuendelea kutumika kwa Mizani ya Rula (*Steel Yard*);
 - (ii) Kauli ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kuhusu Hali ya Chakula nchini;
 - (iii) Kauli ya Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Kampuni ya Uingereza ya *BAE Systems*; na
 - (iv) Kauli ya Waziri wa Nishati na Madini kuhusu Hali ya Umeme Nchini kati ya tarehe 14 – 18 Agosti 2011. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wa Maendeleo wa miaka 15 wa Taifa, Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba kabla ya kuanza kwa mjadala wa Bajeti, mlipata fursa ya kupokea, kujadili na kujitisha mpango wa kwanza wa maendeleo wa Taifa wa miaka mitano, kuanzia mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016.

Mpango huu unakusudia kuharakisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa kipindi kilichobaki cha uhai wake wa miaka 15 hadi 2025. Kwa kutumia mpango huu, katika kila kipindi cha miaka mitano, nchi yetu inatakiwa kujipima kwa vitendo kujua tumefikia wapi katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ambayo inaelekeza Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo 2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mpango huo, tumeamua kutekeleza vipaumbele vichache kulingana na rasilimali kidogo tulizonazo. Kwa mfano, mpango wa miaka mitano unatoa kipaumbele cha juu kwa Sekta za Kilimo na Miundombinu ya msingi. Maeneo mengine ni ukuzaji wa rasilimali watu na matumizi ya sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano. Nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kushiriki kikamilifu katika mjadala wa mpango huo. Michango yenu ilikuwa mizuri na itaisadia sana Serikali katika utekelezaji wa mpango huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza kuwa katika utekelezaji wa mpango huu na mipango mingine itakayofuata hadi 2025, Serikali itaelekeza matumizi ya rasilimali zake katika vipaumbele vichache ili kupata manufaa makubwa yaliyokusudiwa. Hivyo, awamu tatu za utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa miaka 15 zitajikita katika ajenda kuu tatu zifuatazo:-

Awamu ya kwanza, kufungua fursa mbalimbali zitakazochochea ukuaji wa uchumi kwa kasi kubwa hasa sekta ya kilimo, nishati na miundombinu (2011-2015). Awamu ya pili, ujenzi wa misingi ya maendeleo ya viwanda (2016-2020); na Awamu ya tatu, kuimarisha ubunifu na ushindani wa biashara Kimataifa (2021-2025). (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuwaelimisha wananchi katika Majimbo yao kuhusu mpango wetu wa miaka mitano tunaoanza kuutekeleza mwaka huu. Aidha, nawaomba wananchi na wadau wote wa maendeleo washiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mpango huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu umuhimu wa uwekezaji nchini, ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote duniani kwa sasa unasukumwa na mambo makubwa mawili ambayo ni ushiriki na uwekezaji wa sekta binafsi na ukuaji na maendeleo ya sayansi na teknolojia, ikiwemo teknolojia ya habari na mawasiliano. Tupende tusipende na ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wetu, lazima na sisi kama Taifa tujikite kwenye utekelezaji wa masuala hayo. Lazima tutumie kila mbinu ya kuvutia wawekezaji kwenye sekta zote na hasa kwenye sekta ya kilimo ambayo tuna fursa kubwa kwa maana ya ardhii kubwa yenye rutuba na vyanzo vingi vya maji. Nchi zote duniani zilizofungua milango ya biashara na kuvutia uwekezaji wenye tija zimepata mafanikio na maendeleo makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua nafasi ya sekta binafsi kuwa injini ya kukuza uchumi (*engine of economic growth*) na kuzalisha ajira na ndiyo maana Serikali imetayarisha sera na kutunga sheria mbalimbali za kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuendeleza sekta binafsi. Tangu mwaka 1986 Serikali imetekeleza mageuzi makubwa ya sera za uchumi jumla (*Macroeconomic Policies*) na Kitaasisi (*Structural Reforms*) ambazo zimetambua nafasi ya sekta binafsi katika kukuza uchumi. Mwaka 1997 ilitungwa Sheria ya Uwekezaji (*Act No.7, The Tanzania Investment Act, 1997*) na Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Act No. 19, The Public Private Partnership Act, 2010*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, upo uhusiano mkubwa kati ya uwekezaji na ukuaji halisi wa Pato la Taifa. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2000 hadi sasa tumeshuhudia ukuaji wa uchumi wetu ukiendelea kuimarika na kukua kwa wastani wa asilimia 6.8 kwa mwaka. Naomba nitumie fursa hii kuwakumbusha kwa kifupi Watanzania wote takwimu za ukuaji halisi wa Pato la Taifa kuanzia mwaka 2000, ambapo ukuaji wa uchumi ulikuwa asilimia 4.9; mwaka 2001 asilimia 6.0; mwaka 2002 asilimia 7.2; mwaka 2003 asilimia 6.9; mwaka 2004, asilimia 7.8; mwaka 2005 asilimia 7.4; mwaka 2006 asilimia 6.7; mwaka 2007 asilimia 7.1; mwaka 2008, asilimia 7.4; mwaka 2009 asilimia 6.0; na mwaka 2010 asilimia 7.0. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaonyesha kuwa ukuaji huo mzuri wa Pato la Taifa umechangiwa na ukuaji wa sekta ya mawasiliano ambayo ilikua kwa wastani wa asilimia 16.4, katika kipindi hicho cha miaka kumi, sekta nyingine zilizochangia ukuaji huo ni sekta ya Madini ambayo ilikua kwa wastani wa asilimia 11.5, sekta ya Ujenzi asilimia 9.5, sekta ya Fedha asilimia 9.4, sekta ya Viwanda asilimia 8.0, sekta ya Afya asilimia 7.6, sekta ya Majengo asilimia 6.6, sekta ya Utalii na Biashara asilimia 6.3 na sekta ya Kilimo asilimia 4.3. Ni dhahiri kuwa ukuaji huo wa wastani katika kila Sekta umetokana kwa kiwango kikubwa na uwekezaji wa ndani na nje wa sekta binafsi na kwa kiasi fulani sekta ya umma. Kwa leo ninaomba nzungumzie kidogo juu ya mchango na umuhimu wa sekta binafsi. Mheshimiwa Spika, kuhusu takwimu za thamani ya Mitaji ya Uwekezaji wa moja kwa moja kutoka Nje (*Foreign Direct Investments - FDIs*) zinaonesha kuwa jumla ya mitaji ilioingizwa nchini katika kipindi cha miaka kumi ni sawa na dola za Kimarekani bilioni 5.6 ambayo ni sawa na shilingi triliioni 8.8 kwa kutumia kiwango cha sasa cha ubadilishaji shilingi kwa dola za Kimarekani. (*Makofii*)

Thamani ya mitaji hiyo iliongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni 463.4 sawa na shilingi bilioni 385 mwaka 2000 hadi dola za Kimarekani milioni 744 mwaka 2008 sawa na shilingi bilioni 881 na ilishuka kidogo hadi dola za Kimarekani milioni 573 sawa na shilingi bilioni 821 mwaka 2010 kutokana na m dororo wa kiuchumi katika kipindi hicho. Hata hivyo, pamoja na m dororo huo, Tanzania iliendelea kuongoza kwa kuvutia wawekezaji katika kipindi hicho katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Sekta zilizoongoza katika kuvutia mitaji mikubwa ya uwekezaji wa moja kwa moja (*FDIs*) ni uzalishaji viwandani; mawasiliano; madini; utalii; majengo ya biashara na ujenzi na usafirishaji. Uwekezaji katika sekta hizi siyo tu kwamba umevitia mitaji, bali umeongeza ajira, mauzo nje, umeingiza teknolojia mpya, na kubaini masoko mapya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia takwimu hizo, siyo sahihi hata kidogo kupuza mchango wa uwekezaji katika uchumi wetu. Ndiyo sababu tumekuwa tukisifiwa na wenzetu wanaotuona huko nje kwamba ukuaji huu wa uchumi unaiwezesha nchi yetu kufikia uchumi wa kati haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tupo miongoni mwa nchi kumi duniani ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa, na miongoni mwa nchi 17 za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo zinaongoza katika kukua kwa uchumi, kupunguza umaskini na kuzingatia utawala bora. Vilevile, tupo miongoni mwa nchi nne duniani, mbili kati ya hizo kutoka Afrika zinazoshiriki Mpango wa Ubia wa Kukuza Uchumi (*Partnership for Growth*). Mifano yote hii ni ushahidi tosha kwamba Tanzania inafanya vizuri katika kujenga misingi imara ya uchumi. Lakini ninyi wote ni mashahidi, Serikali za Awamu ya Tatu na Nne chini ya uongozi madhubuti wa Chama cha Mapinduzi imebidi zichukue hatua thabiti za kufanya mageuzi makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ili kufikia hatua hii. Mageuzi haya ili yakamilike na kufanikiwa ni lazima yawepo mageuzi makubwa ya kifikra, kimatendo na mahusiano na jamii na dunia kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya, sina budi kuwatahadharisha Watanzania wote kwamba safari ya kukamilisha kazi ya kuwaletaa Watanzania maendeleo kamili bado ni ndefu na lazima tuongeze zaidi juhudii hizi na kamwe tusibweteke. Ni dhahiri kwamba hadi hapa tulipofikia Tumethubutu, Tumeweza, kinachohitajika sasa ni kusonga mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunachohitaji ni utashi wa kisiasa na dhamira ya kweli. Tukiamua kuundoa umaskini tutaweza, kwani kama alivyosema Mtaalamu Justin Yifu Lins, Mchumi Mkuu wa Benki ya Dunia; "*Poverty is not a genetic condition.*" Umaskini siyo hali inayotokana na tatizo la kurithishwa. "*It is a set of factors producing an outcome; alter the factors and the outcome changes.*" Ni hali inayotokana na mambo kadhaa wa kadha ambayo husababisha matokeo fulani hasi ambayo ukiyabadilisha tu, matokeo hayo hubadilika na kuwa chanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mageuzi yoyote huja na hofu na hivyo kusababisha wasiwasi miongoni mwa jamii. Lakini tukitaka maendeleo ni lazima yawepo mageuzi ya dhati. Hivyo, mageuzi sharti yaendane na kujitoa mhanga na ni lazima mageuzi yoyote katika nchi yalenge kuboresha maisha ya watu maskini walio wengi na siyo vinginevyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mpango wa maendeleo wa Taifa umelenga kuifikisha Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Hili ni lengo zuri, lakini wachumi wanatuambia kuwa ili Tanzania ifikie lengo hilo ni lazima uchumi wake ukue kwa wastani wa asilimia 8 -10 kwa miaka 30 hadi 40. Uzoefu wa nchi nyungine kama China unaonesha kuwa baada ya kutimiza kiashiria hicho, ndipo misingi ya kuelekea kwenye Taifa lenye uchumi mkubwa inapoweza kuanza kujidhihirisha. Hadi sasa Tanzania imeweza kusimamia vizuri uchumi wake ambao umeendelea kukua kwa wastani wa asilimia saba kwa miaka kumi iliyopita. Rai yangu kwa Watanzania wote ni kwamba, hapa tulipofika tusirudi nyuma, tusonge mbele ili ndani ya miaka 15 chini ya Mpango huu wa Maendeleo ya Taifa tufike tunapolenga yaani kuwa nchi ya uchumi wa kati. Kutokana na uzoefu tuliuopata na hatua mbalimbali tulizopitia, sioni kwa nini Tanzania isiweze kufika hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, historia ya nchi zote duniani inatuonyesha kuwa Mataifa yote yalianza kama nchi maskini zilizotegemea zaidi nguvu kazi ya wananchi wake katika kilimo na sehemu nyungine kama uvuvi kwa ajili ya mahitaji ya wananchi wake. Kutegemeana na aina ya rasilimali zilizomo katika nchi, kila nchi iliamua ni rasilimali gani waliyonayo ambayo inawapa fursa zaidi katika kuwaletea maendeleo ya haraka wananchi wake. Rasilimali hiyo ndiyo waliyoutumia kubadili hali ya maisha ya wananchi wake na nchi kwa ujumla. Kwa upande wa Tanzania, fursa tulizonazo na tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa hili, ni pamoja na ardhi nzuri, madini, misitu, vivutio vingi vya utalii, maji ya bahari, maziwa na mito, bandari inayotumiwa na nchi nyngi zinazozunguka nchi yetu na kadhalika. Vyote hivi vikisimamiwa vizuri na kwa maslahi ya wananchi maskini, umaskini utaondoka ndani ya kipindi kilichopangwa, tena bila wasiwasi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika mukutano huu tunaohitimisha leo, moja ya hoja zilizojadiliwa kwa hisia kali na tofauti ni suala zima la uwekezaji hususan umiliki wa ardhi. Miongoni mwetu, kuna wanaotafsiri uwekezaji mkubwa kwenye ardhi kuwa ni unyang'anyi, uporaji na wizi wa ardhi ya Watanzania. Hali hii imezia dhana potofu ambayo inajijenga mionganoni mwa baadhi ya Watanzania kwamba unapotaja neno mwekezaji kwa tafsiri ya haraka haraka ni mtu mporaji, mwizi na laghai. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Watanzania wenzangu tuwe waangalifu na kauli za namna hii, kwa kuwa tutawatisha wawekezaji wanaotaka kuja na kuwafukuza kabisa wawekezaji ambao tayari wapo hapa nchini. Jambo ambalo ni hatari sana kwa uchumi na maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Bunge ni taasisi ambayo ina heshima ya kipekee duniani kote. Bunge ndiyo taasisi inayotunga Sheria. Kwa maana hiyo, kile kinachosemwa ndani ya Bunge na Mbunge ye yote yule kinaheshimika sana. Wawekezaji na wananchi wote wanafuatilia kwa karibu na kwa umakini mkubwa majadiliano yote ya Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge. Aidha, kutokana na ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, majadiliano yote yanayotokea hapa Bungeni yanaonekana au kusikika duniani kote. Watanzania wengi kote mijini na vijijini wanatuona na kutusikia. Wawekezaji kokote walipo wanatusikia na kutuona. Hivyo, maneno tunayosema kuhusu wawekezaji siyo tu kwamba yanaweza kuwaogopesha na kuwafukuza, bali yanachochea chuki mionganoni mwa wananchi dhidi yao hao wawekezaji.

Uwekezaji ni ushindani, uwekezaji ni biashara. Hakuna mwekezaji anayependa kuwekeza mahali ambapo atapata hasara, hususan wakati huu ambapo kumekuwepo na m dororo wa uchumi. Lakini wakati tunayaongea hayo ni dhahiri pia kwamba tunapingana na juhudzi za Serikali na hasa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuwavyutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza nchini mwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie tu mfano mdogo wa maneno ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliyoyatumia wakati akihutubia mukutano wa wawekezaji uliofanyika Milan, Italy tarehe 18 Julai, 2007. Katika mukutano huo aliwema na naomba ninukuu kwa Kiingereza, lugha aliyoutumia kwenye mukutano huo: "*Tanzania, is no doubt, a great place to invest in Africa today. By saying this I am not trying to brag for nothing. I am simply saying the obvious. For over the past decade we have put in place the most conducive investment environment you can think of. We have flung our doors wide open for anyone interested to bring his money and do business*

with us in Tanzania. There are no restrictions or preconditions attached. You just bring your money, you do business. Period. Bureaucratic red-tape has almost been severed." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Rais ni kwamba Tanzania haina shaka, ni nchi inayofaa kuwekeza katika Bara la Afrika. Hali ya uwekezaji ni nzuri na milango iko wazi bila ukiritimba. Maneno haya mazito ya Mheshimiwa Rais ambayo amekuwa akiyatumia mara kwa mara kila anapopata nafasi ya kukutana na wawekezaji ndani na nje ya nchi yana dhamira ya dhati ya kuruhusu wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza nchini mwetu bila bughudha yoyote. Ninawaomba sana Watanzania tuelewe hilo na tusibeze uwekezaji ndani ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili, Mheshimiwa Freeman Mboge, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Waziri Kivuli wa Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI wakati akichangia majadiliano ya Hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii naye alitukumbusha jambo hili kwa maneno yafuatayo; namnukuu; "Mheshimiwa Naibu Spika, niingie katika biashara ya utalii, na hapa wa uwindaji. Nilim-quote Baba wa Taifa kwa sababu mwaka 1961 alijua suala la biashara ya utalii hatuwezi kulifanya wenyewe bila kuwa na wageni, huo ndyo ukweli. Kuwafukuza wageni nimeshasema siyo kipimo cha uzalendo hasa linapokuja hili suala la biashara ya uwekezaji wa utalii. Kwa bahati mbaya sana na ni kweli Mheshimiwa Waziri katika siku za usoni ni vema Wizara yako ikaandaa semina kutufahamisha na kufundisha Waheshimiwa Wabunge ni nini maana ya biashara ya utalii wa uwindaji? Watu wengi wana tabia ya kufikiri unapewa kitalu kama hiki kina wanyama unakwenda kuwinda swala na tembo, biashara imeishia hapo. Uwekezaji wa utalii ni *highly professional*. Ni utalii unaohitaji utalaam wa hali ya juu. Skills za hali ya juu na ni *capital intensive*." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Mboge ni kwamba tunawahitaji wawekezaji na hivyo tusiwfukeze kwa maneno na matendo yetu. Kutokana na maneno hayo ya Mheshimiwa Mboge, napenda kusitiza kuwa tunahitaji wawekezaji katika sekta zote. Ninaelewa ziko nchi ambazo kutokana na ushindani katika kuvutia wawekezaji wanatoa hadhi ya VIP kwa baadhi ya wawekezaji. Ninaomba tuwalinde wawekezaji wa sekta zote na tusichague baadhi ya sekta tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi ambalo Bunge hili na Watanzania wote kwa jumla tunapaswa kulihimiza ni Serikali kuwa makini inapoingia mikataba na wawekezaji ili uwekezaji huo uweze kuwa wa manufaa kwa pande zote mbili kwa mwekezaji na Taifa. Watumishi wa umma wanaoingia mikataba mibovu nao sharti wachukuliwe hatua kali kwa mujibu wa sheria zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo; taarifa mbalimbali za Mashirika ya Kimataifa zinaonesha kuwa hali ya chakula duniani, na nchi jirani siyo ya kuridhisha. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula (*World Food Programme*) za mwezi Agosti, 2011 idadi ya watu wanaokabiliwa na upungufu wa chakula katika nchi zilizo kwenye pembe ya Afrika (*Horn of Africa*) hususan Somalia, Kenya, Uganda, Ethiopia na Sudan Kusini imefikia takriban watu milioni 13, hawa wote wanahitaji chakula cha msaada. Uhaba huo wa chakula unatokana na ukame pamoja na vita vya wenyewe kwa wenyewe katika baadhi ya nchi hizo. Hali hii ni hatari kwa nchi jirani kama ya kwetu. Madhara ya uhaba wa chakula yatakayotokea katika nchi hizo na hasa Kenya na Uganda ama nchi nyingine ya jirani, yataathiri sana ukuaji wa uchumi wetu, tupende tusipende. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uhaba huo wa chakula kwa majirani zetu ni changamoto kubwa kwa nchi yetu ambayo nayo inakabiliwa na upungufu wa chakula katika mikoa 15 kwenye maeneo ya jumla ya Wilaya 58. Upungufu wa chakula katika nchi jirani umesababisha ongezeko la bei ya chakula hasa mazao ya nafaka na hivyo kuchochaea kushamiri kwa biashara ya mazao ya chakula kutoka Tanzania kwenda katika nchi hizo. Kutokana na hali hiyo, naomba nitoe rai kwa wananchi kuchukua tahadhari ya kujivekea akiba ya chakula cha kutosha kabla ya kuza mavuno yao yote ya msimu uliopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumbaini vilevile kwamba hata sukari sasa imeanza kupatikana kwa bei kubwa na kwa uhaba mkubwa, lakini sukari hiyo nchi jirani hasa Uganda na

Kenya inanunua zaidi ya mara tatu au nne kwa bei ambayo sasa inapatikana hapa nchini na hiyo inaonesha dhahiri tatizo liliyvo kubwa katika nchi hizo za jirani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua za kukabiliana na tatizo la upungufu wa chakula nchini kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Serikali imeimarisha akiba ya chakula kwenye maghala ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (*NFRA*) ambapo hadi tarehe 22 Agosti, 2011 kulikuwa na tani 143,609.8 za mahindi;

(ii) Mwezi Julai, 2011 Serikali imetoa tani 29,777 za chakula kwenye Halmashauri 26 zenye upungufu mkubwa wa chakula;

(iii) Serikali itaiwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) kifedha ili iweze kununua chakula cha kutosha kutoka kwa wakulima wa mikoa yenye ziada ya chakula ambayo ni Rukwa, Iringa, Mbeya na Ruvuma;

(iv) Tunaendelea na mchakato wa kuhamisha akiba ya chakula kutoka katika maghala ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula ya Sumbawanga, Makambako na Songea na kuyasafirisha kwenda Mikoa yenye uhaba mkubwa wa chakula ya Shinyanga, Singida, Arusha na Dodoma;

(v) Ununuzi wa mahindi kwenye mikoa yenye ziada ya Nyanda za Juu Kusini unaendelea, na kuanzia tarehe 8 Mei, 2011 hadi tarehe 22 Agosti, 2011 ni tani 12,610.4 ambazo zimenunuliwa; na

(vi) Serikali itaendelea kusitisha uuzaji wa mazao ya nafaka nje ya nchi hadi mwezi Desemba, 2011 ili kukabiliana na upungufu wa chakula hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 31 Julai, 2011 wafanyabiashara wakubwa wa nafaka nchini walikuwa na jumla ya tani 124,524 za nafaka, zikiwemo tani 113,000 za ngano, tani 11,000 za mahindi na tani 520 za mchele. Katika kipindi kama hicho mwaka 2010 akiba ya ngano ilikuwa tani 137,909, mahindi tani 11,520 na mchele tani 3,072 katika maghala ya wafanyabiashara hao ambayo ni kubwa ikillinganishwa na ya sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wananchi kutumia aina mbalimbali za vyakula tulivyo navyo na tuepuke kuchagua vyakula. Kwa wale wenye mifugo wanashauriwa wauze mifugo yao ili wanunue chakula. Vilevile nawahimiza wafanyabiashara wenye uwezo wa kununua chakula kutoka maeneo yenye chakula kingi kufanya hivyo, na wawauzie wananchi bila kuwalangua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kipaumbele kwenye kilimo; kutokana na mabadiliko ya Hali ya Hewa ambayo yanatishia uzalishaji na upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini, ni muhimu kutoa kipaumbele katika sekta ya kilimo. Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano umetoa kipaumbele cha kwanza katika sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi na ufugaji nyuki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwaomba Watanzania wenzangu kwanza tupende kilimo kwani ndicho kitakachotusa idia kukuza uchumi na kuondokana na umaskini kwa haraka. Vijana watapata ajira endelevu kwenye kilimo na viwanda vyetu vitapata malighafi ya kutosha. Natoa wito kwa wakulima kuongeza tija ya uzalishaji katika maeneo waliyo nayo ya kilimo. Kipaumbele kitolewe katika kilimo cha umwagiliaji, kutumia mbegu bora, pembejeo na zana bora za kilimo. Nitumie nafasi hii kuziagiza Halmashauri zote nchini kuweka msukumo wa kipekee kwenye kilimo na kutumia kikamilifu skimu za umwagiliaji katika maeneo wanayoyasimamia ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika hapa Bungeni, Serikali ilipata michango mingi mizuri ambayo tunaahidi kuwa tutaifanya kazi. Kwa kifupi naomba kuelezea maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya mbolea nchini ni takribani tani 400,000. Kati ya hizo, ruzuku ya Serikali ni tani 180,000 sawa na asilimia 45. Hadi tarehe 31 Julai, 2011 upatikanaji wa mbolea ulikuwa tani 153,479.9 sawa na asilimia 38.4 ya mahitaji ya mbolea. Hata hivyo kiwango hiki cha mbolea kilichopo kitaongezeka hadi tani 357,000 sawa na asilimia 89 ya mahitaji baada ya kuingizwa nchini kiasi cha tani 206,000 kati ya sasa na mwisho wa mwezi Septemba, 2011. Mbolea hiyo imeagizwa na makampuni ya *Export Trading, YARA* na *Premium Agrochem*. Vilevile Kiwanda cha Minjingu baada ya kupata mashine mpya kinawenza kuzalisha kiasi cha tani 250,000 kwa mwaka na hivi sasa kuna mbolea zaidi ya tani 20,000 ambazo zinasubiri kusambazwa. Kwa maana hiyo, hatutarajii kuwa na upungufu wa mbolea katika msimu wa 2011/2012 kama ambavyo imekuwa katika miaka iliyopita. Serikali inaendelea kuyahimiza makampuni kuchukua asilimia 80 ya mbolea hiyo ambayo kwa sasa ipo Dar es Salaam, na kuipeleka Mikoani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya zao la pamba; michango ya Waheshimiwa Wabunge hasa wale wanaotoka mikoa inayozalisha pamba walielezea kwa uchungu tatizo la kushuka kwa bei ya zao la pamba katika soko la dunia, jambo ambalo limesababisha bei za hapa nchini kushuka na kuwa chini ya shilingi 1,100/= kwa kilo. Kwa sasa bei ya pamba katika soko la dunia imeanza kupanda hata bei katika soko la ndani imeanza kupanda pia. Hivi sasa bei ya ushindani kwa kilo moja ya pamba ni kati ya shilingi 900/= na 1,100=/. Aidha, wanunuzi wote walioomba leseni ya kununua pamba wamepewa. Kila mnunuzi anaruhusiwa kununua pamba eneo lolote aliloomba. Tunawasihi wakulima wa pamba wauze pamba yao sasa wakati bei inaendelea kuwa nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya sekta ya mifugo, uvuvi na nyuki, kwa muda mrefu, Serikali imekuwa ikitoa msukumo kwa sekta za mifugo, uvuvi na nyuki, lakini kasi ya ongezeko la tija katika sekta hizo bado hairidhishi. Napenda kutumia fursa hii kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa katika Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano Serikali imedhamiria kutoa msukumo wa kipekee katika sekta hizo. Kama tulivyofanya katika sekta ya kilimo, ambapo tunatekeleza Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*).

Sasa wakati umefika wa kubuni mipango maalum ya kuendeleza sekta za mifugo, uvuvi na ufgaji nyuki kama ulivyo wa *ASDP*. Lengo ni kuwezesha sekta hizi kukua kwa kasi na kuchangia kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa haraka. Hili ni kwa sababu wananchi wetu wengi wanategemea sekta hizi katika maisha yao ya kila siku. Wizara husika zitafanya kazi na Tume ya Mipango kuandaa Mipango mahsusini chini ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa itakayotoa msukumo mkubwa katika maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imejizatiti kutekeleza Azma ya Kilimo Kwanza ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo kuititia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme - ASDP*) na Programu Kabambe ya Uendelezaji na Modenaizesheni ya Ushirika. Lengo la Taifa katika mipango hii ni:

(i) Kujitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada kwa kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula;

(ii) Kupanua kilimo cha umwagiliaji na kuweka msukumo maalum katika matumizi ya teknolojia mpya za umwagiliaji pamoja na kutumia nishati za juu na upepo katika kusukuma maji shambani, kutumia maji ya ardhini, mabwawa, mito na maziwa kwa kumwagilia kwa matone ili kufikia lengo la hekta milioni moja chini ya Mpango wa Taifa wa Umwagiliaji ifikapo mwaka 2015;

(iii) Kupanua uzalishaji na ubora wa mazao ya bustani (mbogamboga, matunda na maua) na kujenga uwezo wa wakulima na vyama vyao vya ushirika kutayarisha, kufungasha na kuuza bidhaa na mazao yao nje ya nchi;

(iv) Kuongeza uzalishaji wa mbegu bora na kuhimiza matumizi ya kanuni za kilimo bora ili kuongeza tija katika kilimo;

(v) Kupanua uzalishaji wa mazao makuu ya biashara ambayo ni pamoja na pamba, kahawa, chai, korosho, tumbaku, pareto na zabibu. Kuongeza pia uzalishaji wa mbegu za mafuta na kuhimiza usindikaji; na

(vi) Kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi kwa utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Kilimo katika Kanda ya Kusini ya Tanzania (*SAGCOT*) na kuhimiza ushirikishwaji na uwekezaji wa sekta binafsi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuleta Mapinduzi ya Kilimo nchini. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote tushirikiane na Serikali kutoa msukumo na kipaumbele kwenye kilimo. Mimi naamini kilimo ndicho kitakachotukomboa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kulipa kodi, katika majadiliano yaliyofanyika katika kipindi chote cha Bunge hili la Bajeti, moja ya mambo ambayo yamechukua uzito mkubwa ni mahitaji makubwa ya fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli za Serikali ikilinganishwa na kiasi kidogo cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Wizara zote. Wote tulishuhudia mjadala wenye hisia kali wa kuitaka Serikali kuongeza fedha katika maeneo muhimu kiuchumi. Ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa mapato amba o umesababisha Wizara nydingi kupewa kiwango kidogo cha fedha za Bajeti, lazima Serikali iangalie upya vyanezo vyake vya mapato.

Mheshimiwa Spika, moja ya vyanezo vikubwa vya mapato kwenye nchi mbalimbali ni utozaji na ukusanyaji wa kodi. Yapo maeneo yenye fursa kubwa ambayo yaktumika vizuri yanaweza kuongeza wigo wa mapato. Ili ukusanyaji wa Mapato uongezeko ni lazima:-

(i) Kuangalia upya mfumo wa ukusanyaji kodi kutoka katika vyanezo mbalimbali, ikiwemo Sekta za maliasili zetu kama vile madini, mazao ya misitu, uvuvi na kudhibiti misamaha ya kodi;

(ii) Kuendelea kutekeleza mkakati wa kurasimisha rasilimali na biashara zisizo rasmi;

(iii) Kuboresha mazingira ya uwekezaji na ukuaji wa sekta binafsi;

(iv) Kuboresha mfumo wa kodi unaotumika katika kutoza sekta isyo rasmi. Hii ni pamoja na kusimamia usajili wao;

(v) Kuimarisha usimamizi wa ridhaa ya kulipa Kodi kwa kuboresha huduma ili kuzuia kuwepo kwa dalili za uvujaji mapato; na

(v) Kuchukua hatua kali za Kisheria kwa wale wote watakaobainika kukwepa kodi na wale wafanyakazi wa umma wanaowasaidia kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, upo msemo wa wenzetu wa Ulaya na Marekani usemao: "*Nothing is certain but death and taxes.*" Ni kweli msemo huu hauna ladha kuutumia, lakini unaonesha umuhimu wa kulipa kodi. Kwa tafsiri nyepesi unaonesha ugumu wa kukwepa kulipa kodi kama ilivyo vigumu kukwepa kifo. Wapo waandishi wa zamani amba walijaribu kutafsiri msemo huu uwe mwepesi kidogo, lakini ukweli ukabaki na umuhimu wake. (*Makof*)

Sheria ya Kodi inatamka bayana majukumu ya mamlaka ya kukusanya kodi nchini. Kwa maana hiyo, ni lazima kila mlipa kodi atimize wajibu wake. Kwa upande wake, mlipa kodi ana haki ya kutendewa haki sawa bila upendeleo kwa kuzingatia Sheria za Kodi na kupata huduma bora kutoka kwa chombo chetu cha ukusanyaji kodi ambacho hapa kwetu ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza baadhi ya walipakodi wakubwa kwa Serikali na amba o wamefanya vizuri kati ya kipindi cha mwaka 2005 na 2011. Kwa kipindi hicho, makampuni yaliyongoza kwa kulipa kodi ni pamoja na:-

(i) *Tanzania Breweries Ltd.* (shilingi bilioni 165.4);

- (ii) *National Microfinance Bank* (shilingi bilioni 108.6);
- (iii) *Tanzania Cigarette Company* (shilingi bilioni 92.1);
- (iv) *National Bank of Commerce* (shilingi bilioni 89.9);
- (v) *CRDB Bank Ltd.* (shilingi bilioni 79.2);
- (vi) *Tanzania Ports Authority* (shilingi bilioni 76.8);
- (vii) *Tanzania Portland Cement* (shilingi bilioni 73.4);
- (viii) *Airtel (T) Ltd.* (shilingi bilioni 63.6);
- (ix) *Tanga Cement Company Ltd.* (shilingi bilioni 43.6);
- (x) *Standard Chartered Bank Ltd.* (shilingi bilioni 40.0);
- (xi) *Citibank (T) Ltd.* (shilingi bilioni 35.7);
- (xii) *Resolute (T) Ltd.* (shilingi bilioni 32.1);
- (xiii) *Tanzania International Container Terminal Services* (shilingi bilioni 25.9);
- (xiv) *Tanzania Distillers Ltd.* (shilingi bilioni 13.4); na
- (xv) *Group Five International (PTY) Ltd.* (shilingi bilioni 9.5).

Napenda kutoa rai kwa makampuni yote nchini kuiga mfano huu mzuri. Wito wangu kwa makampuni, wafanyabiashara wakubwa kwa wadogo na wananchi wote ni kuongeza juhudini katika kufanya biashara zao ili zizalisho kwa wingi na kupata faida kubwa zaidi. Faida kubwa itachangia katika kuongeza mapato ya Serikali kwa njia ya kodi na hivyo kusaidia kukuza uchumi, kuongeza Pato la Taifa na la mwananchi mmoja mmoja na kuondoa umaskini. Niwadhihirishieni kwamba Serikali inatambua umuhimu wao kwa maendeleo ya nchi yetu na itahakikisha inaongeza juhudini zake za kuweka mazingira wezeshi kwa makampuni hayo kufanya shughuli zao vizuri ili kuwezesha kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uongezaji wa pato la Mtanzania, lengo la Dira ya Taifa ya Maendeleo ni kuiwezesha Tanzania kuwa na uchumi wa kipato cha kati (*Middle Income Country*) ifikapo mwaka 2025. Kwa mujibu wa takwimu za taasisi ya Taifa ya takwimu (*National Bureau of Statistics*) za mwaka 2010; wastani wa kipato cha Mtanzania umefikia dola za Kimarekani 545, sawa na shilingi 770,464. Hivyo katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka 15 tunayo changamoto kubwa ya kuongeza kwa kasi kubwa kipato cha Mtanzania ili kufikia lengo lilokusudiwa la kufikia dola za Kimarekani 3,000 ambazo ni sawa na shilingi milioni 4.8 kwa mwaka au shilingi 400,000/= kwa mwezi ifikapo mwaka 2025 na hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kueleza kidogo kuhusu mwenendo wa takwimu za Mikoa kuhusu kiashiria hiki cha wastani wa kipato cha mwananchi (*Regional Per-Capita Income*). Mtiririko wa nafasi za Mikoa kwa mwaka 2010 za wastani wa kipato cha mwananchi kwa mwaka ni kama ifuatavyo:-

Dar es Salaam	-	shilingi 1,740,947
Iringa	-	shilingi 979,882
Arusha	-	shilingi 945,437
Mbeya	-	shilingi 892,877
Kilimanjaro	-	shilingi 879,432
Ruvuma	-	shilingi 866,191

Mwanza	-	shilingi	829,647
Manyara	-	shilingi	772,364
Tanga	-	shilingi	763,203
Morogoro	-	shilingi	744,234
Rukwa	-	shilingi	726,658
MtWARA	-	shilingi	700,436
Lindi	-	shilingi	673,096
Mara	-	shilingi	642,528
Pwani	-	shilingi	572,466
Tabora	-	shilingi	528,832
Shinyanga	-	shilingi	510,023
Kigoma	-	shilingi	499,428
Kagera	-	shilingi	491,713
Dodoma	-	shilingi	485,211
Singida	-	shilingi	483,922

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zinaonesha kuwa theluthi moja tu ya mikoa yote ya Tanzania ndio yenye wastani wa pato la mtu ambalo ni juu ya wastani wa pato la mwananchi Kitaifa la mwaka 2010 la shilingi 770,464. Vilevile takwimu hizo zinaonesha kuwa mikoa mitano ya mwisho kwa mlinganisho wa wastani wa kipato cha mwananchi ni Shinyanga, Kigoma, Kagera, Dodoma na Singida. (*Makof*)

Hata hivyo, hali halisi inaonesha kuwa Mikoa hii ina fursa nyingi za kuongeza mapato kutokana na shughuli mbalimbali za uchumi, na fursa za kibashara zilizoko lakini takwimu za mapato ya mikoa hii haziwiani na hali halisi za maisha ya wananchi wa mikoa husika kwa fursa walizonazo. Mikoa niliyoitaja ndio inaongoza kwa eneo kubwa la ardhinizi na idadi kubwa ya mifugo nchini ambayo pia ina fursa kubwa ya kuwaongezea mapato. Pia mikoa hii ina idadi kubwa ya wananchi wanaojishughulisha na kilimo cha mazao yenye tija kubwa kama vile pamba, karanga, alizeti na ufuta. Aidha, biashara imeshamiri sana kwenye mikoa hii, hivyo hakuna sababu ya mikoa hii kuwa nyuma katika kipato cha mwananchi. Vilevile mikoa mingine yote inayo fursa tele za kuwaongezea wananchi wake kipato na kupunguza umaskini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuzungumzia suala hilo kwa sababu kiwango kidogo cha pato la mwananchi ni changamoto kubwa kwa viongozi wote kuanzia ngazi ya Wizara, Mikoa, Wilaya na kila Mkurugenzi wa Halmashauri na watendaji katika ngazi zote. Viongozi na watendaji wote tunatakiwa kujibu hoja ya namna ya kuongeza Kipato cha mwananchi kwa kuelekeza nguvu kwenye sekta za uzalishaji na huduma za kiuchumi pamoja na biashara zenye tija. Faraja ninayoipata hapa ni kwamba tunazo fursa tele kwenye sekta ya kilimo, ufugaji, uvuvi, urinaji wa asali, utalii, maliasili, madini na biashara. Fursa hizi zikitumika vizuri zinaweza kuongeza kipato cha Mtanzania na kuwezesha kupunguza umaskini kwa haraka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tatizo ninaloliona mimi ni kuwa bado hatujawa wabunifu zaidi na tunahitaji kuwashirikisha wananchi katika kuibua na kutekeleza miradi ya maendeleo. Natoa wito kwa viongozi wote kujipanga vizuri ili kuwawezesha wananchi wetu kuondokana na kipato kidogo kwa kuongeza tija na uzalishaji katika sekta zote. Kwa maoni yangu ningependa kila kiongozi, katika ngazi zote na hasa wakurugenzi wa Halmashauri wajielekeze katika kutafakari mbinu watakazotumia kuongeza pato la mwananchi katika maeneo waliyopangiwa kuyasimamia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mchango wa viwanda vidogo vidogo katika maendeleo ya nchi, wakati Serikali ikielekeza nguvu zake katika sekta ya kilimo na sekta nyingine zenye uwezo wa haraka wa kukuza uchumi, kuinua Pato la Taifa na hatimaye kuondoa umasikini, lazima tuangalie pia uendelezaji wa sekta ya viwanda na hasa Viwanda Vidogo (*Small and Medium Enterprises – SMEs*) kwa ajili ya kusindika mazao. Nchi nyingi zimewewa mkazo mkubwa katika kuiendeleza sekta hii. Aidha, uchumi wa nchi hizo hutegemea sana sekta hii na hivyo zimewewa mikakati maalum kwa ajili ya kuiendeleza. Serikali ya Tanzania ilitambua mapema umuhimu wa sekta hii na hivyo ikaanzisha Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) mwaka 1973 ili kuratibu sekta hii tu. Vilevile mwaka 2003, Serikali ilitunga Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na

Biashara Ndogo (*SME Development Policy*) iliyotoa mwongozo wa namna ya kuiendeleza sekta hii ikiwemo kutatua changamoto zinazoikabili. Mpango wa Maendeleo ya miaka mitano 2011/2012 - 2015/2016 unasitiza kuwepo kwa viwanda vya msingi ambavyo vitatumia malighafi inayopatikana humu nchini. Aidha, msisitizo uko katika kuweka mazingira mazuri ya biashara ya kuwezesha pia kuanzishwa kwa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (*SMEs*) vyenye kukuza ajira. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta hii katika uchumi wa nchi ni mkubwa na uko katika nyanja nyngi. Kwanza Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imekuwa ikitoa mchango mkubwa wa kuongeza thamani mazao ya kilimo na maliasili. Vilevile sekta hii imekuwa ya msaada mkubwa katika kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno (*Post Harvest Losses*). Wajasiriamali wadogo wengi wamekuwa wakijihuisha na usindikaji wa vyakula. (*Makofî*)

Mbali na taasisi nyngi zinazotoa mafunzo ya usindikaji wa vyakula, *SIDO* imeweza kutoa mafunzo ya usindikaji kwa wajasiriamali zaidi ya 7,000 katika mikoa yote ya Tanzania. Wengi wa wajasiriamali hao sasa wanajishughulisha na usindikaji wa vyakula. Sekta hii pia ina fursa nzuri ya kutumia malighafi zinazopatikana nchini. (*Makofî*)

Pili, sekta hii imeendelea kutoa mchango mkubwa katika ajira kwa Watanzania. Hii ni kwa sababu sekta hii huwezesha makundi ya kijamii, hasa wanawake na vijana ambaeo wengi wao wamekosa ajira katika sekta nyngine kutokana na viwango vyao vidogo vya elimu na uzoefu mdogo wa kuweza kupata nafasi ya kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Serikali itaendelea kuweka mkazo mkubwa wa kuendeleza sekta hii ili iweze kutoa ajira zaidi na kuboresha vipato vya wananchi na hatimaye kupunguza umaskini.

Tatu, sekta hii ni chimbuko la maendeleo ya ujasiriamali na sekta binafsi ya nchi yetu. Historia inaonesha kuwa wajasiriamali wengi waliofanikiwa walianza na sekta hii na hatimaye wakakua. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara ili kuwezesha maendeleo ya viwanda vidogo nchini. Programu ya Kuboresha Mazingira ya Biashara (*BEST*) kwa kiasi kikubwa ililenga kurahisisha mazingira ya utendaji wa sekta hii. Pia Serikali imeanzisha mifuko mbalimbali ya mitaji ikiwemo ule wa Kuendeleza Ujasiriamali (*National Entrepreneurship Development Fund-NEDF*) ili kuwasaidia wajasiriamali wadogo kuanzisha na kuendeleza biashara zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha sekta hii kwa kadri uwezo wa Serikali utakavyoruhusu. Ninatoa rai kwa wadau wengine ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, wabia wa maendeleo, taasisi zisizo za Kiserikali na sekta binafsi tushirikiane kuendeleza sekta hii, kwani ina fursa nzuri katika kuongeza ajira, kukuza uchumi na kuondoa umaskini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala la maendeleo ya utalii nchini, utalii ni sekta ambayo ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa sekta nyngine za kiuchumi na kijamii kama vile usafirishaji, viwanda, biashara, kilimo, mifugo, sanaa za mikono na michezo. Utalii ni tasnia pekee ambayo huweza kuongeza ajira kwa haraka sana. Inakadiriwa kwamba kila mtalii mmoja anapokuwa nchini huchangia takriban fursa 12 za ajira za aina mbalimbali. Vilevile tasnia ya utalii inachangia robo ya mapato ya fedha za kigeni tunazopata kwa mwaka. Kwa kiasi kikubwa utalii wetu umetegemea sana mbuga na hifadhi za wanyamapori kwa upande wa Tanzania Bara na utalii wa ufukweni kwa upande wa Zanzibar. Masoko yetu makuu ya watalii ni Marekani, Uingereza, Ujerumani, Italia, Afrika Kusini, Canada, Uholanzi, Hispania, Australia na Ufaransa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hali ya biashara ya utalii katika mwaka 2010, idadi ya watalii kutoka nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 10 kutoka watalii 714,367 mwaka 2009 hadi watalii 782,699 mwaka 2010. Watalii hao walitembelea vivutio mbalimbali hapa nchini na waliliingizia Taifa dola za Kimarekani bilioni 1.25 ikilinganishwa na dola za Kimarekani bilioni 1.15 zilizopatikana mwaka 2009. Ongezeko hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa na juhudzi za kutangaza na kuhamasisha utalii nje ya nchi pamoja na uboreshaji wa sekta ya huduma za kitalii, hususan hoteli na miundombinu ndani ya nchi. (*Makofî*)

Mwaka 2011, watalii wa Kimataifa waliotembelea Hifadhi za Taifa kuanzia Januari hadi Juni wameongezeka kwa zaidi ya asilimia 21.73 hadi kufikia watalii 197,736; ikilinganishwa na watalii 162,437 waliotembelea hifadhi hizo katika kipindi hicho, mwaka 2010. Vilevile katika kipindi hicho hicho watalii wa ndani wameongezeka kwa zaidi ya asilimia 152 kutoka watalii 121,976 mwaka 2010 hadi 308,038 mwaka 2011. Hizi ni dalili kwamba juhudini za Serikali na wadau wote wa utalii katika kukuza utalii nchini zimeanza kuzaa matunda tarajiwa. Hata hivyo hatuna budi kuendeleza juhudini hizi maradufu ili kuongeza Pato la Taifa. (*Makofii*)

Pamoja na mafanikio hayo na mengine ambayo yalitajwa vizuri kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii wakati wa kuwasilisha Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2011/2012, zipo changamoto zinazoikibili sekta ya utalii na Wizara kwa ujumla. Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia majadiliano ya Wizara hii wameainisha changamoto nyingi kuanzia watumishi wasiokuwa waaminifu, utoroshaji wa nyara za Serikali, ujangili kwenye mbuga za wanyama na nyingine nyingi. (*Makofii*)

Napenda kuwaahidi Watanzania kuwa Serikali haitakaa kimya kuona maliasili zake zinaabiwa na kunufaisha watu wengine na siyo Watanzania. Uchunguzi wa kina utafanyika kwa hoja zote zilizotolewa hapa Bungeni na hatua stahiki zitachukuliwa kwa wale wote watakaobainika kuhujumu rasilimali zetu. Nichukue nafasi hii kuwaagiza wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na taasisi zake kufanyakazi kwa uadilifu na uaminifu mkubwa kwa manufaa ya Taifa letu. Kumbukeni vyeo mlivyopewa ni dhamana na Taifa haliwatarajii kutumia dhamana hiyo kwa manufaa yenu binafsi, bali kwa manufaa ya Watanzania wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha sekta ya utalii nchini inakua na kuendelea. Pamoja na mambo mengine, Serikali itaendelea kufanya yafuatayo ili kuongea tija ya sekta ya utalii hapa nchini:-

- (i) Kushirikiana na wadau wa maendeleo kuelekeza rasilimali zaidi katika kujenga na kuboresha miundombinu itakayochochea maendeleo ya utalii hapa nchini, hususan maeneo ya Kusini na Magharibi mwa nchi;
- (ii) Kuhamasisha uwekezaji kwenye maeneo ya utalii na kuandaa mazingira bora ikiwemo kuimarisha mafunzo kwa watoaji huduma za utalii nchini;
- (iii) Kuendelea na zoezi la kupanga hoteli katika madaraja ili kudumisha ubora wa huduma za malazi;
- (iv) Kuongeza kasi katika kutangaza vivutio vya utalii katika masoko mapya na kudumisha utangazaji kwenye masoko ya asili;
- (v) Kuhamasisha uwekezaji katika huduma zinazokidhi matakwa ya watalii wa ndani; na
- (vi) Halmashauri kuhamasisha uwekezaji katika huduma za utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Tanzania inafikika kwa urahisi na kwa muda mfupi kutoka nchi za Ulaya Mashariki, Asia ya Kati na Mashariki ya Mbalii. Hali hii imeboreka zaidi baada ya baadhi ya Mashirika ya Ndege ya nje kama ya nchi za Qatar, Uturuki na Oman kuongeza safari za kuja nchini. Hivyo, napenda kuwakumbusha wadau wote wa utalii nchini kuwa, ili kukuza biashara na uchangiaji wa sekta ya utalii katika uchumi wa Taifa, hatuna budi kujipanga na kufanya kampeni maalum kutangaza utalii katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi za SADC ili kukuza Utalii na kuongeza Pato la Taifa na ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niruhusu niongelee kidogo sekta ya elimu na hasa matokeo ya kidato cha sita na nafasi ya Chuo Kikuu Huria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kidato cha sita, matokeo ya mtihani wa kumaliza kidato cha sita mwaka 2011, yanaonesha kuwa watahiniwa 44,720 walifanya mtihani wa kumaliza kidato cha sita. Kati yao watahiniwa 41,142 walifaulu sawa na asilimia 92.1 ya watahiniwa wote. (*Makofii*)

Jambo la kutia moyo ni kuwa wanafunzi walifanya vizuri katika masomo ya sayansi ikilinganishwa na miaka ya nyuma hasa mwaka 2010. Kwa mfano, ufaulu wa Hisabati uliongezeka kutoka asilimia 79.1 ya wanafunzi 5,882 mwaka 2010 hadi asilimia 81.5 ya wanafunzi 6,723 mwaka 2011, Kemia uliongezeka kutoka 77.4 ya wanafunzi 8,480 mwaka 2010 hadi asilimia 80.0 ya wanafunzi 9,071 na Fizikia uliongezeka kutoka asilimia 63.2 ya wanafunzi 5,125 mwaka 2010 hadi asilimia 67.0 ya wanafunzi 5,724 mwaka 2011. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii ni hatua nzuri katika maendeleo ya sayansi hapa nchini ikizingatiwa kuwa masomo ya sayansi yamekuwa na ufaulu usioridhisha kwa muda mrefu. Napenda kutoa pongezi kwa wanafunzi na wadau wote waliohusika katika kuleta mafanikio haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Bunge tumeshaonesha kuridhishwa kwetu na juhudhi za wanafunzi hawa kwa kuwaalika wavulana kumi na wasichana kumi waliofanya vizuri kwenye mtihani huo Kitaifa ndani ya Bunge lako Tukufu na kuwapongeza kwa kuwapa zawadi. Aidha, kupitia Bunge lako Tukufu tulitoa zawadi ya meza za maabara zinazohamishika kwa Shule za Sekondari saba za Kata zilizosaidia kuandaa baadhi ya wanafunzi walikaribishwa hapa Bungeni. Kwa kushirikiana nawe Mheshimiwa Spika, tulizindua meza hiyo hapa kwenye viwanja vya Bunge. Hizi zote ni jithada za kutoa msukumo kwa wanafunzi, walimu, wazazi na wadau wengine ili kuinua ufaulu wa masomo ya sayansi. (*Makofii*)

Napenda kuwahamasisha wanafunzi wapende masomo ya Hisabati na Sayansi. Bila Hisabati na Sayansi katika karne hii ya utandawazi ni dhahiri kuwa hatutakuwa na watu wabunifu na wagunduzi katika kizazi chetu. Tuandae mazingira bora ya kuwasaidia watoto wetu kupenda kusoma masomo ya Sayansi na Hisabati ambayo yana fursa kubwa katika soko la ajira na pia yana umuhimu wa kipekee katika mazingira ya dunia tunayoishi leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, elimu ya juu na nafasi ya Chuo Kikuu Huria; Tanzania ina Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki 42. Kumekuwa na mafanikio makubwa katika elimu ya juu katika miaka ya hivi karibuni. Kwa mfano, udahili katika Vyuo vya Elimu ya Juu uliongezeka kutoka wanafunzi 45,501 mwaka 2006/2007 hadi 140,000 mwaka 2010/2011 katika Vyuo Vikuu vya Umma na binafsi. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 206 kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Chuo hiki ndicho kimekuwa kinadahili idadi kubwa ya wanafunzi kuliko Vyuo Vikuu vingine vyote nchini katika miaka ya hivi karibuni. Kwa mfano, katika mwaka 2007/2008, Chuo kilidahili wanafunzi 25,829 sawa na asilimia 34 ya wanafunzi 76,172 waliodahiliwa katika Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki katika mwaka huo. Katika mwaka 2010/2011, Chuo Kikuu Huria kilidahili wanafunzi 44,272 sawa na asilimia 32 ya wanafunzi 139,638 waliodahiliwa katika Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki mwaka huo. Idadi hiyo ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo Kikuu Huria inadhihirisha umuhimu wa chuo hicho kwa maendeleo ya Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki kilichoanzishwa mwaka 1993, kinatoa mafunzo kwa Watanzania kwa gharama nafuu kuliko Vyuo Vikuu vingine nchini. Aidha, Chuo kinatoa fursa ya kusoma bila mwanafunzi kulazimika kuacha ajira yake na kinatoa elimu kulingana na ratiba ya mwanafunzi katika shughuli zake za siku hadi siku. Hii ni fursa muhimu kwa Watanzania wote wanaotambua kuwa elimu haina mwisho. Nataka niwapongeze kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mama Anne Kilango na wenzake wote ambaao nao wamepata fursa ya kutumia Chuo hiki katika kujiedeleza. Chuo Kikuu Huria huendesha elimu na mafunzo kwa kutumia mbinu mbalimbali za kufundisha kwa msafa. Elimu ya masafa inaweza kufanوليوا kama elimu inayotolewa na chuo, taasisi au kikundi cha wanataaluma kwa kutumia mbinu za *TEHAMA* ambapo wanafunzi hufanya mawasiliano na wahadhiri kwa mtandao, redio au televisheni bila kuwepo darasani kama ilivyo kwenye vyuo vingine vya masomo kwa njia ya darasani".

Elimu ya masafa inaweza kutolewa mahali popote hata katika ngazi ya vijiji ni iwapo umeme wa uhakika na mawasiliano ya simu, redio, video, na intaneti yatakuwapo. Vituo vinaweza kuanzishwa na watu wengi wakapata elimu hiyo kwa kuunganishwa na chuo chenye wahadhiri wenye sifa walio mbali na sehemu hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa mawasiliano ya simu, redio, video na intaneti katika elimu ya masafa, ninaelewa tunazo changamoto za kuhakikisha miundombinu ya mawasiliano ipo hadi vijiji ni. Wakati Serikali inajitahidi kupanua mtandao wa mawasiliano hadi vijiji ni, napenda kuwasihii Watanzania hususan watu walio kazini (*in-service*) kuchangamkia elimu hii ya masafa kwa kujunga na Chuo Kikuu Huria Tanzania na vyuo vingine vinavyotoa elimu kama hiyo. (*Makof*)

Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kuwa hadi sasa wanaume ndio wanaochangamkia fursa hii kwa wingi kuliko wanawake. Kwa mfano mwaka 2007/2008 wanawake waliodahiliwa na Chuo Kikuu Huria walikuwa asilimia 23 tu ya wanafunzi 19,909 waliodahiliwa. Mwaka 2010/2011 wanawake walikuwa asilimia 30 ya wanafunzi 44,272 waliodahiliwa. (*Makof*)

Hivyo, nawahimiza wanafunzi wa kike bila kujali tofauti za umri kutumia fursa hii ya elimu ambayo inamwezesha mwanamke kupata elimu wakati akiendelea na majukumu yake kwa familia na Taifa. Nawaomba wananchi wote kujunga na utaratibu huu wa elimu kwa masafa ili kujiletea maendeleo ya haraka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajali za barabarani, nimeongea kwa kirefu masuala mbalimbali yanayohusu uchumi na maendeleo ya nchi yetu, lakini kabla sijahitimisha hotuba yangu, niruhusu kwa masikitiko makubwa kuongelea tena kuhusu ajali za barabarani. Takwimu zinaonesha kwamba ajali za barabarani zimekuwa zikiongezekwa kwa kasi ya wastani wa asilimia nane kwa mwaka kati ya mwaka 2005 na 2010 na idadi ya vifo vilivyotokea iliongezekwa kwa wastani wa asilimia 8.3 kwa mwaka katika kipindi hicho. Utafiti uliofanywa na Wizara za Ujenzi, Uchukuzi na Mambo ya Ndani ya Nchi unaonesha kuwa ajali hizo husababishwa na uzembe wa watumiaji wa barabara, ubovu wa magari na ubovu wa barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa kukabiliana na tatizo la ajali za barabarani, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kutekeleza mabadiliko makubwa katika suala la usalama barabarani kama ifuatavyo:-

- (i) Kutunga Sera ya Usalama Barabarani mwezi Septemba 2009;
- (ii) Kuanzia mwaka huu wa fedha wa 2011/2012, Serikali itaanzisha Wakala wa Taifa wa Usalama Barabarani (*National Road Safety Agency*) kwa kutumia Sheria ya Wakala wa Serikali ya mwaka 1997. Wakala huu utasimamia kwa karibu Sheria ya Usalama Barabarani;
- (iii) Katika mwaka huu wa fedha wa 2011/2012, Serikali italeta hapa Bungeni Muswada wa Sheria mpya ya Usalama Barabarani badala ya Sheria iliyopo ya mwaka 1973; Sheria hii itawezesha kutekelezwa kwa mikakati ya kukabiliana na ajali ikiwa ni pamoja na kuainisha muundo wa kitaasisi wa kusimamia usalama barabarani;
- (iv) Kuanzisha utaratibu kufunga vifaa vya kuwezesha ufuatiliaji wa mahali gari lilipo wakati wowote na mwendo kasi wake kwa kuanzia na mabasi na malori ya kwenda mikoani;
- (v) Kuanzisha utaratibu wa mafunzo, majoribio na mitihani ya nadharia na vitendo kwa madereva walio kazini;
- (vi) Kuendeleza elimu ya darasani kuhusu usalama barabarani katika Shule za Msingi na Vyuo vya Ualimu na Umma kuititia redio, luninga, magazeti, na matangazo mbalimbali; na
- (vii) Askari wa Usalama Barabarani kuendelea kuwachukulia hatua kali za kisheria kwa wale wanaovunja Sheria za Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Spika, ajali hizo za barabarani zinajumuisha pia ajali za pikipiki na bajaji. Ajali zilizohusu pikipiki na bajaji nazo zimeongezeka kutoka jumla ya ajali 1,683 mwaka 2007 hadi 4,363 mwaka 2010.

Ongezeko hili ni wastani wa asilimia 38 kwa mwaka. Jumla ya vifo vilivyotokana na ajali hizo ni watu 193 mwaka 2007 ikilinganishwa na vifo 683 mwaka 2010, sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 53 ya vifo kwa mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na ongezeko hili la ajali na vifo Serikali imefanya yafuatayo:-

(i) Mwaka 2010, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*) imetunga Kanuni za Sheria ya Leseni za Usafirishaji ya mwaka 1973, kuhusu usafiri wa pikipiki na bajaji iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2009;

(ii) Kanuni hizo zinawataka waendesa pikipiki na bajaji kuzingatia masharti yafuatayo:-

(a) Pikipiki na bajaji zitaruhusiwa kupita na kuegeshwa katika barabara mahsus na maeneo yaliyoainishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(b) Mwendesha pikipiki haruhusiwi kubeba zaidi ya abiria mmoja;

(c) Mwendesha bajaji haruhusiwi kubeba zaidi ya abiria watatu;

(d) Mwendesha pikipiki na bajaji anapaswa kuzingatia kikomo cha mwendo kasi kinachooneshwa katika alama za barabarani na kwa wakati wowote haruhusiwi kuendesha kwa mwendo unaozidi kilomita 50 kwa saa;

(e) Mwendesha bajaji haruhusiwi kupakia idadi ya abiria inayozodi idadi iliyoinishwa katika leseni yake ya usafirishaji abiria;

(f) Mwendesha pikipiki anapaswa kuvalaa kofia ya chuma yenye alama inayooonesha eneo lake la usafirishaji wa abiria;

(g) Mwendesha pikipiki anapaswa kuhakikisha kuwa abiria wake amevalia kofia ya chuma;

(h) Mtoto wa umri wa miaka tisa au umri wa chini yake haruhusiwi kuwa abiria kwenye pikipiki;

(i) Mwendesha pikipiki haruhusiwi kutumia simu ya mkononi au chombo kingine cha mawasiliano wakati anaendesa pikipiki;

(j) Mwendesha bajaji atapaswa kuzingatia kuwa na mikanda ya usalama ya kuwafungia kwenye viti kila abiria na ni sharti bajaji ziwe na milango pande zote mbili ili kuwakinga abiria;

(k) Mtoto wa umri wa miaka tisa au umri wa chini yake haruhusiwi kuwa abiria kwenye bajaji isipokuwa kama ameambatana na abiria mwenye umri mkubwa;

(l) Mwendesha pikipiki au bajaji anapaswa kuzingatia sheria ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, tayari *SUMATRA* kwa kushirikiana na Halmashauri zote nchini zimetiliana saini makubaliano ya kusimamia utekelezaji wa kanuni hizo katika maeneo ya Halmashauri. Aidha, *SUMATRA*, Jeshi la Polisi wa Usalama Barabarani na Halmashauri kwa pamoja wanatekeleza mikakati ya kuhakikisha kuwa waendeshaji wa pikipiki na bajaji wanazingatia kanuni hizi ili kupunguza ajali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sina maelezo ya kutosha kuonesha masikitiko yangu kuhusu kiwango cha kutisha cha ajali za barabarani zinazotokea mara kwa mara katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Ninachowea kusema ni kuwataka wahusika wakuu katika Serikali kuchukua hatua za dhati na kwa haraka kutekeleza sera, sheria, kanuni, mipango na mikakati mbalimbali iliyokwishaanzishwa ya kukabiliana na ajali za barabarani. (*Makofii*)

Naiagiza Wizara ya Ujenzi kuhakikisha inawasilisha hapa Bungeni mwezi Novemba, 2011 Muswada wa Sheria mpya ya Usalama Barabarani ili kuwezesha utekelezaji wa haraka wa masuala mbalimbali yatakayoainishwa na Sheria hiyo kwa lengo la kudhibiti ajali za barabarani mapema zaidi. Aidha, askari wa usalama barabarani kwa kushirikiana na *SUMATRA* na Halmashauri mbalimbali nchini kwa pamoja wasimamie utekelezaji wa Kanuni za Sura ya 317 ya Sheria ya Leseni za Usafirishaji ya mwaka 1973 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2009, kuhusu usafiri wa pikipiki na bajaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda kusitiza maeneo machache yafuatayo:-

Moja, upo uhusiano mkubwa kati ya ukuaji wa uchumi na uwekezaji. Tumeweza kusimamia uchumi wa nchi yetu na kuwezesha kukua kwa viwango vinavyordhisha ambavyo hata Mataifa mengine na Mashirika ya nje yanatusifia. Hata hivyo, bado safari ni ndefu ya kuwaletea maendeleo Watanzania. Tunahitaji mageuzi makubwa kifikra na kiuchumi ili kutuwezesha kufikia lengo letu la kuondoa umaskini. Tunazo fursa ambazo tukizisimamia vizuri umaskini utaondoka katika muda mfupi zaidi. Niwaombe Watanzania wenzangu tutumie fursa hizo ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza nchini bila bughudha. (*Makofii*)

Pili, tunalo tatizo la uhaba wa chakula katika nchi zote za Mashariki ya Afrika Tanzania ikiwa ni mojawapo. Tatizo hilo linakua kutokana na ukame unoaoendelea. Nawaomba wananchi wote kuchukua tahadhari ya kutumia chakula kidogo tulichonacho. Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa chakula nchini. (*Makofii*)

Tatu, tunayo nafasi ya kutumia kilimo katika kubadili maisha ya Mtanzania. Kilimo Kwanza ndio kaulimbiu na azma yetu ambayo ni kichocheo katika kusukuma yale yaliyomo katika Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*) kwa vitendo. Nasisitiza kwamba kaulimbiu ya Kilimo Kwanza siyo mbadala wa *ASDP*. Tuitumie kaulimbiu hii kusukuma shughuli zilizoainishwa katika mpango huu kuendeleza kilimo kwa kasi zaidi. (*Makofii*)

Nne, sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na nyuki zinategemeana kwa kiasi kikubwa. Watanzania wengi wanategemea matumizi ya mazao ya sekta hizi kama chakula lakini vilevile kama silaha ya kupambana na umaskini. Tushirikiane na Serikali kuziendelea sekta hizi ili kuondoa umaskini kwa wananchi wetu. Tunayo fursa kubwa katika sekta ya nyuki, tuanze kuitumia vizuri sekta hiyo kujenga uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Tano, tumepitisha Bajeti ya Serikali ambayo inategemea sana ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa vyombo vya nje. Tuongeze juhudhi kufanya kazi ili mapato yaongezeka na hivyo kuongeza makusanyo ya kodi. Aidha, tutumie fedha za Bajeti tulioipitisha iwe mfano wa kuigwa kwa kupanga na kutumia vizuri rasilimali tulizonazo. (*Makofii*)

Sita, mwisho, tunahitaji kwa dhati kabisa kuweka akili zetu zote katika kuongeza uzalishaji katika sekta zote za kilimo, viwanda, na kuboresha huduma za utalii. Tuongeze kasi katika kuhamasisha uzalishaji na tija katika maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, shukrani; napenda nimalizie kwa kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha mkutano huu. Nikushukuru kwa namna ya pekee wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa katuongoza vizuri kulingana na Kanuni za Bunge. Aidha, niwashukuru Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe na Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole kwa kuongoza vizuri baadhi ya Vikao vya Bunge wakati wa mkutano huu. (*Makofii*)

Ninawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu ya dhati na yenye mantiki kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, watumishi na wataalam wote wa Serikali waliosaidia kujibu maswali na hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge zilizojitokeza hapa wakati wa mkutano huu. Vilevile nawashukuru waandishi wa habari kwa kuwapatia wananchi habari kuhusu majadiliano yaliyokuwa yanaendelea hapa Bungeni. (*Makof*)

Napenda kuwashukuru madereva wote ambao wamekuwa makini katika kazi ya kuwaendesha viongozi wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na wataalam kutoka sehemu mbalimbali nchini na kuwawezesha kufika hapa Dodoma kuhudhuria mkutano huu wa nne. (*Makof*)

Vilevile nawashukuru wananchi wa mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Mhandisi Dkt. James Alex Msekela kwa ukarimu wao kwa muda wote tulioaka hapa. Navishukuru pia vyombo vya Ulinzi na usalama ambavyo vimehakikisha muda wote tumekaa kwa amani na kwa utulivu mkubwa. (*Makof*)

Mwisho namshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashilillah na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa huduma nzuri zilizowezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa katika mkutano huu bila matatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpa pole Dkt. Kashilillah kwa maradhi yanayomsumbuwa wakati wa kipindi tulichokuwa hapa na kumtakia apone haraka na kurejea katika afya njema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakati tunahitimisha mkutano huu leo na kuelekea katika Majimbo yetu, nitumie muda huu kumwomba Mwenyezi Mungu awatangulie, awalinde na awaongoze katika safari ya kurejea nyumbani. Tunapokaribia kumaliza mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani, napenda niwatakie Waislamu wote na wananchi wote kwa ujumla *Idd El Fitr* njema na Mungu awabariki sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi tarehe 8 Novemba, 2011 siku ya Jumanne, saa 3.00 asubuhi litakapokutana katika ukumbi huu, hapa Dodoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makof*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji nina mambo machache ya kueleza hapa. Kwanza tunatambua kuwepo kwa Mama Tunu Pinda, mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunakushukuru kwa futari ulyotukaribisha siku ile, ahsante sana. (*Makof*)

Halafu pia nina tangazo lingine kwamba Wabunge wa CHADEMA walikuwa na kikao wakamchagua Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Chiku Abwao na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya kuwa Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Baraza la Wanawake Tanzania (BAWACHA). Tunawapongeza. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 2(2) na Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 mtakumbuka kwamba tarehe 24 Agosti, 2011 Bunge lilitipisha Azimio la Kuunda Kamati Teule kwa ajili ya kuchunguza uhalali wa utaratibu wa Wizara kuchangisha fedha kwa ajili ya kupitisha Bajeti na kubainisha endapo kitendo cha Katibu Mkuu Kiongozi kutoa taarifa kwa waandishi wa habari juu ya uchunguzi wa suala la fedha zilizokuwa zikichangishwa na Wizara ya Nishati na Madini kimeingilia au kuathiri madaraka ya Bunge. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, aidha Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai aliwatangazia kuwa nitaiunda rasmi Kamati Teule hiyo na kuwaarifu. Kazi ya kuunda Kamati Teule imekamilika na napenda kuwatangazia kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, Kamati Teule itafanya kazi kwa hadidu za rejea zifuatazo:-

(i) Kuchunguza utaratibu uliobainika wa kukusanya fedha kwa ajili ya kukamilisha uwasilishaji wa hotuba za Bajeti za Wizara Bungeni. Katika hiyo hadidu ndogo ni kwamba tuangalie uhalali wa utaratibu kisheria au kikanuni.

(ii) Iwapo fedha hizo huwa zinakasimiwa katika Bajeti husika.

(iii) Matumizi halisi ya fedha zinazokusanywa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hadidu rejea ya pili ni kuitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu uchunguzi alioufanya kuhusiana na agizo la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kuchangisha fedha zilizo chini ya Wizara hiyo kwa ajili ya kufanikisha uwasilishwaji wa Bajeti ya Wizara hiyo Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hadidu rejea ya tatu, kuchunguza mfumo wa Serikali kujibu hoja zinazotolewa Bungeni na taratibu za kullarifu Bunge matoeko ya utekelezaji wa hoja hizo. Hapa tuna rejea ndogo ndogo kwamba tuangalie usahihi wa utaratibu uliotumiwa na Katibu Mkuu Kiongozi kwa suala la ndugu David Jairo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini.Pia kubaini kama utaratibu huo umeathiri dhana ya Haki na Madaraka ya Wabunge. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hadidu rejea ya nne ni kuangalia nafasi ya mamlaka ya uteuzi kwa ngazi ya Makatibu Wakuu katika kushughulikia masuala ya nidhamu ya anaowateua. Nirudie tena kuangalia nafasi ya mamlaka ya uteuzi kwa ngazi ya Makatibu Wakuu katika kushughulikia masuala ya nidhamu ya anaowateua. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hadidu rejea ya tano ni kuangalia mambo mengine yoyote yenye uhusiano na masuala haya. Kwa hizi ndiyo hadidu rejea ambazo tumewaandikia wenzetu ambaao watatufanya kazi hii. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nimewateua Wabunge wafuatao kuwa Wajumbe wa Kamati Teule, wa kwanza ni Mheshimiwa *Engineer Ramo Matala Makani*, nimemteua Mheshimiwa *Gosbert Begumisa Blandes*, nimemteua *Mchungaji Israel Yohana Natse*, nimemteua Mheshimiwa *Khalifa Suleiman Khalifa* na nimemteua Mheshimiwa *Martha Jachi Umbulla*. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Kamati Teule itafanya kazi kwa kipindi kilichozidi wiki nane na itawasilisha taarifa yake Bungeni wakati wa Mkutano wa Tano wa Bunge kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 119 ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007. (*Makofi*)

Hitimisho, ni imani yangu, ya Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla kuwa ninyi niliowateua mtafanya kazi hii kwa makini, busara na uaminifu mkubwa, mkiongozwa na Katiba ya nchi, sheria na kanuni zetu na vilevile mtatoa haki kwa watu wote watakaohusika na suala hili. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya haya yote napenda nichukue nafasi hii mimi binafsi niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Tulipoanza Bunge hili mwanzoni mwa Bajeti tulionekana kama *The Comedy*, watu walitouona walituona kituko kabisa. Lakini napenda kuwashakikishieni mwisho tunaomaliza hapa mmeonekana kweli Waheshimiwa ambaao mmefanya kazi yenu kwa uzuri kabisa, mmefanya kazi yenu kwa kuvumiliana, kusikilizana na kujenga hoja pamoja. (*Makofi*)

Kuna mambo ambayo mlifkiria muwe kitu kimoja hata kama mlikuwa na pande mbalimbali na yakafanikiwa. Mimi nadhani tunakokwenda tunayo sababu nzima kabisa ya kujivunia kwamba tutakuwa Bunge imara, mtafanya kazi yenu kwa uadilifu na mkisikiliza hotuba

aliyotoa Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa. Haya aliyo sema yote maana yake ninyi mfuatilia mgongoni hapa aliposema, si ameahidi humu ndani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi naamini kabisa Kamati zote za Bunge zitasimama imara kuifua tiliar Serikali ili tuweze kupata nchi nzuri, nchi ambayo wananchi wote wanaweza kuifurahia na kila mtu atuamini sisi kama ni Wabunge tunaowawakilisha. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nilisema kwamba mzunguko wa Kanuni zetu ndiyo tumemaliza sasa. Mzunguko wa Kanuni zile sasa tumemaliza hakuna tulichoachaa. Kwa hiyo mwezi Novemba kabla ya kuanza tutafanya marejeo ya Kanuni tulizofanya, makosa tuliyofanya tusahihishe na mengineyo kusudi sasa tuanze kufanya kazi yetu kwa umakini kabisa na pale ambapo adhabu inatakiwa kutolewa sasa itakuwa inatolewa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mimi naamini tutakuwa makini. Lakini katika kufanya kazi hiyo na pengine kutokufahamu sana Kanuni mara kwa mara ilionekana meza inawakera baadhi ya Wabunge. (*Makofi*)

Mimi nasema jamani kwanza ni kanuni. Lakini kama nilivyowaambia toka mwanzo tukika hapa mwenzio akisema msitengeneze uadui, Mwenyekiti akikosea hapa msibebe uadui. Kwa hiyo, chuki na hila zozote mlizonazo vichwani mwenu mziache hapa hapa mkiondoka. Muache humu humu na ziozee humu humu. Hakuna aliyefanya kazi kwa ajili ya kumkomoa mtu mwingine ye yote. Naomba hilo tulielewe kabisa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tutakapoendelea itakuwa hivyo, mtakuwa na michango mikali kwa mtu mwingine na mwingine, lakini maana yake isiwe ni uadui. Kwa hiyo, jamani kwa wale ambao walikwazwa kwa namna moja au nytingine naomba tusameheane, mjue tunapofanya kazi Bunge hatuna uadui na mtu ye yote wala chuki na mtu ye yote. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo naomba kuwahoji kuhusu kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuahirisha Bunge hadi tarehe 8 Novemba, 2011. (*Makofi*)

(Hoja illolewa iamuliwe)
(Hoja illamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Sasa naomba msimame tuimbe Wimbo wa Taifa.

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wimbo wa Taifa uliimbwa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha Bunge mpaka tarehe 8 Novemba, 2011 tutakapokutana hapa saa tatu asubuhi siku ya Jumanne. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge naahirisha Bunge mpaka tarehe hiyo.

(Saa 12.32 jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 8 Novemba, 2011 Saa Tatu Asubuhi)